# BUNGE LA TANZANIA

# MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NANE

**Kikao cha Kumi na Nne – Tarehe 2 Julai, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mhe. Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI.

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma) kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:**

Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Utekelezaji wa Ofisi ya Rais (Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma) kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

**SPIKA:** Nakushangaa Mwenyekiti George Malima Lubeleje, umenunanuna na hali jana Waziri Mkuu alikuwa katika Jimbo lako. *(Kicheko/Makofi)*

**MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA (MHE. SHOKA KHAMIS JUMA):**

Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Utekelezaji wa Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma) kwa mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka 2007/2008

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 116

**Majengo Yaliyokuwa ya Wapigania Uhuru Kongwa**

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR** aliuliza: -

Kwa kuwa Tanzania imesifika na inaendelea kusifika kwa kusimamia Amani na kujitolea mhanga katika kupigania uhuru wa nchi za Kusini mwa Afrika; na kwa kuwa eneo la Kongwa, Mkoani Dodoma ni sehemu iliyotumika kuwahifadhi wapigania uhuru toka Msumbiji, Namibia na Afrika Kusini na yapo majengo yaliyotumiwa na wapigania uhuru hao:-

(a) Je, Serikali imeyatunzaje majengo hayo ili yawe kielelezo kwa vizazi vya nchi hizo na Tanzania kwa ujumla?

(b) Je, wananchi wa eneo hilo la Kongwa wamefaidika vipi na uhifadhi wa wapigania uhuru hao baada ya nchi zao kujitawala?

(c) Je, viongozi wangapi waliowahi kuhifadhiwa katika eneo la Kongwa au waliofuata baada yao wamewahi kulitembelea eneo hilo?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wengine mtakaouliza maswali hamtatoa salamu za aina hiyo kwa sababu mchakato huo bado unaendelea na kwa kila jimbo. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge wa Dimani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika eneo la Kongwa mkoani Dodoma yapo majengo ambayo yaliwahi kutumiwa na wapigania uhuru kutoka nchi za Kusini mwa Afrika hadi mwaka 1974. Baada ya hapo majengo hayo yameendelea kuhifadhiwa na Wizara au Taasisi mbalimbali za Serikali zilizokabidhiwa katika nyakati tofauti. Kwa hivi sasa majengo hayo kupitia maombi ya wananchi wa Kongwa yanatumika kama sehemu ya Shule ya Sekondari ya kutwa chini ya usimamizi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Maumbile (*structures*) ya majengo, makaburi yao na mahandaki likiwemo alilotumia Hayati *Comrade* Samora Machel yamebaki kama yalivyojengwa na kwa hakika ni vielelezo vinavyotumika kwa vizazi vya nchi hizo. Hivi karibuni, yaani tarehe 21 Juni, 2007, Mkuu wa Wilaya ya Kongwa alipokea ugeni wa Serikali ya Msumbiji kutoka Televisheni ya Taifa ambao ulitembelea eneo hilo la kihistoria na kupiga picha.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa eneo la Kongwa wanafaidika kwa kuyatumia majengo hayo kuwapatia vijana wao elimu ya sekondari hadi kidato cha nne. Aidha, mipango ya baadaye ya bodi ya shule hiyo ni kuifanya iweze kutoa elimu ya sekondari hadi kidato cha sita.

Mheshimiwa Spika, viongozi waliowahi kuhifadhiwa katika kambi ya Kongwa ni pamoja na aliyekuwa Rais wa Namibia Mheshimiwa Sam Nujoma, Rais wa kwanza wa Msumbiji, Hayati Samora Machel na aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa SWAPO nchini Namibia, Mheshimiwa Hifikepunye Pohamba. Viongozi waliotembelea kambi hiyo kwa madhumuni mbalimbali ni wengi wakiwemo mabalozi na wafanyakazi wengi wa nchi husika hapa nchini. Viongozi waandamizi wa majeshi na watendaji mbalimbali wa Serikali katika nchi hizo. Aidha, kati ya viongozi waliohifadhiwa hapo na baadaye kuweza kutembelea kambi hiyo ni Mheshimiwa Sam Nujoma, aliyekuwa Rais wa Namibia ambaye alifika tarehe 3 Julai, 2000 na Mheshimiwa Hifikepunye Pohamba aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa SWAPO ambaye alitembelea hapo tarehe 5 Julai, 2003. Mheshimiwa Hifikepunye Pohamba kwa sasa ndiye Rais wa nchi ya Namibia.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake kutokana na suala hili lakini alichokuwa akizungumza Mheshimiwa Waziri ni kwamba majengo hayo hivi sasa yanatumika kama shule. Lakini pamoja na hayo, mbali ya kuwepo shule, je, Serikali haioni kwamba bado kuna umuhimu wa kuendelea kuzihifadhi sehemu hizo za Kongwa na kuzifanya kuwa kivutio kimojawapo cha watalii na kumbukumbu za kihistoria hasa njia za chini kwa chini zilizokuwa zinatumiwa na Mheshimiwa Machel na sehemu nyingine kuliko kuziweka kama zilivyo hivi sasa?

Lakini la pili kwa kuwa sioni faida, je, wananchi wa Kongwa wamefaidika vipi kwa kuwekewa majengo yale kuwa shule? Je, hao waliokowako hapo wamewasaidia vipi wananchi wa Kongwa katika kuendeleza shughuli zao za kijamii katika sehemu ile?

**NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI**: Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishasema katika jibu la msingi kwamba maumbile kwa maana ya majengo, hasa hasa yale ya makaburi na mahandaki yamebaki kama yalivyo kwa ajili ya vizazi vya sasa na vijavyo vya nchi hizo kupita na kuangalia historia yao ya nyuma. Siamini kama Mheshimiwa Hafidh Ali lile analosema kwamba kuwepo kwa shule pale sio jambo la faida, naamini hasemi kwa dhamira; naamini kuwepo kwa shule ni suala la msingi na tusingeweza kutumia yale majengo kwa kitu kingine chochote. (*Makofi*)

Na. 117

**Kuigawa Tarafa ya Mpwapwa**

**MHE. GEORGE MALIMA LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa Tarafa ya Mpwapwa iliyopo wilayani Mpwapwa ni kubwa sana ina kata tisa (9) na jumla ya watu 140,000:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuigawa Tarafa hiyo ili kupata Tarafa tatu za Mpwapwa yenyewe (Kata za Mpwapwa mjini, Vinghawe na Chunyu); Tarafa ya Mima (iwe na Kata za Mima, Berege na Mkanana) na Tarafa ya Matomondo (itakayokuwa na Kata za Matomondo, Kimagai na Godogode)?

(b) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba kuigawa Tarafa ya Mpwapwa kufanya Tarafa tatu (3) za kiutawala kutasaidia sana kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi wa maeneo hayo kuliko ilivyo sasa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, uanzishwaji wa maeneo mapya ya utawala hapa nchini huzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa. Aidha, vipo vigezo vya kuzingatia, mahsusi kwa uanzishwaji wa Tarafa kama vile:

- Idadi ya watu wasiopungua 50,000;
- Idadi ya kata zisizopungua 10;
- Ukubwa wa eneo lisilopungua kilomita za mraba 500; na
- Uwezo wa uongozi na watumishi kuhudumia eneo jipya la kiutawala.

Mheshimiwa Spika, Tarafa ya Mpwapwa ina ukubwa wa kilomita za mraba 2,744.7, na jumla ya watu 143,962 katika kata tisa (9) za tarafa hiyo. Tarafa anazopendekeza Mheshimiwa Mbunge za Mpwapwa Mjini zitakuwa na kilomita za mraba 966.2 na jumla ya watu 52,913; Mima itakayokuwa na kilomita za mraba 903.4 na jumla ya watu 52,645, na Matomondo itakayokuwa na kilomita za mraba 874.7 na jumla ya watu 38,404; zitakuwa na kata tatu tu kila tarafa moja. Kwa kuwa tarafa ya sasa ya Mpwapwa yenye kilomita za mraba 2,744.7 na kata 9 ina idadi kubwa ya watu, yaani watu 143,962 ambao ni karibu mara tatu zaidi ya idadi ya chini kivigezo, ni dhahiri kuwa ingestahili kugawanywa. Hata hivyo, ili kuepuka kuigawa zaidi tarafa ya Mpwapwa na hatimaye kuikosesha vigezo vya kupatikana tarafa mpya, kupitia Bunge lako Tukufu, namshauri Mheshimiwa Mbunge kuzingatia wazo la kuigawa katika Tarafa mbili za Mpwapwa mjini na Mima na kuondoa pendekezo la kuanzisha Tarafa ya

Matomondo ambayo itakuwa na idadi ya watu 38,404 ambayo ni chini ya kigezo.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika sehemu (a) hapo juu, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kuigawa Tarafa ya Mpwapwa kutusaidia sana kuongeza huduma karibu na wananchi. Lakini ili kuendana na vigezo vilivyopangwa ni

vizuri kuigawa Tarafa hiyo katika Tarafa mbili badala ya tatu kwa kuanzia. Ni matarajio ya Serikali kwamba Mheshimiwa Mbunge kwa kupitia vikao vya wilaya na mkoa watajadili rasmi mapendekezo ya kuigawa Tarafa na hatimaye kuyawasilisha katika Ofisi ya Waziri Mkuu kwa tathimini zaidi.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali ya nyongeza. Kwanza, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, kwa jibu lake zuri. Je, katika bajeti ya mwaka 2007/2008 ukiacha tarafa ya Matomondo, Serikali itakuwa tayari kuzigawa tarafa mbili za Mpwapwa na Mima? Pili, kwa kuwa Serikali za Mitaa ni Serikali kamili; na kwa kuwa Halmashauri za Wilaya zina madaraka na mamlaka kamili; je, kwa nini zisiachiwe Halmashauri za Wilaya, Miji na Manispaa kugawa vijiji, kata na kadhalika na kuipa taarifa TAMISEMI hasa ikizingatiwa kuwa mchakato wa kugawa vitu hivyo huchukua muda mrefu? Je, Serikali itakuwa tayari kukubali kwamba sasa Serikali za Mitaa ziachiwe kugawa vijiji na kata?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kwa heshima nimjibu Mheshimiwa Lubeleje, maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Labda nianze na hili la pili. Kwa sasa ni jambo lisilowezekana kugawa tarafa, kata, na vijiji kwa sababu suala hilo lipo chini ya mamlaka ya kisheria ambayo yamebainisha wazi nani anapaswa kufanya kazi hiyo. Kwa hiyo ugawaji unaweza kufanyika tu hadi hapo sheria zitakapobadilishwa, kwa sasa hilo haliwezekani.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu suala lake la kwanza, kuhusu zile tarafa mbili, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, kazi ya kwanza ni lazima jambo hili litoke kwenye Halmashauri inayohusika ili kuweza kushirikisha jamii kwa mawazo aliyonayo Mheshimiwa Lubeleje. Yakifika kwetu baada ya kuwa yamepitia mchakato wote hadi *RCC*, kwa kawaida na sisi tunafanya tathimini mpya na kupanga ni namna gani tunaweza kuanzisha tarafa, kata au vijiji. Kwa hiyo, bado tunamshauri jambo hili lianzie huko baadaye tukilipata tutajua nini cha kufanya, nakushukuru.

Na. 118

**Uundaji wa Miji Midogo – Singida Kaskazini**

**MHE. ZUBEIR A. MAULID (K.n.y. MHE. LAZARO S. NYALANDU)** aliuliza:-

Kwa kuwa, uundaji wa Miji midogo nchini unalenga kuharakisha maendeleo ya wananchi wanaokaa vijijini; na kwa kuwa miji midogo ya Mtinko, Ilongero, Ngamu, Msange, Mgomi na Ngimu katika Jimbo la Singida Kaskazini inastahili kupewa hadhi hiyo mara moja ili kuleta chachu ya maendeleo Jimboni;

Je, Serikali inatoa tamko gani la kutimiza azma hiyo ya wananchi wa Singida Kaskazini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lazaro Samuel Nyalandu, Mbunge wa Singida Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu unaotakiwa kuzingatiwa katika kuanzisha mamlaka ya Mji mdogo ni pamoja na wakazi wa eneo (kijiji au vijiji) kwenye eneo ambalo linastahili kuanzishwa mamlaka ya mji mdogo kupeleka suala lao kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ambamo kijiji hicho kimo. Mkurugenzi anayehusika ataandaa mapendekezo kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa na Waziri mwenye dhamana. Vigezo hivyo ni pamoja na idadi ya watu isipungue 10,000; Eneo lisilopungua kilomita za mraba 580; Maduka ya rejareja yasiyopungua ishirini (20); Mahakama ya Mwanzo na kuwepo kwa huduma za kijamii kama vile shule, vituo vya afya, zahanati, maji, barabara, soko kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa kitaifa katika kila sekta husika. Makao Makuu ya Kata/Tarafa ya eneo kuwa limejengeka kimji na linaweza kupimwa kwa kufuata kanuni na uendeshaji miji.

Mheshimiwa Spika, Tangazo la Serikali Na. 353 la tarehe 17 Septemba, 2004 lilionesha kuwa Tanzania ina miji midogo 90 yenye hadhi ya kuwa mamlaka ya miji midogo. Kwa Vijiji vya Ngamu, Msange, Mgomi na Ngimu havijafikia vigezo vya kuwa mamlaka ya miji midogo isipokuwa vijiji vya Mtinko na Ilongero ambavyo vinakidhi baadhi ya vigezo. Kuanzisha kwa miji ni gharama, hivyo tunashauri kuimarisha miji midogo iliyokwisha tangazwa na Serikali badala ya kutangaza kuongeza miji mingine. Mamlaka za miji midogo zinapoundwa ni vizuri kushirikisha ngazi zote kuanzia kijiji hadi mkoa. Kama nilivyoeleza hapo juu ni vyema Mheshimiwa Mbunge akazingatia kuanzisha miji midogo ya Mtinko na Ilongero ambayo imekidhi haja. Mamlaka ya miji midogo ni mamlaka ya Serikali za Mitaa iliyopo kwenye mamlaka za wilaya. Mamlaka hizi zinaanzishwa pale ambapo palikuwa ni kijiji ambacho kimeanza kuendelezwa na kuwa na mazingira ya kimji. Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa amepewa madaraka ya kutangaza kijiji au vijiji vilivyofikia sifa zilizowekwa kuwa mamlaka za miji midogo kwa mujibu wa kifungu cha 22(3) cha Sheria Na. 7 ya 1982.

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri anakiri kwamba vijiji vya Mtinko, Ilongero vina sifa ya kuwa miji midogo je, sasa atawaeleza nini wananchi wa eneo hilo kwamba ni lini Serikali itatoa ahadi lini itaweza kuwatimizia matakwa yao hayo kwa sababu hilo ni kati ya mambo ambayo ni chachu ya maendeleo katika eneo husika? Kwa kuwa vipo vijiji vingi sana ndani ya nchi ambavyo vinafikia vigezo, sasa ili kuharakisha maendeleo ya maeneo pamoja na matakwa hayo ambayo yataweza kufikiwa na Halmashauri husika, je, Serikali inasema italiharakisha kwa spidi ipi?

**SPIKA:** Kabla sijamwita Naibu Waziri kujibu swali, navutiwa sana pale ambapo Mbunge kutoka eneo jingine la Muungano anafahamu maneno kama Mtinko na

kadhalika, nadhani ni vema. Natoa wito kwa Wabunge wa Tanzania Bara nao kwenda Micheweni na kadhalika kuweza.....! *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba vijiji vya Mtinko na Ilongero angalau vimefikia vigezo vya kuanzishwa kuwa Halmashauri ya mji mdogo. Ninachomshauri Mheshimiwa Mbunge ni kwamba wafuate ule utaratibu ambao ni pamoja na kuwashirikisha wananchi wa eneo husika, yaani vijiji hivyo watoe mapendekezo yao wayapeleke kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya. Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya akiona kwamba yanakidhi vigezo hivyo ndipo atakapopeleka mapendekezo hayo kwa Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa kupitia kwenye vikao vya *RCC* na kadhalika.

Lakini naomba nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge kwamba mwaka 2004 kama nilivyosema kwamba kuna Halmashauri za miji midogo 90 zilitangazwa na Serikali katika Tangazo Na 353. Lakini ukiangalia katika miji yote hii midogo 90 iliyotangazwa, ni miji karibuni mitano tu ambayo imeshaanza utekelezaji. Kwa hiyo, tatizo liko katika Halmashauri zenu, naomba muwaambie Wakurugenzi waweze kuanzisha mamlaka hizo. Sisi kwenye Gazeti la Serikali tumeshatangaza, na ninayo orodha katika Tangazo la Serikali Na. 353, tunaomba Waheshimiwa Wabunge au mtu yeyote anayetaka kuona kama Halmashauri yake imeanzisha mji mdogo aje aangalie ili kwenda kuchochea kule kwa wananchi.

**MHE. ZITTO Z. KABWE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Naamini Mheshimiwa Naibu Waziri wakati anajibu alikuwa na maana ya mamlaka za miji midogo na sio Halmashauri za miji midogo. Kwa sababu mwaka jana katika marekebisho ya sheria za Serikali za Mitaa, Serikali ilitaka kupendekeza kwamba baadhi ya miji midogo iunganishwe na kuunda Halmashauri za miji midogo. Hii inatokana na tatizo kwamba mpaka sasa Mamlaka zote ambazo zilitangazwa mwaka 2002 hazijaanzishwa. Sasa sijui Serikali inatoa kauli gani juu ya suala hili ili kuziondolea mzigo Halmashauri kuhusiana na suala la kuanzisha miji midogo, kwa kuwa kuna miji midogo mingi ambayo imetangazwa lakini bado haijaanzishwa? Nilikuwa naomba Serikali itoe kauli rasmi juu ya hili.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa miji hiyo 90 ilitangazwa, na kama nilivyosema kwenye jibu langu la nyongeza kwamba sasa mchakato huu unatakiwa ufanywe na Halmashauri husika. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge katika mabaraza yenu ya Halmashauri naomba muwashauri Waheshimiwa Madiwani wengine pamoja na Wakurugenzi ili kufuata mchakato wa kuanzisha hizi mamlaka za miji midogo. Hatuwezi tukaanzisha mamlaka nyingine wakati hizo za nyuma bado hazijatekelezwa.

Na. 119

**Kuwepo kwa Mawasiliano ya Simu**

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA (K.n.y.MHE. MAGDALENA SAKAYA)** aliuliza:-

Kwa kuwa kukosekana kwa mawasiliano katika maeneo mengi hapa nchini kumeathiri huduma za maendeleo ya wananchi; na kwa kuwa mawasiliano ni muhimu sana kwa ufanisi wa shughuli mbalimbali:-

Je, Serikali itahakikisha lini kuwa mawasiliano ya simu yanapatikana kwenye kata ya Usinge, Urambo yenye wafanyabiashara na wakulima wengi sana ili waweze kutumia fursa hiyo kujiendeleza kiuchumi?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Serikali inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa huduma za simu hasa za mikononi zitolewazo na makampuni ya simu hapa nchini. Huduma hizo ni muhimu sana katika kuchochea shughuli za kibiashara, kiuchumi, kijamii na ulinzi.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Simu *TTCL* ambayo kwa hivi sasa inakamilisha ujenzi wa simu za mikononi zinazotumia teknolojia ya *CDMA* katika mji mdogo Kaliua na Urambo, ina mpango wa kufanya uchunguzi wa kitaalamu ili kuona uwezekano wa kupeleka mawasiliano ya simu za *CDMA* katika mji wa Usinge, kutuwekea mtambo wa Kaliua na pia kulijumuisha eneo hilo katika mpango wa maendeleo wa mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *Celtel (T) Ltd*. imeweka mnara wake Usinge (Luhanjo *Hill*) ambao uliwashwa mwezi Mei, 2007 na unahudumia eneo lote la Usinge. Aidha, tunapenda pia kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge kuwa Kampuni hiyo imeshaweka mawakala wa kutosha kutoa huduma katika kata ya Usinge wakisaidiwa na wakala mkuu aliyepo mjini Urambo. Juhudi za *Celtel* zinaendelea kukamilisha minara ya Ukumbi, Siganga na Kamila *Hill* kuunganisha mawasiliano ya Luhanjo *Hill* kwenda hadi Nguruka, minara ambayo imeshawashwa.

Aidha, katika kudumisha shughuli zake katika maeneo ya Urambo, Kampuni ya *Tigo* ambayo kwa sasa inawafikia kwa taabu wananchi waishio maeneo ya Urambo, ina mpango wa kufanya uchunguzi wa kitaalam na kulijumuisha eneo hilo katika mipango yake ijayo. Pia Kampuni ya *Vodacom* ina mpango wa kuanza kutoa huduma zake katika maeneo hayo mwaka huu baada ya kukamilisha upembuzi wa masoko katika eneo hilo. Serikali inajitahidi kuhakikisha kwamba eneo hilo pamoja na maeneo mengine ya Urambo, yanapata mawasiliano ya simu za mikononi na hivyo kuwanufaisha wakulima na wafanyabiashara wa maeneo hayo na hatimaye kuongeza ufanisi wa shughuli mbalimbali ambazo ni chachu ya maendeleo ya wananchi.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, asante sana. Kwanza, kwa kuwa kampuni ya *Celtel* tayari imeshaweka mnara hapo Msinge; na kwa kuwa *Tigo* ndio inafanya utafiti hivi sasa; na kwa kuwa minara hii ikiwa mingi inaharibu mazingira na kwa vile *Vodacom* na *Zantel* wameshirikiana kutumia minara hiyo; je, ni kwa nini hiyo kampuni ya *Tigo* na hizo nyingine zisitumie minara hiyo ya *Celtel*?

La pili, kwa kuwa kumekuwa na vishawishi vya vivutio vya biashara katika huduma hizi za simu za mikononi na matangazo mbalimbali yanatolewa kupunguza unafuu, na wengi hata ukinunua vocha ya shilingi 5,000 wanakwambia utapata 6,000; je, mpaka sasa hivi *TICRA* imeweza kufuatilia kama kweli makampuni haya yanafanikiwa au ni janja ya makampuni haya?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, tutamwomba meneja wa kampuni ya *Vodacom* aendelee kushirikiana na kampuni ya *Celtel* kuona kama anaweza kuweka simu kwa kutumia minara yake. Lakini inategemea kampuni ya *Vodacom* ina mwelekeo gani wa biashara katika Urambo kama wanakokwenda wao ni sawasawa na wanakokwenda kule wenzetu wa *Vodacom*. Ni kweli vishawishi mbalimbali vimetolewa kwa kampuni za simu na tunashukuru kwamba angalau mtu wa kawaida anaweza kupiga simu kwa kutumia koponi ya 200 na 500. *TICRA* sasa hivi inashughulikia ipasavyo kuona kama kweli koponi zinazotolewa zinakidhi tija ya pesa ambayo imeanishwa. Namwomba Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi tunalifuatilia kwa karibu suala hilo.

**MHE. MANJU S. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza, lakini kabla sijauliza naomba niwapongeze Mheshimiwa Kigunge Gombale Mwiru na Mheshimiwa Anna Abdallah kwa kutuzwa jana kwenye sherehe za Serikali za Mitaa. Baada ya hayo naomba niulize swali langu.

Kwa kuwa Usinge ipo karibu kabisa na Nguruka na *Celtel* wameweka mtambo Nguruka ambao una muda mrefu haujawashwa, na wataalamu kila baada ya miezi miwili wanakwenda wanazunguka na kurudi na kuwafanya watu wa Nguruka kila wakitaka kupiga simu watafute vichuguu kwa kutumia mtambo ambao upo Usinge; je, Serikali inasema nini kuhusu kuwashwa kwa mtambo wa *Celtel* uliowekwa Nguruka ambao sasa umekuwa kama ni wa maonyesho?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Manju Salum Msambya, kama ifuatavyo:

Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Msambya kwamba hakuna mfanyabiashara yeyote anayeweza kupoteza pesa zake bure. Kama kuna mnara umejengwa Usinge basi umejengwa kwa madhumuni maalumu na kuna kazi ya utafiti ambayo inaendelea. Napenda nimhakikishe kwamba shughuli shughuli zao za utafiti zikimalizika basi mnara ule utakuwa unafanya kazi kama minara mingine ambayo inafanya kazi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabungetuokoe muda, tunaendelea sasa katika Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika swali ambalo lilikuwa liulizwe na Mheshimiwa Pindi Chana linaulizwa na Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o kwa niaba yake.

Na. 120

**Kituo cha Matrekta**

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O (k.n.y. MHE. PINDI H. CHANA)** aliuliza:-

Kwa kuwa kilimo ndio msingi wa uchumi wetu na kuna nafasi ya kimkakati katika *mordenisation* ya uchumi wa Tanzania; na kwa kuwa kilimo cha kisasa sharti kiwe muhimu katika kujenga msingi wa uchumi wa kisasa:-

(a) Je, Serikali inatambua kuwa kilimo cha matrekta ni mongoni mwa aina za kilimo cha kisasa?
(b) Je, mfuko wa pembejeo umewakopesha wakazi wangapi ili wanunue au kukarabati matrekta katika wilaya za Iringa, Njombe, Makete, Ludewa, Mufindi, na Kilolo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mbunge wa Viti Maalum, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inatambua sana kuwa kilimo cha kutumia matrekta ni miongoni mwa aina za kilimo cha kisasa. Kwa kutambua hivyo, mfuko wa Pembejeo wa Taifa umekuwa ukitoa mikopo yenye riba nafuu kwa ajili ya kukarabati matrekta machakavu yanayoweza kutengenezeka na kununua matrekta mapya ili kuongeza eneo la kilimo na uzalishaji wa mazao?

(b) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa 2003/2004 hadi Mei, 2007 jumla ya mikopo 23 ilitolewa kwa Mkoa wa Iringa. Kati ya hiyo mikopo 16 ni ya wakazi wa Iringa na mmoja kwa mkazi wa Njombe. Aidha, mikopo 17 ilitolewa kwa ajili ya kukarabati matrekta na mikopo sita (6) kwa ajili ya ununuzi wa matrekta mapya?

Mheshimiwa Spika, pamoja na eneo linalofaa kwa kilimo kuwa hekta milioni 44, ni hekta milioni 10 tu zinazolimwa. Eneo hilo linalimwa asilimia 70% kwa kutumia jembe la mkono, 20% wana makazi na 10% kutumia matrekta. Ili kukidhi mahitaji tunahitaji kuingiza nchini kwa wastani wa matrekta 1500 – 1800 kwa mwaka lakini hivi sasa tunaingiza matrekta 200 – 300 tu kwa mwaka. Jukumu la kuagiza matrekta liko mikononi mwa sekta binafsi ikiwa ni pamoja na makampuni yanayouza zana za kilimo na mabenki ambayo hayavutiwi kibiashara kukopesha wakulima wasio na dhamana. Nawashauri Waheshimiwa Wabunge kuwahamasisha wakulima, wafanyabiashara wenye

uwezo, vyama vya ushirika na mashirika na makampuni yenye uwezo kuagiza matrekta na kuanzisha vituo vya kukodisha matrekta ili viweze kuhudumia kibiashara wakulima walio wengi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ledian M. Mng'ong'o swali la nyongeza!

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Mkoa wa Iringa ni Mkoa ambao unategemewa katika uzalishaji wa zao la chakula na hasa mahindi; na kwa kuwa nchi inajitegemea kwa chakula, lakini inaonekana kwamba 70% ya kilimo ni cha kutumia Jembe la mkono; je, Serikali haioni kwamba kuna haja sasa ya kutilia umuhimu wa kuangalia mikoa ambayo inazalisha kwa wingi zao la chakula kwa kuweza kuipa pembejeo na kuhakikisha kwamba vituo vya matrekta vinakuwepo Serikali ikiwa imehamasisha yenyewe badala ya kuacha wananchi au Wabunge wahamasishe ili? La pili, kwa kuwa kilimo hiki tunasisitiza kwamba Vyama vya Ushirika na *SACCOS* ziweze kuwa ni njia mojawapo ya kuendeleza kilimo. Je, Serikali itakuwa tayari kukopesha matrekta kwa *SACCOS* na Vyama vya Ushirika vilivyopo mikoani vikiwemo vikundi vya Wanawake?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o, kama ifuatavyo:-

Kama anavyojua, Serikali imekuwa ikitoa pembejeo za kilimo kwa maana ya mbegu, mbolea na mfuko huu ambao nimeusema wa pembejeo ambao umeanzishwa mwaka 1994 kwa Sheria Namba 9 pia unaruhusu watu kukopa pembejeo pamoja na matrekta. Lakini matrekta haya Serikali haiagizi matrekta bali inatengeneza mazingira mazuri kwa wafanyabiashara ambao wanataka kuagiza matrekta waweze kuagiza na kuyakopesha. Kuhusu suala la Vyama vya Ushirika kuagiza matrekta ni kweli kwamba wanaweza wakafanya hivyo lakini kwa masharti yafutayo:- Ni lazima maombi hayo yapitishwe na Halmashauri ambayo inahusika na lazima chama hicho cha Ushirika kiweze kuwa na shamba linalozidi ekari 50 na vilevile wanatakiwa wawe na dhamana isiyohamishika pamoja na hatimiliki. Lakini kwa pembejeo pia wanatakiwa wawe wameshafanya biashara ya pembejeo kwa miaka isiyopungua miwili lakini wawe pia na leseni.

**SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Michael Lekule Laizer!

**MHE. MICHAEL LEKULE LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa wakulima wanaoweza kununua matrekta mapya au kukarabati matrekta ya zamani ni wakulima wakubwa; je, Serikali itawasaidiaje wakulima wadogo wadogo ambao hawakufikia kiwango hicho ili nao kuwakopesha majembe ya kukokotwa na wanyama ili nao waachane na majembe ya mikono?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Michael Lekule Laizer anaelewa kwamba fimbo ya mnyonge ni ushirika na fimbo ya mnyonge ni umoja. Wananchi wengi ambao hatuna uwezo inabidi tujiunge kwenye Vyama vya Ushirika na *SACCOS* ili tuweze kuwa na nguvu ya kukopa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunahamia Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Charles Muguta Kajege, Mbunge wa Mwibara.

Na. 121

**Uwezeshwaji wa Wananchi wa Mikoani**

**MHE. CHARLES MUGUTA KAJEGE** aliuliza:

Kwa kuwa viwanda na biashara nyingi ziko katika Mkoa wa Dar es Salaam pekee, hali inayosababisha wimbi kubwa la vijana wanaotafuta kazi na wanaokimbia umaskini na maisha magumu mikoani kukimbilia Dar es Salaam; na kwa kuwa mikakati mingi inayofanywa na Serikali miaka ya nyuma haijamaliza tatizo hili:

(a) Je, Serikali ina mikakati gani mbadala ya kutatua tatizo hilo ili wananchi walioko mikoani pia wapate fursa za kujiendeleza kimaisha na kupunguza umaskini kama wenzao waishio Dar es Salaam?

(b) Je, mikakati hiyo itachukua muda gani kuleta matumaini na mafanikio kwa wananchi hao?

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI** alijibu:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Kajege, Mbunge wa Mwibara, lenye sehemu (a) na (b), naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:

Serikali ya Awamu ya Nne imepania kutekeleza azma yake ya kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania kwa kuhakikisha kuwa wananchi wote wanawezeshwa. Ili kutimiza azma hii, Serikali imechukua hatua mbalimbali zikiwemo; Kuanzisha Wizara inayoratibu masuala yote ya uwezeshaji wa wananchi, na kuanzisha Baraza la Taifa la Uwezeshaji. Aidha, Serikali inajitahidi kufikisha huduma za jamii vijijini ikiwemo Barabara, maji safi na salama, huduma za afya, huduma za ugani na ruzuku ya pembejeo. Vilevile Serikali inatekeleza miradi ya uwezeshaji wa wananchi vijijini kupitia mfuko wa *TASAF* ambao unafadhili miradi mbalimbali iliyoainishwa na wananchi vijijini. Mradi wa *SELF* nao unatoa mikopo kwa wajasiriamali wadogo wadogo vijijini kwa lengo la kupunguza

umaskini wa kipato na kuongeza ajira. Hatua zote hizi zinalenga katika kupunguza umaskini hasa vijijini.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Kajege, Mbunge wa Mwibara, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inaendelea na Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania yaani MKURABITA ambao utasaidia wananchi kupata hatimiliki zitakazowawezesha kupata mikopo kutoka kwenye asasi za fedha. Ili kuharakisha uwezeshaji mikoani, Serikali imetenga shilingi bilioni 1 kwa kila Mkoa kwa mwaka 2006/2007 ili kuwawezesha wananchi kiuchumi na kuongeza ajira. Aidha, Kamati za kusimamia mpango wa kuwawezesha wananchi kiuchumi na kuongeza ajira zimeundwa kutoka ngazi ya Taifa hadi ngazi ya Kata. Kamati hizi zina jukumu la kuwahamasisha wananchi kuunda na kuimarisha Vyama vya Kuweka Akiba na Kukopa yaani *SACCOS* kwa lengo la kujenga tabia ya kuweka na kukopa, na vilevile kuwasaidia wajasiriamali kuboresha shughuli zao za kiuchumi. Aidha, Mpango Kamambe wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Development Programme (ASDP))* umeanza kutekelezwa na kupitia mradi huu Serikali inatarajia wananchi wa vijijini watapata fursa za kuinua kipato chao kutokana na kuboresha kilimo na hivyo kusaidia juhudi za kupunguza umaskini wa kipato. Hali kadhalika, Serikali inatekeleza Mpango Kamambe wa Taifa wa Umwagiliaji (*National Irrigation Master Plan*) ambao utasaidia kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo na hatimaye kuongeza vipato vya wananchi wa vijijini. Serikali pia inahimiza Sekta Binafsi kuendelea kuwekeza katika viwanda vya usindikaji mazao (*Agro – processing Industries*). Hili litasaidia kuongeza thamani ya mazao ya wakulima na kuongeza ajira kwa wananchi waishio vijijini na hivyo kuongeza vipato vyao.

Mheshimiwa Spika, naamini kwamba Mheshimiwa Mbunge atakumbuka kwamba Serikali kwa kupitia Bajeti yake imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya ruzuku ya mbolea ili kukiinua kilimo cha mazao ya chakula na biashara. Hatua zote hizi zinalenga katika kuinua kilimo na kuongeza pato la wananchi vijijini. Aidha, Serikali inalenga kukifanya kilimo kiwe cha biashara yaani (*Commercialisation of Agriculture)* kwa njia ya kuongeza uzalishaji na tija; hii itasaidia wananchi wa vijijini kushiriki katika biashara kwa njia ya kuongeza uzalishaji wa eka za kuboresha mifugo yao ili wajipatie vipato zaidi.

(b)Matarajio ya Serikali na hasa kwa kuzingatia malengo ya MKUKUTA na Malengo ya Maendeleo ya Milenia (*Millennium Development Goals – MDGs*) ni kupunguza umaskini kwa 50% ifikapo 2015 na kuondoa kabisa umaskini uliokithiri mwaka 2025 kama Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inavyoeleza. Kama mikakati na mipango kamambe iliyoandaliwa ikitekelezwa vizuri kwa ushirikiano mkubwa wa wadau wote, tunatarajia kufikia mafanikio kwa wananchi walio wengi ifikapo mwaka 2025 kama Dira ya Taifa ya Maendeleo inavyoelekeza.

**SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Charles M. Kajege!

**MHE. CHARLES MUGUTA KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwanza, nampongeza Waziri wa Uchumi na

Uwezeshaji kwa majibu yake mazuri, lakini nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mojawapo ya malengo ya miradi midogo midogo yaani *SELF* ni kutatua tatizo kama hili, je, ni kwa nini mradi huo haujaanza kutekelezwa Jimboni kwangu Mwibara?

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI**: Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Kajege, Mbunge wa Mwibara, kwa swali lake la nyongeza kama ifuatavyo: Ni kweli kwamba mradi wa *SELF* haujaenea nchi nzima, kwa hivi sasa umefikia kiwango cha mikoa 14 lakini kwa kutambua hali ya kipato katika Jimbo la Mwibara basi tutajitahidi na hii *SELF* ifike.

**SPIKA:** Ahsante tunaendelea! Waheshimiwa sasa ni zamu ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, swali lilikuwa liulizwe na Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mbunge wa Sumve, lakini kwa niaba yake Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba atauliza.

Na. 122

**Makao Makuu ya Mahakama Kuu ya Rufaa ya Afrika Mashariki kuwa Arusha**

**MHE. KABUZI FAUSTINE RWILOMBA (K.n.y. MHE. RICHARD M. NDASSA)** aliuliza:

Kwa kuwa nchi yetu ina uzoefu mkubwa katika nyanja za kisiasa na Afrika nzima inalijua hilo hata imeweza kwa nyakati tofauti kutumiwa na nchi jirani katika mapambano ya kutafuta uhuru wa nchi zao; na kwa kuwa Mahakama ya Kimataifa inayosikiliza kesi za mauaji nchini Rwanda ipo Arusha na pia Makao Makuu ya Kamati ya Ukombozi Barani Afrika (*OAU Liberation Committee)* yalikuwa Dar es Salaam na kwa kuwa Makao makuu ya Tume ya Ushirikiano wa Nchi Maskini Duniani ambayo Hayati Mwalimu Julius Nyerere alikuwa Mwenyekiti wake; na kwa kuwa makao makuu ya Ushirikiano wa Kiuchumi na Kisiasa Kikanda Barani Afrika, makao makuu ya Afrika Mashariki (*EAC*) pamoja na Bunge la Afrika Mashariki vyote vipo Arusha na kwamba kuwepo kwa Taasisi hizo nchini mwetu pamoja na mambo mengine hutangaza nchi yetu kiutalii na kuongeza mzunguko wa fedha; je, Serikali haioni kuwa ni wakati muafaka sasa wa kuhamasisha ili makao makuu ya Mahakama Kuu ya Rufaa ya Afrika Mashariki iliyondwa hivi karibuni iwe Arusha?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Richard Ndassa, Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo: Mahakama ya Rufaa ya Afrika Mashariki iliyoanzishwa hivi karibuni ni kitengo cha Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyokuwepo na siyo Mahakama mpya.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki tangu kuanzishwa kwake imekuwa inaendesha vikao vyake mjini Arusha ambako yuko Msajili na Wafanyakazi wengine wa Mahakama. Vilevile ramani ya jengo jipya la makao

makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambalo litajengwa Arusha, pamoja na mambo mengine, inabainisha ofisi na nyumba zitakazotumiwa na Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Bunge la Afrika Mashariki na Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Richard Ndassa, kwa jinsi anavyofuatilia kwa karibu ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na nia yake ya kutaka Tanzania makao makuu ya taasisi mbalimbali. Mbali ya kuwa Makao makuu ya Jumuiya pia tumeomba kuwa makao makuu ya Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki, Kamisheni ya Sayansi na Teknolojia ya Afrika Mashariki na makao makuu ya Kituo cha Uokoaji kwenye Maziwa. Aidha, tutaendelea kuomba Tanzania kuwa Makao Makuu ya Taasisi mbalimbali za Jumuiya kadri fursa zitakavyokuwa zinajitokeza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba swali la nyongeza!

**MHE. KABUZI FAUSTINE RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri lakini nina maswali mawili ya nyongeza:

Kwa kuwa baadhi ya mambo ambayo yanatakiwa yafanyiwe kazi katika Ushirikiano wa Afrika Mashariki ni pamoja na usafiri, naomba Mheshimiwa Waziri anieleze kwa kuzingatia kuwa Ziwa Victoria ndiyo kiungo kikubwa cha hizi nchi za Afrika Mashariki mpaka sasa kuna mikakati gani ya kuimarisha usafiri katika Ziwa Victoria? Pili, kwa kuwa kuna mradi au Tume ya *Livemp* ambayo inaangalia Ziwa Victoria na inasemekana Makao Makuu huenda yakaenda Kisumu lakini Sehemu kubwa ya Ziwa Victoria iko upande wa Tanganyika; je haoni kwamba kuna umuhimu wa kuleta hii *Livemp* ije Mwanza kwa sababu sehemu kubwa inayotakiwa kushughulikiwa iko upande wa Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI**: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba kama ifuatavyo:

Upande wa Ziwa Victoria, nchi wananchama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki walianzisha Tume ya kuendeleza Bonde la Ziwa Victoria na Makao Makuu ya Tume hii yapo Kisumu lakini Tume hii ilivyo kama zilivyo Tume nyingine za Afrika Mashariki ina watalamu kutoka nchi mbalimbali wakiwemo Watanzania. Lakini vilevile, mojawapo ya jukumu la Tume hii ni kuangalia maendeleo ya Ziwa Victoria na pia usalama wa usafiri ndani ya Ziwa Victoria na ndiyo maana Sheria ya Usafiri ndani ya Ziwa Victoria iko tayari na muda si mrefu itapelekwa kwenye Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki na vilevile Tume hii inafanya mambo mengine mengi, mojawapo kama nilivyosema tumeanzisha *Centre* ya kuangalia uokoaji ndani ya maziwa na makao makuu yake yatakuwa Mwanza kama tulivyoomba, na dalili zinaonyesha kwamba hakuna nchi nyingine ambayo imeomba ukiondoa Tanzania.

Kuhusu Mradi wa *Livemp* ni mradi ambao ulitekelezwa awamu ya kwanza kuhusu mazingira ya Ziwa Victoria na mambo mengine ya kuhifadhi Ziwa Victoria, sasa tupo katika harakati za kuteleza awamu ya pili na kila nchi ina *Coordinators* wa mradi huu. Kwa hiyo, kama mradi uko chini ya *Commission* ya Ziwa Victoria lakini huwezi ukajenga makao makuu ya mradi kwa sababu kila mradi una mwanzo na mwisho, utaanza utekelezwe hivi karibu ukikamilika Tume itaendelea kuendeleza Ziwa Victoria kama ambavyo inaendelea hivi sasa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe swali la nyongeza!

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa swali la msingi limeeleza kwamba nchi yetu ilitumiwa na nchi jirani katika mapambano ya kutafuta uhuru; je, Serikali haioni kwamba umefika wakati sasa iweze kudai fidia kwa sababu zile nchi sasa zina uchumi mzuri kama Afrika Kusini, Msumbiji na Uganda watulipe fidia kwa mali iliyotumika na wananchi waliopotea na wale waliokufa walipwe?

**SPIKA:** Naona kama halihusiani, kwa sababu swali la msingi lilikuwa ni la ushirikiano, kwa hiyo, bado tupo Afrika Mashariki, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Yahya Kassim Issa.

Na. 123

**Mchakato wa Kujiunga na Shirikisho la Afrika Mashariki**

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA** aliuliza:

Kwa kuwa Tanzania ni Jamhuri ya Muungano wa Sehemu mbili yaani Tanzania Bara na Tanzania Visiwani; na kwa kuwa hivi sasa tuko katika mchakato wa kujiunga na Shirikisho la Afrika Mashariki; je, Serikali inatoa kauli gani iwapo sehemu moja ya Jamhuri ya Muungano inahisi haitakuwa na maslahi ya kujiunga na Shirikisho la Afrika Mashariki?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo: -

Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki umeainisha hatua nne za mtangamano kama ifuatavyo: Hatua ya Kwanza ni Umoja wa Forodha, Hatua ya Pili ni Soko la Pamoja, Hatua ya Tatu ni Sarafu Moja na Hatimaye Shirikisho la Kisiasa la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Chimbuko la kuangalia uwezekano wa kuharakisha uanzishwaji wa Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki ni Mkutano wa kilele wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika Jijini Nairobi, Kenya tarehe 27 – 29 Agosti, 2004 na kuunda Kamati ya kuangalia uwezekano wa kuharakisha uanzishaji wa Shirikisho la Kisiasa katika kipindi kifupi kadri iwezekanavyo.

Kamati iliwasilisha ripoti yake kwa Wakuu wa Nchi Wanachama katika Mkutano wao wa Kilele uliofanyika tarehe 29 na 30 Mei, 2005, jijini Dar es Salaam. Wakuu wa Nchi Wanachama waliipokea Ripoti husika na waliagiza kuwa wananchi washirikishwe kutoa maoni na mapendekezo yao juu ya kuharakisha au kutoharakisha kuundwa kwa Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki.

Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Kassim Issa kama ifuatavyo: Kama nilivyokwisha fafanua hapo juu mchakato uliokuwa unafanyika wa kukusanya maoni ya wananchi kuhusu hoja ya uharakishwaji au kutoharakisha Shirikisho la kisiasa ulifanyika katika nchi zote tatu, yaani Kenya, Uganda na Tanzania kwa wakati mmoja. Maoni ya wananchi ndiyo yanayotarajiwa kutoa mwelekeo kuhusu kasi na hatua gani zichukuliwe kuelekea Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, Uanachama wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ni wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama nchi moja. Kutokana na hali hiyo katika mchakato wa kukusanya maoni ya Wananchi, Tanzania inashiriki kama Taifa moja la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, uamuzi wa Serikali kuhusiana na hoja ya suala la kuharakisha au kutoharakisha Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki utatokana na maoni ya wananchi wote wa Tanzania kama Taifa moja.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia kwa karibu kuhusu ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahya Kassim Issa swali la nyongeza!

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:

Kwa kuwa Shirikisho hili linajumuisha baadhi ya mambo aliyoyataja kwamba ni ya Muungano; na kwa kuwa mpaka sasa kuna matatizo ambayo hayajakamilika kuhusu taratibu ya mambo yetu ya Muungano; je, ni nini hatima ya Zanzibar kutokana na Shirikisho hili?

Pili, kwa kuwa katika majadiliano yaliyojitokeza sehemu mbalimbali kutoka kwa Wabunge hadi Wawakilishi kwa Zanzibar imedhihirisha wazi kwamba na hawa ndiyo wawakilishi wa wananchi wa Tanzania nzima; na kwa kuwa katika maoni yaliyojitokeza ni kama suala hili limewawia vigumu kwa Watanzania kwa hivi sasa kama mapema kujiunga katika Shirikisho hilo.

Je, kama hivyo ndivyo huoni kwamba kufanya hivyo itakuwa hatari wakati inakwenda kinyume na maamuzi ya wananchi katika Tanzania hii?

**SPIKA:** La pili si sahihi kwa sababu hayo maamuzi bado hatujayapata, ndiyo maoni yanaendelea kukusanywa, lakini swali la kwanza la nyongeza Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI**: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyosema baadhi ya mambo ni ya Muungano. Katika masuala ya Ushirikiano kama anavyosema baadhi ya mambo ambayo yamekuwa yakijitokeza hapa na pale kuna Kamati Maalumu chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo ilikuwa ikiendelea kuyafanyia kazi na kadri yanavyojitokeza Kamati inaendelea kuyafanyia kazi na hiyo haiathiri chochote kuhusu ushiriki wetu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Niseme tu kwamba hatima ya Zanzibar katika Shirikisho la Afrika Mashariki kama nilivyosema ni kwamba Tanzania inashiriki katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kama Tanzania, kama kuna mambo yetu ndani ya Tanzania tunayazungumza kama Tanzania lakini tukienda kule tunakwenda kama Tanzania na kunakuwa hakuna tatizo lolote.

Mwisho, niseme kwamba Kamati iliyokuwa inakusanya maoni ndiyo kwanza inakamilisha ripoti yake, tusubiri hiyo ripoti iwe tayari na baada ya hapo tutaangalia tufanye nini kadri ya mawazo ya watu wengi yatakavyokuwa yamejitokeza kwenye ripoti hiyo.

**SPIKA:** Tuhamie Wizara ya Maji, swali linaulizwa na Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mbunge wa Kigamboni, kwa niaba yake Mheshimiwa Musa Azzan Zungu.

Na. 124

**Ukosefu wa Huduma ya Maji – Mjimwema**

**MHE. MUSA AZZAN ZUNGU (k.n.y. MHE. MWINCHOUM A. MSOMI**) aliuliza:

Kwa kuwa kwa muda mrefu sasa huduma ya maji katika Kata ya Mjimwema haipatikani baada ya kukatwa kwa umeme kutokana na malimbikizo ya madeni katika kisima cha Mtaa huo ambacho gharama zote ziko chini ya Ofisi ya Mhandisi wa Maji Mkoa wa Dar es Salaam; na kwa kuwa Rais Mstaafu Aboud Jumbe Mwinyi anaendelea kukitumia kisima hicho:

(a) Je, Serikali haioni kuwa inamdhalilisha Kiongozi Mstaafu kwa Jamii?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kulipa deni la umeme *TANESCO* ili umeme urudishwe na kisima kuanza kufanya kazi mara moja?

(c) Je, Wananchi wataishi bila majisafi na ya uhakika mpaka lini?

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Waziri wa Maji! Wakati unakwenda kujibu nimepokea karatasi kutoka Kambi ya Upinzani kwamba angalau wale wa CHADEMA wanavutiwa sana na vazi lako na la Mheshimiwa Anne Richard Lupembe. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mbunge wa Jimbo la Kigamboni, napenda kutoa maelezo yafuatayo:

Mheshimiwa Spika, visima vilivyochimbwa na Serikali wakati wa ukame wa mwaka 1997/1998 viligawanywa kwenye makundi matatu ya uendeshaji:

(i) Visima vilivyobaki chini ya uendeshaji wa *DAWASA* na kuwa sasa vinaendeshwa na *DAWASCO*;

(ii) Visima vilivyomilikishwa kwa Taasisi za mashule, zahanati na vituo vya afya.

(iii) Visima vilivyokabidhiwa kwa jumuiya za wananchi kuviendesha. Jumuiya hizi ni mitaaa na kata katika Manispaa za Kinondoni, Temeke na Ilala.

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Umilikishaji ulieleza bayana majukumu ya umiliki, yakiwa ni pamoja na kulipa gharama za umeme (au dizeli), ulinzi na matengenezo madogo madogo. Aidha, wamiliki walikasimiwa madaraka ya kukusanya pesa za mauzo ya maji.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye vipengele (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali haina nia ya kumdhalilisha Kiongozi Mstaafu, Mheshimiwa Aboud Jumbe Mwinyi kwa jamii kukosa maji. Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma inamhudumia Mzee wetu Aboud Jumbe Mwinyi kwa karibu zaidi kwa huduma mbalimbali na ikiwemo huduma ya maji na imemchimbia visima binafsi viwili vya kutumia Mzee wetu.

Kisima namba 170/97 kilichopo Mji Mwema, Kigamboni ambacho kinamhudumia Mstaafu huyo kilikabidhwa kwenye Uongozi wa Kata ya Mji Mwema ambacho kwa kusaidiana na Halmashauri ya Manispaa ya Temeke wamekuwa wakilipa ankara zake za umeme wakati *DAWASA/DAWASCO* wakitoa msada wa matengenzo makubwa pale yanapohitajika. Kisima hiki kiliharibika mwaka 2004 na pia kukatiwa umeme ambapo marekebisho yalifanyika mwaka 2006 na bili za umeme kulipwa, kwa sasa huduma imerejeshwa kama kawaida.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango wa kuongeza huduma ya majisafi na majitaka jijini Dar es Salaam na kwa sasa kupitia *DAWASA* inaendelea kutekeleza mradi

wa kulaza mabomba mapya kwa ajili ya kusambza maji kutoka mtambo wa Mtoni na Ruvu chini kuelekea Kigamboni na maeneo mbalimbali ya jiji la Dar es Salaam. *DAWASA* inatekeleza miradi chini ya mpango wa huduma za maji na usafiri wa mazingira kwa jamii (*CWSSP*) kwenye maeneo ya Maweni na Ungindoni.

Miradi hii iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji na inahusisha uchimbaji wa visima virefu, kulaza mabomba, kujenga matanki, kutoa elimu ya uendeshaji na usimamizi wa mradi. Ni matumaini yangu kuwa mara miradi hiyo miwili itakapokamilika itapunguza kero ya maji katika maeneo ya Kigamboni.

Serikali itaendelea na mipango yake ya kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji katika Jimbo la Kigamboni.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na mikakati mizuri ya maji ambayo ameieleza, naomba kujua ni lini mikakati hiyo ya mabomba ya maji itapita katika Jimbo la Ilala?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kufuatana na jibu langu la awali ni kwamba kwa sasa hivi miradi hiyo yote itahudumiwa; na kwa sasa kuna kampuni ya Kichina ambayo ni Kandarasi Tatu imeanza kushughulikia Miradi ya Maji na imeanza kulaza mabomba katika sehemu mbalimbali za Jiji za Dar es Salaam ikiwemo Kigamboni na Ilala. Kwa hali hiyo, nina imani kabisa kwamba baada ya muda katika utekelezaji huo na Ilala itafikiwa na maji yatafika kila sehemu ya Jiji la Dar es Salaam.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, navuta muda kidogo ili tumalize swali la mwisho kwa sababu hata hivyo kulikuwa na taarifa nyingi zilizotolewa ambazo zimetumia muda wa maswali. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma, majibu ya ziada…..!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika**,** kwa niaba ya Waziri wa Maji, napenda kumpongeza Naibu Waziri wa Maji na pia napenda kutoa maelezo ya nyongeza kutokana na swali la Mheshimiwa Mwinchoum.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwaomba wananchi wa Mji Mwema kuacha kutumia jina la Mheshimiwa Aboud Jumbe kwa kuwa tulishawaandikia barua mara nyingi kuwafahamisha kwamba hicho kisima Mheshimiwa Aboud Jumbe hakitumii na tumekwishamchimbia visima vyake kwa sasa. Lakini mara nyingi wamekuwa wakilitumia hilo jina kila wanapotaka kuepuka ulipaji wa bili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda kutoa kauli kwamba kwao kuendelea kutumia jina lake kila ambapo wanataka kukwepa bili ndiyo wanamdhalilisha

Mheshimiwa Aboud Jumbe. Kwa hiyo, nawaomba wananchi wa Kata ya Mji Mwema waache kabisa kutumia jina la Mheshimiwa Mstaafu Aboud Jumbe. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nina uhakika Mheshimiwa Waziri wamesikia.

**Na. 125**

**Mahitaji ya Gari la Majitaka Ziwani**

**MHE. MOHAMED RAJAB SOUD** Aliuliza:-

Kwa kuwa nyumba za Askari Polisi Ziwani '*Police Quarter'* pamoja na uchakavu wake pia kuna tatizo kubwa la miundombinu ya maji taka:-

Je, ni lini Serikali itawapatia gari la majitaka ili kuondoa tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Usalama wa Raia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, Mbunge wa Jang'ombe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba nyumba za askari Polisi katika Kambi ya Ziwani ni chakavu, na kwamba miundombinu ya majitaka hairidhishi.

Mheshimiwa Spika, Kambi hiyo ilijengwa wakati eneo hilo halina nyumba. Baadaye ikatokea kujengwa nyumba za raia kuizunguka kambi ya polisi bila kuzingatia mipango maalumu ya mji wa Zanzibar. Miundombinu hiyo ilijengwa kupeleka majitaka baharini moja kwa moja kukidhi mahitaji ya Kambi, lakini kwa sasa baada ya wananchi kujenga karibu na Kambi hiyo, majitaka kutoka nyumba jirani hutiririshwa katika miundombinu hiyo na kusababisha adha kwa askari wanaoishi hapo Kambini.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya uwezo mdogo wa bajeti yetu, Serikali haitaweza kununua gari la majitaka kwa ajili ya kusafisha majitaka katika kambi hiyo kwa sasa, lakini hali ya fedha ikiruhusu Serikali inaona umuhimu wa kufanya hivyo upo.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Baraza la Manispaa la Mji wa Zanzibar linaendelea kuifanyia ukarabati na kuisafisha miundombinu ya majitaka katika kambi hiyo ili kuondoa adha ya tatizo hilo. Ushauri wa Mheshimiwa Soud tumeupokea na pindi bajeti itakaporuhusu tutanunua gari la majitaka.

Aidha, Serikali kupitia Jeshi la Polisi ina mpango wa kujenga nyumba za polisi katika Kambi ya Ziwani ambapo tatizo la majitaka litakuwa limepatiwa ufumbuzi wa kudumu.

**MHE. MOHAMED R. SOUD:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini pamoja na majibu yake pembezoni mwa hiyo sehemu ya Bomani kulikuwa na mji unaitwa Matarubeta huko zamani sana, ulitangulia kabla ya kujengwa majengo ya Bomani. Lakini pia kuna tatizo ambalo limejitokeza na linasumbua zaidi nalo ni gari la majitaka. Pamoja na majibu yake namwomba aangalie zaidi umuhimu wa kupatikana gari la majitaka kutokana na usumbufu wanaopata hivi sasa; je, Mheshimiwa Naibu Waziri, anafikiria nini katika hilo kuwasaidia Askari hao waondokane na adha hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika swali langu la msingi kwamba tunalifahamu tatizo lililopo ni kubwa, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, lakini kwa sababu ya hali halisi ya uwezo wa kifedha kwa sasa Serikali kupitia Jeshi la Polisi haina uwezo wa kununua gari la majitaka. Pale ambapo tutakuwa na nguvu na uwezo wa kifedha basi jambo hilo tutalipa nafasi maalumu ili kuondoa tatizo katika Kambi hiyo. Lakini hata hivyo, kama nilivyosema kwamba tunajenga nyumba pale kwenye Kambi hiyo, na nyumba hizo tukizijenga tutatilia maanani suala zima la miundombinu ya majitaka ili kuhakikisha kwamba majitaka pale yanaondoka na liwe ni suala la kudumu.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali umepita. Sasa matangazo! Naanza na wageni, Mheshimiwa Hawa Ghasia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ameniomba niwatangaze wageni wake ambao ni binti zake, mmoja anaitwa Hina Ally na mwingine ni Nasra Yahya amemwita yeye ni kitindamimba kwa sasa anavyosema. Wako wapi sasa…? Tunaomba wasimame! *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni ambao ni wanafunzi 60 na walimu 19 kutoka shule ya msingi Irunda, Kiomboi ambao ni wageni wa Mheshimiwa Diana Chilolo na Mheshimiwa Mgana Msindai. Naomba wasimame pale walipo. Wanafunzi wa Irunda pamoja na walimu karibuni sana, mmependeza sana na sare zenu zina sweta nadhani kuna baridi huko. Ahsante. Karibuni sana! *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao wanafunzi ambao idadi haikutajwa, kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara *CBE* sijui ni wa Dar es Salaam au Dodoma! Naomba wasimame. Karibuni sana wasomi wetu na viongozi wa baadaye. Tunapenda mnapokuja kuangalia jinsi tunavyoendesha demokrasia hapa katika Bunge. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni kutoka Mkoa wa Tabora, Mheshimiwa Khadija Nkumba, ni Mheshimiwa Diwani wa Viti Maalum, Manispaa ya Tabora, naomba asimame, yule pale! Mgeni wa Mheshimiwa Siraju Kaboyonga. Yupo pia Mheshimiwa Furaha Hassan Ikunji, Diwani wa Manispaa ya Tabora. Ahsante, karibuni sana! *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, katika mlolongo huo nafurahi kumtambulisha Diwani Jaffari Kakila wa Kata ya Usisha, Jimbo la Urambo Mashariki. Usisha kwa kuwafahamisha tu ni moja ya zile ngome zangu kule katika Jimbo; na Diwani huyu ni mtu muhimu sana kwangu hasa kwa ajili ya mwaka 2010.

Naomba Diwani Jaffari Kakila uwasalimie sana ndugu zetu, Ilani ya Uchaguzi inatekelezwa, barabara ya kutoka Usisha-Mabundulu shilingi milioni 25 za *TASAF* zimekwenda. Sekondari ya Usisha tayari, mradi wa maji Katunguru tumekwishapata fedha za Marekani. Kwa kweli sidhani kama unaona watu wanapita wapite huko! Ahsanteni sana. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, ameniomba nitangaze kuwa leo saa 7.00 kutakuwa na kikao cha Kamati ya Kilimo na Ardhi, Chumba Namba 227.

Mheshimiwa Alhaj Mohamed Missanga, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, ameniomba nitangaze kwamba saa 7.00 leo kutakuwa na Mkutano wa Kamati katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Nadhani wanakutana na baadhi ya watu ambao ni wadau na kadhalika, ndiyo maana wamehitaji ukumbi mkubwa.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2007/2008 - Ofisi ya Waziri Mkuu na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

*(Majadiliano Yanaendelea)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, napenda kwanza kuunga mkono hoja. Pili, nampongeza mtoa hoja

Tatu, napenda nitumie wasaa huu kuishauri Serikali iangalie upya sheria za usalama wa barabarani.

Mheshimiwa Spika, mimi nakerwa sana na magari hasa daladala, *hiace* na *pick ups/*malori ambayo yamefunga ngao kwenye magari yao.

Mheshimiwa Spika, magari yenye ngao za mbele na nyuma zina vurugu sana barabarani, waendesha magari wana tabia ya kuchomekea magari mengine bila utaratibu kwa kuwa wanajua ngao zao zitavunja gari lingine na yeye mwenye ngao anabaki bila kudhurika.

Mheshimiwa Spika, ngao hizo kwanza ni pana sana kuzidi upana wa kawaida wa gari kusika hali inayompa nguvu mwendeshaji mkorofi kukwangua wenzake barabarani.

Mheshimiwa Spika, ngao hizo pia zimechomelewa misumari ama mikuki kitu ambacho ni hatari kwa magari mengine. Pamoja na mengine muhimu yatakayozingatiwa katika kuboresha usalama barabarani, naiomba Serikali ipige marufuku ufungaji wa ngao kwenye magari yote nchini, hii itakuwa ni *fair game* barabarani. Hakuna atakayetumia vurugu kwa imani ya kinga ya ngao yake.

Mheshimiwa Spika, naiomba pia Serikali iweke msisitizo wa mabasi yote ya abiria kuhakikisha yanakuwa na mlango wa dharura. Mabasi mengi hayana milango, yamezibwa kabisa nyuma na mlango huo umechomelewa mabati ambayo hayana usalama hata kwa mwendeshaji na abiria hawaoni nyuma yao kuna nini.

Mheshimiwa Spika, nimesikia wakuu wa usalama barabarani katika Mikoa mbalimbali wasisitize magari yawe na mlango wa dharura, lakini sijasikia amri ya kuwapa siku au muda wa kuwa wametekeleza agizo hilo. Hii si jambo la utashi, nashauri Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa nafasi yake avalie njuga.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nimpongeze Waziri Mkuu wa hatua mbalimbali ambazo amezichukua na zimesaidia sana kuboresha maisha ya Watanzania. Pongezi ziiendee Serikali yetu, hasa kwa ujenzi wa shule za sekondari, uboreshaji wa posho za Madiwani na kuamsha pesa za kusaidia maendeleo ya majimbo na mengine mengi.

Mheshimiwa Spika, mwisho naitakia heri hoja hii ipite kwa kauli moja na Mungu awape afya njema. Ahsante sana.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Wilaya na Jimbo la Siha kutoa pole kwako, Serikali na ndugu, jamaa na marafiki wa Marehemu Amina Chifupa kwa msiba uliotukumba tukiwa hapa duniani, Bwana ametoa na Bwana ametwaa, jina la Bwana lihimidiwe.

Pili, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba nzuri aliyoitoa wakati akiwasilisha Makisio ya Wizara yake.

Mheshimiwa Spika, kipekee, napenda kuishukuru Serikali kwa kukubali kuunda Halmashauri 11 ambazo miongoni mwake imo Halmashauri ya Wilaya ya Siha. Wananchi wa Wilaya hii mpya wamenituma niseme ahsante sana kwa Serikali yetu ambayo inaoongozwa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. Kwa namna ya kipekee ya kulipa fadhila kwa Rais wetu ni kutoa kila aina ya ushirikiano kwa Serikali kwa kutekeleza yale yote ambayo anayatoa kama maelekezo kwetu.

Aidha, tunatambua kwamba Serikali kutukubalia kuwa na Halmashauri ya Wilaya ya Siha, tunafanya uamuzi wa wananchi kuwa na fursa ya kujiamulia mambo yao wenyewe bila kuhitaji kusubiri maamuzi ya Makao Makuu ya Mkoa na yale ya *centre* kwa taratibu ambazo zimewekwa. Utaratibu wa *D and D* ni ushahidi wa kutosha

kuonyesha nia njema ya Serikali ya kutoa madaraka zaidi kwa wananchi katika kujiletea maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la lisilopingika kwamba kwa kukubali kuanzishwa Halmashauri 11 za Wilaya ikiwemo ile ya Siha tunasukuma na kuharakisha maendeleo ya wananchi kama alivyoainisha Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri Mkuu na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, jambo hili linafurahisha zaidi Serikali Kuu inapojipunguzia majukumu yake kwa kupeleka majukumu hayo katika Halmashauri zake za Wilaya kupitia Wizara za TAMISEMI, Kilimo, Chakula na Ushirika, Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Miundombinu, Afya na kadhalika. Naamini mkakati huu utazaa matunda ya haraka na hivyo kuleta mapinduzi ya hali ya juu katika maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa ya viongozi na wawakilishi wa wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha na zile nyingine 10 itakuwa ni kuharakisha tunaweka mipango mizuri ambayo itatafsiri kwa vitendo ndoto/malengo na nia waliyokuwa nayo wakati wanaomba kuwa Wilaya mpya ya Siha. Miradi yetu lazima ifanane na matatizo tuliyonayo katika Wilaya mpya ya Siha. Kipaumbele chetu kwa sasa na kama ilivyo kwa nchi nzima ni elimu ikifuatiwa na hifadhi ya mazingira katika maeneo yote ambayo uharibifu mkubwa umefanyika. Afya ni eneo lingine ambalo tutalipa kipaumbele kwa sababu jamii yetu hasa ile ya wafugaji imebaki nyuma katika huduma mbalimbali ikiwemo afya, zahanati kwa kila kijiji ni lengo ambalo litatuondolea matatizo ya afya.

Kwa kifupi, sisi wananchi wa Wilaya mpya ya Siha tunaipokea Halmashauri mpya ya Siha kama changamoto ya hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo chetu lazima kibadilike ili kuweza kuleta tija na kuongeza mapato ya Halmashauri yetu. Ni hivyo hivyo, hata kwa mifugo yetu.

Kuhusu sayansi na teknolojia ya kisasa ni nyenzo muhimu ambayo tutaitumia katika kuleta mapinduzi ya kilimo Wilayani Siha. Hii ina maana kuwa tutahimiza kilimo cha umwagiliaji na huduma za ugani ili kuleta mapinduzi ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa mara nyingine nirudie kutoa ahsante za wananchi wa Siha na kwamba naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri Mkuu.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, ujenzi wa ofisi ya Mbunge, Itigi. Kama Mbunge wa Manyoni Magharibi sina ofisi Jimboni kwangu, Makao Makuu ya Jimbo yapo Mjini Itigi lakini imetengwa ofisi Manyoni katika Jimbo la Mashariki. Hii inaniletea usumbufu wa gharama kubwa na kunifanya niwe nje ya Jimbo. Sina nyumba ya kulala Manyoni, nalazimika kufikia nyumba ya kulala wageni.

Mheshimiwa Spika, nilishaliweka wazi suala hili kuelezea ni kwa nini nipewe kipaumbele kujengewa ofisi Itigi. Ombi langu, naomba Serikali itenge fungu kwa ajili ya

ujenzi wa ofisi ya Mbunge, Itigi katika Jimbo la Manyoni Magharibi ambalo Mbunge atakuwa karibu zaidi na wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mgogoro wa mpaka wa Kalangali, malalamiko ya wananchi ni kwamba upimaji wa eneo la Kalangali ulifanywa na wataalamu waliopendelea upande mmoja, upande wa Sikonge kwa misingi ya ukabila. Makao Makuu ya Mpima Ramani, Bwana Masesa, Mkoa, Ofisi ya Ardhi, Bwana Fumbuka, Wilaya Ofisi ya Ardhi, Bwana Masanja. Mpakani pale Kalangali kiongozi wa jadi, *Chief* Masanja. Ni kutokana na malalamiko haya tuliiomba Serikali ichukue hatua na ahadi ilitolewa kuwa *UCLAS* wangekuja kupima upya kama *independent body.* Haya tuliarifiwa na Mheshimiwa Celina Kombani, Naibu Waziri wa TAMISEMI, mpaka sasa hakuna hatua ya *UCLAS* kuja kupima maeneo hayo na tayari kumetokea watu kupigana.

Mheshimiwa Spika, enelo la Kalangali na hata Kiyombo ya sasa ni maeneo ya jadi ya Wilaya ya Manyoni. Kiyombo ya zamani ilivunjwa wakati operesheni vijiji ya mwaka 1974/1975 watu wake walisambaa na baadaye walikusanya na kuingia ardhi ya Manyoni na kuanzisha Kiyombo mpya. Ombi langu, naomba *UCLAS* waje haraka wapime maeneo hayo.

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mheshimiwa Spika, naomba kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Bububu kutoa salamu za rambirambi kufuatia kifo cha Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Amina Hamis Chifupa, Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi, *Amin!*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la msongamano wa magari Jijini Dar es Salaam. Nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ubunifu wake alioufanya kwa hatua ya kujaribu kupunguza msongamano wa magari Jijini Dar es Salaam. Aidha, naipongeza Serikali kwa hatua zake inazozichukua kwa upanuzi wa barabara Jijini humo kwa madhumuni ya kukidhi haya ya usafiri.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ongezeko la magari Jijini Dar es Salaam hauendani sawia na mtandao wa barabara ambazo kwa wakati ule zinajengwa zilizingatia magari machache tu na yenye ujazo mdogo, ninashauri kama ifuatavyo:-

(i) Serikali iandae *master plan* ya Jiji lote kwa ajili ya kuboresha barabara na reli *(city train)* ili kuondoa usumbufu kwa wakazi wa Jiji la Dar es Salaam baada ya ukamilishaji wa ujenzi wa miundombinu kwa kuzingatia *master plan* hiyo.

(ii) Kwa kuwa moja ya matatizo makubwa yanayosababisha kuwepo hasa msongamano wa magari jijini ni kwenye makutano ya barabara *(road junctions),* Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu ichukue hatua za makusudi za kujenga *fly overs* kwenye makutano ya barabara. Hii itasaidia sana kupunguza kwa kiasi kikubwa *traffic jams.*

(iii) Serikali ichukue hatua za makusudi ya kuanzisha miji midogo pembezoni mwa Jiji la Dar es Salaam ikiwa ni pamoja na ujenzi wa ofisi za Serikali pamoja na huduma za jamii kama vile shule za msingi, sekondari, vyuo, hospitali, *super markets* na kadhalika. Hii itasaidia kwa kiwango kikubwa kupunguza msongamano wa magari ambapo wananchi wengi watakuwa hawafuati huduma tena jijini kama ilivyo sasa.

(iv) Serikali ianze sasa kufikiria kuanzishwa kwa usafiri wa kutumia *city train* katika maeneo ambayo wananchi wengi wanaishi kwa mfano, Ubungo, Gongo la Mboto na kadhalika.

(v) Serikali iliwezesha Shirika la *UDA* kwa kulipa mtaji wa kununulia mabasi makubwa kama yale ya miaka ya 1970 na kuondoa magari madogo ya daladala ambayo uwezo wa kuchukua watu wengi ni mdogo.

Mheshimiwa Spika, suala la Mfuko wa Mikopo wa Elimu ya Juu, suala hili limekuwa likipigiwa kelele sana na wanafunzi, je, Serikali ina mipango gani ya kulitatua suala hili ili kutoa nafasi nyingi kwa wanafunzi kwenye vyuo mbalimbali nchini. Hivi ni kwa nini mabenki yetu hayashirikishwi kutoa mikopo hiyo ili hata wale wanaofaulu katika daraja la tatu na la pili waweze kupata nafasi hizo? Ni matumaini yangu kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ataliangalia hilo.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naiunga mkono kwa asilimia mia moja.

**MHE. ALI JUMA HAJI:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii nami kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Chaani kuungana na wenzangu katika kutoa mkono wa pole kwa wafiwa wote wa Marehemu Mheshimiwa Amina Chifupa na kumuombea Marehemu Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema peponi, *Amin!*

Mheshimiwa Spika, baada ya rambirambi sasa niende kwenye hotuba. Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake ambayo kwa kweli imejitosheleza yenyewe. Napenda pia nichukue fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri pamoja na watendaji wote ambao kwa namna moja au nyingine wametoa mchango wao wa hali na mali katika kuiandaa hotuba hii hadi kufikia Mheshimiwa Waziri Mkuu kuiwasilisha mbele ya Bunge hili Tukufu. Wote nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo sasa nianze mchango wangu kwenye suala la barabara.

Mheshimiwa Spika, ni juzi tu Bunge lako hili limepitisha Bajeti ya Serikali ambayo imepandisha bei ya mafuta kwa kiwango kidogo tu pamoja na ushuru wa magari kwa ajili ya kupata fedha ili tuweze kujenga barabara zetu

ambazo nyingi zao ziko katika hali mbaya ili ziweze kupitika kirahisi na kwa usalama zaidi.

Mheshimiwa Spika, hili sio jambo baya hata kidogo kama vile ulivyolalamikiwa na wenzetu wa upande wa upinzani.

Mheshimiwa Spika, nasema hili ni jambo jema sana kwani bila kufanya hivyo tutapata vipi fedha za kutosha kutokana na vyanzio vyetu vya mapato vya ndani?

Mheshimiwa Spika, ni lazima kwanza tujitahidi sisi wenyewe kutafuta fedha za ndani na baadaye ndiyo tuombe misaada ya kuongezea.

Mheshimiwa Spika, nasema tena hili ni jambo jema sana kwani iwapo barabara zetu zitajengwa vizuri ni wazi zitaleta changamoto kubwa kwa wawekezaji na hata wakulima wetu watakuwa na mori kubwa ya kulima kwani watakuwa na uhakika wa kusafirisha mazao yao mara baada ya mavuno yao bila ya kuwaharikibia njiani kutokana na ubovu wa barabara.

Mheshimiwa Spika, sasa hapa namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa vile yeye ndiye msimamizi mkuu wa shughuli za Serikali awe mkali sana katika kulisimamia suala hili la ujenzi wa barabara ili hapo baadaye wananchi wetu wajionee wenyewe kwamba ni kweli Serikali yao ya awamu ya nne ilikuwa na msimamo madhubuti na wa uhakika juu ya ongezeko hilo la bei ya mafuta na ndipo hapo tena wapinzani wetu na wenyewe wataona umuhimu wa jambo hili.

Mheshimiwa Spika, nasema tukaze kamba tujenge barabara na maendeleo mengine mengi yatajileta yenyewe.

Mheshimiwa Spika, sasa nigusie suala la Halmashauri zetu. Hivi sasa Serikali Kuu imeanzisha utaratibu wa kuzinyima ruzuku kila Halmashauri iliyopata hati chafu wakati wa ukaguzi wa mahesabu kwa utendaji mbaya kutokana na ubadhilifu na ufujaji wa fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, mimi kwa mawazo yangu naona utaratibu huu siyo mzuri na si wa busara kwa sababu kuinyima fedha za ruzuku Halmashauri iliyopata hati chafu ni kutowatendea haki wananchi wa Halmashauri hiyo ambao wenyewe hawana hatia na kuwakosesha maendeleo yao kwa kosa la watendaji wachache wasio waaminifu. Jambo la msingi ni kuwachukulia hatua kali za kisheria mtendaji yeyote akiwa Mhasibu, Mkurugenzi ama mwingine yeyote atakayebainika kufanya ubadhilifu huo badala ya kuiadhibu Halmashauri nzima na kuwakosesha fedha za maendenelo wananchi vinginevyo itakuwa ni sawa na mchungaji kumpiga bakora ng'ombe wa nyuma wakati anayechelewesha msafara ni ng'ombe wa mbele.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba nizungumzie suala la unyanyasaji wa kijinsia.

Mheshimiwa Spika, hapa nagusia katika baadhi ya koo zinazowanyanyasa wanawake waliofiwa na waume zao na watoto waliofiwa na baba zao. Kwa kweli jambo hili linatia uchungu mkubwa sana. Kabla sijaelezea hali ya unyanyasaji huo naomba kwanza niwapongeze wasanii wote wanaoendeleza michezo yao kuigiza. Wasanii hawa wanatuonyesha baadhi ya michezo yao ambayo inaelimisha ama kuonyesha jinsi gani mwanamke na watoto wanavyonyanyaswa mara baada ya mume kufariki.

Mheshimiwa Spika, nichukue mfano wa mchezo mmoja wa kuigiza uitwao Hatia. Katika mchezo huu yupo mzee mmoja anaitwa Ngirisho kwa jina la mchezo, mzee huyu ameonyesha kumtesa shemeji yake ambaye ni mke wa Marehemu kaka yake na kumdhalilisha vibaya sana na kudiriki hata kumwambia hana haki ya jambo lolote aliloacha mumewe.

Mheshimiwa Spika, sina haja ya kuelezea mchezo huu, lakini kama hali ile iliyoonyeshwa kwenye mchezo ule, ipo kweli katika jamii zetu za Tanzania, basi nimuombe Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali kwa jumla kuweka sheria kali sana dhidi ya watu wote wenye tabia ya kuwanyanyasa wanawake na watoto waliofiwa na wazazi na waume zao. Tena niombe sheria hiyo ifanyiwe kazi kwa nguvu zote kama vile inavyofanyiwa kazi sheria ya ubakaji na ukeketaji na hili nalo lifanyiwe kazi. Wanateseka sana watoto na wanawake wanaofiwa na waume zao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja asilimia mia moja. Ahsante sana.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Spika, Serikali haikuonyesha umakini katika suala la kupambana na UKIMWI na dawa za kulevya, fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya ya kupambana na UKIMWI ni za wafadhili hatuna hata senti moja ya fedha za ndani. Hali hii inasikitisha. Ni vema Serikali ikatenga fedha za ndani kwa ajili ya gonjwa hili.

Mheshimiwa Spika, Serikali haikufanya utafiti wa kutosha katika zoezi la kuwahamisha wafugaji kutoka bonde la Ihefu, Mbarali wafugaji wengi wamepoteza familia zao ikiwa ni pamoja na wanawake na watoto. Wengine wamepoteza mifugo yao mingi kwa kufa wakati wa safari kutokana na ugonjwa na matatizo mengine.

Mheshimiwa Spika, Serikali iongeze juhudi zake za kupambana na rushwa hapa nchini katika taasisi zake zote kuanzia ngazi za vijiji hadi Serikali Kuu.

**MHE. STEPHEN J. GALINONA:** Mheshimiwa Spika, nimekwisha unga mkono hoja hii lakini kwa ufinyu wa muda nilibakiza *point* zifuatazo wakati nikichangia kwa kauli.

Kwanza, naomba kukumbusha ombi la Wilaya ya Iringa la kugawa Kata mbili kubwa zenye Vijiji 10 kila moja, nazo ni Magolilwa igawanywe itokee Kata mpya ya Luhota, Mgama igawanywe itokee Kata mpya ya Lyamugungwe. Mapendekezo yako TAMISEMI tangu mwaka 2004.

Kuhusu Kamati za Halmashauri, Kifungu cha 74 cha Sheria ya SM kinaunda Kamati za Kudumu tatu/nne ambazo Wenyeviti wake huingia katika Kamati muhimu ya Fedha, Mipango na Utawala. Kisha zipo Kamati zisizozidi tatu zinazoundwa chini ya Kifungu cha 74(2) ambazo Wenyeviti wake siyo Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Mipango na Utawala nashauri tuondoe ubaguzi na uonevu huu ili Wenyeviti wote waingie katika Kamati ya Fedha, Mipango na Utawala.

Kifungu cha 78(1) kinakasimu shughuli kadhaa kwa Kamati mbalimbali isipokuwa zile zilizoainishwa katika Kifungu kidogo cha 2. Lakini Kanuni Na. 40 inapingana na Kifungu hicho kwamba hakuna *delegation* iliyofanyika kama inavyoelekea kuwa kule Iringa.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwangu kwamba utekelezaji wa maamuzi ya Kamati utachelewa ikizingatiwa kwamba Baraza hukutanika mara moja tu katika miezi mitatu. Nashauri utaratibu huo uhuishwe kwa lengo la kuharakisha utekelezaji kulingana na dhana ya kasi mpya.

Mwisho, kwa mara nyingine tena naunga mkono hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu na ninawatakia kila la kheri wote katika ofisi hiyo.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya hotuba ya Waziri Mkuu kimaandishi. Awali kabisa napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake iliyozigusa sekta zote. hotuba hii imetuonyesha jinsi Serikali yetu inavyotekeleza Ilani na Sera za Chama cha Mapinduzi kwa awamu. Tujipe moyo tutafika tu, bora tusimamene imara na kuendelea na mipango yetu ya utekelezaji kwa umakini kama ambavyo Serikali imekwishaanza.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa mikakati mingi mizuri ya maendeleo ambayo imeandaa katika sekta zote na mingine imeanza kutekelezwa. Mikakati kwa upande wa kilimo nimeguswa na *ASDP,* Miundombinu ya maendeleo ya ujenzi wa barabara, ukarabati wa hospitali, ujenzi wa shule na vyumba vya madarasa kwa ushirika wa Serikali, *TASAF* na wananchi, programu ya maji na mengine mengi.

Mheshimiwa Spika, nianzie na barabara ya Kibiti - Lindi maeneo ya Ndungu - Somanga. Kwa kweli hili eneo limekuwa kero kubwa kwa kipindi cha kuanzia Novemba hadi Mei. Kipindi hiki kimekuwa ni cha matatizo makubwa kwani husababisha abiria kulala porini mara kwa mara kwa siku kadhaa. Kweli hii ni shida kubwa hasa kwa

akinamama na watoto. Naomba Serikali iwe na usimamizi wa karibu kwa maeneo haya hata hapo mkandarasi atakapokuwa amefanya ukarabati wa kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kilimo *(ASDP)*. Mpango huu wa maendeleo ya kilimo ni mzuri sana na itawainua wananchi wengi kiuchumi. Ninachopenda kuongezea hapa ni kuwaomba wahusika wa mpango huu wazingatie kutoa *package* nzima kwa kila mradi ili kuhakikisha kuwa vikwazo vinaondolewa na miradi inakuwa endelevu. Kwa mfano, mradi wa ufugaji uzingatie maswala ya kuwepo zizi bora na dawa.

Mheshimiwa spika, mradi wa ghala la kuhifadhi mazao kama ya nafaka, uzingatiwe kuwa kuna wakati kijiji husika kinaweza kisipate mavuno ya kutosha hivyo wanaweza kuhitaji fedha (mkopo) wa kununua nafaka kutoka maeneo jirani yaliyopata mavuno mazuri. Kwa wakulima wa korosho, zikitolewa mashine za kubangulia ni vizuri ikatolewa seti nzima kwa ajili ya uchakataji. Kimsingi wananchi hushirikishwa kuibua miradi lakini ingekuwa ya jinsi ya kuiwezesha miradi kuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, watendaji wa Mitaa na Kata katika maeneo mengi Mkoani Mtwara hawana ofisi zinazoeleweka, wengine hutumia magofu yanayovuja na wakati mwingine kuhama kipindi cha mvua. Tatizo hili husababisha uharibifu wa nyaraka muhimu. Je, Serikali ina mpango gani juu ya suala hili?

Mheshimiwa Spika, Madiwani wakiwezeshwa wanaweza kufanya kazi nzuri zaidi na kuimarisha ushirikiano na Serikali. Hivyo, niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuiomba Serikali, pamoja na kuwaongezea kiasi cha posho iwakopeshe usafiri angalau wa pikipiki.

Mheshimiwa Spika, taa za barabarani ni muhimu kwa manispaa zetu. Halmashauri ya Mtwara kama Manispaa kwa sasa inalo hitaji kubwa la taa za barabarani ili kusaidia wakati wa usiku hasa ziweze kupunguza uhalifu utokanao na vijana wajiitao tukale wapi.

Mheshimiwa Spika, nimalizie na suala la vifo vingi vya uzazi ambavyo taarifa zake hazifiki hospitalini. Vifo hivi hutokea majumbani na kutotambulika kwake husababisha takwimu kuwa za chini kuliko hata ule wastani wa Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri ni Wilaya ya Tandahimba ambapo 70% ya vifo vya uzazi havitolewi taarifa. Ningependa kujua Serikali ina mpango gani juu ya suala hili? Kweli tatizo hili ni kubwa na huchangia umaskini na kuongeza tatizo la watoto waliopo katika mazingira magumu. Tafadhali Serikali iliangalie hili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Spika, mimi ni Mbunge wa Jimbo la uchaguzi la Moshi Mjini tokea Chama cha CHADEMA. Soko la mtumba la Kiboroloni liko katika Kata ya Kiboriloni ambayo kuanzia Serikali ya Kata, Diwani na Mbunge inaongozwa na CHADEMA tangu mwaka 2000.

Hili soko lina historia ndefu na ni maarufu sio hapa Tanzania peke yake, bali hata nchi jirani zinalitegemea. Ujenzi wa mji mdogo wa Kiboriloni ambao unakua haraka sana, umejengwa kukidhi mahitaji ya soko, yaani nyumba zote ni magodauni, maduka, migabawa, *guest houses,* vyoo na *facility* zote zinazohitajika kwenye soko kubwa kama hili. Baada ya kulifunga *infrastracture* yote ya Kiboriloni imebakia bila kazi. Cha kushangaza, wenye ma-*godown,* hawaruhusiwi kuweka mitumba, wala kuuza mitumba. Wananchi wa Kiboriloni wamerudishwa kwenye lindi la umaskini bila sababu.

Mheshimiwa Spika, katika utawala wa sheria, wananchi walipaswa kushirikishwa katika maamuzi makubwa kama haya yanayogusa maisha ya watu, lakini hawakushirikishwa. Mimi nikiwa Mbunge, pia ni Diwani na maamuzi tuliyopitisha katika Halmashauri ya Manispaa ya Moshi ni kuondoa wafanyabiashara ndogo ndogo (Wamachinga) wanaofanya biashara zao barabarani na tuliamua kuanzia katikati ya mji na sio kata za pembezoni. Hata siku moja haijawahi kuletwa mbele ya *Council* hoja ya kulifunga soko la mitumba la Kiboriloni.

Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara wa Kiboriloni, wamekuwa mbele sana kutoa michango ya maendeleo katika Kata ya Kiboriloni. Kwa kipindi cha tangu mwaka 2000 mpaka sasa, wamechangia ujenzi wa sekondari ya Kata, ambayo ilikuwa ya kwanza katika Manispaa ya Moshi, *primary schools* mbili na ukarabati wa barabara za Kiboriloni. Sasa tulikuwa na mpango wa upanuzi wa *secondary school* ili iwe *high school.* Kilio cha wana Kiboriloni ni kuwa kufunga soko la Kiboriloni kutaathiri maendeleo yote ya Kata hii. Kuhamishiwa soko hili *Memoriam,* ni kwa muda na hakuna sehemu maalumu iliyotengwa kwa ajili ya soko hili. Kiwanja cha *Memoriam,* ni kiwanja cha michezo na kukifanya soko ni kinyume kabisa na nia ya Mheshimiwa Raisi wetu wa kufufua michezo Moshi Manispaa. Pia inakuwa ni kichekesho kwa kuwa Manispaa imekwishaandika andiko na kuliuza kwa wafadhili kutafuta mwekezaji kujenga kiwanja hicho kwa hadhi ya Kimataifa, soko la Kiboriloni lina wafanyabiashara 800, na siku ya siku ina wateja zaidi ya 5000.

Mheshimiwa Spika, viongozi wote tumeapa kwa kutumia Katiba ya nchi yetu, kuwatumikia wananchi wote bila kujali itikadi zao na kuhakikisha haki inatendeka. Kisa cha kuhamisha soko la Kiboriloni ni la kisiasa na sio la kimaendeleo. Kata hii ni ngome ya CHADEMA kwa kuwa mimi Mbunge natoka hapo na ni msemo unaosemwa na viongozi wa CCM kuwa kuvunja nguvu za CHADEMA ni kuvuruga shuhuli za uchumi. Ili tuweze kummaliza Ndesamburo kisiasa, ni kuiua Kiboriloni kwani viongozi hao wanadhani Kiboriloni ndio inampa nguvu kushinda chaguzi za Ubunge. Hii ni zana potofu na inazidi kukiangamiza chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara wote wa Kiboriloni na Moshi kwa ujumla wao wamenituma, kwa unyenyekevu mkubwa, kumpigia magoti Waziri Mkuu, awaonee huruma na kuliangalia tatizo hili kwa moyo wa huruma kwani familia zaidi ya watu 15,000 wanaadhirika kwa kitendo hiki cha kufunga soko la Kiboriloni kwa misingi ya siasa bila kutizama kiuchumi. Mheshimiwa Waziri Mkuu zoezi la kufunga soko hili

lilifanyika saa nane za usiku bila wahusika kuwepo na mali za mamilioni ziliangamizwa na polisi.

Mheshimiwa Spika, sina matatizo na Bajeti ya Waziri Mkuu, nilichotaka kuwasilisha ni kilio cha wana Kiboriloni wanaoonewa bila sababu za msingi bali kwa misingi ya itikadi. Kwa sasa wanangojea kwa hamu kubwa kurudia tena maisha yao ambayo kwa sasa yamekatishwa.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Spika, naomba nami nipate nafasi ya kuchangia kimaandishi ili kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Kwanza nikubaliane na hoja hiyo kwa sababu ni hoja ambayo imegusa maeneo mengi yanayowagusa wananchi. Kuhusu kipengele kinachohusu dawa za kulevya, naishauri Serikali kwa makusudi mazima iandae operesheni ya kuwatambua na kuwakamata wote wanaohusika na hatimaye kuchukuliwa hatua kali ambayo itakuwa ni fundisho kwa wenye tabia hiyo. Tunapozungumzia dawa za kulevya, tunazungumzia yale yanayotoka nje ya nchi na yale ambayo yanatoka humu nchini. Kwa haya ya nchini ni pamoja na bangi ambayo inalimwa na wananchi wanaofahamika. Nao ni vema pia wasakwe na kisha kuchukuliwa hatua. Mara nyingi vijana ambao wamekuwa wakikamatwa kuhusika kuingiza dawa za kulevya kutoka Pakistani, wamekuwa wakiachiwa huru baada ya ndugu zao kuwawekea dhamana.

Nikizungumzia kuhusu ufujaji wa fedha za Serikali na hasa zile za Halmashauri ambazo zimekuwa zikiibiwa kinyume na taratibu, ni kwamba wapo watumishi ambao wamekaa kituo kimoja kwa muda mrefu na uzoefu wao huo kuingilia kwenye matumizi mabaya ya fedha. Lipo tatizo kuhusu barabara za vijijini kutokutengenezeka kutokana na Halmashauri kukosa fedha. Ni kwa mantiki hiyo wananchi wanashindwa kupitisha ama kusafirisha mazao yao hadi kwenye soko.

Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ilizungumzia wafugaji. Lipo tatizo kubwa ambalo limekuja kujitokeza kwamba mbali na wafugaji hao kutokuwa na elimu lakini pia maeneo mengine wanakopelekewa mifugo, ni maeneo ambayo huwa hayafai kwa mifugo. Wakati mwingine mifugo inakufa. Kwa mfano wafugaji wa ng'ombe ambao wana asili ya kufuga wapatao 6000 nahangaishwa na mifugo yao ipatayo 30000 kwa kuwapeleka mahali ambapo majani yaliyopo ni sumu na kusababisha ng'ombe kufa.

Baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia zote.

**MHE. HEMED MOHAMMED HEMED:** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa mimi ruhusa ya kutoa maoni yangu katika hotuba hii iliyo mbele yetu.

Pia nimshukuru Waziri Mkuu kwa umahiri wake katika kuisoma hotuba hii. Pamoja na kukamilika mema katika hotuba hiyo, pamoja na hayo nami ni vyema nitoe mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, nianze na miundombinu, katika Jiji la Dar es Salaam, inaeleweka kwamba walio wengi wanakimbilia Jiji la Dar es Salaam hivyo ni kuufanya mji huo uwe na ongezeko la watu kila dakika. Sababu kuu zipo, kwanza ni mkoa peke unaoongoza kiuchumi na ofisi nyingi za Serikali kuwepo Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na sababu hizi, ndio sababu ya barabara kuwa chache na kupatikana kwa msongomano wa magari, jambo ambalo hupelekea ajali. Hivyo basi ni lini Serikali itatatua tatizo hili?

Mheshimiwa Spika, kuhusu biashara haramu, ongezeko la rushwa kila leo linaongezeka kwa kasi. Mtazamo wangu, mimi rushwa inachangiwa na ukosefu wa huduma kwa wananchi. Hivyo basi ni vyema Serikali iweke maeneo mengi yatakayomwezesha mwananchi kupata huduma kiurahisi, kwa kufanya hivi tutaweza kupunguza rushwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu dawa za kulevya, vijana ambao ni nguvu kazi ya nchi yetu wanaathirika sana kutokana na dawa hizi. Tujiulize, nchi yetu ina mipaka na kila eneo hili lina taasisi ya kuchunguza mabaya yote yasiingie nchini. Tuna bandari ya nyanja za kutulia ndege yaani *Airport.* Nia ni moja kunusuru nchi. Serikali iko wapi hata dawa hizi zinaingia ndani ya nchi yetu na kuhatarisha maisha ya vijana wetu? La kusikitisha dawa zinaingizwa nchini na baadhi yake zimekamatwa lakini aliyeleta dawa hizo hajulikani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo kuwa ni uti wa mgongo wa nchi yetu, sioni juhudi za Serikali kuwapa motisha wakulima wetu, mkulima ndio anainusuru nchi na balaa la njaa ndiye wa chini katika nchi yetu. Hii leo wakulima mazao yao hayana soko na sasa wanalazimika kuuza kwa bei duni. Ni lini Serikali itatatua suala hili? Ahsante.

**MHE. USSI AMME PANDU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nataka kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa juhudi zake anazozichukua katika Wizara hii ili kuona wananchi wa nchi hii wanaishi na kupata huduma zote muhimu kwa lengo la kufikia ile Sera ya Chama Tawala kuona kuwa maisha bora kwa kila Mtanzania inawezekana.

Mheshimiwa Spika, shughuli za Bunge, ukurasa wa 8 wa kitabu hiki unazungumzia shughuli za Bunge kwamba Serikali itaendelea kwa awamu kwa Waheshimiwa Wabunge kujengewa ofisi zenye hadhi kwenye majimbo yao. Hiki ni kitendo cha kupongezwa sana na tunaomba pamoja na kujenga ofisi 40 kwa awamu ya kwanza na majimbo ya Zanzibar naomba sana yapatiwe ofisi kwani hatuna ofisi majimboni, aidha, naipongeza Serikali kwa kuanzisha mfuko wa maendeleo ya jimbo ambao utawezesha kuleta maendeleo zaidi, lakini pia kuonekana kwa ile ari mpya nguvu mpya na kasi mpya kwa Serikali ya Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara za Serikali za Mitaa, ukurasa wa 19 Serikali inaendelea kuboresha mtandao wa barabara, naomba nipongeze sana kwa hilo kwani Serikali inaendelea na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya

mwaka 2005. Lakini la kusikitisha Zanzibar kuna barabara ya Amani - Mtoni ambayo barabara hii imeahidiwa na Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu kuwa barabara ile kwa awamu ya pili ingemalizwa kabla hajaondoka madarakani, mpaka ameondoka madarakani haikumalizwa. Mheshimiwa Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano analijua suala hili na hata Mheshimiwa Waziri Mkuu tumezungumza tatizo hilo na akaahidi kulisimamia, lakini mpaka muda huu barabara ile yenye urefu usiozidi kilomita tatu bado haijapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu akishirikiana na Mheshimiwa Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kulipa uzito suala hilo ili kuwajengea imani wananchi na wanachama wetu kwa ahadi ya Mheshimiwa Rais mstaafu lakini pia kukijengea heshima Chama chetu cha Mapinduzi kwenye ahadi pale kinapoahidi.

Mheshimiwa Spika, mwisho nakushukuru na naunga mkono hoja kwa asilimia zote. Ahsante.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, napongeza hotuba nzuri yenye malengo na mikakati mizuri, Mheshimiwa Waziri Mkuu fedha nyingi za Serikali zinaenda kwa wananchi vijijini lakini Serikali za Vijiji kupitia maafisa watendaji hawaelezi wananchi kiasi cha fedha zinazoletwa na Serikali kwa ajili ya shughuli mbalimbali kama kilimo, afya, barabara, shule na kadhalika. Maafisa watendaji na Madiwani wanakusanya michango kwa wananchi bila kuwaeleza Serikali nayo imechangia kiasi gain, ukiuliza wananchi Serikali imekuchangieni nini wanasema hakuna kwa sababu hawapewi taarifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu zao la Kahawa, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu zao la kahawa lisimamiwe kwa karibu ili tuweze kufikia lile lengo la tani 120 ifikapo mwaka 2010. Kila mwaka taarifa itolewe ili tuone tunakwendaje hadi tufikie lengo.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii na kupongeza uongozi wa Waziri Mkuu akisaidiwa na Mawaziri wake ambao kwa kipindi hiki wamejitahidi kuongeza kasi ya utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Spika, angalau kasi mpya anayoifanya Waziri Mkuu ingekwenda sambamba na watendaji wote wa Serikali kuu na ile ya Serikali zetu za Mitaa, nchi hii ingekuwa kwa kasi kubwa. Bado uzembe, ubadhirifu na utii wa woga unalipunguzia kasi hiyo ya Waziri Mkuu kupata matarajio yake. Bado kuna haja ya kuendelea kuwachuja watumishi wazembe na wasiofaa waadhibiwe kwa kuzingatia kanuni na sheria zetu za kazi, lakini kwa kasi kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri atusaidie kusafisha wakuu wa idara za Halmashauri ya Manispaa yetu ya Sumbawanga ambao walihusika na kusababisha Manispaa kukosa fedha za maendeleo kwa kipindi cha miaka miwili mfululizo. Mpaka sasa hatuna wakuu wa Idara zipatazo tano. Hatuwezi kusafisha hesabu zetu kwa kuendelea kutegemea wasaidizi wa idara ambao uwezo wao na utaalamu ni finyu. Ni kwa msingi huo huo tunaomba adhabu ya kukosa fedha za maendeleo kwa

kipindi cha miaka miwili mfululizo kisiwe kigezo. Sababu inaeleweka ambayo ni kukosa watalaamu.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa mara nyingine tena niombe yafuatayo, moja, gari la zimamoto lipatikane kama ahadi ya Serikali ya mwaka jana, pili, ombi langu kwa miaka mitatu iliyopita inahusu kupatikana angalau kilomita 2 hadi 3 ya barabara za lami kwa mji huu ambao hauna hata kilomita moja ya lami. Huu ni mji pekee (Manispaa) ambao hauna barabara zake la lami. Ombi hili naomba lipewe kipaumbele.

Tatu, ombi la barabara za vijijini vinavyozunguka Manispaa ya Sumbawanga. Tuna vijiji 28 nje ya Mji wa Sumbawanga. Hivyo tuombe gari kwa ajili ya kusimamia/ukaguzi wa shughuli za ujenzi kwa ujumla.

Nne, gari la wagonjwa tumekuwa tukiliomba kwa muda mrefu. Tunaomba safari hii tusaidiwe kulipata. Hatuna gari la wagonjwa na tano, mipango ya nyuma ya kuagiza magari makubwa kwa ajili ya Halmashauri zote, ingefaa uendelee, maana kwa sasa gari zilizoletwa miaka saba iliyopita zimechoka. Hili suala ni muhimu ili kupunguza gharama za kukodi magari makubwa kwa shughuli zetu za maendeleo ambayo ndiyo muhimu kwa kusukuma kazi za kujitolea.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii pia kupongeza uongozi wa sasa wa Serikali Mkoani na Wilaya. Mkuu wa Mkoa Ndugu Daniel Ole Njolay na Mkuu wake wa Wilaya wa Sumbawanga *Major* Matala, wameanza vizuri sana kusimamia maendeleo ya Mkoa. Tuna imani kuwa sasa Mkoa umepata viongozi ambao wananchi wamefurahishwa nao, nami naungana nao katika kazi ya kuleta maendeleo yetu. Namshukuru Rais na Waziri Mkuu kutuletea wakuu hawa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa msiba mzito uliotupata kwa Mbunge mwenzetu Marehemu Amina Chifupa, Mungu amrehemu kwa kumpa mapumziko mazuri. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri iliyojaa dira na yenye nia ya kuboresha maendeleo ya Watanzania. Zaidi nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa utendaji wake wa uwajibikaji kwa kuzungumza, kuchangia au kuelekeza bila kujali msimu. Pamoja na maendeleo makubwa yaliyopatikana baada ya Uhuru mimi binafsi namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu nguvu zake zote hivi sasa azielekeze katika miundombinu hasa ya barabara, kwa sababu hakuna kinachoshindikana isipokuwa tu ni mipango mizuri na mshikamano wa pamoja hii itasaidia sana pindi nchi ikifuguka kwani hapo ndipo sera ya MKUKUTA itapoanza kutekelezwa sababu asilimia kubwa ya wakulima mazao yao yatafika katika Jiji Kuu ambapo mzunguko wa fedha na wachanganuaji wa mambo ndipo walipo, hivyo kuwapelekea wakulima kufaidika.

Mheshimiwa Spika, moja katika dosari kubwa hivi sasa lipo katika barabara zetu, sehemu kubwa ya raia wetu wanakufa kutokana na uzembe unaosababishwa na uendeshaji mbaya wa baadhi ya madereva wetu, hivyo kitengo hiki cha sehemu ya maafa tafsiri yake ianzie katika kinga na siyo kusubiri maafa yoyote yakamilike lakini kubwa zaidi si vibaya hata Mheshimiwa Waziri Mkuu, akatoa tamko la tahadhari kwani si suala dogo, hivi sasa kwani limefikia kiwango cha kuita janga la ajali za barabarani.

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka jana naomba kwa kupendekeza Mheshimiwa Waziri Mkuu ni wa Jamhuri ya Muungano, hivyo alipaswa walau kuwa na ofisi ndogo Zanzibar, hivyo kutoa huduma yake angalau kila baada ya miezi mitatu kwa siku mbili, hii itasaidia sana *physically* kuona na kuelekeza zile taasisi za Muungano na zaidi sehemu ile ya ushuru ambayo inalalamikiwa sana.

Mheshimiwa Spika, katika suala la elimu, tumepiga hatua kubwa sana hasa katika mpango wa MMEM na MMES, lakini suala hili Mheshimiwa Waziri Mkuu, inampasa akae na atulie sana pamoja na kukaa chini na watalaamu wa nje na ndani kupeana ushauri na jinsi ya kuwapata walimu bora na wenye viwango, hivi sasa watoto wanaosoma shule za kulipia ndio wengi wanaofaidi taaluma sababu wanavyomaliza shule wanakidhi soko la ushindani la ajira, aidha, wao ndiyo wengi wanaofaidika na elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, lazima nigusie kwa kuipongeza ofisi ya mazingira kwa uhamasishaji wake mzuri wa utunzaji na hasa katika upandaji miti. Lakini lazima pia nitoe rai ya kuongezwa nguvu zaidi sehemu ya fukwe za bahari zetu kwani zinatosha, hivyo watalaamu wetu wanapaswa kuzipeleka nguvu huko kwa maslahi ya vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, siwezi kumalizia mchango wangu bila kutaja msongamano wa magari Jijini Dar pamoja na kuonekana kwamba mpango unaobuniwa na Serikali ya Japan huenda ukaleta matumaini ya Jiji haiwezekana kufumuliwa kwa kupanua barabara, ila kile kilichosemwa na mipango kuhusu utanuzi wa ujenzi wa shughuli nyingine kubuniwa Kibaha na kwingineko kutasaidia kuliko hivi sasa magari yote asubuhi na jioni hutiririka kwa mwelekeo mmoja wa katikati ya Jiji.

Mwisho natahadharisha waandishi wa habari juu ya mipaka yao ya uandishi wa habari, ili zaidi iwe kuelimisha zaidi kuliko uchonganishi. Naunga tena mkono hoja asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. MARTHA UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kutoa rambirambi kwa wafiwa wote na hasa kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Amina Chifupa, Mungu ailaze mahali pema roho ya marehemu. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba nzuri yenye kuonyesha ufanisi mkubwa wa kuitekeleza Ilani ya CCM. Aidha, ni nzuri kwa sababu inatuonyesha kwa ufasaha tulikotoka, tuliko na tunakokwenda. Pili,

naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Nne kwa jitihada kubwa ya kuleta maendeleo kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, mimi nachangia maeneo matatu kama ifuatavyo, kwanza huduma za jamii - elimu. Mengi yamesemwa kuhusu hitaji la shule za bweni, mahitaji ya shule za bweni katika Jiji la Dar es Salaam au Zanzibar, kwa mfano siyo hitaji sawa na ya Mkoa wa Manyara au maeneo ya wafugaji. Matatizo yetu ni makubwa na hatari iliyopo ni kuwa watoto wetu wengi hawatasoma bila shule za bweni au *hostel,* watoto wa kike wanashawishiwa kuolewa, mabanda na vyumba wanazo kodi ili kuishi karibu na shule zinahamasisha wasichana kupewa mimba, mabanda hayo hayana maji wala umeme, chakula ni shida, tusipowajengea watoto misingi bora ya elimu tokea chini *(form one)* na kuendelea hatutakuwa na wanataaluma wazuri. Ni wazi kuwa watoto wa wafugaji wasipopewa mazingira mazuri ya kusoma hawatafaulu vizuri mitihani ya juu na hivyo kufanya vibaya hata kwenye *courses* mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ombi kwa Serikali, itoe kipaumbele cha kuwajengea shule za bweni wanafunzi wa Mikoa ya pembezoni kama Manyara na mingineyo.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, huduma za kifedha vijijini. Kwanza binafsi naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Nne kwa kufaulu kutekeleza jambo ambalo ni jipya katika utendaji wa Serikali na Taifa hili. Mfumo huu uliotekelezwa ni mfumo mpya, lakini kwa muda mfupi sana (mwaka mmoja) Serikali imetoa mikopo mingi yenye gharama kubwa kwa *SACCOS* nyingi na vikundi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, maoni yangu, Serikali isikatishwe tamaa na malalamiko ya watu wasioelewa ugumu wa shughuli hii. Hakuna hata Mtanzania mmoja anayepaswa kulalamika kuwa kazi hii haiendi haraka kwa sababu shughuli ya mikopo haipaswi kwenda haraka.

Mheshimiwa Spika, kuanzisha *SACCOS* katika sehemu mbalimbali ni jambo moja, lakini *SACCOS* iliyoweza kurejesha mikopo kwa ufanisi ni jambo lingine. Kupima ufanisi wa jambo hili la uwezeshaji ni kutokana na jinsi *SACCOS* na vikundi vilivyokopa zilivyoweza kurejesha, sijaona popote kwenye hotuba kuwa kwa *SACCOS* zote zilizokopeshwa tangu mwaka jana fedha zilizorejeshwa ni kiasi gani. Hii ni muhimu sana kwa sababu urejeshwaji wa mikopo ndiyo kipimo cha mafanikio *(achievement of objective).* Bila urejeshaji hatutawafikia wananchi wengi shilingi bilioni moja ni kiasi kidogo sana isipo-*revolve*. Hivyo Serikali iwe makini sana, jinsi ilivyofanikiwa kuhamasisha uanzishwaji wa *SACCOS*, sasa jukumu la kila mmoja wetu iwe kuhamasisha kwanza urejeshaji wa mikopo na pili uwekaji wa akiba ili kujijengea tabia ya kujiwekea akiba na hatimaye kuondokana na umaskini. Changamoto kubwa kwa huduma hii ni uanzishwaji wa benki vijijini ili kutunza fedha za wananchi. Shilingi bilioni moja ili-*involve* baada ya miaka 5 hadi 10 ni fedha nyingi sana na kama hakutakuwa na huduma za benki itakuwa taabu kubwa. Hii watu pia wafanye biashara ya uhakika baada ya miaka 5 hadi 10 takwimu zitakuwa kubwa na kuhitaji *computer* ili kuweka kumbukumbu sahihi. Kumbukumbu (takwimu) sahihi inawajengea watu imani na kuhakikisha usalama wa fedha zao.

Mheshimiwa Spika, Serikali iweke tahadhali ya mambo hayo muhimu sana kwa utunzaji wa fedha. Wilaya zetu kama Simanjiro na Kiteto hazina kabisa huduma za benki, kutolewa na umeme vijijini kutaathiri biashara ndogo ndogo na hivyo urejeshaji mbovu na hafifu. Aidha, Serikali iharakishe barabara zinazounganisha Makao Makuu ya Mkoa (Babati) na Wilaya zake zote ili *SACCOS* ziendeshwe biashara za uhakika.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ni kuhusu dawa za kulevya, naipongeza sana Serikali kwa kuvalia njuga suala hili, tatizo hili lipo zaidi sana maeneo ya mijini japo hata vijijini imefika, kuna tatizo kubwa hasa kwa vijijini ambalo sijaona kama hotuba hii, ama Serikali kwa ujumla imegusia, tatizo la upikaji na unywaji wa pombe haramu ya gongo, Serikali iamini, isiamini, hili ni tatizo kubwa vijijini na hasa kwa Mkoa wetu wa Manyara.

Naomba Serikali jinsi ambavyo imejidhatiti kupambana na dawa za kulevya, ipambane pia na kutokomeza pombe hii haramu ya gongo ambayo inaathiri nguvu kazi ya Mkoa wa Manyara na kwingineko.

Mheshimiwa Spika, maombi rasmi, kwanza Rais, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete hajatutembelea wananchi wa Wilaya ya Mbulu na hivyo hatuna hata ahadi moja ya Rais. Tunamwomba Rais aje kutembelea Wilaya ya Mbulu na kutupa ahadi ili na sisi tuorodheshwe kwenye mikakati ya kutekeleza ahadi za Rais na ikiwezekana, walioahidiwa mwisho watekelezewe kwanza.

Pili, wananchi wa Mkoa wa Manyara wanalalamika sana kuwa Mawaziri wengi na Naibu Mawaziri wao hawajafika Mkoani Manyara ikilinganishwa na Mikoa mingine. Tunampongeza sana Waziri Mkuu, kwa kutembelea Wilaya zetu. Pia tunampongeza Mheshimiwa Shamsa Mwangunga na Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Mwantumu Mahiza, japo wamefika angalau mkoani tunaamini watatembelea pia na vijiji na Wilaya kujionea matatizo au mafanikio. Tunaomba sana Mawaziri watutembelea, wananchi wanawapenda viongozi wao hata kama hawaleti chochote cha maendeleo kuja tu ni jambo kubwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Waziri Mkuu kwa asilimia mia moja. Naomba kuwasilisha.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nieleze machache juu ya hoja ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, suala la ajira binafsi kwa vijana bado hatujalipa nafasi kubwa kuandaa mkakati au sheria ndogo ndogo za kuwasaidia kupata haki yao kwa mujibu wa kazi wanazozifanya.

Mheshimiwa Spika, vijana wanaofanya kazi majumbani, nyumba za wageni, kwenye hotelini, kwenye vilabu vya pombe wanatumia nguvu zao na muda mrefu lakini wanachokipata, hakilingani na kazi yenyewe. Ushauri wangu Serikali ilete sheria hapa

Bungeni kuwalinda na kuwasaidia vijana hawa, kwani na wao wanahitaji maslahi yao ya baadaye, kulinga na muda wa kazi au miaka yake kazini.

Mheshimiwa Spika, nayasema haya kwa sababu wamiliki au wadhamini na wenye hoteli, nyumba za kulala wageni na hata majumbani wanawafukuza kazi kwa lugha mbaya, wanawanyanyasa kinyume na haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, suala la UKIMWI limekuwa likizungumzwa mara nyingi Bungeni, huku ikionekana semina, warsha, kongamano zimetosha kinachotakiwa na kuwapatia walengwa yaani waathirika wa UKIMWI vijijini, fedha na haki nyingine wanazotakiwa kupata. Nashauri kutilia mkazo siku ya kupima UKIMWI mwezi Julai iambatane na utoaji zawadi au motisha ili kuweza kuhamasisha watu kujitokeza zaidi. Nashauri Serikali iandae utaratibu wa kampeni maalumu ambapo napendekeza iitwe wataje wenzako uliostarehe nao.

Mheshimiwa Spika, kero ya wale wanaoambukiza wenzao inafaa lishughulikiwe ipasavyo na ni vyema tufanye uhakiki wa kuwatambua wageni waliopo Dodoma kipindi hiki wote wanakuja kwa kazi au wamekuja kutafuta namna ya kueneza UKIMWI nina wasiwasi, hivyo naishauri Serikali kufanya uhakiki kuwatambua wageni wasio na kazi maalumu tuanze kutoa funzo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, Homa ya Bonde la Ufa *(RVF)* imepelekea vifo 139 vya watu na wanyama 50,000 hivyo kuna athari kubwa katika mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini, kwani kuna familia zimeathirika sana, baba amefariki na ng’ombe wamekufa, mama hana uwezo wa kuwasomesha watoto, hivyo naishauri Serikali kufanya sensa ya kuzitambua familia duni zilizokumbwa na vifo vya Bonde la Ufa ambao watoto wao hawaendi shule, hivyo misisitizo wangu ni kwamba naishauri Serikali kuwasomesha wanafunzi ambao familia hizo hazina uwezo kwani kilichotokea, hakikutarajiwa ni vyema Serikali ikatoa baraka zake na angalizo la jicho la huruma.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. Ahsante.

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja ya Waziri Mkuu. Nimefarijika sana na taarifa kuwa hadi tarehe 31 Mei, 2007 jumla ya wajasiriamali 21,789 walipata mikopo ya masharti nafuu yenye thamani ya shilingi bilioni 17.9. Hakika, Watanzania wengi wamefaidika katika kipindi kifupi sana. Lakini ukweli unabakia kuwa mikopo hii imeelekezwa zaidi kwa wajasiriamali wadogo wadogo wa Mijini na sio wa vijijini kwenye wakulima wengi wadogo wadogo. Nasema hivi kutokana na uzoefu nilioupata Kyela ambapo masharti ya Kibenki ya mikopo hii hayazingatii mazingira maalumu ya uzalishaji wa mazao ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, mikopo hii inatoa muda mfupi, mwezi mmoja kwa ukopaji kwanza kurejesha na inamtaka mkopaji aurejeshe mkopo wake kila mwezi. Tatizo ni kuwa wakulima wana vipindi maalumu vya mavuno ambavyo havizingatiwi. Kwa mfano tu, mkulima wa mpunga wa Wilaya ya Kyela anaanza mchakato wa kilimo hicho mwezi

Novemba na baada ya miezi nane yaani mwezi Julai ndipo anavuma! Mkopo kwa mkulima wa mpunga uwekewe masharti ya kurejesha baada ya miezi tisa na mazao mengine yaendane na muda wa mavuno. Hapo ndipo wakulima watakiwa wamesaidiwa.

Pili, naipongeza Serikali kwa ubunifu wa kuingia mikataba ya utendaji wa Halmashauri kwa lengo la kuboresha udhibiti. Lakini utaratibu huu unakuja kuwa mbaya pale ambapo Halmashauri inavurunda. Badala ya watendaji kuadhibiwa, Wilaya nzima inaadhibiwa kwa kunyimwa ruzuku. Hii si sawa sawa kwani tunawaadhibu wananchi kwa makosa yasiyo yao. Kuinyima Wilaya ruzuku ni kuinyima maendeleo na adhabu za aina hiyo si nzuri, zinakosa mantiki.

Vile vile chombo kilicho na dhamana ya kukagua utekelezaji wa Bajeti za Halmashauri yaani Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kunahitaji kuboreshwe ili kuimarisha utendaji kazi wake uweze kutoa huduma bora kwa Halmashauri. Nasema hili kwa sababu Halmashauri ya Wilaya ya Kyela dhahiri imeonewa katika ukaguzi wa hesabu za mwaka 2005/2006 na hivyo kupewa hati yenye dosari/mashaka *(qualified opinion)* na kupelekea kukoa ruzuku ya maendeleo *(Capital Development Grand - CDG).*

Mheshimiwa Spika, kutokana na uhaba wa nafasi, nitatoa mifano michache tu. Kwanza, hoja ya kwanza ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu (*CAG*) ilisema dawa za binadamu zinazonunuliwa toka *MSD* za shilingi 6,944,350/= hazikupokelewa. *CAG* alipaswa ajue kuwa taratibu za *MSD* zinataka Halmashauri zilipe fedha kwanza ndipo baadaye zipewe huduma hiyo. Aidha, sheria ya manunuzi ya Serikali inaagiza malipo yafanyike pale tu huduma husika inapokuwa imetolewa. *This is a serious predicament* kwa Halmashauri zote. Ukweli ni kuwa Kyela ilitumia sehemu ya fedha ya *basket fund* shilingi 13,975,950 kununulia dawa za hospitali za Wilaya. *MSD* inaweza kutoa dawa za shilingi 7,031,600/= tu na kufanya bakaa ya thamani ya dawa zisizopokelewa hadi Juni 2006 kuwa shilingi 6,944,350/= Serikali Kuu iingilie kati suala hili.

Pili, hoja ya pili ya *CAG* ni kuwa maduhuli yaliyokusanywa yameonyesha pungufu kwa shilingi 211,554,353/= upungufu huo haupo, tatizo ni tafsiri tofauti ya sheria, kanuni na taratibu za ufungaji wa hesabu kati ya *CAG* na Halmashauri yetu. *CAG* kachukua jumla ya mapato ya Halmashauri kwa lengo la kupima malengo ya Bajeti ya Halmashauri kutoka kwenye *detailed statement of revenue.* Amelinganisha na jumla mapato kwenye *consolidated income and expenditure statement* na kupata tofauti ambayo ameiita maduhuli pungufu. Hii ni kinyume na *section 8.1- 8.4.4* ya *local authority accounting manual* inayoelekeza kuwa mapato yanayohusiana na ununuzi wa mali za kudumu si mapato yanayokwenda kuingizwa kwenye *consolidated income and expenditure statement*. Badala yake yanakwenda kwenye *balance sheet* kuongeza mtaji wa Halmashauri *(Capital applied).*

Mheshimiwa Spika, hoja ya tatu ya *CAG* ni kuwa matumizi yameonyeshwa kuwa pungufu ya shilingi 289,395,383, kama nilivyoielezea hoja ya pili, fedha zinazotumika kununua mali za kudumu haziingizwi kwenye *income and expenditure account* bali zinaonyeshwa kwenye *balance sheet,* kama rasilimali za kudumu. Hii ni kwa mujibu wa

*local authority accounting manual* kifungu cha 8.4.4. Mkaguzi alichokifanya ni kuchukua jumla ya matumizi kwenye *detailed statement of expenditure,* akalinganisha na matumizi yaliyopo kwenye *consolidated income and expenditure statement* bila kufanya marekebisho ya matumizi ya rasilimali za kudumu. Huu ndiyo msingi wa hoja ya tatu ya *CAG* ambayo haiendani na *local authority accounting manual section 8.4.4.*

Mheshimiwa Spika, mkanganyiko zaidi naupata ninapolinganisha kesi ya Halmashauri ya Kyela na Manispaa ya Tabora. Halmashauri ya Kyela haikuhusisha *capital receipts* kwenye *income and expenditure statement* kwa kuzingatia masharti ya *local authority accounting manual 8.1-8.2.3* ikapata hoja ya ukaguzi. Manispaa ya Tabora ikahusisha *capital receipts* kwenye *income and expenditure statement*. Vile vile imepata hoja ya ukaguzi. Sasa *which is which?* Hesabu za Manispaa ya Tabora zilichapishwa katika Gazeti la Mwananchi Tarehe 18 Juni, 2007.

Napendekeza kufanyika kwa haraka kwa kikao cha pamoja kati ya *CAG* kwa maana ya wakaguzi wake, waweka hazina wa Halmashauri, wakaguzi wa ndani na washauri wa fedha. Kwa lengo la kukubaliana juu ya utaratibu muafaka wa upungufu wa hesabu ili mikanganyiko niliyoielezea awali isitokee tena na kuwaumiza wananchi bila sababu. Narudia tena kuunga mkono hoja.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikupongeze wewe kwa umahiri wako wa kuongoza mijadala humu Bungeni hali ambayo inaimarisha amani, mshikamano na umoja wa Kitaifa katika mfumo wa vyama vingi.

Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze kwa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa namna anavyosimamia shughuli za Serikali nje na ndani ya Bunge. Hotuba ya Waziri Mkuu, kuhusu Bajeti ya Ofisi yake ni kielelezo dhahiri kwamba Mheshimiwa Edward Lowassa, ni shupavu, jasiri na mahiri kwa vile imegusa maeneo yote ya shughuli za Serikali. Pia hotuba hiyo imeeleza mafanikio na changamoto zilizopo lakini ikaeleza pia namna ya kukabiliana na changamoto hizo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika yafuatayo, kwanza ni kuhusu posho za Madiwani, posho iliyopendekezwa bado ni ndogo lakini pia ni Halmashauri chache zenye uwezo wa kuwalipa Madiwani posho hiyo. Hata hiyo shilingi 30,000 inalipwa kwa kusuasua.

Nashauri Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, ifikirie kuzipa ruzuku Halmashauri kwa ajili ya kulipa posho hiyo. Ruzuku kwa ajili ya miradi mbalimbali inayotolewa kwenye mikoa iliyo mbali na Dar es Salaam izingatie bei za bidhaa mbalimbali na pia bei ya mafuta ya mgari. Fedha za MMEM na MMES zitolewe kwa kuzingatia bei za vifaa vya ujenzi katika Mikoa na Wilaya husika.

Mheshimiwa Spika, Serikali itafakari upya na kwa makini kuhusu kuzinyima fedha za maendeleo Halmashauri zinazopata hati chafi za ukaguzi wa mahesabu. Uandishi wa vitabu vya mahesabu hufanywa na watalaamu walioletwa na Serikali

kwenye Halmashauri. Serikali inapozinyima Halmashauri wanaoumia ni wananchi kwa kosa lisilo lao.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuwapa pole wazazi wa marehemu Amina Chifupa na kuiombea roho yake ipumzike kwa amani. *Amin.*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kuhusu barabara. Pongezi kwa kuongeza fungu la barabara toka shilingi bilioni 25 mpaka shilingi bilioni 25 hii ni hatua nzuri na natumaini itasaidia kwa kiasi kikubwa katika kutengeneza barabara zetu za Serikali za Mitaa.

Hata hivyo hofu yangu juu ya ufanikishwaji mzima wa zoezi husika ni ugawanywaji wa rasilimali hiyo katika kila Halmashauri hali inayopelekea mgao kuwa kidogo mno, hivyo kutokutatua tatizo *permanently* hali inayopelekea kila mwaka barabara husika kupata mafungu.

Ushauri wangu ni kwamba ili tuweze kutatua matatizo moja kwa moja *(permanently)* kuna umuhimu wa kufanya matengenezo kwa ujumla wake ili kuepuka kurudia rudia kwa ukarabati hivyo kuongeza gharama. Itagharimu kiasi kidogo cha fedha kama barabara zitakuwa zinajengwa kwa *phases* na kwa gharama halisi ya kutatua tatizo moja kwa moja. Mfano katika Bajeti ya sasa hivi Manispaa ya Kinondoni imetengewa shilingi milioni 200 tu za ukarabati wa barabara. Wakati hizo shilingi milioni 200 hazitoshi hata kufanyiwa ukarabati barabara ya ndani tangu Kimara Kona – Makoka – Kibangu – *Riverside* ambayo mngesaidia sana kupunguza foleni inayotoka Kimara ambayo kwa sasa imekithiri. Kata ya Makuburi ina wakazi 40,000 ukarabati husika itakuwa na tija sana.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wa Viti Maalum kuingia kwenye vikao vya Halmashauri. Pamoja na kwamba sheria imeshapitishwa na Bunge na imeshasainiwa na Rais, bado wakurugenzi wa baadhi ya Halmashauri hasa za Jiji la Dar es Salaam hawatoi taarifa za vikao kwa Wabunge husika. Hii inazua hofu ya nini hasa Wakurugenzi hao wanakificha. Ombi langu ni kwa Waheshimiwa Mawaziri, wakati wa kujibu hoja za Wabunge, kutoa tamko litakalokuwa elekezo kwa Wakurugenzi kote nchini kutekeleza wajibu wao kama ambavyo sheria mpya ya Serikali za Mitaa inayoelekeza.

Kuhusu ujenzi wa ofisi za Wabunge, katika Mkoa wa Dar es Salaam una idadi ya Wabunge 12, ofisi za Wabunge zilizopo ni tisa tu, hata fedha za ukarabati, samani zilizotolewa kwa mfano, shilingi milioni 18 zinatengwa kwa madhumuni ya kukarabati ofisi tisa tu zilizopo, hakuna fungu lililotengwa kwa madhumni ya kujengwa ofisi nyingine. Yawezekana hoja ya kujengwa kwa ofisi mpya ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ikawa sehemu ya suluhisho. Hata hivyo jengo hilo ndio kwanza liko kwenye hatua za awali hata kuanza kujengwa bado wakati hitaji la ofisi liko pale pale.

Mheshimiwa Spika, ushauri, kuna umuhimu Wizara iangalie ni kwa jinsi gani ofisi zilizokuwepo zigawanywe kwa Wabunge kwa usawa hata ikibidi ku-*share office.*

Kwa ufupi ni kwamba hakuna hata Mbunge mmoja wa Kambi ya Upinzani mwenye ofisi katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mgawanyo wa rasilimali, taarifa za Mikoa zinaonyesha kwamba Mikoa iliyo nyuma kimaendeleo ndiyo inayopewe kiasi kidogo cha pesa. Kuna hoja kubwa sana kuanza kutoa kipaumbele kwenye Mikoa iliyo nyuma. Vile vile kuna umuhimu wa kuwa wa mkakati wa kuhakikisha malengo ya makusanyo ya sekretarieti ya Mkoa yanatekelezeka kwa 100% Mikoa mingi inashindwa kufikia malengo ya mapato, huku wakitumia mafungu yao yote kwa asilimia 100 yanayojumuisha pia kasma za kuboresha mazingira ya kazi. Ipo haja ya kuchukua hatua za dhati.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kuchangia hotuba hii. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Fuoni tunatoa mkono wa rambirambi kwa familia zote zilizopoteza ndugu, jamaa na marafiki zao katika ajali mbaya ya basi la *Mohamed trans* iliyotokea Mkoani Singida na ile iliyotokea Mkoani Arusha na kuwatakia wawe na subira na Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuendelea naunga mkono hoja hii. Naomba kuchangia kero iliyopo katika Jeshi la Polisi. Tanzania. Jeshi la Polisi, ni hazina kubwa ya nchi katika kuweka usalama wa wananchi pamoja na ulinzi wa nchi yetu na viongozi sasa kutowatendea mazuri pamoja na kutowaondoleo kero ambazo zinawakabili ni hatari kwa nchi na wananchi wake wote.

Mheshimiwa Spika, katika majeshi yote yaliopo nchini ni Jeshi la Polisi peke yake ndilo lenye mikataba miwili wakati vya kustaafu, pensheni na kiinuo mgongo. Hii ni kero kubwa ambayo haijapatiwa ufumbuzi bali ni ahadi tu ambazo zimetolewa tangu awamu zilizopita. Ndugu zetu hawa ni wasikivu wanapowekewa ahadi na viongozi wao lakini kila kukicha wanastaafu ,wanaongezeka bila mafanikio.

Mheshimiwa Spika, mimi nina hofu kubwa na kundi hili lisije likakosa imani na Serikali yetu. Naomba Serikali ichukue hatua za haraka kuondoa utaratibu huu wa kiinua mgongo na tuachane na kauli ya utaratibu huo wamechagua wenyewe hasa kwa kuwa wastaafu wanalipwa kiinua mgongo. Wanakuwa na hali ngumu sana ya maisha ukilinganisha na anayelipwa pensheni. Lazima tukubali hakuna mwanadamu hata mmoja anayetaka kuishi kwa taabu lakini lazima tukubali hakuna elimu nzuri iliyotolewa katika kuchangia njia hizi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuondoa mfumo huu, pia Serikali iwatupie jicho la rehema wastaafu hawa japo kwa miaka miwili, miwili au mmoja waliochukua malipo ya mkupuo ambao nao walichagua kulipwa hivyo na baadaye Serikali iliendelea kuwalipa na hayo yote ni kutaka maisha mema kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, kuna usumbufu mkubwa sana kwa wastaafu wa Jeshi la Polisi hasa wenye vyeo vya chini kuanzia *Staff Sergeant* hadi *Private*. Wakati wa

kufatilia mafao yao Dar es Salaam, makao makuu. Wastaafu hawa husumbuka sana kwa safari ya kwenda na kurudi hadi wanachoka na wakati mwingine mafaili yao hayaonekani na wala hakuna juhudi yoyote ya kutafuta faili hilo. Kuna kesi nyingi za kupotea mafaili na kuna wastaafu tangu mwaka 2004 hadi leo hawajapata mafao yao na bado wanahangaika na wengine wameshakufa na familia zinahangaika na wengine wameshachoka na kusema wanamwachia Mungu.

Mheshimiwa Spika, kauli hizi si nzuri kwa Serikali yetu na Chama chetu cha Mapinduzi kwa hivyo, naishauri Serikali ipanue shughuli hizi kwa kugawa kwa Kanda ili kuwapunguzia usafiri na usumbufu uliopo sasa wa shughuli zote kufuatilia Dar es Salaam. Pia Serikali ingilie kati kwa kutafuta njia ya utatuzi wa wastaafu waliokwama kwa kupotea mafaili yao, hilo linawezekana tukikusudia.

Mheshimiwa Spika, utunzaji wa mali za Serikali, kwa masikitiko makubwa naiomba Serikali ichukue hatua za haraka kukinga jingo la Bunge la Ukumbi wa Pius Msekwa ambalo liko katika hali mbaya, linavuja sana na liko katika hatari kuharibika kwa miundombinu iliyokuwemo na inasikitisha kuona Serikali imetumia fedha nyingi na kuliachia liharibike. Wahenga walisema usiache mbachao kwa msala upitao na usipoziba ufa hutajenga ukuta.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nianze kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri anazozifanya kwa kutetea na kuhakikisha maisha ya Watanzania yanakuwa bora, wanaendelea na kuondokana na umaskini kwa kupitia fedha nyingi zinazotengwa kwa ajili elimu, barabara, kilimo, afya, maji na kadhalika. Pia nawapongeza sana Mheshimiwa Mizengo Pinda na Naibu Mawaziri wote wanaowasaidia. Kwa kweli kazi mnayoifanya ni ya mfano na ya kuigwa.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi fedha nyingi sana zitapelekwa kwenye Halmashauri zetu za Wilaya. Mpaka sasa kuna Halmashauri nyingi hawana Wakuu wa Idara wenye sifa hasa waweka hazina. Napendekeza na kushauri watafutwe watumishi wenye sifa wapelekwe Wilayani haraka sana. Mpaka sasa kuna watumishi wamekaa kwenye kituo kimoja cha kazi kwa zaidi ya miaka saba mpaka miaka 20 hawa watumishi wamekuwa mzigo kwa Halmashauri husika na wengi wao wamekuwa wafanyabiashara kwa hiyo, utendaji wao wa kazi umezorota sana. Nashauri ofisi yako ifanye sensa na Watumishi waliokaa muda mrefu wahamishwe haraka sana.

Kuna watumishi wengi wanaharibu Wilaya moja badala ya kuchukuliwa hatua wanahamishiwa Wilaya nyingine mfano halisi Injinia Msomba alikwua mhandisi wa ujenzi Tandahimba, huyu ndiye aliyetangaza *tender* kwa siku moja kuanzia asubuhi mpaka saa saba mchana akawa amempata mkandarasi kufanyakazi na saa saba mchana siku hiyo hiyo akalipwa shilingi milioni 13.0 na kampeni iliyofanya kazi hiyo ni ya kwake. Aliyekuwa Mbunge wa Tandahimba akaeleza tatizo hilo mpaka Wizarani na pia akalileta kwenye Kamati ya *LAAC* na Kamati ikaandika barua kwa Waziri ili mtumishi huyu achukuliwe hatua. Hakuna hatua iliyochukuliwa bali alipata uhamisho kuja Wilaya ya Iramba ambako napo anaharibu kazi. Pia kazi nyingi za ujenzi wa barabara anaipa kampuni yake.

Mheshimiwa Spika, sasa umefika wakati wa kupeleka maafisa kilimo, afya, ushirika na kadhalika kwenye kata ambapo ndipo fedha za maendeleo zinatakiwa kupelekwa. Wananchi wa Iramba Mashariki wana shida sana kwa sababu kutokana na umbali na Makao Makuu ya Wilaya huwa hawapati huduma kama vile pensheni zao, huduma za mahakama, matibabu na kadhalika, wananchi wa Iramba Mashariki wanapata matatibu Wilaya ya Mbulu tena kwenye Hospitali ya Kanisa kwa hiyo, wanalazimika walipie. Huduma za *basket fund* wao hawapati naendelea kuomba Wilaya ya Iramba igawanywe Iramba ya Mashariki iwe na Wilaya yake.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri Mkuu, kwa hotuba yake nzuri aliyotoa Bungeni. Waziri Mkuu Mheshimiwa Edward Lowassa ni mchapa kazi hodari sana.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana ofisi ya Waziri Mkuu walitoa fedha shilingi milioni 300 kwa ajili ya barabara ya Myangalua mpaka Kipeta fedha hizo zimetumika vizuri katika kulima sehemu ya barabara hiyo. Waziri wa TAMISEMI alipofika katika tarafa ya Kipeta aliona juhudi hizo na alitoa ahadi kuwa mwaka huu Serikali itatoa fedha kwa ajili ya sehemu iliyobakia ambayo inahusu mlima wa Kipala. Pia Serikali ilitoa ahadi kuwa itatoa fedha za kumalizia kazi iliyobakia, naomba tupewe pesa kumalizia matengenezo ya mlima.

Kuhusu maendeleo ya kilimo cha mazao ya chakula na biashara ninatoa ushauri kwa mikoa itakiwe kuwa na programu na malengo ya utekelezaji wa kilimo katika mikoa yao. Kuwepo na uwajibikaji, mazao ya mbegu za mafuta yapewe msukumo wa pekee ili Taifa liweze kujitosheleza kwa mafuta ya kupikia katika chakula, uwepo msukumo mkubwa wa kuweka kipaumbele katika uanzishaji wa viwanda vya uzindikaji wa mazao ya kilimo na ufugaji na mbolea ya ruzuku katika mkoa wa Rukwa, Mbeya, Ruvuma na Iringa isambazwe katika mikoa kwa kutumia *TFC* badala ya watu binafsi. Mpango wa uwezeshaji kwa wananchi usimamiwe vizuri hasa wakulima na wafugaji. Tafsiri ya ujasiriamali umetafsiriwa kuwa wahusika ni wafanyabiashara. Wakulima na wafugaji hawapewi ujasiriamali katika uzalishaji mali ndio muhimu sana.

Napendekeza kuwa Halmashauri za Wilaya zishindanishwe katika shughuli za maendeleo na kwa hiyo, zipangwe kwa madaraja kutoka daraja la I hadi la VII kipimo hiki kitasaidia sana kuharakisha maendeleo. Upelekaji wa madaraka kwa Halmashauri, Manispaa na Miji uende sambamba na uwezeshaji wa uwezo wa kiutendaji (*Capacity Building*).

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kama ifuatavyo:-

Kuhusu ujenzi wa ofisi za Wabunge, kwanza napenda kuishukuru sana Serikali kwa kuamua kujenga ofisi za Wabunge. Hata hivyo napenda kushauri kwamba kuwe na utaratibu mzuri wa kujenga ofisi hizi kwa maana ya kutokuwa na upendeleo kwa baadhi ya Wabunge na mikoa. Aidha, naiomba Serikali itoe utaratibu mzuri wa kuzihudumia

ofisi za Wabunge na aina ya huduma zinazostahili kuwepo/kutolewa kwa ofisi ya Mbunge. Nashauri utolewe waraka maalumu wa Serikali kuhusu mambo yote hayo.

Kuhusu Mfuko wa Jimbo *(Constituency Development Fund),* hili ni eneo lingine ambalo napenda kuipongeza sana Serikali kwa kuanzisha mfuko wa Jimbo pamoja na pongezi hizo napenda kutoa ushauri ufuatao:-

Kwa kuwa ukubwa wa Majimbo unatofautiana kwa ukubwa wa eneo, idadi ya watu na shughuli za kiuchmi, ni busara Serikali izingatie vigezo hivyo katika kugawa fedha kwa ajili ya maendeleo. Kwa mtazamo wangu naona haitakuwa sahihi kutoa pesa za maendeleo ya Jimbo kwa kiwango sawa kwa Majimbo yenye vigezo vinavyotofautiana sana kama nilivyovitaja hapo juu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano Jimbo A lina ukubwa wa kilomita za mraba 9,500 na idadi ya watu wapato 600,000 na Jimbo B lina kilomita za mraba 50 na idadi ya watu wapatao 30,000. Kugawa pesa sawa katika Majimbo yenye tofauti kubwa za namna hiyo haitakuwa sahihi, utaratibu unaotumika na mfuko wa barabara *(Road Fund Board)* katika kugawa pesa ndio utumike.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa nichangie ni kuhusu pembejeo za kilimo zenye ruzuku ya Serikali, katika kipindi cha mwaka 2006/2007 Serikali ilitenga shilingi bilioni 19.5 za ruzuku kwa ajili ya mbolea na mbegu na jumla ya tani 110,836 ya aina mbalimbali za mbolea zilipatikana.

Sasa jambo la kushangaza, Waziri Mkuu katika hotuba yake anasema jumla ya tani 89,323 za mbolea za aina mbalimbali zitapatikana, kinachonishangaza ni kwamba badala ya Serikali kuongeza idadi ya mbolea ya ruzuku, inapunguza idadi ya mbolea ya ruzuku. Wakati huo huo Serikali inatueleza kwamba inaongeza kiasi cha mbolea ya ruzuku, imeongeza vipi? Soma ukurasa wa 30 wa hotuba ya Waziri Mkuu naomba maelezo katika jambo hili. Aidha, badala ya kuleta pembejeo (mbolea na mbegu) mwezi Novemba/Desemba naomba pembejeo hizo ziwahi kuja, zikiletwa mwezi Septemba/Oktoba zitawasaidia wakulima wetu kupanga mipango yao ya kilimo vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuzungumzia suala la kuigawa Wilaya ya Mbozi. Wilaya ya Mbozi ina kilomita za mraba karibu 9,500 na ina idadi ya watu wanaokadiriwa kufikia 600,000, Kata 26 na Vijiji vipatavyo 175. Ni wazi kwamba Wilaya yenye ukubwa wa namna hiyo ni mgumu sana kutawalika.

Kwa kuzingatia hayo, Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi imekuwa ikiomba tangu mwaka 2000 na zaidi ya mara mbili Halmashauri imewasilisha mkoani maombi hayo ili yafikishwe ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kwa ajili ya kuigawa Wilaya ya Mbozi katika Wilaya mbili. Mimi binafsi nimewahi kuzungumza na Mheshimiwa Mizengo Pinda, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na alikiri kufahamu juu ya ombi hilo. Sasa naomba Serikali itekeleze, sisi wananchi wa Wilaya ya Mbozi juu ya ombi hili la muda mrefu tuwe na matumaini gani?

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara naipongeza sana Srikali kwa kutenga kiasi cha shilingi 1,843,200,000/= pesa ambazo zitatolewa na *DANIDA* chini ya *Road Sector Programme (RSPS-3).* Pesa hizo zitatumika kujenga barabara ya Mlowo Kamsamba kwa kiwango kizuri cha changarawe. Hata hivyo barabara hiyo yenye kilomita zaidi ya 100 kutoka Mlowo kwenda Kamsamba, inaonekana itatengenezwa kilomita 75 tu, je, kilomita zinazobaki zitatengenezwa kwa utaratibu gani? Je, daraja la mto Momba linalounganisha Wilaya ya Mbozi na Sumbawanga Vijijini litajengwa kwa pesa ipi na lini?

Mheshimiwa Spika, naomba nijue kuhusu shamba Na. 208 la *NAFCO*, Magamba. Shirika la *NAFCO* lilishindwa kuendesha shamba hilo mnamo mwaka 1994. Tangu kipindi hicho shamba hilo lenye ukubwa wa ekari 12,051 limekuwa likikodishwa kwa wakulima kwa shilingi 5000/= hadi 10,000/= kwa ekari. Baada ya *NAFCO* kushindwa kuliendesha shamba hilo liliwekwa chini ya *PSRC* kwa misingi ya kulibinafsisha. Katika kipindi chote hicho wananchi wamekuwa wakitegemea sana shamba hilo .

Hata hivyo kati ya mwezi Februari na Machi, mwaka jana *PSRC* iliwasimamisha wananchi kulima shamba hilo kwa maana kwamba shamba hilo lipo tayari kupewa mwekezaji. Jambo la kusikitisha hadi leo hii hakuna mwekezaji aliyepewa, na wananchi wamenyimwa kulima shamba hilo kwa misimu miwili sasa. Hivi katika hali hii wananchi wataondokana na umaskini kweli?

Mheshimiwa Spika, wananchi wanaiomba Serikali iwauzie wao shamba hilo kwani uwezo wa kuzalisha wanao. Na kama Serikali imezamilia bado kulibinafsisha shamba hilo pamoja na maombi yangu kwa Serikali ya kutoa shamba hilo kwa wananchi hao, basi naomba Waziri mwenye dhamana ya masuala hayo akaonane na kuzungumza na wananchi wanaozunguka shamba hilo juu ya azma hiyo ya Serikali ya kulibinafsisha shamba hilo.

**MHE. VUAI ABDALLA KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwanza na awali ya yote nakupongeza wewe kusimamia vyema Bunge la Jamhuri ya Muungano hasa Mkutano wa nane cha Bajeti mwaka huu wa 2007/2008, namtakia kila kheri na Mwenyezi Mungu akuzidishie uwezo zaidi. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake na kuusimamia vyema Uwaziri wake na kuwa na imani na wananchi wake, Wabunge, Mawaziri hadi Mheshimiwa Rais wetu.

Mheshimiwa Spika, utalii ni sekta inayotusaidia na kutupeleka mbele Watanzania na kutupatia fedha za kigeni ndani ya nchi yetu kwa hiyo Serikali itazame vyema kwa mfano misitu na wanyama waliomo na wanyama nao wasiwindwe, kuwe na ulinzi zaidi na elimu itolewe zaidi na vizuri kwa watendaji wa Wizara ngazi zote hadi wapokeaji wageni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bandari, bandari zetu zote ni sehemu katika Pato la Taifa letu, kwa hiyo, naiomba Serikali isimamie zaidi na kuboresha njia zote za bandari ili ziweze kuingiza bidhaa na kutoa nje. Pia *TRA* wafahamu kazi wanayofanya ni ya Taifa lao na wajali maslahi yawe ndani ya nchi yao, na kwa upande mmoja Serikali ni ya

Jamhuri ya Muungano Tanzania na Tanzania ni Zanzibar na Tanzania Bara, bandari ya Zanzibar iwezeshwe kupitisha mizigo au bidhaa na kusiwe na ubaguzi wa *TRA* kwa ushuru na pingamizi na magari ya Zanzibar yakiingizwa Tanzania Bara kusiwe na usumbufu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *SACCOS,* naomba *SACCOS* zipewe nguvu hasa kwa kuzingatia husaidia wananchi kama wajane, wagonjwa wa UKIMWI na wenye kipato cha chini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo, kilimo vile vile kiwe kilimo cha kisasa na hakiwezi kuwa cha kisasa bila elimu kwa hiyo, naomba wananchi waelimishwe na wapatiwe mashamba, nafaka, mbolea na zana zote ziwe rahisi kwa kuwezeshwa pamoja mikopo ya *CRDB* na *NMB.* Kwa niaba wananchi wa Magogoni na mimi mwenyewe, naunga mkono hoja.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nitoe pongezi za dhati kwa niaba ya wananchi wangu wa Hai kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri sana yenye ufafanuzi wa kina kwa hali halisi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nitoe pongezi kwa hali ya uchumi kuwa nzuri pamoja na hali mbaya ya hewa iliyotukumba hapo mwanzoni mwa mwaka jana.

Katika ukurasa wa 14 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumzia mfumo wa stakabadhi za mazao ghalani, ninapongeza hatua hizo na pia ninaomba huu mfumo uje Wilayani kwangu.

Nitoe rai ya kuendelea kuzijenga barabara za Kitaifa, kwenye barabara za Serikali za Mitaa napendekeza wahandisi wapelekwe kwenye Halmashauri zetu ili hizo pesa zinazopelekwa ziwe na tija.

Mheshimiwa Spika, tuimarishe vyanzo vyetu vya utalii pamoja na kubuni vipya tukienda sambamba na kudhibiti mianya yote ya ufujaji wa mapato ya utalii. Kwa upande wa kilimo napendekeze tuimarishe zaidi kilimo cha umwagiliaji ili tuweze kulima mazao mengi zaidi na haswa yale ya kupeleka nje ya nchi.

Pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu pia ni kwenye uhimizaji wa elimu ya sekondari kwa nchi nzima na haswa kule kwetu Hai. Pia natoa pongezi kwa kuanzishwa kwa Kamati za Ushauri za Wilaya kwa maana ya kuwashirikisha wadau mbalimbali na hii ni pamoja na *D by D.*

Mheshimiwa Spika, pia natoa pongezi kwa mishahara ya watendaji na posho za Madiwani. Napendekeze kuwa Waheshimiwa Madiwani wakopeshwe vyombo vya usafiri japo pikipiki ili kurahisisha utendaji wao.

Mheshimiwa Spika, nitoe ombi la kuimarisha idara ya maafa kutokana na majanga yanayotukumba kama yale ya upepo mkali yaliyotukumba kule Hai. Pia

napendekeza haja ya kuwa na ufuatiliaji wa pesa katika idara ya UKIMWI *(TACAIDS)* kwani kuna ufujaji siku nyingi.

Mheshimiwa Spika, kuna umuhimu mkubwa sana wa kufanya ukaguzi wa haraka na mkubwa kwa vyombo vya usafiri wa umma yaani mabasi kwani ajali ni nyingi mno kwa mfano mengi ya mabasi ndiyo nayo yalikuwa ni malori na hata yanapojengewa *body* hata milango ya dharura hakuna, utakuta kuna bati kubwa kabisa kwenye milango ya nyuma.

Mheshimiwa Spika, nikimalizia tunakuunga mkono wewe Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mheshimiwa Rais katika vita ya kuweka nidhamu ya matumizi ya fedha za Serikali. Naunga hoja mkono.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafsi hii ili niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Kwanza nampongeza yeye pamoja timu yake kwa hotuba nzuri na kazi nzuri. Mchango wangu pia nitauwasilisha kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo naomba nijiunge na Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kutoa pole kwa familia ya Marehemu Amina Chifupa Mpakanjia, Mungu amlaze mahali pema peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Spika, sifa nyingi anazomwagiwa Mheshimiwa Marehemu Amina Chifupa hazifai kuachwa hivi hivi bali naishauri Serikali, atafutwe mwandishi mzuri iwe ni wa kujitolea na kulipwa atakayeweza kuandika kitabu cha mambo mbalimbali aliyoyafanya ili kuweza kuwa na kumbukumbu nzuri itakayotumika kumuenzi kwa kuendeleza kazi zake. Nadhani ni utaratibu mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja kwenye mkutano wa uwekezaji, akiwa mgeni wetu rasmi, mwezi Oktoba, 2006, wajasiriamali wachimbaji wadogo waliomba wasaidiwe katika nyezo, uwezeshaji wa utaalamu na masoko. Mheshimiwa Waziri Mkuu ali-*delegate* jukumu hilo kwa Mheshimiwa Marehemu Juma Akukweti. Sasa kwa kuwa hayupo jukumu ni letu sote, sasa nina ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, tunalo shirika la *STAMICO* ambalo kwa sasa lipo kwenye foleni ya kufungwa na *PSRC.* Shirika hilo lingeweza kuwa ni mkombozi mkubwa kwa wachimbaji wadogo wadogo, kuwa mwavuli wao, kwa mfano kusaidiwa vifaa vya kuchoronga, kutafuta masoko na kuwasaidia kuongeza ujuzi. Wafanyakazi wa Shirika hilo kwa sasa wengi wapo kwenye likizo isiyo na malipo. Nashauri tusitishe ufungaji wa Shirika la *STAMICO* na badala yake liboreshwe kwani wakati ule lilistahili kufikia hapo, lakini kwa sasa ni wakati mwafaka wa kulifanya liweze kusaidia wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, mfano kwa sasa *STAMICO* ina leseni ya kutafuta *limestone* Mikindani, Mtwara. Likifanikiwa watakuwa wamewezesha uwekezaji wa kiwanda cha

saruji Mtwara na hivi kuwezesha matumizi mazuri ya gesi ya *Mnazi Bay* ambayo inakadiriwa kuwa na uwezo wa kuzalisha *MW 300,* kuongeza ajira kwa watu si chini ya 5,000. Pia wachimbaji wadogo wa *Gypsum* wa Kilwa wataweza kupata soko badala ya kuagiza toka nje. Hata hivyo mwaka 2004 kulikuwa na Tume ya Dkt. Kipokola kuhusu sera ya madini na hatma ya *STAMICO.* Nashauri iangaliwe na ifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Spika, mkoa wa Ruvuma ni mkoa wenye rasilimali nyingi sana. Tuna ardhi yenye ukubwa wa takribani kilomita za mraba 63,000, tuna Ziwa Nyasa lenye kilomita za mraba karibu 4,000, fukwe safi zenye vina virefu na *cliffs.* Udongo wake ni mwekundu na wenye rutuba *(loam soil),* tuna mabonde mazuri sana kwa kilimo cha mpunga, lakini pia tuna madini mengi aina ya dhahabu na aina mbalimbali za *gemstone.* Pia tuna mbuga kubwa za wanyama *Selous* na Liparamba na mvua za kutosha.

Katika *Tanzania investment report, 2004 FDIs* Ruvuma ni kati ya mikoa yenye kiwango cha chini kabisa (3%) cha uwekezaji ikilinganishwa na mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Kilimanjaro, Dar es Salaam na Arusha ambayo inaoongoza ni karibu asilimia 88. Lakini yote hiyo ilisababishwa na kutokuwa na miundombinu hasa ya umeme na barabara. Tulikuwa kama yatima, miaka 45 ya Uhuru makao makuu hamna umeme wa kuaminika na Mbinga ambapo ni Makao Makuu ya Wilaya kongwe haina umeme kabisa.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru sana Serikali hasa katika kipindi hiki kuamua kuelekeza nguvu sasa mkoa wa Ruvuma. Barabara ya Masasi - Tunduru - Songea *Mbamba Bay,* tumepata pesa, umeme Makambako - Songea, Serikali yetu na wafadhili wetu Sweden tunashukuru sana. Ombi letu Bajeti ya mwaka kesho kazi hizo ziripotiwe kuwa zimemalizika au kuwa na *progress* nzuri. Tuna uhakika baada ya kukamilisha kasi yetu ya maendeleo itakuwa haielekezi. Leo tuna hali hii ni wa nne kwa uchumi je, wakati huo hali itakuwaje? Hatutaiangusha Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, pia natoa wito kwa wawekezaji wa ndani na nje kuwahi kushika maeneo ya kuwekeza wasije wakajilaumu wenzao wakiwahi. Naomba pia kufahamu kuhusu jenereta za Mbinga, mara ya mwisho wakati nafuatilia nilielezwe kuuwa *Letter of Credit (LC)* ilikuwa ipo Wizara ya Fedha bado haijasainiwa. Sasa sijui hali ikoje kwani nafahamu utengenezaji utatumia wiki 55 na mahitaji ya Mbinga *(KvA 320* tu).

Kuhusu hospitali yetu ya Songea ina matatizo makubwa, mimi binafsi nimetembelea hospitali zetu kubwa zote lakini matatizo huzidiana. Inanishangaza kuona Mbunge anapochangia badala ya kueleza hoja zake, kuumizwa na maborehso ya hospitali ya Songea. Jamani mkumbuke wote tunapata ila katika nyakati tofauti na vipaumbele tofauti. Suala la mgao mkubwa sana kwenye mikoa yenye mapato makubwa hiyo ni sera ya Majimbo. Kama hivyo wote tufikishwe kwanza kwenye uwekezaji uliofanana. Mikoa mingine ni maarufu kwa kulima chakula na joto ya jiwe ya njaa kila mtu anaifahamu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuwashirikisha wananchi kwenye kazi za maendeleo kwanza napongeza maeneo yako ya ukurasa wa 68, *"if you .....problem."* Nami naongeza: *"Give a man a fish and you feed him for a day; teach him how to fish and you*

*feed him for a life time," Steven R. Covey – Principle Centered Leadership.* Pia, *"The power of positive thinking; The power of appreciation and create the power within yourself (Better yourself series)."*

Mheshimiwa Spika, nami naungana nawe, wala isikukatishe tamaa. Suala la kukataza wananchi, wasijitolee katika kujiletea maendeleo yao wenyewe ni suala la uharamia na hujuma ya rasilimali watu katika Taifa letu. Watoto wanaosaidiwa ni wetu sisi wenyewe. Anayefaidika wa kwanza na mtoto ni mzazi mwenyewe. Hata hivyo shule, zahanati ni mahitaji ambayo wananchi wenyewe tunavyopita kwenye kata na vijiji wanaomba na kukerwa na uhaba uliopo. Hebu tuweni wajasiriamali kwa kuwa *innovative,* kuwa *creators, action oriented people as well as good reflectors* wa kujua tunakotoka na tunakokwenda. Umaskini wetu umetengeneza wavu mkubwa sana. rushwa, magonjwa, elimu duni, njaa, vifo vya watoto na kadhalika. Lazima tutumie kila aina ya mbinu ya kujitoa tuliopo. Baadaye tutalegeza kamba *automatically*. Kama watu hawatachangia ni kuwafanya wawe tegemezi kwa wafanyakazi na wafanyabiashara wachache. Huo utakuwa ni uonevu na unanyima kiu ya kujituma wale wanaothubutu *change of attitude* ndiyo muhimu hata kama kwa sasa mtoto hapati elimu ya kiwango, ni bora kuliko kumwacha kabisa kwanza umri wake unaomwingiza katika *labour market* ni mdogo na hivyo kujiunga kijiweni na kuendelea kuwa tegemezi. Tuchukulie shule hizo kwa sasa ni sawa na kambi, hawezi kukosa kitu kabisa! Ataambulia hata kuwa na marafiki na tabia njema.

Mheshimiwa Spika, tuna tabia ya kuto-*appreciate,* ambayo inanyong'onyesha watu kufanya zaidi na pia kuwatisha watu wetu kuwa hatuwajali hiyo ni hujuma kubwa kuliko ya pesa, kwani inawaharibu watu kisaikolojia na kuongeza chuki miongoni mwetu na *impact* yake inadumu kizazi hadi kizazi.

Mheshimiwa Spika, *CDF* watu wanaipiga vita, mimi sioni *logic.* Hebu wawe *flexible* na kuboresha sehemu wanazofikiri kuleta mapungufu kuliko kuzuia mabadiliko yanayolenga maendeleo, hii nitaichangia zaidi kwenye Muswada wa Mfuko wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, kuhusu makongamano/warsha, wengi wanashindwa kuelewa kuwa hakuna *investment* kubwa na muhimu kiuchumi kama kunoa vichwa. La msingi ni kuona *effectiveness* ya programu yenyewe. Hiyo naunga mkono.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mikopo, malalamiko ya mikopo maarufu kwa jina mabadiliko ya JK ni changamoto. Katika mchango wangu wa awali nilisema Serikali iwe jasiriamali, ikopeshe watu. Serikali imekopesha, malalamiko ni mengi sawa, lakini tunajifunza nini? Ni kwamba hiyo inaonyesha ukubwa wa hitaji la mikopo. Benki zote haziendi vijijini na watu wetu walikuwa hawana pa kusemea kwani zile benki ni binafsi na zinaangalia faida. Lakini pia waliopewa kugawa walishakuwa na tabia zao za kutowaamini wajasiriamali wadogo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo watu wengi wamefaidika na mikopo hiyo na kuzifanya benki nyingi kuwa *more proactive* na nyingine kushusha riba. Isitoshe mikopo hii ina *experience* ya mwaka mmoja tu, wakati kuna mabenki yenye *experience* ya miaka

45. Tumefanikiwa sana, tunachotakiwa ni kuboresha tu na sio kurudi nyuma. Safari hii hata akina yakhe wamepata mkopo.

Mheshimiwa Spika, ila kinachotakiwa ni ku-*support* zaidi katika mafunzo ya *income generating activities*. Ruvuma tumeshaanza *Ruvuma Entrepreneurship incubator (Better Life Tanzania)* lengo letu ni kuangua na kulea wajasiriamali vifaranga hasa kwa akinamama na vijana. *Challenge* yetu ni namna ya kupata mikopo ya kuatamia. Kwani ugumu ni *partners* kutokuwa *flexible* na kukubali mawazo mapya.

Hata hivyo hali inaonyesha mwanzo mzuri, endapo itafanya vizuri basi tutasambaza *model* hiyo kwa wenzetu wa maeneo mengine. Tunaomba tupate dhamana itakayotuwezesha kuwa na *overdraft* wakati kifaranga kijasiriamali kinapokuwa tayari kuanza kazi. Mpaka sasa kwa muda wa miezi miwili toka tuanze tumeangua vifaranga vijasiriamali 67 ambao bado tunawakuza kwa kushirikiana na asasi nyingine kama *SACCOS, SIDO, TIRDO, VICOBA* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, suala la nauli daladala naomba *SUMATRA* wafanye hesabu na watangaze bei mpya mara moja ili kuondoa usumbufu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafi wa jiji (najihusisha na taka), ni muhimu kuwa na *temporary station* (vidampo) za taka katika kila Mji mdogo. Wote tunajua kila nyumba lazima iwe na choo. Sasa mbona tunapopanga miji yetu tunasahau vyoo vya mji ambayo ni sehemu ya kuhifadhi taka? Ni kitu muhimu sana! Matokeo yake ni kutupa taka barabarani na sheria ya mtu kutunza usafi wa eneo linalozunguka mbona hatuisisitizi? Hiyo haihitaji pesa ya Serikali, kinachotakiwa ni kuwajengea watu mazoea tu. Tena hata wakipigwa faini zitasaidia kuwalipa hao mgambo wetu wa ukaguzi tayari ni ajira.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uanzishaji wa miji midogo nje ya jiji ni sahihi kabisa, tumechelewa lakini pia kuwepo na soko la chakula au bidhaa lenye bei ndogo nje ya mji ambalo siku ya Jumamosi watu wawezeshwe kwenda huko kwa usafiri nafuu. Mfano tiketi ndani ya saa tatu kwa shilingi 400 kwenda na kurudi, hii itasaidia kujenga utamaduni wa *shopping* kwa wiki na kubana matumizi. Pia *supplus* ya *SGR* inaweza kuuzwa huko na kuwa-*encourage* wakulima kuwa na soko la mazao yao. Hiyo nilijifunza Norway, mwaka 1996.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo kwa heshima na taadhima naunga mkono hoja.

**MHE. ALHAJ PROF. JUMA A. KAPUYA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri iliyoelezea kwa ufasaha mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Nne katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi yaliyoanza kujitokeza mapema kabisa. Yako mambo ambayo kutokana na Makadirio ya Ilani malengo yake yalikuwa yafikiwe mwaka 2010. Leo malengo haya yamefikiwa na kufanikiwa kwa kiwango kikubwa sana. Mifano halisi ni kama vile elimu. Ilani ilituelekeza tuweze kuingiza sekondari asilimia 90 kwa nchi nzima ya watoto wote

waliofaulu wamepata nafasi ya sekondari. Ipo mikoa ambayo imeweza kuchukua asilimia 100 ya watoto waliofaulu. Hiki ni kitendo cha kujivunia sana.

Pia kuna mafanikio makubwa katika ujenzi wa barabara za lami nchi nzima. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa jinsi anavyojituma kwa yeye mwenyewe kusimamia utafutaji wa fedha za ujenzi wa barabara ya lami toka Manyoni kupitia Itigi-Tabora - Kaliua hadi Kigoma. Mimi na wananchi wa Urambo Magharibi, tunampongeza sana na pia tunamshukuru kwa kufanikisha Mkataba wa ujenzi wa Daraja la Mto Malagarasi. Kitu hiki kilikuwa ni ndoto kwa muda mrefu sana, sasa ndoto hiyo Mheshimiwa Rais wetu wa Awamu ya Nne kaitafsiri kwa vitendo. Tunampongeza sana na tunaomba asikatishwe tamaa na maneno ya watu wasioelewa kinachoendelea au wasiotaka kuelewa. Tunaahidi kuwa sisi ambao ni sehemu ya utendaji wake tutaifanya kazi ya kuelimisha wananchi usiku na mchana.

Mheshimiwa Spika, yapo mafanikio pia katika sekta za afya, japo hapo tunaiomba Serikali iongeze kasi ya kufundisha watalaamu ili zahanati zetu Wilayani Urambo ambazo zimekaa muda mrefu bila kufunguliwa ziweze kufunguliwa na kuanza kazi.

Mheshimiwa Spika, suala la maji hususani mradi wa *World Bank* tunaomba lipatiwe msukumo mpya ili wananchi wa Wilaya ya Urambo ambao wako katika mradi huu waweze kunufaika mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba nijielekeze katika suala la utawala, hapa nakusudia kuelezea nia ya wananchi wa Urambo Magharibi kuomba eneo lao sasa Serikali ilibadili na kuwa Wilaya ya Kaliua. Hii ni katika kutekeleza dhana nzima ya kupeleka madaraka kwa wananchi ili kuongeza kasi ya maendeleo yao. Mchakato wa kuiomba Serikali Kaliua kuwa Wilaya umeanza siku nyingi. Tayari wananchi wa vijiji vyote walishawasilisha mihutasari ya vikao vya Serikali zao na yote imeonyesha kulisemea sana ombi hilo. Pia, *WDC* nazo zote zimekwishakaa na kwa kauli zenye kufanana zimeunga mkono ombi hili. Hatimaye, Baraza kamili la Halmashauri ya Wilaya ya Urambao *(Full Council)* nalo limeafiki ombi hili kwa kauli moja. Hili lilifanyika baada ya vikao vya Kamati za wataalamu na Kamati za Baraza lenyewe kulifanyia uchambuzi wa kina suala hili.

Kamati zote ziliona hii ni hoja iliyokamilika. Kwenye *full council* iliyojadili suala hili na kulipitisha kwa kauli moja, Wabunge wote wawili walikuwepo, Mheshimiwa Samuel Sitta, Spika na Mbunge wa Urambo Mashariki na Mheshimiwa Alhaj Profesa Juma Athumani Kapuya, Mbunge wa Urambo Magharibi na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Sababu za kuomba kuigawa Wilaya ya Urambo na kuzaa Wilaya ya Kaliua zimeambatanisha katika kiambatisho A.

Mheshimiwa Spika, ni maombi yetu sisi wananchi wa Wilaya ya Urambo na hususan wananchi wa Urambo Magharibi, Serikali iridhie maombi yetu haya na kuagiza Wilaya mpya ya Kaliua kuanzishwa.

Baada ya kusema hayo, narudi tena kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa TAMISEMI, watendaji wao Wakuu wa Wizara na Wizara kwa ujumla kwa hotuba yao nzuri inayotupa dira sisi ambao ni sehemu ya timu ya Serikali katika kufanikisha utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, maelezo kuhusu Wilaya ya Urambo, Wilaya ya Urambo ni kati ya Wilaya sita za mkoa wa Tabora. Wilaya hii ilianzishwa rasmi tarehe 1 Julai, 1975. Inalo eneo la kilomita za mraba 25,995; ambayo ni sawa na asilimia thelathini na nne ya eneo la Mkoa wa Tabora. Kati ya eneo hilo, asilimia kumi na moja sawa na kilomita za mraba 2,859.4 hutumika kwa makazi na kilimo na eneo lililobaki la 89% au sawa na kilomita za mraba 23,135.55 ni misitu, mbuga na maji. Makao Makuu ya Wilaya yapo Mji Mdogo wa Urambo, wenye watu wanaokadiriwa kufikia 25,000. Umbali toka mjini Tabora ambao ndio Makao Makuu ya Mkoa wa Tabora ni kilomita 90.

Mji wa Urambo unafikika kwa barabara, reli na ndege ndogo. Wilaya ya Urambo ipo katika *Latitude* $40^{o}00$*” – *$50^{o}00$*”* na *Longitude* $30^{o}00$*: -* $32^{o}37$*”* na ipo mita 1,100 juu ya usawa wa bahari. Hali ya joto ni kati ya nyuzi $21.3^{o}C$ na *25.7oC.* Kipindi cha joto ni kuanzia mwezi Agosti hadi Oktoba ya kila mwaka. Aidha, Wilaya ya Urambo, hupata mvua kuanzia mwezi Oktoba hadi Mei, mwaka unaofuata, kukiwa na kipindi cha ukame cha karibu wiki mbili za mwezi Januari/Februari, kwa wastani, Wilaya hupata mvua kati ya mm 900 hadi 1,300 ambazo huongezeka toka Mashariki kwenda Magharibi.

Wilaya ya Urambo, inapakana na Wilaya za Nzega, Uyui na Sikonge kwa upande wa Mashariki na kwa upande wa Kusini inapakana na Wilaya ya Mpanda (Mkoa wa Rukwa). Upande wa Kaskazini inapakana na Wilaya ya Kahama (Mkoa wa Shinyanga) na kwa upande wa Magharibi inapakana na Wilaya ya Kigoma (Mkoa wa Kigoma). Wilaya ya urambo ina majimbo mawili ya uchaguzi, Tarafa 4, Kata 23, vijiji 97 na vitongoji 462 kama ifuatavyo:-

(a) Jimbo la Urambo Magharibi katika Tarafa ya Kaliua kuna vitongoji 154, vijiji 36, kata 7, tarafa ya Ulyankulu ina kata 4, vijiji 15, vitongoji 98.

(b) Katika Jimbo la Urambo Mashariki katika tarafa ya Ussoke ina kata 4, vijiji 15, vitongoji 73 na katika tarafa ya Urambo kuna kata 8, vijiji 31 na vitongoji 137.

Pia kuna vijiji 11 vinavyounda eneo la makazi ya wakimbizi la Ulyankulu toka Burundi, waliokimbia nchi hiyo tangu miaka ya 1972/1973. Eneo hili lipo katika Tarafa ya Ulyankulu; na lina Kata tatu.

Idadi ya watu, kulingana na Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2002, Wilaya ya Urambo ina jumla ya wakazi wapatao 370,796, kati ya hao, wanawake ni 187,567 na wanaume ni 183,229. Kuna jumla ya Kaya 62,633. Wastani wa ukubwa wa kaya moja ni watu 5.9. Ongezeko la watu kwa mwaka linakisiwa kuwa 4.2%. Hivi sasa idadi hiyo ya

watu imefikia 468,121 kutokana na uhamiaji wa kasi hasa toka kwa wafugaji. Idadi hii imepatikana toka kwa watendaji wa kata.

Maelezo ya eneo linalokusudiwa kuwa Wilaya mpya ya Kaliua, eneo linaokusudiwa kuwa Wilaya ya Kaliua lina ukubwa wa kilomita za mraba zipatazo 15,000, ambayo ni sawa na asilimia 58 ya eneo la Wilaya ya sasa. Kwa kuzingatia idadi ya watendaji wa kata idadi ya wakazi hivi sasa ni 240,146 kati yao wanaume wakiwa 99,505 na wanawake 140,641. Idadi hii ni sawa na asilimia 53 ya wakazi wa Wilaya ya Urambo. Idadi ya kaya ni 58,864 zikiwa na wastani wa wakazi 4.01 kwa kila kaya (Sensa ya mwaka 2002), idadi ya wakazi ilikuwa ni 184,039 kati yao wakiwa wanaume 65,505 na wanawake 118,534 kwa idadi ya kaya 38,864 ikiwa na wastani wa watu 4.7)

Mgawanyo wa watu kikata, idadi ya watu katika kata 23 ni kama ifuatavyo:- Pamoja na tarafa za Kaliua ya Ulyankulu zinazopendekezwa kuunda Wilaya ya Kaliua. Eneo hili linalokusudiwa liwe Wilaya mpya na Kaliua ndio lenye wageni wakazi *(setter visitors)* ambao idadi yao ni 64,667 na kwa hiyo, kufanya jumla ya wakazi wa eneo hili kufikia 304,813.

Kutokana na baadhi ya kata kuwa kubwa sana na idadi ya wakazi kuwa kubwa pia, inawezekana kata hizo kugawiwa na kupata kata mpya sita na tarafa moja. Kata ambazo zinaweza kugawanywa ni kata za Kazaroho, Kata ya Ushokola na Kata ya Imalaupina. Kata ya Ukumbisiganga kuwa kata ya Ukumbisiganga na kata ya Uyumbu. Kata Kashishi kuwa kata ya Kashishi, Kata ya Seleli na Kata ya Sasu. Kata ya Igagala kuwa kata ya Igagala na Kamsekwa. Hivyo, kata ya Igagala kuwa kata ya Igagala na Kamsekwa. Hivyo kata sita ambazo zitazaliwa ni kata za Igwisi, Imalaupina, Uyumbu, Sasu, Seleli na Kamsekwa.

Mgawanyo wa Kata hizi, utasaidia kuboresha utoaji huduma za jamii na uchumi hatimaye kuongeza kasi ya kuondoa umaskini wa wananchi hivyo kuboresha maisha yao. Inapendekezwa, kuongeza tarafa moja ya Ukumbisiganga. Ongezeko la Tarafa moja kutasaidia kuleta ufanisi katika utawala, usimamizi na utaratibu wa shughuli za Serikali. Wilaya inayopendekezwa itakuwa na tarafa tatu za Kaliua, Ulyakulu na Ukumbisiganga na jumla ya Kata 17 kama inavyoonyeshwa hapa chini mahindi, mihogo, maharage, njugu, ufuta, karanga, alizeti, mpunga michikichi na viazi.

Mazao ya biashara, kilimo ndiyo shughuli kuu ya kiuchumi na mazao ya chakula na biashara ikiwa ni pamoja na tumbaku, pamba, alizeti, ufuta, milonge mahindi, mihogo, mpunga, viazi vitamu na kadhalika huzalishwa kwa kiwango cha kutosha na ziada. Tumbaku ya kukaushwa kwa mvuke ndiyo zao kuu la biashara na limekuwa likilimwa kwa zaidi ya miaka hamsini sasa. Zao hili linachangia kwa sehemu kubwa katika pato la wananchi, Halmashauri ya Wilaya, na Serikali Kuu (Fedha za Kigeni).

Kilimo cha tumbaku, kinalimwa kupitia vyama vya msingi. Eneo linalopendekezwa, lina vyama vya ushirika vya msingi (vya tumbaku) 32, na wakulima wa kujitegemea sita. Zao la tumbaku ya kukaushwa na mvuke huliingizia Taifa fedha nyingi za kigeni na mkoa wa Tabora unaongoza kwa uzalishaji nchini ambao inazalisha

zaidi ya asilimia 70 wakati eneo linalopendekezwa kuwa wilaya ya Kaliua linazalisha zaidi ya asilimia 50 ya uzalishaji wa wilaya. Mfano msimu 2004/2005 eneo hili lilizalisha kilo milioni 7.2 ikiwa ni zaidi ya asilimia 51 ya uzalishaji wa wilaya.

Tumbaku bora zaidi Kitaifa, huzalisha toka eneo hili katika kijiji cha Kanoge kata ya Mwongozo. Eneo linalopendekezwa lina jumla ya shule za msingi 73 zenye wanafunzi 48,333 kati yao wasichana 22,629 na wavualana 25,698. Walimu 272 *(IIIA), (IIIB/C)* 201, na *Diploma* sita. Wastani wa mwalimu kwa wanafunzi ni 1:58. Vipo vyumba vya madarasa 890 na kufanya wastani wa wananfunzi wa darasa 1:80 ikilinganishwa na kiwango cha Taifa 1:45. Wastani wa wanafunzi kwa dawati ni 1:4, na wanafunzi kwa kitabu 1:3. Eneo hili lina mkakati wa kuboresha elimu ya msingi kwa kuongeza vyumba vya madarasa, nyumba za walimu 234; vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Kasi ya ujenzi ni kubwa kutokana na wananchi wake kutumia na kujitolea kuandaa tofali za kuchoma kupitia makato ya mwanzo ya mazao ya biashara (Tumbaku). Vilevile kujitolea kwa nguvu zao.

Eneo linalopendekezwa kuwa Wilaya lina shule za sekondari 10 na zote zinamilikiwa na Serikali. Kati ya Kata 11 za hivi sasa mfano, Kaliua, Ukumbisiganga, Igagala, Ichemba, Kashishi, Uyowa Mwongozo, Makazine na Kazaroho, Kata nne zilizobaki zinaendelea na ujenzi ikiwa katika hatua mbalimbali mfano, Mwongozo, Usinge, Ugunga na Ushokola. Upo uwezekano wa shule hizi kufunguliwa mwakani (2007). Ujenzi wa shule hizi kwa sehemu kubwa unagharimiwa na wananchi wenyewe na msaada kidogo toka wahisani na Serikali. Ipo *cluster* moja Kata ya Kaliua. Shule moja ya Kaliua sekondari imeruhusiwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kuwa madhehebu ya Kanisa la Moravian hivi sasa wanajenga sekondari ya bweni katika Kata ya Kalua Kata ya Ukumbisiganga wameanza ujenzi wa sekondari ya pili pale Kangeme ili kutosheleza mahitaji yao ianzishe mikondo ya Elimu ya Juu *(High School)* mwaka 2007.

Eneo linalopendekezwa lina chuo kimoja kikubwa cha *VETA* (Ulyankulu) kinachotoa Elimu ya Ufundi Stadi za Fani mbalimbali zikiwemo umeme, ushonaji, cherehani, uchomeleaji wa vyuma, fundi bomba, magari na kompyuta. Wahitimu baada ya kumaliza eneo yao hujiajiri wenyewe. Hivi sasa madhehebu ya waislamu nao wameanzisha ujenzi wa Chuo cha *VETA* katika Kata ya Kaliua.

Kuhusu afya, eneo linalopendekezwa lina zahanati kila kijiji. Zahanati hizi ni za Serikali zimejengwa kutokana na nguvu za wananchi na msaada kidogo toka Seriklini na wahisani. Vipo vituo vya afya viwili kati yake kimoja kinamilikiwa na Serikali (Ulyankulu) na kimoja Shirika la Dini la *RC* (Kaliua). Kuna mpango wa kukipandisha hadhi kituo kimoja cha afya (Kaliua) kuwa hospitali teule hivi karibuni. Upandishwaji hadhi unatokana na ukubwa wa kiwango cha huduma bora inayotolewa mfano, upasuaji, *X-Ray,* malazi na huduma ya gari la wagonjwa *(ambulance).* Wastani wa huduma ni zahanati moja kwa watu 14,000 ili ikilinganishwa na viwango vya kitaifa vya zahanati 1:10,000.

Huduma za kiuchumi, viwanga vidogo vidogo. Viwanda vidogo na vya kati vipatavyo 40 vinapatikana katika eneo hili, na vinajishughulisha na utoaji huduma katika nyanja zifuatazo; uhunzi, useremala, uokaji mikate, utengenezaji majiko, magari na pikipiki. Aidha, kila kijiji kina mashine zisizopungua nne zinazotoa huduma ya kukoboa na kusaga nafaka.

Kuhusu usafiri na usafirishaji, miundombinu iliyopo. Eneo hili lina miundombinu ya aina tatu yaani barabara, reli na viwanja vya ndege.

Kuhusu barabara, ina barabara zinazomilikiwa na Mkoa *(Regional Roads)* zenye urefu wa kilomita 186 barabara hizi zimewekewa changarawe na hupitika mwaka mzima. Barabara hizi za mkoa zinaunganisha eneo hili na Wilaya nne za jirani mfano, Kigoma, Nguruka, Uvinza, Malagarasi, (Kigoma) Tabora, Nzega na Urambo (Tabora). Mbali ya barabara hizo, kuna kilomita 190 barabara zinazohudumiwa na Wilaya, barabara hizi zimewezesha Kata zote kuunganishwa kwenye barabara za Mkoa. Jumla ya kilomita 587 ni barabara za vijiji na kwa sehemu kubwa zinahudumiwa na Serikali za vijiji na kwa sehemu kubwa zinahudumiwa na Serikali za vijiji pamoja na Makao Makuu ya Kata. Barabara hizi zimewezesha upatikanaji wa huduma za uchumi na jamii, mfano usambazaji wa pembejeo za kilimo. Bidhaa, ubebaji wa mazao na usafiri wa abiria. Aidha, upo mpango wa ujenzi wa barabara kiwango cha changarawe utakaounganisha eneo hili na Wilaya za Mpanda (Rukwa) na Kahama (Shinyanga). Wahisani (Serikali ya Ubelgiji) wameonesha nia ya kusaidia ujenzi huu katika kipindi cha mwaka wa fedha 2006/2007. Ujenzi unakadiriwa kugharimu shilingi bilioni 13 kwa kilomita 300.

Kila kijiji kina mkakati wa kutengeneza madhabati kwa ajili ya kukabiliana na maeneo makorofi ili barabara zao zipitike mwaka mzima. Kuhusu reli, eneo la reli katika eneo linalopendekezwa kwa Wilaya lina urefu wa kilomita 250; ikiwa ni sehemu ya reli ya Kati kutoka Dar es Salaam kupitia Tabora kwenda Kigoma na reli ya pili ya Tabora – Mpanda. Vipo vituo vya reli kama Kaliua, Kombe, Usinge (reli ya kwenda Kigoma) na Uyumbu, Kangeme, Zugimlole, Lumbe, Usinga na Ukumbi Kakoko (kwenda Mpanda). Kituo cha Kaliua ni njia panda kwenda reli ya Kigoma na Mpanda.

Kuhusu ndege, vipo viwanja viwili vinavyotumuka kwa usafiri wa ndege ndogo kama Kaliua na Kabanga. Viwanja hivi vimewekewa changarawe hivyo imewezesha kutolewa kwa huduma mwaka mzima. Viwanja vingine viwili kama Luganjo na Mukuba vipo kwenye vitalu vya uwindishaji wa utalii na kutumika kipindi cha kiangazi tu kwa ajili ya huduma za kitalii.

Kuhusu hali ya mawasiliano ya simu, eneo hili lina mawasiliano ya simu za mkononi, upepo *(Radio Call)* na simu kupitia Shirika la Reli Tanzania *(TRC).*

Kuhusu simu za mkononi, huduma hii inatolewa na Kampuni ya *Celtel.* Ipo minara minane katika maeneo tofauti ambayo imewezesha huduma kupatikana katika kata zote kwa asilia 100. Hivi sasa Kampuni za *Vodacom* na *Tigo* nazo zimeanza kujenga minara yao ili kuendelea kuboresha mawasiliano.

Simu kupitia Shirika la Reli *(TRC):* Huduma inapatikana katika vituo vyote 9 vya Reli vilivyo katika eneo hili. Simu ya Upepo *(Radio Call),* mawasiliano ya *radio call* yanapatikana katika Kata 5 kati ya 11. *Radiocall* zimewekwa kwenye vituo vya Afya/Zahanati, (Usinge) na vituo vidogo vya Polisi (Kaliua, Ukumbisiganga, Lumbe na Ulyankulu). Kuwepo kwa mawasiliano haya ya aina tatu, kumewezesha eneo hili linaloomba kuwa Wilaya kuwa na mawasiliano ya urahisi na uhakika kwa Kata zote mwaka mzima.

Kampuni ya *Vodacom* inaanzisha huduma zake na imekwisha nunua maeneo sita katika sehemu mbalimbali kwa ujenzi wa minara. Mawasiliano ya kampuni hii itahusu Kata 9 kati ya 11 kabla ya Machi 2007. Kampuni ya *Mobitel (Buzz/Tigo)* imekwisha ainisha maeneo yatakayojengwa minara kwa ajili ya huduma kwenye Kata 6 kati ya 11 kabla ya mwezi Aprili, 2007. Kampuni ya simu ya *TTCL* ina mpango wa kuboresha huduma za simu za *Digital* iliosisitishwa kabla ya mwezi Aprili, 2007. Huduma hii itawezesha kupatikana kwa huduma za simu za mezani (Ofisini na Majumbani), *Telex* na *Fax* ifikapo mwezi Aprili 2007.

Inapendekezwa mji mdogo wa Kaliua kuwa Makao Makuu ya Wilaya ya Kaliua kwa sababu zifuatazo:-

(i) Kipo kituo cha Polisi chenye ghala ya kuhifadhia silaha pamoja na selo ya kuhifadhia watuhumiwa wa jinsia zote.

(ii) Mahakama ya Mwanzo ipo na inatoa huduma nyakati zote. Eneo la mahakama ni kubwa na jengo lake likikarabatiwa linaweza kutoa huduma ya mahakama ya Wilaya.

(iii) Kipo kituo kikubwa cha afya, kinachotoa huduma zinazolingana na hospitali mfano *X-ray,* upasuaji, madaktari wanaotembelea maeneo *(visiting doctors),* vyumba vya kulala na gari la kubeba wagonjwa.

(iv) Umeme wa uhakika *(National Grid)* upo kuwezesha mahitaji ya maofisi na wnanchi.

(v) Ipo barabara ya kudumu inayounganisha Makao Makuu ya Wilaya – Urambo na Mkoa wa Tabora. Hivi sasa barabara hii inajengwa kwa kiwango cha lami na itaiungnaisha Kaliua na Wilaya jirani ya Kigoma. Aidha, barabara inajengwa kwa kiwango cha changarawe itakayounganisha Kaliua na Wilaya za Kahama (Shinyanga) na Mpanda (Rukwa). Zipo barabara zinazoiunganisha Kaliua na Kata zingine zote katika eneo hili linalopendekezwa kuwa Wilaya ya Kaliua.

(vi) Usafiri wa mabasi makubwa na madogo *(Minibus)* upo wa uhakika na kutosha kwa wasafiri kwenda Kigoma, urambo na makao makuu ya Mkoa wa Tabora kwa mwaka mzima.

(vii) Usafiri wa garimoshi (Reli) ni wa uhakika, pia ni njiapanda ya kwenda Mpanda (Rukwa), Kigoma na Dar es Salaam, Mwanza kupitia Tabora.

(viii) Kipo kiwanja cha ndege cha changarawe kwa ajili ya ndege ndogo na kinatumika mwaka mzima.

*(ix)* Huduma ya maji ya bomba ipo na inawezeshwa na kisima kirefu kinachoendeshwa na mtambo mkubwa wa nguvu ya miongozi ya jua *(solar)*.

(x) Huduma ya Benki inapatikana mjini Urambo *(NMB)* umbali wa kilomita 30 tu na pana barabara ya uhakika ya kudumu ambayo hivi sasa inajengwa kwa kiwango cha lami. Kutokana na kasi ya kukua kwa uchumi, benki iliyokuwa Tarafa ya Kaliua itafufuliwa.

(xi) Mawasiliano ya simu za mkononi, upepo *(Radiocall)* na kupitia njia ya Reli yanapatikana muda wote, hivyo kuwezesha Kaliua kuwa kiungo cha mawasiliano na Kata zote za eneo linalopendekezwa kuwa Wilaya

(xii) Zipo hoteli na nyumba bora za kupanga watumishi wa Serikali na taasisi mbalimbali.

(xiii) Kaliua ina hoteli na nyumba za kulala wageni zaidi ya kumi na mbili zenye uwezo wa kuhudumia wageni zaidi ya 200 kwa wakati mmoja. Kutokana na kukua kwa uchumi na kuongezeka kwa wageni, kasi ya kujenga nyumba mpya za wageni imeongezeka.

(xiv) Maduka makubwa ya vifaa vya ujenzi na maofisini yanapatikana.

(xv) Vituo vikubwa vya mafuta vipo viwili na hutoa huduma za mafuta ya magari na mitambo mengine pamoja na mafuta ya kulainisha mitambo.

(xvi) Zipo kumbi kubwa tatu zenye uwezo wa kuhudumia watu zaidi ya 800 kwa wakati mmoja. Kumbi hizi zinamilikiwa na Taasisi za Serikali na watu binafsi zina uwezo wa kuhudumia vikao vya kiserikali na burdani kwa wananchi.

(xvii) Maeneo ya burdani, i.e. Viwanja na maeneo ya wazi kwa wakubwa na watoto yapo na baadhi yamekwisha endelezwa.

(xviii) Majumba ya Ibara kwa madhehebu yote yapo ya kutosha.

(xix) Mbali ya sababu zilizotajwa hapo juu, kubwa zaidi ni utayari wa wakazi wa mji mdogo wa Kaliua kupokea uamuzi pamoja na kuendeleza makao makuu ya Wilaya wanayoiomba ni mkubwa.

Sababu ya kuomba Wilaya ya Kaulia toka Wilaya ya Urambo ni pamoja na kuboresha huduma za kiuchumi na kijamii kama miundombinu ya barabara, hospitali, mfumo wa soko na kadhalika. Eneo hili huzalisha mazao ya biashara na chakula zaidi ya asilimia 60 ya uzalishaji wa Wilaya ya Urambo, lakini uendelezaji wa miundombinu haulingani na kiwango cha uzalishaji wake. Mfano, Mkoa wa Tabora unazalisha zaidi ya asilimia 70 ya tumbaku hii inazalishwa eneo hili. Mwaka 2004/2005, eneo hili lilizalisha tani milioni 7.7 sawa na asilimia 52 ya tumbaku iliyozalishwa Wilaya ya Urambo.

Sehemu kubwa ya mazao ya chakula ya Wilaya ya Urambo yanazalishwa eneo hili, hususan Tarafa za Ulyankulu na Kaliua. Mazao haya hulisha sehemu ya Tabora (Nzega na Tabora). Wilaya ya Urambo na baadhi ya Wilaya ya Mikoa ya jirani (Kahama na Shinyanga).

Pamoja na uzalishaji huu maeneo mengi ya eneo hili ynakabiliwa na matatizo ya miundombinu kiasi cha kutofikika nyakati za masika. Mfano kata ya Ukumbi Siganga.

(i) Kuongeza kasi ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii hivyo kuchangia uongezekaji wa kasi ya wananchi kujiletea maendeleo. Kutokana na kuboreka kwa huduma za kiuchumi na kijamii, kutatoa nafasi ya wananchi kutumia fursa mbalimbali zilizopo kwenye eneo hili kuongeza kasi ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii hivyo kuboresha maisha yao. Mfano: kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara pia kuanzisha mazao ya kudumu ya biashara hali hii. Itawezesha eneo kujenga uchumi imara na endelevu utakaohimili, mabadiliko ya kiuchumi duniani.

(iii) Kuwezesha uvunaji endelevu wa rasilimali zilipo kwenye eneo kwa azma ya kuongeza pato la Taifa na kuinua hali ya maisha ya wananchi wa eneo hili. Sehemu kubwa ya eneo linaloombewa kuwa Wilaya (kilomita za mraba 8,000 sawa na asilimia 53) imetawaliwa na misitu, mbuga za wanyamapori na maji (mito), mabwawa na maziwa) iliyohifadhiwa na isiyohifadhiwa. Baadhi ya maeneo ya wanyamapori yanatumika kwa uwindaji wa kitalii kwa kiwango kidogo sana (kilomita za mraba 2000). Aidha, yapo maeneo yameonyesha kuwa na dalili za madini na vito. Ukiacha uchimbaji wa wachimbaji wadogowadogo wa dhahabu, Rasilimali yote hii haijaendelezwa vya kutosha kuchangia pato pale Nsungwa la Taifa na kuboresha mapato ya wakazi wake.

(iv) Kupata eneo dogo linaloendelezeka haraka na kutawalika kirahisi. Wilaya ya Urambo ni kubwa sana i.e. kilometa za mraba 25,995; na idadi ya wakazi pia ni kubwa kama 370,796 kwa sensa ya mwaka 2002 na wakazi 468121 kwa makadirio ya sasa. Ukubwa huu unaathiri kasi ya uendelezaji na kuweza kutawalika kirahisi. Mfano, baadhi ya rasilimali (Fedha na

Nyenzo) toka Serikalini hutolewa kama Wilaya. Isitoshe vyombo vya usafiri vinavyotolewa na Serikali hutolewa kwa Wilaya bila kuzingatia ukubwa wa Wilaya.

(v) Khuus kuimarisha ulinzi na usalama wa watu na mali zao, ulinzi na usalama wa eneo hili umekuwa ukiathirika kutokana na kuwepo na wakimbizi (Kambi ya Ulyankulu) na pia kupakana na Kambi ya Wakimbizi (Katumba – Wilaya ya Mpanda). Aidha, ukubwa wa eneo pamoja na idadi kubwa ya watu kama ilivyoelezwa hapo juu, imefanya juhudi za kudhibiti uhalifu unaofanywa na baadhi wakimbizi hawa kwa mali na maisha ya wakazi wa eneo hili kutotoa matokeo mazuri sana. Kuwepo kwa dalili za baadhi ya wakimbizi kuhamia kuishi na kuzaliana katika baadhi ya vijiji (Kijiji cha Lumbe) ni matokeo dhahiri ya ukubwa wa eneo lisilodhibitika kwa urahisi. Ni jambo la busara eneo hili likawa Wilaya inayojitegemea ili kuimarisha udhibiti wa vitendo haramu vya wakimbizi hivyo kuimarisha ulinzi na usalama wa wakazi wa eneo hili pamoja na mali zao. Mgao wa Askari na vitendea kazi vyao haviendani na ukubwa wa Wilaya. Kuifanya Kaliua kuwa Wilaya nina hakika kutawezesha kusahihishwa kwa kosa hili na kwa hiyo ulinzi kuimarika zaidi.

(vi) Kutokana na sababu hizo hapo juu inatoa mwanya kwa watu wenye mawazo potofu kubeza juhudi na mafanikio makubwa ya (Serikali) za kuwaletea maendeleo na kuboresha hali ya maisha ya wananchi wake.

(vii) Utayari na ari ya wananchi, mara kadhaa wananchi wa eneo hili wamekuwa wakiomba na kurudia mara kwa mara kwa viongozi wa Kitaifa wanapozuru eneo lao kuomba iwe Wilaya inayojitegemea. Ari ya wakazi ya kujiletea maendeleo ni kubwa. Mfano katika kipindi cha miaka miwili tu (2005 – 2006) Kata zote katika eneo hili zitakuwa zimekamilisha ujenzi wa Shule za Sekondari. Kila kijiji kimekamilisha ujenzi wa zahanati na kuunganishwa na barabara. Sehemu kubwa ya mafanikio haya yametokana na nguvu za wananchi wenyewe na mchango mdogo toka Serikali na wahisani. Zipo dalili za eneo hili kukamilisha ujenzi wa nyumba za walimu, madarasa na madawati ya Shule za Msingi na Sekondari katika kipindi cha miaka miwili ijayo. Kimasingi uhitaji, utayari na ari ya wananchi kuwa na wilaya yao ni kubwa sana.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika katika Kikao hiki tukiwa wazima na wenye afya njema. Napenda kukupongeza wewe, Naibu Spika na Wenyeviti kwa kuliongoza Bunge vizuri pamoja na azma yako ya kulifanya Bunge letu kuwa Bunge bora katika Afrika.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa hotuba yake nzuri pamoja na wananchi wa Jimbo langu la kwa kazi nzuri waliyofanya

wakati wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005. Kwa vile nchi yetu imeingia katika mabadiliko mbalimbali ya kisiasa, kiuchumi na kijamii wakati umefika sasa wa kuwa na Katiba mpya yenye kubadilika *(Flexible Constitution*) badala ya kuendelea na Katiba ya sasa ambayo haibadiliki (*Rigid Constitution)*. Pia Katiba ya sasa ilitungwa katika mfumo wa chama kimoja wakati sasa nchi yetu imo katika mfumo wa vyama vingi vya siasa.

Mheshimiwa Spika, kero za Muungano zinapaswa kupatiwa ufumbuzi wa haraka wakati tunajitayarisha kuelekea Jumuiya ya Afrika Mashariki, tunaomba mazungumzo yanayoendelea hivi sasa baina ya *CUF* na CCM yapatiwe ufumbuzi wa haraka ili nchi yetu iendelee kuwa ya amani na utulivu na kuifanya Zanzibar iweze kupiga mbele hatua za maendeleo kwa maslahi ya Wanzazibari wote.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ajali za barabarani na majini pamoja na majanga mbalimbali yamekuwa mengi hapa nchini kwetu. Je, Serikali ina mikakati gani au mipango gani itakayosaidia kupunguza matukio hayo badala ya kusubiri mpaka maada yatokee ndipo hatua zichukuliwe.

Mheshimiwa Spika, wanaofanya ubadhilifu wa fedha wachukuliwe hatua za kisheria. Kukaa katika vituo vya kazi kwa muda mrefu kunachangia kuwafanya baadhi ya watumishi wafanye ubadhirifu wa fedha. Kwa hivyo, kuna haja kwa watumishi kubadilishwa vituo vyao vya kazi kila kuleta ufanisi kazini. Suala la elimu kuongeza majengo ni hatua moja lakini ni lazima hatua hii iende sambamba na upatikanaji wa walimu wenye uwezo, vifaa vya kufundishia na kusoma, maabara na kadhalika. Walimu wawe wa kutosha kulingana na mahitaji vinginevyo wanafunzi watakuwa wanakwenda na kurudi bila ya kufikia lengo lililokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kilimo kipewe uzito unaostahili hasa ukizingatia kwamba kilimo ni uti wa mgongo wa nchi yetu na asilimia 80 ya Watanzania wanategemea kilimo kwa maisha yao. Mazao makuu kama vile kahawa, pamba, korosho, tumbaku, mkonge, chai, pareto na kadhalika, yapewe msukumo unaofaa kwa ajili ya kuongeza uzalishaji utakaoleta tija. Pembejeo na huduma za ugani ziwafikie kwa wakati wakulima walioko vijijini. Wakulima wapatiwe masoko ya uhakika ili waweze kupata bei nzuri ya mazao yao.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu jinsi alivyowasilisha hotuba yake. Kwa kweli hotuba yake haikuacha kitu na imeangalia mambo makuu yote yaliyoainishwa katika Ilani ya CCM ya mwaka 2005. Ni kweli kuwa Serikali imesaini mikataba na kutoa leseni kwa kampuni 10 za utafutaji wa mafuta katika kina kirefu cha maji baharini na kwenye mwambao wa bahari ya Hindi na hii inafanya jumla ya leseni zilizotolewa hadi sasa kufikia 19.

Je, katika mwambao wa bahari ya Hindi ni leseni ngapi zimetolewa na kwa makampuni gani na mangapi na je, katika mwambao huo vinavihusisha visiwa vilivyoko Zanzibar, naomba ufafanuzi?

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa wapo wateja wengi wanaodaiwa na *TANESCO* na kusababisha malimbikizo makubwa ya madini. Aidha, naomba nitoe sisitizo kwa baadhi ya wafanyakazi wa *TANESCO* huwa na tabia ya kuwapatia wateja ambao wana madeni makubwa na kuwatisha na kudai fedha kinyume na Sheria na kuweka mifukoni mwao bila kusababisha mlundikano wa madeni makubwa kwa wateja huku *TANESCO* ikiwa na orodha ile ile ya madeni. Hivyo naomba kuishauri Serikali kulifuatilia suala hilo ili wananchi wanaodaiwa kuweza kulipa *TANESCO* na kupewa risiti za malipo hayo kufuatana na utaratibu uliopo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuweza kuchangia hotuba hii. Napenda kukupongeza wewe pamoja na Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wako wote wawili kwa kuendesha vikao vya Bunge hili kwa umahiri mkubwa na kufuata Sheria na Kanuni za Bunge hili na vile vile hatoa pole kwa wale waliopata ajali mbalimbali na kupoteza maisha yao na wale waliojeruhiwa Mungu awajalie wapone haraka, *Amin*.

Mheshimiwa Spika, ni kweli elimu imepewa Bajeti kubwa na kipaumbele, hili ni jambo zuri kwani elimu ni ufunguo wa maisha kwa kila binadamu na shule nyingi za msingi na sekondari zimejengwa mijini na vijiji na zinaendelea kujengwa. Ni jambo la kupongezwa Serikali na wananchi kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, lakini ni jambo la kusikitisha kuwa shule hizo hazina walimu wa kutosha, hazina madawati, maji, umeme, zahanati na hasa vijijini. Walimu hawana nyumba za kuishi, wenye vipaji vizuri hawaendi huko vijijini kwa matatizo kama hayo baadhi ya shule hakuna mabweni ya wanafunzi wa kike kuwa ni mchanganyiko. Hivyo huleta tatizo la kubeba mimba kiholela na kukatisha masomo yao, je tatizo hili litaondolewa lini?

Mheshimiwa Spika, kilimo pamoja na kuwekewa Bajeti ndogo lakini tuelewe kwamba kilimo ni uti wa mgongo wa Tanzania kwa hiyo, kuna kila haja kilimo kiimarishwe. Wakulima wengi vijijini ruzuku haiwafikii kununua mbolea wala hawana adawa za kuulia wadudu au kukuza mimea, mabwana shamba hawafiki vijijini kuwapa elimu wakulima juu ya kilimo jinsi ya kutumia mbolea ili wapate mazao kiasi kikubwa. Kwa hiyo, tunaomba Serikali kama kuna mtendaji hafanyi wajibu wake asionewe haya, afukuzwe mara moja, hafai na haitakii mema nchi hii wala hamsaidii mkulima.

Mheshimiwa Spika, usafiri na usafirishaji katika Jiji la Dar es Salaam. Jiji la Dar es Salaam lina nafasi pekee katika uchumi wa nchi yetu lakini kuna msongamano mkubwa wa magari. Kwa kweli naipongeza Serikali kwa kuliona hilo na kuazimia kujenga barabara ndogo ndogo ili kupunguza msongamano na kero ya wanaotembea kwa miguu na kupunguza ajali za kugongwa na magari. Namwombea kila la kheri Waziri Mkuu katika maisha yake na Taifa zima kwa ujumla. Mungu ibariki Tanzania.

**MHE. OMAR ALI MZEE:** Mheshimiwa Spika, napenda kufahamishwa ni lini Tume ya Uchaguzi itakuwa taasisi ya kujitegemea kama taasisi nyingine kwa kuwa Tume Uchaguzi ni chombo ambacho kinafanya kazi katika Ofisi ya Waziri Mkuu, uwezekano wa kuchukua majukumu na maelekezo kutoka Wizara husika ni mkubwa. Hivyo basi chombo hiki ni vyema kujitegemea na kwa lengo la kujenga mustakabali wa maelewano hasa katika kipindi cha uchaguzi ambapo pamekuwa na malalamiko mengi hasa katika chaguzi. Vile vile ningependa chombo hiki cha uchaguzi kusimamia chaguzi zote nchini.

Mheshimiwa Spika, daftari la wapigakura kuwa ni chombo nyeti, muhimu sana kwa demokrasia nchini kwa kujenga maelewano na kuaminiana. Napenda kujua dosari zote zitokanazo na daftari la wapigakura ni lini zitatatuliwa kwani kumekuwa na dosari nyingi kwa mfano kutotokea baadhi ya majina ya wapigakura, kuingiliana kwa majina baina ya kituo kimoja na kingine. Vile vile napenda kufahamu ni lini zoezi la kuhakiki daftari la wapigakura litafanyika kwani kuhakiki kutafanya waliokufa kuondolewa katika orodha na waliofikia umri wa kupiga kura wataorodheshwa. Ni vyema kutambua hilo kwa lengo na kuelewana na kutoa haki kwa mpiga kura kutimiza haki yake ya kuchagua na kuchaguliwa kwa lengo la kutimiza demokrasia ya kweli mfumo wa vyama vingi vya siasa.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kutambua na kuelewa kwamba Bunge ni muhimili unaojitegemea kwa lengo hilo utaweza kufanya kazi zake kutokana na mipango ambayo wenyewe umejiwekea. Napenda kuelewa je, hizi ofisi 40 za Wabunge zitajengwa Tanzania Bara tu au na Tanzania Visiwani na hususan Pemba ambapo hakuna Ofisi ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kueleweshwa juu ya uanzishaji na uendeshaji wa mfuko wa maendeleo wa Jimbo, kwa Tanzania Bara utakuwa ukisimamiwa na Halmashauri ni wazo zuri lakini napenda kujua kwa Zanzibar utasimamiwa na nani? Serikali ya Muungano au Serikali ya Mapinduzi? Napendekeza ni vyema kusimamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Wizara ihusikanayo na mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, napenda kuelewa kero ambazo ni za Muungano hatma yake zitakwisha lini na hasa katika kero nyeti ya mgawanyo wa fedha kutokana na misaada ya nje, imekuwa ni tatizo la kila mwaka ni vyema kutafutiwa ufumbuzi wa kufaa pamoja na kero nyingine ikiwemo na ile ya Mheshimiwa Rais juu ya mpasuko wa kisiasa unaoendelea kati ya Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Spika, mwisho namalizia na methali isemayo cheche huzaa moto, ni vyema kero zote zichambuliwe na zipatiwe majibu muafaka ili tujenge nchi yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sote ni wazalendo wa nchi yetu.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Moja nakumbushia ahadi ya Serikali kwenye ujenzi wa barabara ya lami. Barabara ya Manyoni – Itigi –Tabora –Kigoma na Nzega –Tabora –Ipole hadi Mbeya. Upo mpango gani wa uhakika ili ujenzi ukamilike kabla ya 2010?

Pili, napongeza kwa hatua za kuanzisha Halmashauri mpya 11 kwa kuwa Nzega imeanzishwa Halmashauri ya Mji Mdogo naomba maandalizi ya kupiga hadhi ya kuwa Halmashauri ya Mji wa Nzega.

Tatu, kuna mpango wa kuimarisha Shirika la Ndege *(ATC)* ili liwe kichocheo katika ukuaji wa uchumi na hasa suala la utalii? Napendekeza *ATC* iimarishwe kwa kupewa ndege kubwa mpya; na ndege za *propeller* kwa ajili ya mikoani.

Nne, uimarishaji wa Shirika la Reli ya Kati uwe sambamba na kuimarisha Bandari ya Kigoma kwa kupata soko la *DRC* Mashariki. Reli itasaidia kuimarisha uchumi biashara na huduma za jamii. Napongeza juhudi za Wizara kusukuma maendeleo hasa katika elimu. Naomba uwasukume wataalamu hasa watendaji wa Halmashauri kupata hati safi. Adhabu ya wahasibu wanaozembea iwe ya hapo hapo kinyume cha utaratibu wa sasa wa kuchukua hesabu za miaka ya nyuma. Nawatakia kheri.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Manyoni ina ukubwa wa eneo za kilomita za mraba 28,000 sawa na asilimia 58 ya Mkoa wa Singida wenye kilomita za mraba 49,000. Mkoa wa Singida ni wa tisa kwa ukubwa nchini kama takwimu zinavyoonyesha.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Manyoni ni takribani sawa na Mkoa wa Kagera wenye kilomita za mraba 29,000. Idadi ya watu wa Manyoni ni takribani 250,000 kwa sensa ya mwaka 2002; lakini watu wengi wameongezeka. Mwaka huo 2002 watu wengi hawakuhesabiwa kutokana na matatizo ya mpaka na Sikonge, Tabora. Kigezo cha idadi ya watu ili kuunda Wilaya ni watu wasiopungua 100,000 ukigawa Wilaya hii mara mbili kwa kigezo hicho tunakidhi kigezo hicho. Hata hivyo kuna mifano mingi inayoonyesha kuwa Wilaya kadhaa huko nyuma ziligawanywa kwa kuzingatia zaidi ukubwa wa maeneo yao. Mfano mmoja ni Liwale iliyoundwa mwaka 1976 na hadi sasa idadi ya watu haizidi 75,000 na pia Wilaya za Mkoa wa Arusha, Longido, Loliondo Ngorongoro na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kinachotia shaka ni kuona kwamba Mikoa yote nchini ilishapatiwa fursa ya kugawa Wilaya moja au mbili isipokuwa Mkoa wa Singida kama takwimu zinavyoonyesha. Wilaya ya Manyoni ni kubwa kuliko Mikoa ya Tanga kilomita za mraba 27,000, Mara kilomita za mraba 22,000, Mwanza kilomita za mraba 20,000, Mtwara kilomita za mraba 17,000 na Kilimanjaro kilomita za mraba 13,000.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Manyoni ina rasilimali nyingi za kilimo na misitu zikiwemo mbuga za akiba za Rungwa, Kizigo na Mhesi.

Mheshimiwa Spika, ombi na kwa unyenyekevu mkubwa na kwa niaba wananchi tunaomba kipaumbele cha kuigawa Wilaya ya Manyoni sasa ili iwe chachu ya kuleta maendeleo ya maeneo yake. Tunaamini hatua hiyo ndiyo itakuwa mwarubaini wa matatizo yetu mengi wa kuifanya dhana ya *D by D* iwe *more effective* Mkoa wa jirani wa Dodoma sasa hivi wanayo fursa nzuri ya kuendelea baadhi ya kupatiwa Wilaya mpya za

Chamwino, Bahi, Kongwa na inavyoonyesha hata Kondoa iko mbioni kugawanywa. Tayari *procedures* zote za kuomba Wilaya mpya tumefuata na maombo yetu hayo yapo ofisini kwako.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja. Naipongeza hotuba ya Waziri Mkuu imegusa karibu kila sekta, lakini nasikitika nimetafuta neno Pamba halionekani katika kitabu kizima cha Bajeti. Pamba imeajiri watu wengi na inaingiza pesa nyingi za kigeni; kwa hiyo, wakulima wa pamba wapewe ruzuku na wasikatishwe tamaa ikiwa ni pamoja na kutengenezewa barabara zao ili waweze kusafirisha mazao yao kwa urahisi.

Pili, sekta ya wachimbaji hasa wachimbaji wadogo wamekuwa wakitangatanga kufuatia maeneo yao kuchukuliwa na wachimbaji wakubwa na hali hii inaleta migogoro mikubwa baina yao. Hivyo basi naomba kuwe na utaratibu mzuri utakaowezesha wachimbaji wadogo kufanya shughuli zao vizuri na kuwe na maeneo yao maalumu.

Vile vile Wizara ya Nishati na Madini washirikiane na Wizara ya Maliasili na Utalii ili kuepuka migogoro inayojitokeza pale ambapo Wizara ya Nishati na Madini inapotoa kibali cha uchimbaji kwa wachimbaji wadogo na Wizara ya Maliasili na Utalii kuwafukuza katika maeneo hayo na kusababisha mapambano kati ya wachimbaji na Serikali kwa mfano katika eneo la Matabe. Kwa mantiki hiyo Wizara ya Maliasili na Utalii itoe kibali sambamba na kibali ili kuepuka hali kama hii kutokea katika maeneo ya madini.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo naomba wasaidiwe kupata umeme wa gridi ili kurahisisha utendaji wa kazi na kuongeza uzalishaji na Pato kwa Taifa. Hivyo basi nashauri umeme unaotarajia kupelekwa Bukombe upitie katika Jimbo la Busanda kwenye maeneo ya wachimbaji hawa hasa katika vijiji vya Bukori, Nyarugusu, Rwamgasa na Katoro.

Tatu, kuigawa Wilaya ya Geita, Geita ina eneo kubwa sana na idadi ya watu ni karibu laki tisa kwa sasa na ina majimbo matatu makubwa. Hivyo naomba igawanywe kwani kubwa mno kwa kuhudumiwa na Halmashauri moja. Pamoja na kuigawa Wilaya ya Geita, napendekeza iunganishwe na Wilaya ya Sengerema, Bukombe na Chato kuwa Mkoa mmoja. Kwa madhumuni ya kusogeza utawala na huduma karibu na wananchi. Nimependa ziunganishwe na Wilaya ya Bukombe na Chato. Kwa kuwa Wilaya jirani katika Mikoa jirani na zina matatizo makubwa katika kufuata huduma Makao Makuu ya Mkoa kwa sababu ya umbali na vile vile suala zima la kijiografia.

Mheshimiwa Spika, nne kwa kuwa wakulima wadogo wadogo wa Wilaya ya Geita wanazalisha matunda kwa kiasi kulingana na nyenzo hafifu walizonazo naomba wawezeshwe ili watumie nyenzo za kisasa zaidi na kuongeza uzalishaji wa matunda hayo na kuondoa tatizo la umaskini wa kipato na vile vile kukuza uchumi wa Taifa. Pia katika kufanikisha hili naomba tusaidiwe kupata mwekezaji wa kusindika mazao haya ya matunda ili tuweze kutumia juisi itengenezwayo Geita badala ya kuagiza toka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, tano nashukuru kwa kuongeza posho ya Madiwani kwa asilimia mia moja ingawa bado ni kidogo. Naomba wasaidiwe usafiri kwani shughuli zao wote tunazifahamu na wanashindwa kufikia malengo yao ya maendeleo kwa kukosa usafiri wa kuwazungusha katika maeneo yao ya Kata kwani wengi wao hutumia baiskeli au kutembea kwa miguu.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba sana katika ofisi 40 za Bunge zitakazojengwa katika mwaka huu wa fedha, Jimbo la Busanda liwe mojawapo kati ya Majimbo yatakayojengwa ofisi hizo kwani kwa hali halisi Jimbo ni kubwa mno na hakuna ofisi ya Mbunge popote pale katika Jimbo. Naomba nisaidiwe naunga mkono hoja.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia eneo la usafiri katika jiji la Dar es Salaam. Kwa ushauri wangu njia zote zinazochukuliwa sasa ikiwa ni pamoja na kufungua au kuboresha barabara zilizoko ni *very temporary measure. We have to plan for the next 100 years*. Ushauri wangu ni kuwa tuanze kuangalia utaratibu wa *trams* na *underground*, *railway system* wakati wa kujenga haya ni sasa. Tukichelewa haitawezekana watu watajenga majengo ya ghali na *compensation* itakuwa ngumu zaidi kuliko sasa. *We may have to do it now an the only option.*

Mheshimiwa Spika, kuwa na mpango maalum wa kuongeza maghorofa ya *parking*, njia tatu hata zingefanya kazi, itakwamishwa na *lack of parking space* katikati ya mji hivyo *flow of traffic* itaendelea kuwa ngumu.

Pia kuwe na utaratibu wa kutoa vibali kwa magari madogo ili yasiwe mengi yanayoingia mjini baada ya mradi wa magari makubwa kukamilika na uharakishwe. Mfano mji wa Rome ambapo magari madogo binafsi yenye vibali tu ndiyo yanaingia *city centre*. Nimeishi Rome na ninafahamu *system* yao. Utaratibu kama wa *Mlimani City* ufanyike maeneo mengi ya Temeke, Ukonga na kadhalika ili kupunguza au kuondoa sababu ya watu kuingia *city centre.* Huduma nyingi zikipatikana kwenye *satelite centres flow* kwenda mjini itapungua sana. Pia ofisi za Serikali kwenye *satelite areas* ziimarishwe ili wateja wasiwe na sababu ya kuingia *city centre* isipokuwa kwa mambo makubwa tu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na naamini kabisa suala la Dar es Salaam siyo la Dar es Salaam tu bali *planning* ianze pia kwa majiji yetu na miji yote kuepuka hali kama hii siku zijazo. Natanguliza shukrani z dhati.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika nichukue nafasi hii kuipongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo inatoa matumaini mazuri kwa maendeleo yetu hasa kule vijijini. Kama inavyooneka katika Bajeti ya mwaka 2007/2008 kwa fedha nyingi za maendeleo zitaelekezwa katika Halmashauri zetu japo kuwa hazitomaliza matatizo yote lakini zinasaidia kupunguza kero zilizopo kule. Vile vile Halmashauri kadhaa bado zina madeni mbalimbali ambayo yanatakiwa yalipwe. Halmashauri ya Wilaya ya Pangani inadaiwa na vile vile inadai kutoka katika baadhi ya

taasisi. Halmashauri ya Wilaya Pangani inadai deni la shilingi 79,000,000. Ofisi ya Waziri Mkuu iliiandikia Halmashauri ya Pangani kuwa isiendelee kutoza tozo la ushuru wa mashamba yanayomilikiwa na kampuni ya *Amboni Ltd.,* baada ya Halmashauri kufungua kesi ya madai Mahakamani kudai deni hilo na kwamba uamuzi huo ni hatua za muda ufupi huku Serikali ikitafuta ufumbuzi wa kudumu kuhusiana na suala hilo ya deni la shilingi 79,000,000/=. Pamoja na utekelezaji huo Halmashauri imeshindwa kufuta deni hilo la *Amboni Ltd.* kwa sababu zifuatazo:-

(a) Deni hili lipo katika mizani ya hesabu za Halmashauri *balance sheet*.
(b) Deni hilo linahojiwa na ukaguzi wa hesabu za Serikali kuwa kwa nini halijalipwa hadi sasa?
(c) Katika barua ya Waziri Mkuu haielezi kuwa deni hilo litalipwa na nini baada ya Halmashauri kuondoa kesi Mahakamani.
(d) Kibali cha kulifuta kwa kuwa ni deni kubwa kinatolewa na nani hususan kwa kuzingatia hoja za ukaguzi?
(e) Kama deni hili litafutwa kwa njia isiyo kubalika kulingana na taratibu za fedha za Serikali itazua hoja nyingine ya ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, kwa kutilia maanani barua ya Waziri Mkuu tunaomba Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu iilipe Halmashauri deni hilo kwa sababu zifuatazo:-

(i) Kwa kuzingatia kuwa mapendekezo yaliyokuwepo katika barua ya Waziri Mkuu yalikuwa na nia ya kudumisha amani na utulivu hasa katika kujenga uhusiano mwema kati ya mlipaji na Halmashauri.

(ii) Haikupaswa shauri hilo liachwe likielea hewani pasipo kupatiwa ufumbuzi wa kudumu tangu Januari 12, 1999 hadi 2007.

*(iii)* Halmashauri ya Wilaya ya Pangani ni miongoni mwa Halmashauri ambazo uwezo wao kimapato ni mdogo sana na ilishaingia mikataba ya manunuzi kwa kutegemea kuwa italipwa deni hilo na *Amboni Ltd.* Mfumo ulio hai ni ule uliotokea mwaka 2005 ambapo mali za Halmashauri zilikuwa zikamatwe kwa kudaiwa Mahakama kiasi cha shilingi 66,300,000. Aidha, ufumbuzi ulipatikana baada ya Halmashauri kupata mkopo kutoka *Local Government Loans Board (LGLB).*

*(iv)* Halmashauri ya Wilaya ya Pangani inaona *Ambani Ltd.* ilipaswa kulipa deni hilo kwa kuwa tozo hilo lilitozwa chini ya sheria halali ambayo ilitangazwa katika gazeti la Serikali lakini imeheshimu mapendekezo yaliyomo katika barua ya Waziri Mkuu.

*(v)* Hoja ya ukaguzi kuhusiana na deni hilo bado ipo pale pale kwa kuwa wakaguzi wamekataa kuifuta.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kuwa sasa swali hili litapatiwa ufumbuzi wa kudumu kwa kuzingatia ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Naunga mkono hoja.

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Spika, napenda nianze kwa kutoa pole na rambirambi zangu kwa familia na ndugu wa Mheshimiwa Marehemu Amina Chifupa, aliyefariki tarehe 26 Juni, 2007 na kuzikwa tarehe 28 Julai, 2007. Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, bado tunayo matatizo makubwa katika sekta ya ujenzi ambapo bado kazi ni kubwa ya ujenzi wa barabara nchini. Mikoa yetu bado kuunganishwa kwa barabara za lami. Sasa naomba tupate maelezo ni lini hasa kazi za ujenzi wa barabara *(Physical works)* ya Babati – Minjingu na Babati Singida itaanza. Mwanzoni tuliambiwa Machi 2007, baadaye kidogo Februari, 2008 na sasa hatujui itaahirishwa mpaka lini na kwa nini sasa isiwe Februari, 2008? Pia barabara ya Babati-Kondoa - Dodoma hadi Iringa haionyeshi dalili ya kujengwa kwa lami katika kipindi cha miaka miwili ijayo kwa nini?

Mheshimiwa Spika, suala la ajali nyingi barabarani limezidi kupita kiasi. Serikali inajiridhisha vipi kwa hatua zinazofaa ili kutokomozea ajali nyingi? Je, Serikali itakubaliana nami kwamba ajali nyingi zinasababishwa na madereva? Mimi nashauri kwamba kwa suala la *overspeeding* kwenye mabasi, abiria wapewe mamlaka ya kuwadhibiti madereva ili kwenda kwa mwendo unaokubalika.

Tatizo kubwa pia ni uendeshaji wa kibabe wa madereva wa malori. Mimi nashauri kiongozi au afisa yeyote wa Serikali apewe mamlaka ya kuripoti madereva jeuri wa malori na hatua kali zichukuliwe na polisi. Serikali ijenge woga ndani ya jamii wa kuheshimu na kuzingatia sheria. Tuone kwamba tunamkosea jirani au mwenzetu kuliko kuona kama polisi anatuona au vinginevyo. Sheria zifuatwe.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu na wasaidizi wake kutokana na kuzingatia maombi yangu juu ya mgogoro wa Hifadhi ya Tarangire na wanavijiji vya Ayamango, Gedamar na Gijedabung, suala hili liko mahakamani. Kwa jumla mbuga zote mbili yaani Hifadhi ya Manyara na Tarangire, zote za jimboni kwangu zina migogoro ambayo iko mahakamani. Naomba Serikali pamoja na *TANAPA* na Bodi yake waone suala zima la ubinadamu na kwamba pande zote kwa namna moja au nyingine zina mchango wake, suala la fidia ni muhimu, suala la eneo la kuhamia pia ni muhimu zaidi.

Mheshimiwa Spika, suala la ujenzi wa hospitali ya Mkoa wa Manyara linajaribu kuendelea kuwepo kila mwaka. Tunahitaji hospitali ya Mkoa ya kisasa. Mwaka wa fedha uliopita zilitolewa shilingi milioni 100. Mwaka huu hazikutolewa kabisa. Tangu mwaka 2003/2004 Serikali imekuwa ikitoa fedha na dawa katika Hospitali ya Dareda inayomilikiwa na Jimbo Katoliki la Mbulu. Hospitali hii ilikwishawahi kuwa *DDH* ya Wilaya ya Babati na baadaye Hanang.

Hospitali ya Dareda ina uwezo mkubwa zaidi kuliko hospitali ya Mjini Babati na hii imethibitishwa na Mbunge wa Babati Mjini kwamba matengenezo au upanuzi mkubwa unahitajika kwa Hospitali hii ya Wilaya. Ombi langu kwa Serikali lilikuwa zitolewe huduma za *Regional Hospital* katika Hospitali ya Dareda kwa muda wakati tunaendelea kusubiri kukamilika kwa hospitali mpya. Wizara ikatekeleza hivyo lakini uongozi wa Mkoa haukuonyesha ushirikiano pamoja na Wizara kuhitaji maamuzi ya Mkoa. Hata hivyo *minutes* za *RCC* ilionyesha kutokuwa na pingamizi yoyote kwa Wizara kupeleka madawa na fedha Dareda Hospitali na ndicho kinachofanyika sasa. Lakini bado kuna jitihada za uongozi wa Mkoa sasa kutaka kuhamisha fedha zinazopelekwa Dareda ili sasa zikae pale mkoani.

Mheshimiwa Spika, lakini kama ni suala la kuhudumia wagonjwa wengi basi Dareda Hospitali kwa sasa ndiyo *proper*. Mwaka jana (mwaka wa fedha unaoishia sasa) nilifikia hatua ya kupendekeza kwamba hivi ni vibaya kutumia *infrastructure* iliyopo katika sura ya *joint venture* kuliko kutumia fedha kwenye *facility* ambayo tayari inaweza kutoa huduma inayolengwa/inayokusudiwa; kwamba ni rahisi Serikali kupeleka madaktari na manesi wa kutosha Dareda Hospitali huduma zikatolewa ipasavyo na fedha za ujenzi mpya zikasaidia maendeleo mengine. Hii ingekuwa ni *alternative.*

Mheshimiwa Spika, hali ya Hospitali ya Wilaya ya Babati siyo nzuri. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI aliona hali yake hivi karibuni na Mbunge wa Babati Mjini pia amethibitisha katika hotuba yake humu Bungeni.

Tangu mwanzo mimi niliona hali hiyo ndiyo maana wakati Mkoa wa Manyara ulipoanza mimi nilipendekeza Serikalini kwamba Hospitali ya Misheni ya Dareda iweze kutoa huduma ya Hospitali ya Mkoa kwa muda hadi hapo Hospitali mpya ya Mkoa itakapokamilika. Hivyo mwaka mwaka 2003/2004 Wizara ilianza kupeleka dawa na fedha katika Hospitali ya Dareda. Hata hivyo baadaye Wizara iliona ni vizuri kupata *blessing* ya Mkoa. *Minutes* za mkutano wa *RCC*- Manyara ilionyesha kwamba *basically* tunatakiwa Hospitali mpya ya Mkoa lakini wakati huo huo Mkoa hauna *objection* na hatua za Wizara kupeleka fedha na dawa *(MSD) to the tune of shillings 600 million.*

Kama Mkoa hauna *objection* hauna pingamizi kwa mujibu wa *minutes* za *RCC* maana yake nikuafiki na Hospitali ya Dareda ingepaswa kutangazwa rasmi kuwa *the first Regional Designated Hospital.* Kusema kweli Babati ni Hospitali ya Wilaya bado inahitaji *extention* kwa fedha nyingi. Hii ndito hali ya sasa ya Babati nilipenda kukufamishisha *(update)*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninaunga mkono hoja asilimia mia moja na kuipongeza Bajeti hiyo kwa jinsi ilivyopanga mikakati yake. Mimi ningependa kuchangia juu ya mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mimi ninashangazwa na Chama cha *CUF,* kuhusu nembo wanayotumia katika bendera zao na kazi zao za chama chao cha *CUF* ni mizani ambayo ilikuwa inatumiwa katika shilingi ya Sultani Said Bin Sharif Bin Sultan Bin Twalibu Sultani wa mwaka 1892 aliyekuwa anatawala Visiwa vya Zanzibar shilingi ambayo alikuwa anatumia Sultani huyo ndiye yenye nembo ya kadi na bendera ya *CUF.*

Mheshimiwa Spika, na inasemakana kuwa, wakati wa Mapinduzi ya Zanzibar, kilikuwepo kizazi cha Sultani huyo na wengi wao walikimbilia nchi za nje; na kwamba ndio wao wanaoshabikia Upinzani hadi sasa Zanzibar. Je, Serikali haioni kuwa, Chama cha *CUF* ambacho kinatumia nembo ya Sultani Said Sharif kina uhusiano na ukoo wa Kisultani? Na wanataka kuingia madarakani kupitia (demokrasia) kupitia Chama cha *CUF?* Tunaomba Serikali iliangalie hilo. Ushahidi wa shilingi yenye nembo ya *CUF* ya Sultani ninayo. Chunguzeni hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *TASAF,* kazi ya Mfuko wa *TASAF* inakwenda pole pole sana. Barabara ya Nanganga – Ruangwa mradi wa *HIPC* tangu amepewa mkandarasi hadi leo hajamaliza. Barabara ya Njia nne – Chumo – Kipatimu imesimama kwa muda mrefu. Mkandarasi ameweka vifaa vyake tu; amekaa kimya hadi lini? Barabara ya Mingoyo – Kibiti – hadi lini?

Kuhusu posho za Madiwani ziongezewe hadi laki moja. Pia wakopeshwe pikipiki au baiskeli, kuhusu mgawanyo wa Mikoa, Wilaya na Majimbo, na mipaka iangaliwe upya. Sasa hivi watu ni wengi kuna haja ya kuongeza Mikoa, Wilaya, Majimbo, Tarafa, Kata, Vijiji na Vitongoji.

Mheshimiwa Spika, nampa Waziri Mkuu hongera kwa kuliona hilo. Kuanzishwa kwa hilo kutapunguza msongamano wa shughuli Mkoani. Naunga mkono asilimia mia moja.

Mwisho, ninataka nielezee kuwa, kero kubwa katika mikoa yenye ni uwindaji na uchomaji moto katika maeneo ya mapori imejulikana kuwa maeneo mengi ya misitu yanayoungua moto ya uwindaji, yanachomwa na watu wanaomiliki mapori hayo kuwinda. Kwa mfano Selous, waliopewa kumiliki maeneo hayo, ndiyo wanaochoma moto. Tunaiomba Serikali ilichunguze hilo kama ni kweli au si kweli ili sheria ichukue mkondo wake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninasema kuwa naunga mkono hoja asilimia mia moja. Ahsante sana.

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kumpongeza Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri Mkuu na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wasaidizi wake wote kwa hotuba nzuri ya mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali na Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu Serikali yetu tangu awamu ya kwanza hadi sasa tumekuwa na nia ya kuhamia rasmi Dodoma Wizara zote za Serikali kwa awamu. Zoezi hili utekelezaji wake ni mdogo sana hivyo naomba kuiomba Serikali kuongeza juhudi hatimaye Makao Makuu ya Serikali yakamilike penye nia pana njia.

Mheshimiwa Spika, mradi wa mabasi yaendayo kasi katika Jiji la Dar es Salaam una mwelekeo mzuri. Zoezi hilo la mabasi yaendayo kwa kasi itaigharimu Serikali fedha nyingi sana hasa fidia za nyumba na kadhalika. Naomba kutoa ushauri kwa Serikali kuweka miundombinu ya reli na barabara za mabasi yaendayo kwa kasi katika maeneo ya Jiji yanayopimwa hivi sasa huko Temeke, Kinondoni na Ilala ili kwa nia ya kuepusha matumizi makubwa ya fedha na kulipa fidia za bomoa bomoa huko siku za usoni na mamlaka husika zilinde maeneo hayo yasiyovamiwa na wananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuipongeza Serikali kwa uamuzi wake uliofikiwa wa kujenga Ofisi za Waheshimiwa Wabunge 40.

Mheshimiwa Spika, naomba kushauri tena kwamba ujenzi wa ofisi hizo ni vyema ukatumika uwiano mzuri wa kujengwa kila Mkoa ofisi mbili kwa Mikoa kumi na tisa na Mikoa miwili waanze kwa ofisi moja kila Mkoa.

Mheshimiwa Spika, ninaamini hii itaondoa maneno ya upendeleo. Ahsante.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na watumishi wote katika ofisi yake kwa kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, kipekee namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuagiza uanzishwaji wa sekondari kila Kata, Zahanati kila Kijiji na Kituo cha Afya kila Kata. Aidha, kipekee namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa jitihada ya ziada katika kusimamia kwa mafanikio ujenzi wa vyumba vya kuanzia elimu ya sekondari katika Kata ambazo hazikuwa na shule za sekondari. Kusema kweli huu ni mchango wa kujivunia katika jamii yetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi nilizozitoa ninao ushauri kwa Serikali yetu. Kwanza, kabisa nashauri Ofisi ya Waziri Mkuu isimamie kwa karibu viongozi na watendaji walio karibu na wananchi ili watende kazi zao kwa kuheshimu Katiba ya Nchi, Sheria na miongozo ya viongozi wa juu. Baadhi ya viongozi na watendaji kwa maslahi binafsi au kutokujua sheria wanakiuka kanuni za uongozi bora. Lazima viongozi na watendaji wanaodhalilisha na kuwatega wananchi kwa kisingizio cha kusukuma maendeleo waonywe vikali na wakiendelea na tabia hiyo chafu waondolewe katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, pili, naishauri Serikali ifuatilie kwa karibu utekelezaji wa dhana ya kupeleka madaraka kwa wananchi. Baadhi ya Vijiji mikutano mikuu ya Kijiji ambacho ni chombo muhimu cha ushirikishwaji umma aihitishwi! Taarifa za fedha na

utekelezaji wa miradi katika vijiji haitolewi kwa wananchi vijijini na hivyo kuwavunja moyo katika kuchangia miradi ya maendeleo. Mikutano Mikuu ya Vijiji iitishwe kisheria.

Tatu, ili kufanikisha elimu ya uraia na ufahamu wa wananchi juu ya haki zao na wajibu wao, ni vema kila ofisi ya Kijiji ipewe nakala ya Katiba ya nchi, Sheria za Serikali za Mitaa na Vijiji, Sheria ya Ardhi na kanuni zake na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa katika lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, nne naishauri Serikali ipunguze masharti ya kuachia fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(Tanzania Social Action Fund – TASAF)* kwenda vijijini ili kuharakisha maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imeeleza kwa ufasaha mipango na malengo ya Serikali na ofisi yake mwaka wa fedha 2007/2008. Vipaumbele vya Serikali ni sahihi kabisa na mikakati inafaa kutuwezesha kufikia malengo. Hongera sana.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Muleba Kusini kutokana na mazingira yake, likiwezeshwa katika miradi ya umwagiliaji katika vijiji vyetu ambavyo vina mazao ya kudumu tunaweza kupata ndizi nyingi kwa ajili ya biashara, tunaweza kuzalisha maharage mara mbili hadi mara tatu kwa mwaka, mboga mboga, karanga na matunda vinaweza kuzalishwa kwa wingi na hivyo kuwaondolea wananchi umaskini wa kipato.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Muleba ninashukuru Serikali na hususan Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ushirikiano tunaopata katika jitihada zetu za kukamilisha Kituo cha Afya katika Tarafa ya Nshamba yenye watu wapatao laki moja na nusu. Aidha, tunaishukuru TAMISEMI kwa kutupatia shilingi milioni 50 ambazo zimesaidia kujenga awamu ya kwanza ya barabara ya Nshamba-Bunyagongo-Kashanda – Nyarutunfu hadi Nyarugando ili kuokoa maisha ya wananchi hasa wajawazito wanaobebwa kwenye machela kupanda mlima ili kufika barabarani! Tunasubiri fedha tuliyoahidiwa ili kuvunja mlima na kuwezesha Kituo cha Afya kufunguliwa tukipata shilingi milioni hamisini tuliyoahidiwa tangu mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, napenda nimalizie kwa shukrani na pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jinsi anavyochukua hatua haraka sana na sahihi pale Mbunge anapomtaarifu juu ya kero za wananchi. Mimi ni shahidi wa hilo. Naamini Waheshimiwa Wabunge wenzangu watakubaliana nami katika hili. Mheshimiwa Waziri Mkuu anachukua hatua haraka na kujibu papo kwa papo barua za Wabunge na kero kutatuliwa.

Mheshimiwa Spika, pia nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa ushirikiano wao kwangu na kujibu mara moja katika utatuzi wa kero za wananchi ambazo nimezifikisha kwao. Napenda kuwahakikishia ushirikiano wangu katika kujenga Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ahsante sana.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa fursa hii, ili kwa niaba ya wananchi na wapiga kura wangu wa Jimbo la Kwimba nitoe salamu za pole kwa familia ya marehemu Amina Chifupa, kwa mauti yaliyomfika aliyekuwa Mbunge huyu, Mwenyezi Mungu awape uvumilivu na faraja wote walioguswa na msiba huo na yeye aipumzishe roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Aidha, napenda nitumie fursa hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa ushupavu na ujasiri wa Mheshimiwa Waziri Mkuu anavyoisimamia Serikali kwa kipindi chote tangu mwanzo wa Awamu Nne ya Serikali hii. Juhudi za kuiona nchi yetu inaendelea na inayofikia malengo mbalimbali tuliojiwekea ni dhahiri. Nawapongeza vile vile wasaidizi wake mbalimbali na wa nyadhifa mbalimbali wanaowezesha kutekeleza majukumu waliyonayo, nawapongeza sana. Hotuba hii naiunga mkono kwa kuwa ninaamini kuwa yaliyomo yatatekelezwa kwa kiwango cha juu.

Kuhusu huduma za kiuchumi, katika jimbo langu barabara zifuatazo hufadhiliwa na Benki ya Dunia. Mpango huu umesikika kwa muda mrefu sasa bila utekelezaji na taarifa juu ya mradi huu masikioni mwa watu imeanza kuwa kero. Barabara hizo ni Mabuki - Jojiro hadi Malampaka na Jojiro – Ngudu hadi Magu.

Mheshimiwa spika, ombi langu ni kuwa taarifa ya kueleweka kuhusu ratiba yake iwe wazi na ya kweli. Wananchi wangependa kujua kwa uhakika.

Kuhusu huduma za uzalishaji, Jimboni kwangu kuna *ginerries* mbili, *ginerries* ya Mwalujo na *ginerries* ya Sangu. Tangu mwaka 1996 hadi leo nimekuwa nikiomba umeme kwa *ginerries* hizi bila mafanikio. Sababu mbalimbali zimekuwa zikitolewa kutokuzipelekea umeme *ginerries* hizo! Sababu hizo daima zimekuwa na nyongeza ya kuomba tuendelee kuwa na subira. Kinachoumiza ni kuona kuwa umeme tunauona unapelekwa hata kule kiuzito. *Ginerries* hizo zinazidi maeneo hayo. Hali hiyo hata inawakatisha tamaa wawekezaji wa viwanda/ *ginerries* hizi kwani licha ya maombi yangu hata wao wamekuwa wakiandika barua Wizarani na *TANESCO* bila hata majibu. Inasitisha sana.

*Ginerries* zote mbili zilikuwa na mipango ya kuwa na viwanda vya kukamua mafuta, ila wanashindwa kuanzisha kwa kuchelea kuongeza gharama! Kuongezwa kwa viwanda hivyo si tu kungepandisha thamani ya zao la pamba bali pia lingeongeza ajira! Ombi langu ni kuwa maeneo haya yafikiriwe sasa katika Mfuko wa Akaunti ya Milenia *(MCA)*. Iwapo mradi huo utatekelezwa shule saba za sekondari zitanufaika ikiwemo shule moja ya *A Level* na asasi kadhaa za afya kama Kituo cha Afya cha Mwamashimba, na wananchi waliomo katika vijiji kama Hunguwalwa, Mwamashimba Kikuhiji na Shilima. Kukamilishwa kwa mradi huu utafungua maendeleo kwa maeneo hayo ya kusini ya Wilaya ya Kwimba.

Mheshimiwa Spika, mkataba wa utendaji kati ya Halmashauri na Serikali Kuu na ruzuku ya maendeleo, hatua hii ninaipongeza sana. Naamini hatua hii itakuwa na itaendelea kuwa kichocheo cha Halmashauri za Wilaya zetu kufanya kazi vizuri. Halmashauri ya Wilaya yangu imepata hati safi kwa miaka 2 au 3 mfululizo. Ninafahamu umuhimu wake.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili naomba sana Wizara ya TAMISEMI isaidie. Kwa maoni yangu yaelekea Wizara iko karibu zaidi na watendaji wa Halmashauri Wilaya kuliko ilivyo karibu na wananchi katika Halmashauri Wilaya hizo. Miaka miwili iliyopita tulimpokea *DED* kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Magu baada ya kuwa na mgogoro huko. Chini ya kipindi cha mwaka mmoja akawa na mgogoro katika Halmashauri yetu, tukatoa taarifa Wizarani tukiomba watume watu kuja kuangalia chanzo cha mgogoro huo ili watoe usuluhisho muafaka. Wizara haikujibu na haikutuma.

Kwa kipindi cha takriban miaka miwili mizima hapakuwepo na suluhu bila kauli ya Wizara huku mambo yakidorola kwa maafisa kuomba kuhama na kuhamishwa. Ni hivi majuzi tu hatimaye Wizara imekuja na suluhisho la kumhamisha Mkurugenzi kutoka Halmashauri Wilaya kumpeleka Manispaa. Dhahiri hiyo kwetu tunaelewa kuwa Wizara, ilitupuuza. Tunashukuru kama hiyo haitoshi, Mkurugenzi mpya akaja na Afisa Mipango mpya, *DT* mpya pamoja na wasaidizi wao wote kwa vile hata wasaidizi nao walikuwa wamehamishwa. Hati safi tulizopata ilikuwa wa miaka ya Mkurugenzi kabla ya huyu ninayemwongelea. Je, Wizara ya TAMISEMI imetutendea haki?

Kuhusu huduma za jamii, naipongeza Serikali kwa juhudi inazozifanya katika eneo hili hususan elimu, maji na afya. Naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kutayarisha hotuba ya kimapinduzi inayofuatilia kwa karibu kila sehemu ya Ilani ya CCM ya Uchaguzi wa 2005.

Pili, Mheshimiwa Edward Lowassa ni makini katika kusimamia utekelezaji wa Ilani ya CCM. Hongera nyingi.

Aidha naomba niwapongeze Mawaziri wa Nchi, Naibu Mawaziri pamoja na Katibu Mkuu na Watendaji wa Wakuu. Naomba nitamke na kuwashukuru Waziri Mheshimiwa Mizengo Pinda, Naibu Waziri Mheshimiwa Celina Kombani kwa kufika Utete, Rufiji baada ya kupita barabara mbaya.Wananchi wa Rufiji wanatoa shukrani zao nyingi sana. Tunashukuru sana kwa Boma la Utete/Rufiji linakarabatiwa vizuri sana. Ahsante sana.

Maombi yangu ni kuwa barabara ya Nyamwage kwenda Utete Bomani inapitika kwa taabu sana. Tunaomba sasa barabara hii ijengwe kwa ustadi unaostahili yaani iliyonyanyuliwa na ya changarawe madhubuti, wala sio tope kama ilivyo sasa.

Ahadi ya Mheshimiwa Rais mwaka 2005 kuwa barabara ya kutoka Kibiti-Mkongo Utete (kilomita 44). Mheshimiwa Rais aliwahakikishia wananchi kuwa

barabara hiyo itajengwa na itapitika mwaka mzima. Aidha, ahadi ilitolewa hapa Bungeni, kuwa barabara hiyo pamoja na Kivuko cha Utete kitanunuliwa. Lakini ujenzi wa barabara hii inakarabatiwa kwa kiwango cha chini sana. Wakandarasi hafifu wanaopewa zabuni hutia tope juu ya barabara na masika yaliyopita kazi hiyo ni *zero* na barabara ina mashimo makubwa na hayapitiki. Ahadi ya Rais bado haijatimizwa. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu asimamie ahadi ya Rais.

Maombi ya barabara toka Ikwiriri - Mkongo –Mloka – Vikumburu - Kisarawe mpaka Kibaha sasa ichukuliwe na *TANROADS* Mkoa. Kwa vile Mloka ni kituo maarufu cha utalii wa mbuga za Hifadhi ya Selous, tunaomba barabara ijengwe kwa changarawe ili tunyanyue utalii katika mbuga hiyo ya Selous. Utalii wa Hifadhi ya Selous unarudi nyuma kwa ajili ya kukosa barabara kugawa Wilaya ya Rufiji ili iwe na Wilaya mbili ya Rufiji na Wilaya ya Kibiti. Wilaya ya Rufiji ni Wilaya kongwe kwa mfano Makao Makuu yake ya Mji wa Utete ni mahali ilipiganwa vita ya maji maji ya *Resistance Against German Colonization,* inaanza Jaribu mpaka Kingupira karibu na Kipatimo (kwa Mzee Ngombale). Hiyo ni Kaskazini – Kusini na kutoka Mloka mpaka Rufiji *Delta* ni sehemu kubwa na ina matatizo ya kiutawala na utoaji wa huduma kwa wananchi. Aidha, *DC* mmoja hatoshi, wala hatuwafanyii haki wananchi wa Rufiji. Warufiji wanaomba Wilaya ya Rufiji igawanywe ziwe Wilaya mbili ya Rufiji na Kibiti.

Mheshimiwa Spika, bado Ma-*DC* hawakai katika sehemu zao za kazi. Kuna kanuni inayomtaka mtumishi yeyote na hasa Ma-*DC* na Wakurugenzi wa Wilaya wasikae nje ya kituo cha kazi kwa zaidi ya siku 60 kwa mwaka. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu ahakikishe kuwa watumishi wenye madaraka Wilayani wanafanya kazi na kukaa katika sehemu zao za kazi ili wawasaidie wananchi. Aidha, katika Wilaya zilizoko nyuma wapelekwe Ma-*DC* na Wakurugenzi wa wachapakazi ili walete maendeleo. Sio kupeleka mradi kujaza nafasi tu.

Naomba kuunga mkono hoja asilimia mia moja. Mungu awape nguvu ili mtimize shughuli za kuleta maendeleo ya kweli nchini. Ahsante.

**MHE. ASHA MSHIMBA JECHA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

Kuhusu mikopo ya wajasiriamali ni vyema ukaangaliwa utaratibu bora zaidi kuliko utaratibu huu wa sasa, kwani imekuwa na mzunguko mkubwa wa kukatisha tamaa kwa wajasiriamali wadogo wadogo hasa wa vijijini walio mbali na Mabenki au hakuna kabisa. Nashauri mikopo hiyo ipitishwe katika asasi za fedha zilizoko vijijini au kwenye Halmashauri kwa utaratibu maalum. Kwa upande wa Zanzibar ahadi hii ikamilishwe, kwani *(SACCOS)* zipo tayari na zinasubiri kukopa tu.

Kuhusu suala la elimu, naipongeza Serikali kwa juhudi za makusudi zinachukuliwa katika kuboresha elimu, kwani zote duniani zilizoendelea kipaumbele chao cha kwanza kilikuwa kuwapatia elimu wananchi wake. Kutokana na takwimu zilizopo katika ukurasa wa 31 aya ya 46 zinaonesha kwamba watoto wote wenye umri wa

kuandikishwa shule wanaandikishwa kwa asilimia 100 ifikapo mwaka 2015 na hadi Janauri, 2007 wameandikishwa asilimia 96.1. hii ni hatua nzuri na ya kupongezwa.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba asilimia hii ya watoto tunaoanza nao wanaendelea hadi elimu ya sekondari/elimu ya juu. Ni vyema Serikali ikajua nini hasa sababu ya watoto wengi kukatisha masomo kabla ya kufika sekondari, jambo ambalo limechochea ongezeko la vijana kufukuzia mijini bila ya kazi za kufanya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante.

**MHE. MWAKA ABRAHMAN RAMADHANI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nampongeza Waziri Mkuu kwa hotuba yake ya Bajeti ya mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, pia nawapongeza wasaidizi wake Waziri Mheshimiwa Mizengo Pinda na Naibu wake Mheshimiwa Celina Kombani.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa mkono wa pole kwa familia ya marehemu Mheshimiwa Amina Chifupa, Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia kwa kuipongeza Serikali ya CCM kwa kutekeleza sera na Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa kuwafikishia wananchi huduma muhimu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naipongeza Serikali kwa mikakati yake ya kudhibiti dawa za kulevya ikiwa ni pamoja na bangi. Naiomba Serikali ifanye haraka sana tena sana, ujenzi wa kituo maalumu kwa ajili ya kuwatibia walioathirika na dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, dawa za kulevya ni tatizo sugu sana na ni adui mkubwa sana kwa vijana. Naomba kituo hicho kiishe haraka na kipate takwimu ya vijana walio Zanzibar, sambamba na hilo kituo kama hicho kijengwe Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni Magereza yote nchini, ninachoshangaa kusikia kwamba baadhi ya mahabusu na baadhi ya wafungwa wanavuta bangi, wanatumia dawa za kulevya jela, lakini tujiulize wanapataje hizo dawa? Kuna uwezekano mkubwa baadhi ya askari magereza wanahusika kwa biashara hiyo. Askari huwauzia bangi na wanahifadhia humu kwa watu wao maalumu ambao ni wafungwa.

Naiomba Serikali itazame sana Magereza kote nchini na iwekwe sheria kali sana, itakapogundulika askari amekutwa na bangi au dawa za kulevya, si vibaya kuhakikisha kwamba kila askari anapekuliwa kwanza kabla ya kwenda kuwaona au kuwahudumia mahabusu au wafungwa.

Mheshimiwa Spika, katika Magereza yetu kuna utaratibu kwa wale mahabusu wanaobahatika kupelekewa chakula, huwa kinapekuliwa na kumtaka mpelekaji akionje

kwanza chakula kabla hajapelekewa mhusika. Sasa hizi bangi na dawa za kulevya zinapitia wapi?

Mheshimiwa Spika, tunashukuru kabisa mikakati ya elimu kwani katika mwaka 2007/2008 tumeshavuka lengo la mwaka 2010, tunaomba Serikali izidishe nguvu za kutoa huduma za msingi kama walimu, maabara, maktaba na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mwisho nakipongeza chama changu cha CCM kuisimamia Serikali ili itekeleze yale yote yaliyolengwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DEVOTHA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri Mkuu, wafanyakazi wa Wizara na Idara zilizopo katika Ofisi yake, kwa hotuba na utekelezaji mzuri wa Ilani ya CCM. Naomba nichangie mambo matatu kama nyongeza kwa yale mengi yaliyofanyika vizuri.

Kuhusu elimu ya juu (Vyuo Vikuu), naomba Serikali izidi kuangalia suala hili kwa Mikoa ya Kusini ya Lindi, Mtwara, Ruvuma haina Chuo kikuu, Mikoa mingine ina vyuo zaidi ya vitatu au vinne. Naomba Serikali tushirikiane nasi viongozi wa maeneo hayo tupo tayari kuongeza jitihada juu ya hilo Vyuo vya Walimu kama Matogoro kiwe Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Spika, sekta ya fedha bado inatoa mchango mdogo sana katika nchi yetu na hasa vijijini. Suala la mikopo midogo midogo kijijini bado ni tatizo, nashauri kuundwe Kamisheni ya Mikopo Midogo Midogo itakayoshughulikiwa sheria sera na miundo mbalimbali ya kutatua tatizo la mitaji na hasa mikopo midogo hasa vijiji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la jinsia nashukuru, Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumzia masuala mtambuka, bado naamini maendeleo ya nchi yetu yatapatikana tu kama makundi yote ya kijamii yatashiriki katika kujenga uchumi.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna makundi makubwa ambayo mchango wake haujarasilimishwa rasmi. Kundi kubwa la maskini wakirasilimishiwa mali zao wanazomiliki kama vile ardhi, mashamba wataharakisha sana mchakato wa maendeleo.

Kundi la wanawake, kama ilivyo katika kurudisha mamlaka kwa wananchi mkazo ungewekwa pia katika kujenga uwezo wa wanawake katika nyanja zote hasa kiuchumi. Naomba Wizara zote, Idara, Serikali za Mitaa kuwa na mpango wa utekelezaji wenye mlengo wa kijinsia. Makundi ya wazee, walemavu, yatima pia yangepata kauli ya Waziri Mkuu ikiwa ni msisitizo tu kwa yote yanayotekelezwa.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali ianzishe Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ili uwasaidie watu wasiojiweza ambao kundi lake sasa ni kubwa nchini hasa wazee, walemavu, yatima na watu wenye umaskini uliokithiri.

Mheshimiwa Spika, napongeza na kuunga mkono hotuba ya Waziri Mkuu kwa asilimia mia moja.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, utawala bora ni utekelezaji wa sheria kwa usawa kwa wananchi wote. Inapotokezea wananchi au taasisi ya Serikali wanakuwa juu ya sheria hapo utawala bora una walakini mkubwa.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa Pili wa Bunge mwezi Aprili, 2006 nilitaka kuelewa na hatua gani imechukuliwa kwa mauaji ya mwanafunzi Juma Omar na waliojeruhiwa kwa risasi kwa ndugu Shaib Abeid na Bakar Ali Bakar. Wizara ya Usalama wa Raia ilijibu kuwa suala hilo liko katika uchunguzi na kadri ninavyoelewa mimi hakuna hatua iliyochukuliwa mpaka sasa kwa tukio hilo.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali inieleze suala hilo limefikia wapi kwani kuendelea kulipuuza suala hilo linaashiria uhai wa wananchi wetu sio muhimu na katika hali hiyo utawala bora utakuwa ni hadithi.

Mheshimiwa Spika, huu ni ulimwengu unaokwenda na falsafa ya uchumi kwa hiyo ipo haja Muungano wetu uende sambamba na falsafa hiyo.

Mheshimiwa Spika, si sahihi, Tanzania itafute misaada na mikopo halafu ikae na kugawa kwa Zanzibar wakati Zanzibar baada ya marekebisho na makubaliano inaweza nayo ikapata fursa kama Tanzania inazo. Si vyema kubebwa na wewe ukabeba.

Mheshimiwa Spika, kwa kuiruhusu Zanzibar kutafuta mikopo, misaada na kuwa na uhusiano na taasisi mbalimbali duniani si kudhoofisha Muungano bali itapokuwa Zanzibar haina tatizo la kiuchumi Muungano wetu utaimarika zaidi.

Mheshimiwa Spika, tuchukue mfano Shirikisho la Soka Tanzania *(TFF)* itapoteza nini kama *Zanzibar Football Association (ZFA)* itajiunga na *FIFA*. Hapa ni dhahiri Tanzania kwa ujumla wake itafaidika sana na misaada inayotoka *FIFA* kwa nchi wanachama.

Mheshimiwa Spika, ipo haja Serikali kuangalia kwa makini zaidi juu ya vyanzo vya mapato ili wananchi wafaidike kwa kutoingiziwa upandaji wa kodi kwa vyanzo vya mafuta ambavyo vinamuathiri kila mtu. Ahsante.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, nami naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salamu za rambirambi kwa niaba ya wananchi wa Liwale kwa kifo cha aliyekuwa Mbunge mwenzetu Marehemu Amina Chifupa, kilichotokea wakati wa Bunge hili, Mungu amlaze mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla hotuba yote ni kamilifu nami nitachangia kwa baadhi ya maeneo. Nimefarijika kuona kwamba katika mwaka 2007/2008 Serikali itakarabati Hospitali za Mikoa 11 ikiwemo ya Lindi. Hatua hii itaboresha sana huduma

za afya katika Mkoa wa Lindi. Maboresho hayo nashauri yaende sambamba na upatikanaji wa wataalam wenye sifa kwa hospitali hizo za Mikoa hadi Wilaya.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nijikite katika Wilaya ya Liwale, jimboni kwangu. Hospitali ya Wilaya ya Liwale ina wataalam wachache na haina *DMO.* Ipo umbali wa kilomita 250 kutoka Makao Makuu ya Mkoa wa Lindi na barabara ni mbaya sana hasa wakati wa masika. Hiyo ndio Wilaya pekee iliyo mbali zaidi kutoka Makao Makuu ya Mkoa wa Lindi. Hivyo basi ni muhimu kwa Serikali kuisaidia Wilaya hiyo kwa kuipatia *DMO* na wataalamu wenye sifa ili kuboresha huduma za Hospitali hiyo ya Wilaya kabla mgonjwa hajapelekwa Hospitali ya Mkoa umbali wa zaidi ya kilomita 250.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuelezea utata uliojitokeza hasa kwa watumishi wa afya/Wilayani Liwale kufuatia marekebisho ya *scale*. Hivi karibuni baadhi ya watumishi wa afya wamejikuta mishahara yao imekatwa/imepunguzwa ati kwa madai kwamba uongozi wa Halmashauri ulikuwa unatekeleza mwongozo kutoka Serikali Kuu kutokana na mabadiliko ya *scale* zao. Si jambo zuri kwa mtumishi yeyote kupunguzwa mshahara aliokuwa akipata bila sababu za kuridhisha kama vile adhabu kwa kosa fulani. Hayo kama ni kweli kwa watumishi wa Wilaya ngapi wamefanyiwa hivyo? Kama ni kweli hapakuwa na maandalizi ya kutosha kuwaelimisha wahusika kabla ya utekelezaji. Hivyo basi pamekuwa na manung'uniko kwa upande wa watumishi hao kiasi kwamba maisha yao na utendaji wao wa kazi umeathirika sana. Kama hilo lilikuwa ni agizo halali la Serikali nashauri maagizo yanayogusa maslahi ya watumishi Wilayani, viongozi wa Wilaya kama *DC* na Mbunge wajulishwe ili wawe katika picha na sio suala la Halmashauri au Mkurugenzi na ofisi yake pekee vinginevyo utawala bora utakuwa hatarini. Naomba Serikali ifuatilie kwa karibu utekelezaji wa maamuzi yake katika kila Wilaya ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii pia kuelezea utata uliojitokeza kuhusu uchaguzi wa Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri. Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri wa Wilaya ya Liwale ambaye pia ni Diwani wa Liwale Mjini na ni msaidizi wangu wa shughuli za Bunge, alijaza fomu za kuomba tena nafasi hiyo. La kushangaza ofisi ya Mkurugenzi iliandika barua kwa Katibu wa CCM Wilaya kueleza kwamba Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri haruhusiwi kuomba tena nafasi hiyo. Je, ni kweli kwamba kuna mwongozo huo? Kama kweli hali hiyo ilijitokeza kwa Wilaya ya Liwale tu. Wilaya zingine zote katika Mkoa wa Lindi na katika Wilaya nyingi za Tanzania hapakuwa na pingamizi la namna hiyo. Je, maagizo yanayopelekwa Wilaya ya Liwale ni tofauti na zingine? Kwa hili Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Lindi alirekebisha wakati wa Kikao cha Kamati ya Siasa ya Mkoa walipojadili majina ya wagombea wa nafasi ya Makamu katika Halmashauri za Wilaya. Hata jina la mgombea wa Liwale lilirudishwa na akaendelea na uchaguzi huo.

Mheshimiwa Spika, nimefarijika sana kwa hotuba ya Waziri Mkuu ambayo pamoja na mipango mizuri katika hotuba hiyo suala la posho la Madiwani kuongezwa ni muafaka sana hasa kutokana na hali halisi ya ugumu wa maisha kwa watendaji hawa wenzetu ambao tunashirikiana nao kikamilifu kwa shughuli za maendeleo majimboni kwetu. Nimekuwa nikichangia katika Bajeti zilizopita tangu niwe Mbunge kuomba

Serikali iboreshe posho na maslahi ya Madiwani. Nimefarijika kuona Serikali imeliona hilo. Hata hivyo baadhi ya Halmashauri kama ya Liwale haina vyanzo vya kutosha vya mapato, hivyo kifedha hali ni duni.

Naiomba Serikali iziwezeshe Halmashauri duni kifedha ili Madiwani husika nao waweze kunufaika vinginevyo watakaonufaika ni Madiwani walioopo katika Halmashauri za Mijini ambazo zina vyanzo vikubwa na vya uhakika vya mapato yao kama Temeke, Kinondoni na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, narudia tena kusema kuwa naunga mkono hotuba hii asilimia mia moja kwa ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe ushauri na niiombe Serikali mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu programu ya uendeshaji wa mifumo ya masoko ya mazao ya kilimo, tunashukuru Serikali iliamua kuanzia na Mikoa kama ilivyoitaja katika ukurasa wa 14, Ibara ya 22 na Ibara ya 23 na kwa mfumo wa stakabadhi za mazao gharama ambapo napo Wilaya tano zimepangiwa programu hiyo, lakini pia kwa mwaka 2007/2008 programu ya mifumo ya masoko imepanga kwa Wilaya za Kongwa, Moshi, Mwanga, Simanjiro, Chumya, Ileje, Kyela, Makete na Njombe pia ikataja kuibua, kuhamasisha na kuanzisha mfumo wa stakabadhi za mazao ghalani katika maeneo ya Kyela, Madibira, Mbarali na kadhalika.

Swali langu je, maeneo hayo ni maalumu kwa mazao gani kwani inaonekana kama vile Mikoa ya Kanda ya Ziwa haiwezi kuwa katika programu hizo kwani si Mara, Shinyanga, Mwanza, Kagera, Kigoma, Tabora au Singida. Ni lini Mikoa hiyo ambayo ni wadau wakubwa katika kuchangia Pato la Taifa upande wa kilimo wataingizwa katika programu hizo?

Kuhusu afya, Serikali imesema itakamilisha mpango wa ujenzi wa zahanati kwa kila kijiji na kituo cha afya kwa dhana ya kuwashirikisha wananchi kama ilivyokuwa kwa MMES na MMEM kwa sababu Serikali katika ujenzi huo ilikuwa ikisema jenga (MMEM) ukifikisha kwenye lenta Serikali itaezeka, je, kwa utaratibu na kama ilivyosema Serikali inakamilisha mpango wa ujenzi wa zahanati na kutoa mafunzo, Serikali itawasaidiaje wananchi katika ujenzi wa zahanati na vituo vya afya?

Lakini pia Serikali ilitoa ahadi mwaka 2005 ya kukarabati baadhi ya zahanati na vituo vya afya kwa kuahidi kutoa shilingi milioni 14 kwa zahanati na shilingi milioni 52 kwa vituo vya afya, ahadi hiyo hadi leo haijatekelezwa hasa kwenye Wilaya ya Kwimba, tumekuwa tukiulizwa lakini majibu si kwetu pekee kwani kila eneo/zahanati imeshatekelezwa Mashariki ikiwa ni pamoja na kufungua akaunti benki.

Naipongeza Serikali kwa kuongeza posho kwa ajili ya Madiwani toka shilingi 30,000 hadi 60,000 lakini mashaka yangu yanakuja pale Serikali iliposema kuwa hii ni kutokana na uwezo wa Halmashauri ambapo umeendelea kusema tathmini kwa Halmashauri zisizokuwa na uwezo inaendelea kufanyika. Naomba ufafanuzi kwani unaposema kulingana na uwezo wa Halmashauri una maana gani? Je, kwa Halmashauri zisizokuwa na uwezo kama Kwimba Madiwani wake waendelee kupata hiyo 30,000/= kwa nini Serikali isiamue kusema ni 60,000/= kuanzia sasa badala ya kusema tathmini inaendelea kufanyika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masuala ya hifadhi ya mazingira na dawa za kulevya bado ni tatizo kubwa tusipoangalia nchi yetu itakuwa jangwa baada ya miaka 10 ijayo endapo usimamizi wa upandaji miti hautatiliwa mkazo kama siyo kuundia sheria ya kupanda miti. Pia tatizo sugu la vijana wengi hivi sasa wanavuta bangi. Naunga mkono hoja.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, mimi nasikitika sana kuhusu mkoa wangu wa Kagera katika mikakati ya Serikali kuendeleza Mikoa yetu. Sijasikia kwenye mkoa huo, hivi Serikali haioni wakati ndiyo huu sasa wa kasi mpya umefika tukumbukwe angalau kidogo kidogo mambo muhimu ikitupatia usafiri katika Ziwa Victoria, uwanja wa ndege angalau kidogo ukarabatiwe kwa kiwango cha lami itasaidia kidogo siyo mambo ya kudanganyana kwamba walijenga uzio, si kweli uzio haupo ila wa zamani tena wa wavua samaki kuna shida kubwa sana, Serikali ihamasishe wafanyabiashara waache kuuza zana halafu kuwapa shida wananchi kupata.

Matatizo makubwa wakamatwe na wananyang'anywa samaki au mitego yao au kufungwa kuhusu ujenzi wa madarasa, wananchi wengi wamechangia ujenzi, sasa kuna ujenzi wa zahanati je, Serikali haioni kuwa ni mapema sana kulingana na kipato cha wananchi ni kidogo sana, afadhali wakawa wanachangia kidogo kidogo kuliko kuchangia mfululizo ujenzi wa sekondari mpaka sasa kuna wananchi wanaojificha porini kwa ajili ya michango kuhusu mikopo wengi wamechukua mikopo hiyo kama siasa.

Naomba ofisi yako ifafanue wananchi wote maana ya mikopo na kutoa elimu ya mikopo ya *NMB* Benki iache kuzungusha wananchi kuwapangisha foleni kila siku wengi wana watoto mgongoni.

Mheshimiwa Spika, naomba Bajeti hii ilenge mambo muhimu siyo kwenda kwenye mikono ya walio wachache, naomba mikono ya walio wachache kuimarisha maswala hayo yote.

Mheshimiwa Spika, nakutakia kazi njema nyote.

**MHE. AME PANDU AME:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Spika, nianze na mchango wangu kuelezea kuhusu kero za Muungano, kama hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu inavyoeleza ukurasa wa kumi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Muungano wetu umezidi kuimarika na utazidi kuimarika, lakini kero zinapojitokeza zitafutiwe ufumbuzi unaofaa kwa haraka kuliko kusuribi. Kwa mfano, kuna kero za Muungano za kisiasa ambapo wananchi wa Zanzibar wanapomchagua kiongozi wa nafasi ya Urais wa kuiongoza Zanzibar kwa upande wa kura za maoni, kwa kuwa wanakuwa ndiyo chaguo la Wazanzibar basi ndiyo awe huyo huyo, ibadilishwe.

Mheshimiwa Spika, nije kwa upande wa maendeleo ya nchi yetu, maendeleo ya nchi yetu yatapatikana tu kwa kutokuwa na muhula kwa watendaji, mtendaji yeyote atakapokuwa si muadilifu basi asionewe haya, achukuliwe hatua ya kinidhamu ifaayo.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inayo kila kinachohitajika katika kuleta maendeleo. Nchi yetu ina ardhi ya kutosha ambayo ni mali, ina madini ya kutosha ambayo ni mali, ina bahari ya kutosha ambayo ni mali ndani ya bahari viumbe vya kutosha ni mali, nchi yetu ina mapango ya kutosha ni mali, ina mbuga za kutosha ni mali, ina wanyama wa kutosha ni mali na mengi mengineyo ambayo ni mali.

Mheshimiwa Spika, uongozi wa awamu ya nne wote kwa ujumla kuanzia Mheshimiwa Rais na Baraza lake la Mawaziri ni uongozi mzuri sana na ni uongozi unaokusudia hasa kuleta maendeleo Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kujenga sio jambo rahisi, bali kubomoa ni rahisi. Lakini ukweli usiofichika kuwa viongozi wote wanaonyesha nia nzuri ya kuiletea maendeleo nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, iwapo kila mmoja wetu tukiwa na nia nzuri kama viongozi wetu basi hata jambo rushwa litakuwa kwa heri Tanzania.

Mheshimiwa Spika, na mimi naunga mkono hoja.

**MHE. KIUMBWA MAKAME MBARAKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima na kuniwezesha kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, niungane na wenzangu waliochangia kwa kuzungumza kwa kutoa rambirambi kwa misiba iliyotukuta katika nchi yetu katika kipindi hiki cha kuanzia Mei hadi leo hii mwaka huu wa 2007. Nawaombea Marehemu Mungu azilaze mahala pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie suala la uonevu kwa wastaafu wa jeshi la polisi pale wanapolipwa haki zao. Malipo wanayolipwa hayalingani kabisa na kazi zilivyo na pia muda wao wanapokuwa kazini. Mara nyingi utakuta mfanyakazi wa miaka 30 analipwa shilingi 1,200,000/= hii huwa inatofautiana sana na baadhi ya wafanyakazi wanaolipwa mafao yao yakiwa mamilioni ya shilingi.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi unapoliulizia suala kama hilo tunaambiwa, utaratibu huwa wamechagua wenyewe, hii ni kweli. Napenda kuishauri Serikali kuliangalia kwa jicho la huruma sana suala hili ili kuondoa malalamiko ya wengi na kutulaumu kuwa hatuwatetei na kutuwekea fitina kwa Chama Tawala na Serikali.

Mheshimiwa Spika, hiki ni kilio cha muda mrefu na kimelalamikiwa lakini utekelezaji wake ni mdogo mno. Pia wapo wastaafu ambao wakati waliopokuwa kazini viwango vyao vya mishahara na vyeo ni tofauti lakini wakati wa kupewa mafao yao mfano dereva, kuruta na sajenti, haki zao huwa zinalingana na kwa nini iwe hivyo. Naomba Waziri anayehusika atueleze hili ni kweli na kama ni hivyo waweze kujiimarisha kiuchumi ikiwa lengo ni kupiga vita umaskini nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wastaafu kwa jumla, napenda kuishukuru Serikali kwa kuliona na kuliingiza ndani ya Bajeti ya mwaka huu kwa kuweka utaratibu ambao utawawezesha kupata haki zao kwa ufanisi zaidi, lakini kasoro zilizopo naomba zirekebishwe ili kuondoa malalamiko kwa wastaafu hao. Mfano, askari aliyestaafu anashindwa kumiliki hata nyumba ya kuishi na familia yake. Lingine Brigedia wa jeshi analipwa haki iliyo sawa na dereva wake ambaye alikuwa na cheo cha Koplo *(CP)* wakati wa kustaafu kwake.

Mheshimiwa Spika, naomba tukumbuke kuwa hawa ni askari walio na kazi ngumu ya ulinzi wa nchi yetu na raia waliomo ndani. Lazima tuzithamini juhudi zao nzito wakati wanapopambana na maadui zetu na hadi tupate heshima tuliyonayo nchini mwetu. Naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu kuchangia kwa maandishi yale ambayo sikuweza kuchangia kwa kauli.

Mheshimiwa Spika, kuhusu watumishi bora, naomba Serikali ifanye jitihada za makusudi kuipatia Wilaya mpya ya Mkinga watumishi bora sio bora watumishi. Kwa mfano, Katibu Tawala tuliyeletewa alikuwa Kaimu *DAS* aliyeshindwa Lushoto na Kilindi. Mimi binafsi na viongozi wengine Wilayani Mkinga hatuamini kwamba *DAS* huyo ana uwezo wa kuitumikia Wilaya hiyo changa na inayohitaji msukumo mkubwa na kasi kubwa ya maendeleo. Haya nimemweleza Mkuu wa Wilaya, Katibu Tawala wa Mkoa *(RAS)* na pia Mkuu wa Mkoa *(RC).*

Mheshimiwa Spika, nashauri Wilaya hizi mpya zisiwe dampo za kupeleka watumishi walionekana kushindwa kwingineko. Tunaomba tupatiwe watumishi bora, hasa Mkurugenzi wa Halmashauri, Afisa Mipango, Mweka Hazina, Afisa Maendeleo ya Jamii, Afisa Elimu, Afisa Ushirika, Wahandisi na kadhalika. Kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga ilianza vizuri, kukabili ipasavyo changamoto nyingi na kupata kasi kubwa na endelevu ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, pia ipo haja kubwa ya kuboresha watendaji kwa ngazi ya Tarafa, Kata na Vijiji na kuwapatia vitendea kazi muhimu ili kufikisha huduma kwa

wananchi, kuwaongoza na kusimamia mipango na sera kama vile ya nguvukazi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimimiwa Spika, kuhusu ulinzi na usalama. Wilaya hii ina mpaka mrefu na nchi jirani ya Kenya, ina mwambao mrefu wa Bahari ya Hindi na ina umbali mrefu kutoka Kaskazini hadi Kusini na Magharibi hadi Mashariki pamoja na miundombinu hafifu. Hivyo, suala la ulinzi na usalama linakabiliwa na changamoto kubwa sana hasa kwa kuzingatia uhaba mkubwa wa polisi, vituo vya polisi na vitendea kazi.

Nashauri kipaumbele kipewe Wilaya hii katika kuiongezea askari, magari ya doria, boti za doria ina vitendea kazi vingine pamoja na vituo vya polisi pamoja na kutekeleza kwa kasi maalumu, mikakati ya polisi jamii na ulinzi wa ujirani ili kukabili vema uhalifu wa aina mbalimbali ambao ulikuwa na dalili za kuongezeka Wilayani humo.

Mheshimiwa Spika, mpango mkakati na *profile* ya uwekezaji ya Wilaya ya Mkinga na *investment/profile* ya Wilaya ni muhimu sana kwa kuchochea na kuelekeza maendeleo ya Wilaya yoyote. Wilaya ya Muheza ilipata msaada wa *Ireland Aid* katika kuandaa mipango hiyo. Wilaya mpya ya Mkinga inahitaji takribani shilingi 100,000/= kwa ajili hiyo, nashauri Serikali ilifikirie ombi hili kama la umuhimu wa kipekee na kuipatia Wilaya ya Mkinga fedha kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, nafasi ya Mbunge kiitifaki katika uongozi wa Wilaya, muda mrefu tokea Waheshimiwa Wabunge na Bunge lako Tukufu, waliomba kupata ufafanuzi kuhusu hili. Mheshimiwa Waziri Mkuu aliahidi kulifanyia kazi suala hili. Naomba Serikali ifanye hivyo haraka iwezekanavyo. Wabunge tunaendelea kudhalilishwa na tukapewa nafasi inayoeleweka kwenye shughuli za Kiserikali Wilayani kama vile mbio za mwenge na nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja na kumtakia Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wake, Katibu Mkuu na watalaamu wa Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zake afya njema na mafanikio mema ya utekelezaji wa hoja hii.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nami nichukue fursa hii, kutoa salamu za rambirambi kwa msiba wa Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Amina Chifupa, kilchotokea tarehe 26/6/2007. Mungu ailaze mahali pema peponi. *Amin*.

Mheshimiwa Spika, pia nichukue fursa hii nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, anayeshughulikia Bunge na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia UKIMWI na Maafa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, pamoja na Waheshimiwa Naibu Waziri wote na watendaji wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuwasilisha Bajeti ya mwaka 2007/2008 na usimamizi wa shughuli za Serikali kwa kipindi cha fedha cha mwaka uliopita 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii nitoe mchango wangu kwa nia ya kuboresha zaidi shughuli za Serikali kwa kipindi cha mwaka wa fedha za Serikali kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la uchaguzi la Iramba Magharibi wameniomba nizungumzie masuala yafuatayo ili Serikali yetu ya Awamu ya Nne iyatilie maanani kwa nia thabiti ya malengo ya maisha bora kwa kila Mtanzania.

Nashukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu alitembelea Mkoa wa Singida mwezi wa tano mwaka huu 2007, nashukuru kwa hatua zake za kuja kukagua shughuli za maendeleo, zikiwa ni pamoja na barabara, maji, elimu na mambo ya jumla ya kimaendeleo ikiwa ni hatua ya utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2005/2010.

Mheshimiwa Spika, nashukuru juhudi zinazoonyeshwa na Serikali Kuu kuhusu ujenzi wa barabara hasa hii ya kati Dodoma hadi Manyoni, Manyoni hadi Singida kisha Singida hadi mpakani Shelui. Wakati sasa umefika Serikali ikamilishe barabara hii, barabara hii ni muhimu na ndicho kiungo kikuu cha uchumi ni sababu zipi zinazochelewesha kukamilika kwa barabara hii muhimu? Barabara hii sasa imechakaa na kwa kuchoka huko kwa kila siku inaangusha magari, roho za watu zikipotea na hata uharibifu wa vyombo kama magari, inakuwa ikitokea mara kwa mara kwa sababu hizi za ubovu wa barabara. Naomba Serikali ihakikishe sasa wakati umefika barabara hii ikamilike.

Mheshimiwa Spika, mgawanyo wa maeneo ya utawala. Katika kipindi cha mwaka 2005 wakati wa kampeni, aliyekuwa mgombea Urais kwa CCM, ambaye ni Rais hivi sasa alitoa ahadi ya mgawanyo wa Wilaya ya Iramba na hii ilitokana na maombi ya wananchi wa Iramba kumwomba kutokana na sababu za ukubwa na hivyo kupelekea watendaji wa Serikali Wilaya kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu, Wilaya ya Iramba tangu nchi yetu kupata Uhuru haijawahi kugawanywa pamoja na kuongezeka kwa kasi idadi ya watu ambapo sasa Iramba ina idadi ya watu ipatayo 370,000, Kata 26, Vijiji 126, Serikali za Vitongoji 715 na Tarafa saba.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Iramba wanaomba mgawanyo wa Wilaya ili watendaji wa Serikali waweze kuwafikia nao wapate huduma za Kiserikali kwa ari, kasi na nguvu mpya.

Mheshimiwa Spika, juhudi za Serikai ya Awamu ya Nne, zote zimeonekana zinalenga kwa maisha bora kwa kila Mtanzania, nashukuru kwa Serikali kutia nguvu wananchi na hata kufanikisha ujenzi wa sekondari, Jimbo la Iramba Magharibi sasa tayari linazo shule 21 kati ya hizo za sekondari ni 19, kwa maeneo kila kata inayo shule. Mwaka wa fedha 2007/2008 naomba Serikali ifanye juhudi kama ilivyotengwa katika fedha za Bajeti ihakikishe vyote vilivyo muhimu na vihusuvyo sekondari vinakuwepo na kupelekwa katika shule hizi.

Mheshimiwa Spika, rushwa, nasisitiza baada ya sheria mpya ya kuzuia rushwa kupitishwa na Bunge sasa ni wajibu wa chombo hiki, pamoja na mikakati mizuri ya

utekelezaji majukumu yake. Nasisitiza juu ya kutolewa kwa elimu kwa wananchi hasa juu ya mapambano haya ya kupambana na kuzuia rushwa ili mwananchi aone na uelewa wa kutosha kuhusu masuala yote ya kutokomeza rushwa.

Mheshimiwa Spika mwisho, naomba Serikali izidishe uangalizi juu ya watendaji wabovu wale wanaofuja, wazembe kwa mali na shughuli za umma. Watendaji wezi wafukuzwe kazi na kufikishwa Mahakamani. Naunga mkono hoja.

**MHE. MWANAKHAMIS SAID KASSIM:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na kuniwezesha kuchangia hoja hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nami niungane na Wabunge wenzangu katika msiba mkubwa uliotufika kwa kuondokewa na Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Amina Chifupa. Mungu awape subira wafiwa na aiweke roho ya marehemu peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia suala la fedha shilingi bilioni moja kwa kila mkoa. Mheshimiwa Rais aliahidi fedha hizi kwa ajili ya wajasiriamali ili kupunguza umaskini hasa kwa vijana na akinamama. Lakini fedha hizi bado Zanzibar hazijatufikia na muda unakwenda na tumejiandaa kwa akinamama kujikusanya katika vikundi na kuunda vyama vya kuweka na kukopa lakini tunaona mwendo ni wa pole pole sana kwa hiyo tunaomba mipango ikamilike haraka fedha hizo zitufikie kwa haraka na sisi Zanzibar tufaidike nazo.

Mheshimiwa Spika, sasa niongelee suala la wamachinga. Serikali imewahamisha wafanyabiashara wadogo wadogo katika maeneo ya miji kwa nia safi kabisa ya kuweka jiji kuwa safi na amri hiyo imetekelezwa na wahusika na kuwatafutia maeneo mengine wafanyabiashara hao lakini hivi sasa kuna kero kubwa inayofanywa na askari wa jiji kuwasumbua hata wauza kahawa na wale wanaouza madafu wakati biashara zile ni lazima zifanyike mjini, kuwaharibia mali zao kama baiskeli na mikokoteni, machungwa na ndizi mbovu kwa kuwanyang’anya mali zao na kuwapiga.

Mheshimiwa Spika, kahawa haisababishi uchafu na pia wale wauza madafu na machungwa ambao wanatembeza biashara zao wana tabia ya kuchukua taka zao zinazosababishwa na biashara zao kwa hivyo, suala hili ni lazima liangaliwe upya kwa wafanyabiashara pia naomba waangaliwe kwa jicho la rehema, akinamama wanaouza chai pale sokoni Kariakoo mbele ya ofisi ya Posta.

Mheshimiwa Spika, akinamama wale hupikia vyakula vyao majumbani na kuja kuuzia pale. Kina mama wale wanawasaidia watu wengi sana wanaofika sokoni kuuza bidhaa zao kwani sio wananchi wote wanaoweza kula hotelini na chakula kinachouzwa pale bei ni rahisi na chakula kingine hakipatikani katika hoteli ziliozopo pale.

Mheshimiwa Spika, akinamama hawa wanapata taabu sana kwa kumwagiwa chakula chao, kuchukuliwa vifaa vyao na wakati mwingine hata kunyang’anywa fedha zao na kusababisha hasara kubwa kwa akinamama hao ambao wapo pale kwa

kutengeneza azma ya Serikali ya kuondoa umaskini (MKUKUTA). Wamechukua mikopo hiyo na kupata riziki zao. Naishauri Serikali kuwaruhusu akinamama wale waruhusiwe kufanya biashara pale na wawekewe muda wa kuondoka pale kwa siku na ifikapo saa fulani wasionekane. Tutakuwa tumewasaidia kuliko ilivyo sasa.

**MHE. SALIM ABDALLAH KHALFAN:** Mheshimiwa Spika, sote tunaamini kwamba elimu ni ndio ufunguo wa maendeleo. Ili tulete maendeleo katika nchi yetu kisiasa, kiutamaduni, kiuchumi na kijamii kwa ujumla tunahitaji kuwa na rasilimali watu walioelimika. Haitatosha kujenga shule kwa wingi tu bali changamoto kubwa iliyo mbele yetu ni kuziwezesha shule hizi kupatiwa walimu bora na vitendea kazi bora. Kutekeleza haya tunaweza kupata elimu bora. Watanzania tunahitaji elimu bora na sio bora elimu. Shule za dahalia ndio suluhisho.

Mheshimiwa Spika, tatizo la msongamano wa magari jijini Dar es Salaam ni tatizo, linakwamisha shughuli za maendeleo. Hata hivyo nionavyo uamuzi unaofikiriwa wa kuanzisha mradi wa mabasi yaendayo kasi hautakuwa mwarobaini wa tatizo la msongamano. Ingefikiriwa zaidi kuanzishwa kwa barabara nyingi na kuzifufua zile zilizo katika hali ya kutopitika. Uanzishwaji wa mradi wa mabasi yaendeyo kasi Dar es Salam huenda ukazua tatizo la walio na daladala kupoteza ajira.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa kuanzishwa mfuko wa maendeleo ya Jimbo ni sahihi na utakaolifanya Bunge letu lifatane na taratibu za Mabunge ya wenzetu hata wa nchi jirani. Lililo la msingi kwa mfuko huu ni kuzingatiwa kwamba kwa upande wa Zanzibar mfuko huu utaleta ufanisi na utafikia lengo lililokusudiwa endapo utawekwa chini ya Ofisi Ndogo ya Bunge Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, jeshi letu la polisi likishirikiana na vyombo vingine vya ulinzi pamoja na msaada wa raia wema limeweza kutokomeza vitendo viovu vikiwemo vile vya kupambana na ujambazi, dawa za kulevya, rushwa na vitendo vingine mbalimbali vinavyoathiri maisha ya watu na ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mema hayo bado lipo tatizo la unyanyasaji wa raia linalofanywa na vyombo vyetu vya ulinzi. Unyanyasaji wa wachuuzi wa bidhaa ndogo ndogo hatimaye utaligharimu Taifa sana kwa kuzalisha wimbi kubwa la vijana wasio na hata kazi za kubabaisha ambao hatimaye hujiingiza katika shughuli za ujambazi.

Mheshimiwa Spika, ieleweke kwamba lipo tatizo kubwa kwenye fedha shilingi bilioni moja na mikoa za kuwawezesha wajasiriamali. Fedha hizi ni vigumu kuwafikia wajasiriamali walio vijijini. Mabenki yaliyopewa dhamana ya fedha hizo yapo zaidi mijini sasa ni vyema utaratibu wa kuzifikisha pesa hizi kwenye *SACCOS* ungekuwa utaratibu muafaka zaidi. Ahsante.

**MHE. ENG. LAUS O. MHINA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze mchango wangu kwa kuipongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu inayoongelea Bajeti ya mwaka huu 2007/2808. Vile vile niupongeze msimamo mzima wa Bajeti ya mwaka huu

kwa kutoa kipaumbele kwa sekta tano kuu ambazo ni elimu, barabara, kilimo, afya na maji, zinazogusa jamii moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze mchango wangu kwa kuanzia na sekta ya miundombinu. Sekta ya miundombinu, barabara, kabla ya yote napenda kuipongeza Serikali ya Awamu ya Nne kwa juhudi zake za kukarabati barabara nyingi hapa nchini, hili tunaliona katika miji mingi ya hapa nchini ukiwemo mji wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, hali halisi ya barabara zetu kufikia Desemba 2006 inaonyesha kuwa tunazo jumla ya kilomita 85,000, kati ya hizo zenye lami ni kilomita 4,430 na zisizo za lami ni kilomita 80,570. Hiki si kiasi kidogo.

Mheshimiwa Spika, hali ya barabara hususani zisizo na lami si nzuri sana hasa nyakati za mvua. Baadhi ya hizo hazipitiki kabisa nyakati za mvua. Nashauri jitihada ziongezwe zaidi kwenye programu ya ukarabati wa barabara zetu, kwani tunaambiwa na wahenga kitunze kiishi.

Mheshimiwa Spika, mpango wa kukuza hadhi baadhi ya barabara zetu ni mpango mzuri kimaendeleo. Tunazo barabara nyingi ambazo ziko kwenye ngazi ya Wilaya ambazo zinastahili kuwa ngazi ya barabara za mkoa. Mfano mzuri uko kwenye jimbo langu ambapo barabara za Korogwe - Bungu ambayo huunganisha Wilaya ya Korogwe na Lushoto. Mombo - Mzeri ambayo huunganisha Wilaya ya Korogwe na Handeni. Kwetonge – Kizara - Zirai ambayo huunganisha Wilaya ya Korogwe na Muheza.

Mheshimiwa Spika, mawasiliano ya simu, Serikali yetu imeonyesha ni jinsi gani inajali umuhimu wa mawasiliano kwa maana ya simu kwa wananchi wake. Napenda kuipongeza na kuishukuru Serikali kwa kueneza mitambo ya simu katika maeneo mengi ya Jimbo la Korogwe Vijijini.

Ombi letu la kupatiwa huduma za mawasiliano katika tarafa za Magoma na baadhi ya Bungu zimekwishatekelezwa. Maeneo mengi katika Tarafa ya Magoma sasa yananufaika na huduma hii.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Korogwe Vijijini wanaomba ile ahadi ya kujenga mnara wa *Vodacom* katika mji wa Magoma na maeneo ya Bungu yafanyike haraka kama Serikali ilivyoahidi kuwa ifikapo Julai mnara wa *Vodacom* katika mji wa Magoma utakuwa tayari.

Mheshimiwa Spika, pia ipo haja ya kuongeza minara ya mawasiliano katika maeneo ya Mashewa, Kizara na Bungu (Mlima Kishaai).

Mheshimiwa Spika, kuhusu bandari ya Tanga ni moja kati ya bandari za kale sana katika ukanda wa Bahari ya Hindi na ni ya pili hapa nchini. Katika miaka ya 1970 na kurudi nyuma bandari hii ilikuwa maarufu sana kwa usafirishaji wa bidhaa za hapa nchini na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, hali hiyo ilidorora kwa muda mrefu, hata hivyo hali imeanza kuwa nzuri kuanzia miaka ya hivi karibuni kwani takwimu zinatuonyesha:-

| | 2004 | 2005 | 2006 |
|---|---|---|---|
| Meli zilizotia nanga | 215 | 281 | 281 |
| Usafirishaji mizigo | 162,000 tani | 289 tani | 519,000 tani |

Mheshimiwa Spika, bila shaka takwimu hizi zitaendelea kupanda kutokana na kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Sasa umefika wakati muafaka kujenga bandari ya kisasa Tanga. Naomba kuunga mkono hotuba ya Waziri Mkuu.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naungana na Bunge zima, wananchi wa jimbo la Mikumi, ninaloliwakilisha na Watanzania wote kutoa pole nyingi kwa familia ya ndugu yetu mpendwa Mheshimiwa Amina Chifupa, aliyefariki siku chache zilizopita. Mola aihifadhi roho yake peponi, *Amin.*

Pili, nakiri kuwa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imejikamilisha katika kila sekta ya uchumi na maendeleo ya nchi yetu kuelekea malengo yetu ya milenia hadi mwaka 2025. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, kutokana na utangulizi huo, mchango ninaoutoa utakuwa katika *point form* kwa kuelezea matatizo, ushauri na maombi, kadri itakavyostahili kwa vipaumbele katika dhana ya kuliendeleza jimbo la Mikumi na kutokomeza umaskini miongoni mwa wananchi kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maji, mji mdogo wa Mikumi ulikwishakamilisha mchango wa shilingi milioni 12.4 kukidhi masharti ya kutekelezwa chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia. Tatizo sugu ninachoiomba Serikali sasa ni kuingilia kati kiburi na msuguano usiokwisha na uliodumaa kwa kipindi kirefu kati ya Meneja wa Kampuni ya Maji Mikumi na wenzake dhidi ya maelekezo na ushauri na maamuzi yanayotolewa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kilosa. Meneja wa Kampuni ya Maji amekuwa akitumia mbinu zisizo wazi, kufanikiwa kupata *Court Injuction* mahakama ya Wilaya ya Kilosa hususan Jaji Mapunda ili kupinga au kuzuia uchaguzi wa viongozi mbadala wa Kampuni hiyo, kwa wananchi kukosa imani nao, kutokana na tuhuma nyingi kama vile kutozingatia sheria za *replacement* ya moja ya tatu ya wajumbe wa Kampuni hiyo, mahusiano mabaya na wadau wote katika mji huo.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali imtume Waziri au Naibu Waziri aje kutuondolea tatizo hili ambalo linaendelea tangu Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa alipokuwa Waziri wa Maji na aliwahi kulitolea agizo jambo hili ambalo kwa kiburi cha Meneja wa Kampuni ya Maji Mikumi, hadi leo halijatekelezwa na uongozi wa Wilaya na hata Mkoa umeshindwa kulitatua, baada ya Mkuu wa Mkoa, *Major General* Mstaafu Saidi Kalembo, kufika Mikumi na kuelezwa na wananchi katika kikao kuwa hawana imani na uongozi wa Kampuni ya Maji wa sasa.

Mheshimiwa Spika, vijiji vingine ambavyo vimekamilisha mchango wao wa shilingi milioni 9.5 kama masharti ya kutimiza ili miradi yao ya maji chini ya ufadhili (kwa pamoja) wa Benki ya Dunia ni Kifinga, Tundu, Iwemba, Msowero na Lumango. Vijiji hivi vyote viko jirani kabisa kando kando mwa barabara ya lami itokayo Mikumi kuelekea Kidatu. Wananchi wanaamini kwa kuwa wamejinyima kwa kutumia fedha kukamilisha michango hii, nimeombwa nisisitize kwa Serikali kuwezeshwa miradi hii sasa itekelezwe. Ili miradi hii Wilaya ifanikiwe Mhandisi wa Maji (hana *qualifications)* ambaye amekuwa Mungu mtu, tunaomba abadilishwe, ana mahusiano mabaya na watendaji karibu wote.

Mheshimiwa Spika, ni budi niipongeze sana Serikali kwa kupitia *TASAF* kukubali kuifadhili miradi ya visima vya maji katika baadhi ya vijiji vilivyoibua miradi hiyo. Ombi ni kwamba utekelezaji uharakishwe, hali ni mbaya sana hasa katika kijiji cha wafugaji cha Ngaiti, Mbamba na Mhenda/Ihakala na Ulaya Mbuyuni.

Mheshimiwa Spika, kilimo, ili mkoa wa Morogoro utimize agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kuufanya mkoa huu uwe ghala ya kuzalisha na kuhifadhi chakula, naishauri Serikali ifanye mambo muhimu yafuatayo:-

Kwanza tuunde Tume ndogo ya wajumbe na wataalam kutoka Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Wizara ya TAMISEMI na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ili wakajifunze taratibu na maandalizi yaliyofanywa na Kampuni ya Sukari Kilombero na kufanikiwa kuwashawishi wakulima wengi wenye vishamba vidogo, vyenye ukubwa tofauti, kuvifanyia *survey* kwa *PGS* na kisha kuviunganisha kuwa *blocks* kubwa. *Blocks* hizi zinalimwa zao moja la miwa kwa trekta kwa haraka na huduma nyingine za utunzaji zinafanywa pamoja hadi uvunaji na mwisho wake mavuno na mapato yanagawanya *propotionally* kadri *GPS* ilivyoonyesha eneo la kila mkulima.

Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu huu mashamba mengi madogo madogo katika eneo ambalo zao la aina moja kama mahindi, mpunga, alizeti au ufuta ndilo linalimwa, itawezekana wakulima kuungana kwa njia hii kuchanga fedha za kukodi trekta wakamudu kulima na kupanda kwa wakati na kuongeza tija na kiwango cha mavuno yao kwa mwaka. Ni vema *plots scheme* ikajaribiwa. Ikifanikiwa, itaweza kuenezwa sehemu nyingine. Kwa njia hii, ndiyo itawezekana hatua kwa hatua kupunguza adha ya mkulima mdogo mmoja mmoja kutumia jembe la mkono.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili muhimu ni kwa Serikali kusahihisha zaidi upatikanaji mikopo na pembejeo kwa wakati. Lakini kubwa zaidi ni kuandaliwa kwa maeneo ya wakulima kuhifadhi mazao yao hata kama ni kuanzisha *godowns* za kukodishwa wakulima kuhifadhi mavuno yao. La mwisho ni kuwaandalia mahali pa kuuzia mazao yao. Utaratibu na hamasa ifanyike, zianzishwe Kibaigwa ndogo ndogo sehemu kunakozalishwa/mazao ya vyakula kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, mashamba makubwa yaliyotekelezwa, Waziri Mkuu alipotembelea Wilaya ya Kilosa alikabidhiwa na Mkuu wa Wilaya Ndugu Athumani Mdoe, orodha ya wamiliki wa mashamba makubwa na maeneo yake ambayo yametekelezwa kwa miaka mingi. Wananchi wengi katika Kata za Mabwerebwere, Masanze, Ulaya na Zombo wanahitaji kulima ili kutimiza dhana ya kujitegemea. Lakini, hawaruhusiwi kuingilia ardhi ya Natu. Kwa hiyo, kwa niaba ya wananchi hawa, naiomba Serikali kukamilisha taratibu zinazotakiwa ili wananchi waruhusiwe kisheria kumiliki maeneo hayo kwa kugawiwa kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa na naomba kipaumbele kipewe wanavijiji wanaoyazunguka mashamba hayo, ambao baba zao au babu zao walikuwa vibarua miaka ya zamani.

Mheshimiwa Spika, miundombinu na kadhalika, Wilaya zote nchini zina barabara mbaya sana. Kila Wilaya imetengewa fedha kwa ajili ya matengenezo. Kila Wilaya itataka kutengeneza hizo barabra mara fedha zitakapotolewa na ninaamini fedha hizo zitatolewa *simultaneously.*

Mheshimiwa Spika, napenda Serikali itujulishe Wabunge je, imefanya *assessment* ya kina kuona kama hivi sasa kila Wilaya ikitaka kuanza matengenezo ya barabara zake, wakandarasi waliopo nchini wana magreda ya kutosheleza na vifaa vingine vya kuwezesha kila Wilaya itengeneze barabara zake kwa wakati mmoja? Kama jibu ni ndio, hakuna tatizo. Ikiwa jibu ni hapana, Serikali ina ushauri gani?

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza sana Ofisi ya Waziri Mkuu kwa jitihada kubwa ya kuweza angalau kuongeza posho za Madiwani kufikia shilingi 60,000/= kutoka shilingi 30,000/= kwa maana ya asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, hakuna shaka ya jinsi gani Madiwani wanavyofanya kazi katika Kata. Kata ndio msingi wa maendeleo ya nchi. Bila Madiwani Wabunge hatuwezi kusimama na kudai tumefanya shughuli sisi. Naendelea kuitaka Serikali iendelee kuangalia suala la Madiwani na kuaongezea posho kwa kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Utawala Bora, amani na utulivu katika nchi yoyote ni msingi wa maendeleo kiuchumi na kijamii. Tanzania ni nchi yenye amani na utulivu kwa miaka 46 sasa, lakini tumeendelea kuwa maskini sababu kubwa ikiwa ni kutokuwa na utawala bora. Ule msemo kwamba ili tuendelee, tunahitaji vitu vine, watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora/utawala bora. Kwa nchi yetu Utawala Bora haupo. Hii inajitokeza pale ambapo watendaji wanapoamua kwa makusudi kufuja fedha za walipa kodi.

Mheshimiwa Spika, *Report* ya *CAG 2007* inatisha kwamba kwa mwaka mmoja tupoteze 1,200,000,000,000, hii ni aibu na Serikali inapaswa kutueleza hatua zinazochukuliwa ili fedha hizo zirejeshwe.

Mheshimiwa Spika, hali ya siasa si shwari. Tunashukuru kwa muafaka wa *CUF* na CCM unaoendelea ili kurejesha hali ya amani, utulivu na haki kule Zanzibar. Pamoja na jitihada hizo, bado tunahoji mlolongo wa vikao usioisha na ukimya/usiri wa majadiliano hayo ambayo yanatupa hisia kwamba uhalali wake una mashaka. Tunaomba majadiliano haya yafikie ukomo na maamuzi yatolewe hadharani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri wa kutumia njia tatu Dar es Salaam. Katika siku za hivi karibuni, Serikali ilitangaza matumizi ya njia tatu asubuhi na jioni *(peak hours),* na tuliambiwa kuna nchi nyingine duniani zinazotumia mtindo huo. Naomba kujua ni nchi zipi hizo! Serikali lazima itambue jukumu lake la ujenzi wa barabara au kuhakikisha mahitaji muhimu yanakuwepo hata maeneo ya nje ya Jiji kama Tegeta, Mbezi, Ukonga na kadhalika. Barabara tatu ni fujo tupu na pia inasababisha ajali na msongamano zaidi. Ni vyema Serikali inapoamua jambo zito kama hilo, basi wadau wahusishwe.

Mheshimiwa Spika, kashfa ya Benki Kuu, Benki Kuu katika nchi yoyote ndiyo mhifadhi mkuu wa fedha zetu na ndio nyenzo kuu ya uchumi wa nchi yetu. Ni jambo la kusikitisha kuona chombo hiki nyeti kwa uchumi wetu na maendeleo ya nchi hii kinaingia katika kashfa nzito namna hii. Namuomba Waziri Mkuu aingilie kati suala hilo na kuhakikisha kuwa Tume huru inaundwa kuchunguza sakata hili ili wananchi wawe na imani uongozi wake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme, wakati ni Watanzania asilimia 10 tu wanaotumia umeme, bado Serikali imeshindwa kutumia makaa ya mawe huko Kiwira na kwingineko. Lakini cha kusikitisha zaidi hata wale ambao wameshatimiza masharti yote ya kufungiwa umeme ikiwa ni pamoja na malipo, hawapatiwi umeme kwa wakati. Pamoja na vyanzo vingine vya umeme kama gesi na *solar,* bado tunashangaa utatumikaje katika nyumba nyingi za vijijini ambazo ni *full-suit,* nyasi?

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu, elimu bora ni pamoja na walimu bora na vitendea kazi na maabara. Pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kutengewa fedha nyingi, bado tunaishauri Wizara iwekeze zaidi katika nyumba za walimu, maabara na mabweni hususan kwa wasichana ili kupunguza tatizo la ujauzito.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naiomba Serikali izingatie ushauri uliotolewa na Kambi ya Upinzani kwani ni rahisi zaidi mtu aliye nje kuona ubovu wa jambo fualani kuliko walio ndani. Nashukuru!

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu uchumi na kilimo, kasi ya ukuaji wa uchumi ni ndogo ukilinganisha na mahitaji ya nchi. Sasa ni kitu gani kitaweza kuchochea ukuaji wa uchumi kwa kasi na ukabaki endelevu. Mpaka sasa ukiondoa mazao asilia, kwa mfano, Kahawa, Pamba, Katani, Chai, Tumbaku, Korosho na Karafuu, hatujatilia mkazo mazao yasiyo asilia na kama tumeyatilia mkazo, basi ni mazao ya dhahabu, minofu ya samaki na bidhaa za viwandani. Ukiacha utegemee bidhaa za viwandani, dhahabu na minofu ya samaki vinaweza vikaisha. *Stocks* za Samaki

zinaweza kuwa *depleted* kwa *over-fishing*. Dhahabu pia zinaweza kumalizika. Kwa hiyo, kama uchumi wetu utajikita kutokana na mauzo ya dhahabu na minofu ya samaki, siku bidhaa hizo zitakapoisha basi na uchumi utaporomoka.

Mheshimiwa Spika, kilimo pekee ndicho kitakachoweza kututoa hapa tulipo. Kama nguvu kazi yote ambayo haiko kwenye ajira rasmi, ikijielekeza kwenye kilimo, bila shaka tutapiga hatua. Aidha, mkazo mkubwa utiliwe kwenye mazao ambayo siyo asilia ili tuweze kukuza mauzo yetu ya nje kama njia ya kujenga uwezo wetu. Mazao ambayo huko nyuma yalikuwa yanashughulikiwa na Shirika la *GAPEX*, yangetiliwa mkazo mazao kama Ufuta, Karanga, Kakao, Ndizi na kadhalika yanaweza kuwa na nafasi kwa soko la nje.

Mheshimiwa Spika, ili usimamizi wa mauzo ya mazao hayo uwe endelevu, napendekeza paundwe Bodi ya Mazao hayo mchanganyiko ili masoko yake yaweze kubainika mapema.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Afya, pamoja na jitihada za kujenga Zahanati na Vituo vya Afya, naishukuru Ofisi ya Waziri Mkuu kwa azma ya kuziboresha Zahanati hizo na Vituo vya Afya kwa kipindi hiki cha mwaka 2007/2008. Katika Wilaya nyingi ikiwemo Wilaya yangu ya Kilombero kumekuwa na uhamiaji wa wananchi wengi kutoka Mikoa mingi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya mahitaji ya dawa katika Zahanati na Vituo vya Afya vingi yalitokana na makisio yaliyofanywa miaka ya 1980. Licha ya watu kuongezeka huko vijijini, kiwango cha dawa kilibakia pale pale. Napendekeza ugawaji wa dawa kwenye Vituo vya Afya na Zahanati uzingatie idadi ya wakazi katika vijiji na kata husika.

Mheshimiwa Spika, *Decentralization by Devolution,* nampongeza Waziri Mkuu kwa kubaini katika hotuba yake kwamba pamoja na nia nzuri ya kupeleka madaraka kwa wananchi, bado rasilimali fedha na rasilimali watu zinaendelea kubaki Makao Makuu ya Wizara. Hata rasilimali fedha zikienda vijijini bila rasilimali watu, utekelezaji wa miradi utapungua.

Mheshimiwa Spika, Wizara ingetakiwa iwe ndogo kimuundo na rasilimali nyingine iende Wilayani ili kutumia uzoefu na uwezo wao katika matumizi bora ya rasilimali watu. Tukifanya hivi, tutakuwa tumepiga hatua.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kubainisha miradi na majukumu yatakayohamishiwa kwenye Mikoa na Halmashauri kutoka Wizara tano za Kilimo, Elimu, Afya, Maji na Miundombinu. Azma hiyo itakuwa imeoana na malengo ya vipaumbele vitano ambavyo vimetiliwa mkazo kwenye hotuba ya Waziri wa Fedha. Tukifanya hivyo, tutaanza kupiga hatua katika kujenga uchumi imara na kuongeza uzalishaji kwani Maafisa Ugani nao watahamia huko.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Birth Certificate,* katika ziara zetu Wabunge karibu sehemu nyingi tumepata tatizo la upatikanaji wa Vyeti ya Kuzaliwa. Wananchi wengi wamependekeza, huduma hiyo isogezwe ngazi ya Tarafa na kama ikibidi sheria ifanyiwe marekebisho ili pamoja na kumtaja Afisa Tawala hata Katibu Tarafa naye aingizwe katika utaratibu wa kutoa vyeti hivi. Wananchi wengi sasa hivi wanaelewa umuhimu wa kuwa na vyeti vya kuzaliwa katika masuala ya elimu, kupata hati za kusafiria na kadhalika.

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Jimbo la Shinyanga Mjini lenye Kata 13, kwa takwimu za mwaka 2005 lina Kata mbili kubwa mno zenye wapiga kura zaidi ya 10,000 kila moja, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu ninaomba yafuatayo:-

(a) Kata ya Ngokolo igawanywe kuwa Kata mbili yaani Ngokolo A na Ngokolo B.

(b) Kata ya Kambarage igawanywe na kuwa Kata mbili, Kambarage na Mwasele.

Mheshimiwa Spika, ombi hili liwekwe katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara za lami katika mji wa Shinyanga zimejumuishwa katika ahadi za Rais na tayari Manispaa ilikwishawasilisha mpango wa ujenzi huo. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu naomba mpango huo utengewe fedha za kutosha angalau kilomita tano kila mwaka kuanzia mwaka 2008/2009 hadi 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Manispaa ya Shinyanga walimwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu alipotembelea Mkoa wa Shinyanga mwaka 2006 kwamba asaidie upatikanaji wa fedha za ujenzi wa soko kubwa la kisasa. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu, naiomba Ofisi ya Waziri Mkuu isaidie upatikanaji wa fedha kwa mwaka 2008/2009 kwa ajili hiyo. Soko la kisasa litasaidia kupanua biashara ya mazao mbalimbali ya kilimo na mifugo, ajira kwa vijana/wananchi wetu na kuongezea mapato ya Manispaa na Serikali kwa ujumla. Mkoa wa Shinyanga ni maarufu kwa kilimo cha mpunga, dengu, choroko na kadhalika. Biashara ya mazao haya na mengine yanahitaji kuboreshwa kwa kujengwa soko la kisasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mkutano wa Nane wa *Sullivan,* kwa kuwa Mkutano huu muhimu unafanyika Arusha kwa karibu wiki moja, tarehe 2 – 6 Juni, 2008, napendekeza yafuatayo:-

(a) Miundombinu, hususan barabara za Mji wa Arusaha ziboreshwe zaidi kwa maeneo yote na mengi ili kurahisisha usafiri na kuongeza mvuto wa Mji huu muhimu kiutalii. *Harambee* au ufadhili wa ziada wa maboresho ufanyike/utafutwe na kazi husika kutekelezwa mapema. Maboresho hayo

yajumuishe ujenzi wa barabara ya lami eneo la Njiro kutoka ilipoishia sasa. Njiro na maeneo mengine ni muhimu sana kwa utalii wa Mji wa Arusha.

(b) Hali ya Usalama wa watu, barabara na mali, viimarishwe zaidi kwani ujambazi na uhalifu mwingine hapa na pale bado vipo.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nimetoa pongezi nyingi nilipochangia kwa kuongea naomba nielekeze mawazo yangu kwenye hoja iliyowasilishwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miundombinu, barabara zetu za Mkoa wa Shinyanga, Kanda ya Ziwa na Wilaya ya Bukombe ni mbovu sana. Kwa nini katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji ukurasa 47 kifungu 67 Mkoa wa Shinyanga haumo? Ni vigezo vipi vimetumika Mkoa wenye miundombinu mibovu kama Shinyanga usiingizwe?

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Bukombe zipo barabara hazipitiki ambapo kilomita 15 ndizo hupitika ambayo ni barabara kuu kutoka Isaka - Burundi/Rwanda ingawa barabara hii ni mbaya sana magari yanapata ajali. Serikali iniambie barabara hii itaanza lini kutengenezwa?

Mheshimiwa Spika, kuhusu maliasili na utalii. Serikali naomba iwaeleze wana Bukombe na Watanzania kwa ujumla, tarehe 7 Aprili, 2007 kijiji cha Mjimwema, Kata ya Uyovu, Wilayani Bukombe. Idara ya Misitu toka Biharamulo majira kati ya saa 7.00 mchana na saa 9.00 mchana walivamia eneo hilo wakachoma nyumba, wakaharibu baiskeli, wakapiga risasi ng'ombe kumi kwa madai kwamba wako kwenye hifadhi.

Mheshimiwa Spika, mamlaka ya kukiuka haki za binadamu walipata wapi? Je, Serikali inawachukulia hatua gani waliofanya tukio hilo?

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini, kwa nini Serikali inaondoa wachimbaji wadogo wadogo waliopo Matabi? Je, mgodi wa Tulawaka haupo ndani ya hifadhi? Mgodi wa Geita pia. Je, wanaofanya utafiti kwenye pori la Kigosi/Mnyowo hamuoni kuwa nao watafiti ndani ya pori la akiba?

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Serikali ni kuwa ilifanye eneo la Matabi liwe eneo la wachimbaji wadogo wadogo kwa wananchi wa Wilaya ya Bukombe, Geita, Biharamulo na Chato.

Mheshimiwa Spika, barabara zenye urefu wa kilomita 108 (20.3%) ndizo hupitika na barabara zenye urefu wa kilomita 423.8 hazipitiki. Mfano wa barabara ambazo hazipitiki ni pamoja na moja, Buntubili-Bulega-Kakoyoyo-Lulemela-Kashelo-Ilolagulu – Mbogwe –Ushirika -Lunguya to Kahama, pili, Mwalo-Iyegelo-Bugelenga-Nsango-Iponya-Masumbwe-Lugunga-Nyasato-Mbogwe-Mwaenda mwizo-Ivumo to Geita na tatu, Uyovu- Bugege-Namonge- Namalandula.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iziangalie kwani Wilaya itapata maendeleo na kuongeza uchumi wa wana Bukombe wenye kipato chao ni chini ya dola moja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu, tatizo la watoto yatima/wasiojiweza naomba Serikali iangalie utaratibu wa kuwachagua vijana wote. Kwa nini wanaochaguliwa *second selection* wengi wanabaki bila kupata msaada huo?

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali inisaidie kujua vijana wanaofiwa na wazazi wao wakiwa shuleni wanapataje msaada? Kwani wengi wamekuwa wakienda kutafuta ufadhili wa Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Ma-*DC* na Waheshimiwa Madiwani.

Mheshimiwa Spika, Serikali naomba iisaidie Idara ya Utamaduni kwenye Halmashauri za Wilaya zetu wanapata wapi fedha. Mbona Idara hii inasusua sana hawana mwelekeo, hawana fedha, ofisi mbaya, usafiri hakuna, watatimizaje azma ya Mheshimiwa Rais ya kuendeleza michezo?

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja hii.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kuchangia kwa kuzungumza, naomba niendeleze mchango wangu kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ahadi za Serikali. Katika Bunge lako Tukufu ahadi zifuatazo zilitolewa na Serikali kwa maeneo yafuatayo:-

Kwanza, kutengeneza barabara ya Mbalizi-Mkwajuni-Makongolosi kwa kiwango cha changarawe na kiwango cha lami kwenye sehemu tatu korofi. Kwa kuwa kazi bado haijaanza kufanyika, naomba angalau sehemu ambazo ni korofi zijengwe kwa kiwango cha lami wakati au kisubiri fungu kubwa la fedha.

Mheshimiwa Spika, pili, kuweka tuta kwenye barabara ya Njiapanda Galula-Magamba-Namkukwe upembuzi yakinifu tayari umemekwishakamilika. Wakati wa masika barabara hii haipitiki kabisa. Naiomba Serikali ilishughulikie tatizo hilo.

Tatu, kuwalipa wakulima madeni ya pamba kama Serikali ilivyoahidi hapa Bungeni, nne, kuwawinda mamba waharibifu upande wa Kusini mwa Ziwa Rukwa kwenye Jimbo la Songwe, tano, malipo ya mirathi yafanyike kwenye Jimbo la Songwe, sita, malipo ya Bima kwa walimu, saba, kuanzisha kilimo cha umwagiliaji kwenye Bonde la Songwe na nane, kuwawezesha watendaji wa Kata na Vijijini. Ikiwezekana wakopeshwe pikipiki na baiskeli. Naishukuru Serikali kwa kuongeza posho kwa Madiwani.

Mheshimiwa Spika, maombi mapya, moja, Wilaya ya Chunya ina ukubwa wa asilimia 46 ya eneo lote la Mkoa wa Mbeya. Kutokana na kukubwa wa Wilaya hiyo inashindikana kulihudumia kimaendeleo. Nashauri Wilaya hii igawanywe na kuwepo na Wilaya mbili.

Pili, fedha iliyotolewa kwa wajasiriamali bado haijafika kwenye Jimbo la Songwe. Naomba fedha hizo zipelekwe pia kwenye Jimbo hilo kama ilivyofanyika kwenye Jimbo la Lupa.

Tatu, naiomba Serikali ifikirie kutoa posho ya motisha hasa kwa walimu wanaofanyia kazi kwenye mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Spika, mojawapo ya majedwali yaliyoambatanishwa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu inaonyesha kuwa Halmashauri ya Mbulu inadaiwa na Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa kiasi cha shilingi milioni 10. Hiii siyo sahihi kwani Halmashauri hiyo haijawahi kukopa kutoka kwenye Bodi hiyo. Naomba sahihisho lifanyike.

Pili, katika muda wa mwaka mmoja sasa TAMISEMI imewahamisha watumishi muhimu sana zaidi ya nane. Watumishi hao ni Afisa Kilimo wa Wilaya *(crops), DALDO,* Afisa Mipango wa Wilaya, Afisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya, Afisa Mipango Msaidizi wa Wilaya, Afisa Ushirika Mwandamizi wa Wilaya na kadhalika.

Katika nafasi hizo zilizojazwa ni nafasi mbili tu. Afisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya na Afisa Mipango Msaidizi. Bado uhamisho unaendelea na sasa ni katika ngazi ya Maafisa Ugavi. Hali hii imedhoofisha sana utendaji katika Halmashauri kwa vile Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya tuliyeletewa pia ni dhaifu sana. Tunaomba uhamisho wa watumishi kutoka kwenye Halmashauri hii sasa usimamishwe hadi nafasi zote zilizo wazi kujazwa.

Tatu, maombi yetu ya kusajili na kuandikisha vijiji vipya yamekaa kwa muda mrefu Wizarani.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mewnyezi Mungu kwa mema yote aliyonijalia mpaka hivi leo. Pia naomba nitoe pole kwa familia ya marehemu ya Mheshimiwa Amina Chifupa, kwa msiba mzito uliotokea tarehe 26 Juni, 2007 katika hospitali ya Lugalo, Jijini Dar es Salaam. Bwana alitoa na Bwana ametwaa jina lake lihimidiwe . *Amin.*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne kwa jitihada kubwa za ndani ya nchi na nje ya nchi katika kutafuta maisha bora kwa kila Mtanzania. Pia nampongeza Mke wa Mheshimiwa Rais mama Salma Kikwete kwa juhudi kubwa anayoifanya katika kuwasaidia watoto wa kike kielimu.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuchangia hotuba hii iliyopo mbele yetu kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu si tu kwa kuhimiza ujenzi wa shule za sekondari bali pia kwa ufuatiliaji wake wa karibu kero za wananchi zikiwemo *operation* safisha Jiji la Dar es Salaam; kuondoa wafanyabiashara wadogo wadogo

barabarani; kipindupindu na homa ya bonde la ufa. Ameshirikiana na uongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam jinsi ya kupunguza msongamano wa magari na zoezi hili limefanikiwa kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kufanikisha upatikanaji wa *Government Guarantee,* kwa ajili ya Jengo la wafanyabiashara wadogo wadogo (Wamachinga) ambalo linakadiriwa kuchukua wafanyabiashara 10,000 kwa pamoja. Ingawa kumekuwa na urasimu mkubwa kwa kuchukua takriban miezi nane mpaka *Government Guarantee* kupatikana.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni nzuri sana na imekidhi haja za Watanzania walio wengi kinachotakiwa ni utekelezaji tu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo bado kuna mapungufu makubwa katika utendaji kazi ambayo ni lazima yafanyiwe kazi kwa umakini zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwajibikaji katika kazi. Katika Idara za Serikali, Halmashauri na hata taasisi za umma kuna baadhi ya watumishi ambao hawana habari na kasi mpya na pia hawana uzalendo kabisa na nchi yao mara nyingine huwakatisha tamaa watumishi ambao wana nia njema na wachapakazi.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba turudishe utaratibu wa usimamizi wa karibu unaokaribiana na unaopakana. Bila usimamizi wa karibu hatuwezi kupata maendeleo tunayotarajia. Kuwe na utaratibu wa kutoa taarifa za kazi na mpango wake wa kila mfanyakazi kwa kila mwezi ili ijulikane kila mtumishi amezalisha kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, nanukuu maandiko Matakatifu Luka 10, mstari wa 2-3: “Akawaambia mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache; basi mwombeni Bwana wa mavuno apeleke watenda kazi katika shamba lake.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, namwomba Bwana wa Mavuno ambaye ni Rais, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, aongeze watendaji kazi wenye kasi mpya na awaondoe ambao wana usingizi wa pono maana hawataamka kamwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Kwa kuwa ni uchangiaji wa maandishi natoa maelezo yangu kama ifuatavyo:-

Moja, uhamishwaji wa wanyama kutoka Mbeya (Ihefu) kuletwa Mkoa wa Lindi na Mtwara. Napenda kutoa taarifa kuwa mifugo haitoki uko Mbeya tu bali na Mikoa mingine ya wafugaji. Kwa kuwa Jimbo langu ndiyo kiingilio kikuu (Kilwa Kaskazini), naomba miundombinu ifanyike kwa haraka iwezekanavyo kabla ya migogoro ya wafugaji na wakulima haijajitokeza.

Pili, kilimo bora, wananchi wa Kilwa Kaskazini wapo tayari kulima mazao kama vile Ufuta, Korosho, Nazi, Michungwa na mazao ya chakula na kadhalika. Maombi yao ni kuhusu uuzwaji na ugawaji wa pembejeo ufanyike kwa ufanisi, yasitokee yale yaliyotokea msimu uliopita.

Mheshimiwa Spika, tungefurahi kama tungepewa trekta angalau mbili ili wananchi wa Kilwa wanaondokane na kilimo cha jembe la mkono waingie kwenye kilimo cha kisasa.

Tatu, kuhusu gesi, mapato yatokanayo na gesi ya Songosongo Halmashauri ya Wilaya nayo ingepewa angalau chochote kile ili na sisi tujione tuko katika Tanzania ya sasa na nne, Kilwa Kaskazini kuna mapango zaidi ya 21 ambayo yalitumika kujifichia wakati wa vita vya Majimaji. Naomba yafanyiwe taratibu ili yapewe uzito wa juu ili yatambuliwe kitalii. Kumbuka Mapango ya Nang'oma na Namaengo yaliyopo kwenye Kata ya Kipatimu ni makubwa kuliko hata yale ya Amboni, Tanga. Lakini kwa bahati mbaya mapango hayo hayajapewa uzito wake ili yakawa na sifa ya utalii.

Tano, kuhusu hospitali, katika Jimbo langu hakuna hospitali kuu, wananchi wana safari ya kilomita nyingi kwenda kwenye hospitali ya Wilaya iliyopo Kilwa Kivinje kupata matibabu kwa matatizo hayo yote naona sasa ni wakati muafaka wa kuigawa Wilaya ya Kilwa kuwa Wilaya mbili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mawasiliano ya simu katika Tarafa ya Njinjo nayo yanastahili kupewa uzito wake.

Mwisho, pamoja na hayo naunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. KHADIJA SALEH NGOZI:** Mheshimiwa Spika**,** kwanza kabisa naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuniteuwa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nasema ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, pia naomba niungane na Watanzania wenzangu kwa msiba uliotupata kwa kifo cha mwenzetu Mheshimiwa Amina Chifupa, na pia kutoa pole kwa familia zote zilizopoteza ndugu, jamaa na marafiki zao katika ajali mbaya za mabasi. Mungu azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuipongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, hotuba ambayo imeonyesha mafanikio makubwa ya nchi ambayo yamefanyika katika kipindi cha mwaka mmoja na nusu kwa uongozi wa Rais wa Awamu ya Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa iwe changamoto au iwe ndiyo mwongozo wa kila kiongozi mpenda maendeleo katika shughuli zake za kila siku popote atakapokuwa Serikalini imeonyesha uwezo wake

mkubwa wa kusimamia na kutekeleza majukumu yake kikamilifu kama Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 inavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anazoendelea kuzifanya kwa juhudi na maarifa. Nasi tunatakiwa tumuungune mkono na tumsaidie katika shughuli mbalimbali za kimaendeleo ambazo kazianzisha ili ziendelee kuwa changamoto ndani na nje ya nchi. Tufanye kazi kwa bidii na maarifa zaidi na pia sisi viongozi tuhakikishe kuwa kila mwananchi aliye na uwezo wa kufanya kazi halali afanye kazi.

Mheshimiwa Spika, tuwape ushirikiano viongozi wetu hawa wawili Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa na tuwape moyo ili waendeleze amani na utulivu uliopo ndani ya nchi yetu na vile vile waendelee kuimarisha Muungano na kujenga mahusiano mazuri ya kisiasa na kudumisha utawala bora. Mwenyezi Mungu awabariki na tumpe raha Rais na Baraza lake zima ili afanye kazi alizopanga kwa manufaa ya wananchi wa Taifa zima.

Mheshimiwa Spika, mwisho naungana na wenzangu kwa kuunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. NURU AWADH BAFADHILI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kwa niaba ya wananchi wa Jiji la Tanga, napenda kuungana na Wabunge wenzangu kuipa pole famili ya marehemu Mheshimiwa Amina Chifupa, Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, moja, ubadhirifu katika Halmashauri ya Jiji la Tanga. Wakati wa ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu mwaka 2006 alipotembelea Jiji la Tanga wananchi walimweleza kero mbalimbali ikiwemo ya ubadhirifu au ufujaji wa fedha za Halmashauri. Mheshimiwa Waziri Mkuu aliahidi kuundwa kwa Tume kuchunguza ubadhirifu huo, je, nini hatma ya Tume hiyo?

Mheshimiwa Spika, pili, marudio ya uchaguzi Kata ya *Old- Korogwe* (hali ya Mji wa Korogwe). Ulifanyika uchaguzi wa marudio katika Kata ya *Old Korogwe,* vyama vilivyoshiriki uchaguzi ni *CUF,* CHADEMA, *UDP, TLP* na Chama cha Mapinduzi. Mgombea yule aliwekewe pingamizi na mgombea wa CHADEMA kwa hiyo hakugombea. La kushangaza huyo aliyewekewa pingamizi ndiye aliyefungua kesi Mahakamani na mshindi (mgombea wa *CUF*) hajaapishwa hadi leo amepewa *drawn order.* Je, ni kigezo kipi kilichomzua Diwani aliyeshinda asiapishwe wakati Kata husika inakosa mwakilishi katika Halmashauri yao ya Mji? (Ushahidi nimemkabidhi Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI).

Mheshimiwa Spika, kutokuwa muwazi Afisa Mipango wa Jiji la Tanga, mhusika ana tabia ya kutokuwa muwazi kwa Afisa Mipango Miji. Mfano hai ameuza eneo la makaburi aliyozikwa marehemu muwe wangu. Baada ya mazungumzo naye Afisa Mipango Jiji alikiri kusimamia uuzaji wa eneo hilo na akadai ofisi yake imemlipa fidia

aliyedai ni mhusika wa eneo hilo. Ofisi yake ililipa shilingi 309,000. Baada ya mimi kufuatilia alinitaka nirudishe fedha hizo kwenye ofisi yake ili turudishiwe eneo letu. Mimi nilitoa pesa hizo na nikapewa risiti yenye namba Na. A 03467 ya tarehe 8 Desemba, 2006, hadi leo sijarudishiwa eneo hilo na badala yake alinileteа barua kupitia shemeji yangu Saad Mohamedi Mbambu yenye Kumb Na.TAD/124/4 ya tarehe 22 Februari, 2007 ya kuelezea kuwa tayari eneo hilo limekwishapimwa kwa ajili ya umma. Kumbe alilijua hilo mbona alichukua pesa hizo? Je, huu sio utapeli?

Mheshimiwa Spika, tatu, kumnyang'anya miliki halisi wa kiwanja *Plot No.4/29 Block KBI,* Bombo na kumpa mtu mwingine na kuambiwa kuwa iwe ndoto kujenga eneo hilo, je, hii ni hali gani? Haya ya Afisa Mipango Miji ninao ushahidi.

**MHE. MANJU S. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naunga mkono hoja hii. Napenda nieleze wazi kuwa hotuba imesheheni taarifa sahihi zinazogusa karibu sekta na majukumu yote ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu walimu, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kigoma Kusini napenda kuipongeza Serikali kwa juhudi za kuandaa walimu katika shule za sekondari na za msingi. Hata hivyo, kwa niaba ya wapigakura wa Kigoma Kusini naomba ufanywe utaratibu wa makusudi wa kuwapatia walimu kwa upendeleo pekee. Tunaomba ieleweke kwa kuwa huko kuna mazingira magumu na watumishi wengi na sio walimu hawapendi kuwenda huko kwani hakuna vivutio kama barabara, umeme, maji na huduma ya afya ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu lugha ya Kiswahili. Kiswahili kama lugha ya Taifa yaelekee hakipewi umuhimu unaostahili. Serikali inatakiwa itambue kuwa ni sisi tunaotakiwa kukienzi Kiswahili. Hivi ni kwa nini hadi sasa hatujawa tayari kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia na kujifunzia tangu elimu ya msingi, sekondari hadi elimu ya juu?

Hivi Wachina wanajifunza kwa kutumia lugha gani katika mfumo wake wa elimu? Wamepata mafanikio makubwa kiuchumi na kisayansi kwa kutumia lugha yao ya Kichina. Naomba wakati wa majumuisho nipatiwe maelezo ya kwa nini Kiswahili hakipatiwi hadhi inayostahili? Kwa nini hatuwezi kutambua kuwa Kiswahili kitawezesha wanafunzi na wasomi wetu kufanya kazi vizuri kwani watakuwa wanajifunza na kujifundishia katika lugha wanayoifahamu vizuri sana. Kwa kusema hivi haina maana kuwa Kiingereza na lugha nyingine zipuuzwe la hasha, bali zipewe nafasi yake pia.

Mheshimiwa Spika, kupatiwa Wilaya. Ili kurahisisha masuala ya utawala na uongozi sasa ni wakati muafaka kupata Wilaya nyingine mbili zitakazotokana na Wilaya za Kigoma na Kigoma Vijijini kufanyika kwa hili kutawezesha wananchi kupata huduma karibu.

Mheshimiwa Spika, Kamati za ushauri za Wilaya, napendekeza uendeshaji wa Kamati za Ushauri za Wilaya uwe sawa na zile za Mikoa. Kwa nini washiriki wa Kamati za Wilaya hawalipwi posho kama wale wa Kamati ya Mkoa? Natumaini wakati wa

majumuisho nipate maelezo ya namna gani Kamati za Wilaya zitatengewa fedha za kuziendesha kama vile zile za Mkoa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja hii.

**MHE. KHADIJA SALUM AL-QASSMY:** Mheshimiwa Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia leo hii nikawa mzima na nikaweza kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kutoa mkono wa rambirambi kwa kifo cha mpendwa wetu Marehemu Amina Chifupa, Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Spika, kwanza, naanzia kwenye mambo ya afya hasa akinamama wa vijijini wakiwa wajawazito ambao bado hawana mwamko au ni gharama za malipo zinazowasababishia kutokwenda hospitali kujifungua na kusababisha vifo vya watoto na akinamama kwa wingi, naiomba Serikali izidishe mkakati wa makusudi kufuatilia hospitali ambazo bado zinawalipisha wananchi na kuwasababishia kutokwenda hospitali.

Mheshimiwa Spika, vile vile hospitali ya *Ocean Road* ya *Cancer,* ijengwe nyingine kwani hospitali hiyo imekuwa ni ndogo kiasi cha kuwasababishia usumbufu mkubwa sana watu ambao wanatoka katika sehemu mbalimbali, angalau Serikali ingejenga hospitali nyingine kwenye Mkoa mwingine ili kuwapunguzia Watanzania matatizo.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kuiomba Serikali iwahurumie wale Polisi wanaofanya kazi kwenye mazingira magumu kwa mfano, kama wanaofanya kazi kwenye maeneo yenye hatari kubwa na majambazi, wengi waongezewe posho ili wafanye kazi za kuokoa maisha ya watu kwa moyo mkubwa. Vile vile waongezewe mshahara wale askari ambao wamepandishwa vyeo ili iendane na hadhi yao, isiwe vyeo tu.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ifanye mikakati kabambe juu ya usafiri wa watoto wanaokwenda shule japo kwa bei nafuu, kwani hali ya watoto wanaokwenda shule ni usumbufu mkubwa na ni rahisi kwa watoto wa kike kughilibiwa na kuweza kupata mimba kutokana na usumbufu huo. Vile vile wajitahidi kujenga mabweni ili watoto wetu wawe na utulivu kwenye masomo yao.

Mheshimiwa Spika, napenda kuongelea habari ya rushwa pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu kulipa jambo hili kipaumbele, lakini na mimi natoa maoni yangu kuhusu jambo hili.

Mheshimiwa Spika, rushwa haiwezi kuondoka kama Serikali haijachukua hatua za makusudi ili kuondoa urasimu katika baadhi ya Ofisi za Serikali, hasa zile zenye huduma muhimu na vile vile kuboresha maslahi ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu dawa za kulevya ili kumuenzi Mheshimiwa mpendwa wetu Marehemu Amina Chifupa, jinsi alivyolipigia kelele, tunaomba lishughulikiwe kwa nguvu zote hasa ikizingatia hata ile siku aliyofariki dunia ilikuwa ni siku ya kupambana na dawa hizo za kulevya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri katika Jiji la Dar es Salaam na msongamano wa magari, kwa kweli ni usumbufu mkubwa, ingawa Mheshimiwa Waziri Mkuu alilitafutia ufumbuzi wa muda mfupi, lakini haitoshi.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri Serikali ili kulipunguza tatizo hili ni bora ikatengeneza zile njia za *feeder road* ili ule msongamano ukaweza kupungua.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kutoa mchango wangu.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa TAMISEMI, Naibu Waziri wa TAMISEMI na watendaji wote kwa kuandaa hotuba nzuri inayoonyesha maendeleo tuliyofikia na tunakoenda na kuwasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa Bungeni. Baada ya maneno ya utangulizi, naiomba Serikali iangalie mambo yafuatavyo:-

Moja, barabara za Mji wa Dodoma ni mbaya na Serikali inaziona lakini hakuna juhudi za kuzitengeneza. Naomba Serikali ieleze imejiandaa vipi na utengenezaji wa barabara za Mji wa Dodoma kulingana na kasi ya ukuaji wa Mji wa Dodoma ukizingatia Mji huu unakua na vyuo vikuu vinaongezeka.

Pili, ningependa kujua miundombinu ya maji machafu itapanuliwa lini katika maeneo ya ujenzi wa nyumba za makazi zilipo.

Tatu, kwa kuwa suala la ajali za barabarani zimezidi naomba Serikali ifanye utafiti wa kina kwa nini ajali zimekuwa nyingi. Ushauri wangu Serikali iendeshe semina kwa madereva ili kuwakumbukusha wajibu wao na kuwapa moyo katika kazi zao.

Mheshimiwa Spika, narudi tena kuwampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jinsi anavyojituma kusimamia kazi za maendeleo. Namtakia kila la kheri na mafanikio makubwa katika kazi zake za kila siku yeye na wote wanaomsaidia katika ofisi yake.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kutoa salamu za rambirambi kwa wazazi wa marehemu Mheshimiwa Amina Chifupa, kwa kuondokewa na mtoto wao. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi, *Amin* na Mwenyezi Mungu awape faraja ili waweze kuhimili msiba huo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. ZULEIKHA YUNUS HAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naipongeza hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu jinsi ilivyopangika na kueleweka

na pia kwa namna alivyoiwasilisha kwa kuisoma kwa ufasaha na ufanisi. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, nikiwa mwakilishi wa watu wenye ulemavu katika Bunge letu Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, naona kwenye Bajeti Mheshimiwa Waziri hakugusia kuhusu masuala ya watu wenye ulemavu. Labda yamejificha kwenye Wizara inayohusika, hivyo siwezi kulaumu sana.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ambao watu wenye ulemavu wamenituma ni kwamba, kwa kuwa masuala ya watu wenye ulemavu ni mtambuka, ni vyema yangekuwa katika sekta zote za ujenzi wa Taifa ambazo zitawajibika kuwaendeleza na kuwapatia huduma kulingana na mahitaji yao ya kijamii, kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni, kidemokrasia, kimazingira, kisayansi na kiteknolojia. Kutoakana na ukweli huo ni vyema masuala ya watu wenye ulemavu yawe chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo ndiyo yenye uwezo wa kuelekeza na kuagiza Wizara na Idara mbalimbali kwa utekelezaji. Kwa mfano, Tanzania Visiwani, masuala ya watu wenye ulemavu yapo chini ya Ofisi ya Waziri Kiongozi, wakati kabla yalikuwa chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iridhie Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watu wenye Ulemavu mapema iwezekanavyo. Pia Serikali iboreshe miundombinu na huduma kwa watu wenye ulemavu. Aidha, Serikali ifikirie kuongeza kasma ya kununulia visaidizi vitakavyowawezesha watu wenye ulemavu kumudu mazingira yao, kwa mfano, viti vya magurudumu mawili, baiskeli za magurudumu matatu, fimbo nyeupe, mashine za nukta nundu, viungo bandia na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Serikali ihamasishe uondoaji wa umaskini kwa kusisitiza kuwepo kwa mafunzo ya biashara na kazi za amali na utoaji wa mikopo kwa watu wenye ulemavu. Aidha, naishauri Serikali kuongeza nafasi za upendeleo za wawakilishi wa watu wenye ulemavu katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na kwenye vyombo vyote vyenye kutoa shauri.

Mheshimiwa Spika, narudia tena kuunga mkono hotuba ya Bajeti, mimi binafsi na kwa niaba ya watu wenye ulemavu Tanzania.

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Spika, eneo la Hifadhi ya *Emboley Mortangos* lina ukubwa wa hekta 306,200 na limetengwa na vijiji saba vyenye jumla ya watu wapatao 24,858 ukiondoa wavamizi katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kuwaondoa watu waliovamia maeneo ya hifadhi ya *Emboley Mortangos* ilikuwa ni pamoja na kuvunja makazi yao waliyoanzisha kiholela kama vitongoji na kuhakikisha watu hao wanaondoka katika maeneo hayo na wanaacha shughuli zote za kilimo na makazi. Utekelezaji ulianza rasmi tarehe 19 Desemba, 2006 kwa vijiji kuwashirikisha wataalamu wa Idara ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Askari Polisi, Mgambo na viongozi wa Kata na Tarafa. Hadi kufikia Juni, 2007 jumla ya watu wapatao 17,200 waliondolewa katika maeneo yaliyofanyika oparesheni. Zoezi hili

lilienda sambamba na kuwafungulia mashtaka wahalifu wakubwa 12 ambao walibainika kuharibu maeneo makubwa kwa kufyeka kati ya ekari 500 hadi 5000 kwa kila mmoja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Tume iliyoundwa na Mkoa kwenda kusikiliza malalamiko ya akinamama Wilaya ya Kiteto, wananchi wameomba viongozi wafuatao wavuliwe madaraka kwani ndio wanaouza ardhi kwa wavamizi, Diwani wa Sunya, William Kaula anauza Hifadhi ya Siledo, Diwani wa Partimbo akishirikiana na viongozi wafuatao, Maiba Sukana, Mabire Oloikurkur. Tume ilipendekeza hao wote wasimamishwe uongozi kabla ya oparesheni. Maeneo yale yote yaliyofanyiwa oparesheni, wamesharudi katika maeneo yao na waliowarudisha ni wale viongozi walioagizwa na wale Madiwani. Naomba Serikali ifanye kazi yake.

Mheshimiwa Spika, matatizo, wavamizi kufungua mashtaka mahakamani na mahakama kutoa amri ya kusitisha zoezi hilo mpaka kesi yao itakapomalizika na kesi hii itaanza kusikilizwa kwa mara ya kwanza katika Mahakama Kuu Kitengo cha Ardhi Dar es Salaam tarehe 12 Julai, 2007 wakisaidiwa na Taasisi ya Sheria na Haki za Binadamu.

Mheshimiwa Spika, wavamizi 17 bado wako mahakamani, wananchi wanajiuliza wako kwa maslahi ya nani? Kijiji au Serikali ya Kijiji hawajatoa ardhi yao, Halamashauri ya Wilaya haijatoa ardhi, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya haijatoa ardhi, Wizara ya Ardhi haijatoa ardhi! Nguvu ya kwenda Mahakamani inatoka wapi angali wao ni wavamizi wa ardhi?

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Haki za Binadamu, kwanza walianza kutoa elimu kwa wanavijiji wetu wakati wavamizi walipovamia ardhi ya wanavijiji, mpaka wanavijiji wakaanza kuandamana kudai ardhi yao. Kitengo cha Haki za Binadamu kinagonganisha wananchi wavamizi wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya wavamizi wanatishia amani viongozi wa vijiji na kudiriki hata kulipiga mawe gari la Halmashauri na kuvunja vioo lilipokuwa huko kikazi. Aidha, kesi kucheleweshwa kusikilizwa na kufikia maamuzi kwa kuahirishwa mara kwa mara hasa zile kesi za wahalifu wakubwa. Pia Hakimu wa Wilaya analima kwenye Hifadhi sehemu ya Napilukunya na bado anapokea kesi ya wavamizi. Anawezaje kutoa hukumu angali analima kwenye Hifadhi? Kila siku kuiahirisha kesi na kuzingatia *court injunction* kwa wale wahalifu wa mazingira. Naomba huyu Hakimu ahamishwe mara moja!

Mheshimiwa Spika, mazungumzo kati ya *RPC* na Mkuu wa Wilaya ya Kiteto na *OCD,* hakuna ushirikiano wowote. *RPC* anafanya oparesheni bila kumwarifu Mkuu wa Wilaya. Pia, baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wanalima katika maeneo ya Hifadhi, Mfano, Mkuu wa Gereza la Kibaya *(conflict of interest)* na *DT,* Mhandisi wa barabara. Naomba iundwe Tume kama ile ya Ihefu ili wafugaji watendewe haki na ardhi yao.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nichukue fursa hii kuipongeza Serikali ya Awamu ya Nne kwa kazi nzuri ambayo inaifanya ili

kuwaondolea kero Watanzania wote. Pongezi zangu za dhati ziwaendee Rais Jakaya Kikwete na Waziri Mkuu kwa uongozi wao imara ambao umetupatia sifa kubwa kutoka kila pembe ya dunia. Nawapongeza sana!

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, napenda kutoa mchango wangu katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza ni mgawo wa fedha za Halmashauri, kwa muda mrefu sasa Serikali imekuwa ikigawa fedha katika Halmashauri zetu kwa ajili ya ujenzi wa madarasa, ununuzi wa madawati na kadhalika. Tatizo lililopo hapa ni ugawaji usiozingatia gharama za ujenzi ama wingi wa wanafunzi waliojiandikisha katika shule. Kwa mfano, wakati bei ya saruji Dar es salaam ni kama shilingi 10,500/=, mfuko huo huo unauzwa shilingi 18,000/= Wilayani Bunda. Ugawaji kama huu unazikwaza baadhi ya Halamashauri na kuzifanya zishindwe kutekeleza majukumu yake kama zile za Dar es salaam. Pia ugawaji mwingine mbaya uko katika ujenzi wa madarasa katika shule za msingi kwa mfano, wakati Mkoa wa Mara umeandikisha wanafunzi 421,638 ulijengewa madarasa 138, Mkoa wa Pwani uliandikisha wanafunzi 129,517, ulijengewa madarasa 349. Naomba Serikali iliangalie hili kwa umakini mkubwa ili kupeleka rasilimali nyingi kule ambako zinatakiwa.

Pia kuongeza Mahakama ili kuondoa msongamano wa mahabusu magerezani. Kwa muda mrefu sasa kumekuwepo na msongamano wa mahabusu na kesi katika Mahakama zetu zote za Mwanzo hadi Mahakama Kuu. Hali hii ni kero kubwa sana kwa wnanchi wetu. Naiomba Serikali ijenge Mahakama za Mwanzo katika kila Kata na pia kuwaajiri Mahakimu na Majaji wa kutosha ili kuwapatia wananchi wetu haki zao kwa haraka kuliko ilivyo sasa ambapo baadhi ya kesi zina zaidi ya miaka mitano bila kuanza kusikilizwa. Pili, ili Serikali iweze kutatua tatizo la msongamano wa mahabusu katika magereza yetu, napendekeza Serikali ipitie kesi zote ambazo hazijasikilizwa kwa lengo la kuwaachia mahabusu ambao wameshakaa magerezani kwa muda mrefu zaidi kuliko vifungo vyao kama mahakama zingewakuta na hatia. Hatua hii siyo tu kwamba itasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza msongamano, bali pia itatujengea heshima kubwa kwa wananchi wetu na pia kwa washiriki wetu wa maendeleo hasa *Human Rights Groups*.

**MHE. MOHAMED ALI SAID:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mungu kwa kutuwezesha kutuweka katika hali ya afya njema Wabunge wengi waliomo humu na wale wenzetu wachache ambao hali zao siyo nzuri, Mwenyezi Mungu awajaaliye afya njema. Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema peponi Amina Chifupa Mpakanjia.

Mheshimiwa Spika, vile vile nikushukuru wewe mwenyewe binafsi kwa jinsi ulivyoendesha Bunge hili kwa umahiri sana. Nianze kuchangia yafutayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu dawa za kulevya. Suala la dawa za kulevya linakuwa ni tatizo kubwa hapa nchini. Vijana wetu wengi wanaathirika kutokana na dawa za kulevya. Kwa hiyo, naomba sheria zilizopo zinazohusu dawa za kulevya zibadilishwe

na hatimaye sheria kali ziwekwe kuhusu dawa za kulevya ili kuwanusuru vijana wetu kwani sheria zilizopo sasa hivi, zimepitwa na wakati.

Mheshimiwa Spika, pili, hali ya siasa Zanzibar siyo nzuri, lakini kwa vile Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete alizungumzia suala hili katika hotuba yake ya kwanza ndani ya Bunge hili. Ni matumaini yetu kutokana na umahiri mkubwa alionao Rais wetu, suala hili atalitatua vizuri na pande zote mbili zenye kuhusika zitafurahi. Kwa hiyo, naomba mazungumzo ya muafaka yanayoendelea yamalizwe salama kwa muda uliowekwa na kwa mafanikio makubwa, *Amin.*

Mheshimiwa Spika, tatu kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki, naomba katika Jumuiya hii Zanzibar ishirikishwe kama nchi ili nayo iwe na uwakilishi kamili na Jumuiya hii ijulikane kuwa ni Jumuiya inayoshirikisha Tanzania Bara, Zanzibar, Kenya na Uganda kama ilivyokuwa hapo zamani na kwa sababu kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwa kuna baadhi ya nchi tayari zimeshajiunga ma Jumuiya hii, nazo pia zijiunge kwa mtiririko huo wa kuanzia nchi moja hadi namba ya mwisho.

Mheshimiwa Spika, nne, ni kuhusu Jeshi la Polisi. Jeshi la Polisi linafanya kazi nzuri sana, lakini lazima tufahamu kuwa askari wetu wanafanya kazi nzito ndani ya mazingira magumu sana. Kwa mfano, askari wetu wengi hawana nyumba, hawawezi kujikimu kimaisha na kadhalika. Kwa hiyo, naomba askari hawa wajengewe nyumba nzuri kwenye kambi zao na vile vile mishahara yao iboreshwe na mshahara wa askari wa chini uwe shilingi 300,000/= ili waweze kujikimu kimaisha. Nashukuru.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Spika, kutokana na sababu za kihistoria, kijiografia, kimazingira na ukubwa wa eneo la Wilaya ya Tunduru, imezidi kudidimia kimaendeleo. Ninaamini zinahitajika juhudi za makusudi na ikibidi za upendeleo kuisaidia Tunduru iweze kusogea hatimaye kusonga mbele kimaendeleo.

Moja ya njia itakayorahisisha maendeleo kwa Wilaya ya Tunduru ni kuigawa kuwa Wilaya mbili. Wilaya ina Tarafa saba ambazo ni Mlingoti, Nampungu, Matemanga, Nakapanya, Nalasi, Namasakata na Lukumbule.

Mheshimiwa Spika, vikao mbalimbali ngazi ya Wilaya iliwahi kupendekeza mgawanyo kwa kuzingatia jiografia, uchumi na uwiano wa watu uwe kama ifuatavyo:-

(a) Tunduru Kaskazini ijumuishe Tarafa za Mlingoti, Nampungu, Matemanga na Nakapanya.

(b) Tunduru Kusini iwe na Tarafa za Nalasi, Namasakata na Lukumbule.

Mheshimiwa Spika, moja ya mambo ambayo yalikuwa yanawakwaza sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliotangulia katika kuhimiza maendeleo ya Jimbo la Tunduru ni ukubwa wa eneo la Wilaya. Kumbukumbu zinaonyesha, kaka yangu Marehemu Juma Akukweti aliwahi kuiomba na kuishauri Serikali juu ya umuhimu wa kuligawanya Jimbo kuwa ama Wilaya mbili au Majimbo mawili.

Mheshimiwa Spika, kwa mtazamo wa wananchi walio wengi, wazo la kuigawa Wilaya kuwa Wilaya mbili ni muafaka zaidi ya yote kwani itarahisisha kusukuma maendeleo ya Tunduru kwa kasi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuanzishwa Mkoa mpya Kanda ya Kusini, wananchi wa Tunduru walilipokea kwa shangwe kubwa sana wazo la kuanzishwa kwa Mkoa mpya utakaojumuisha Wilaya ya Tunduru, Masasi, Nachingwea na Nanyumbu. Kwa masikitiko makubwa suala hili halijazungumziwa kabisa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Wananchi wa Tunduru na Wilaya zingine nilizozitaja wana hamu kubwa kusikia kauli ya Serikali juu ya suala hili ambalo wamekuwa wakisubiri kwa hamu na kwa muda mrefu sasa.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Ruvuma kupitia vikao vyake halali ulitoa baraka zake na uliridhia kuitoa Wilaya ya Tunduru ijumuishwe na Wilaya zingine kuanzishwa Mkoa mpya kwa maslahi ya wananchi wa maeneo husika. Kuna taarifa ambayo hatujathibitisha kwamba kuna baadhi ya viongozi wa Mkoa wa Mtwara wamekuwa ni kikwazo cha kuanzishwa kwa Mkoa huo kwani hawataki kuziachia Wilaya za Masasi na Nanyumbu ati kwa kuwa ni wazalishaji wakubwa wa zao la korosho.

Mheshimiwa Spika, tutafarijika sana kupata tamko la Serikali juu ya suala hili.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jinsi alivyoweza kutoa tathmini ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika mwaka wa 2006/2007 na kuweka bayana mipango ya mwaka 2007/2008. Naiunga mkono hotuba hii pamoja na kusisitiza yafutayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu nishati, naipongeza Serikali kwa jinsi ilivyotekeleza mpango wa dharura wa kukabiliana na tatizo la umeme lililoikumba nchi yetu kutokana na upungufu wa maji ulioambatana na ukame kiasi cha kupunguza uzalishaji wa umeme wa maji. Mitambo kadhaa itakayotumia gesi asilia imefungwa na inaendelea kufungwa Mjini Dar es Salaam.

Aidha, mtambo mpya wa kutumia dizeli umefungwa Mjini Mwanza. Juhudi hizi zitalimaliza kabisa tatizo la umeme hususan mijini. Hata hivyo naishauri Serikali ielekeze juhudi zake katika kukabiliana na tatizo la umeme vijijini. Bila umeme vijijini nchi yetu haitoweza kupiga hatua za maendeleo ya viwanda vidogo vidogo vijijini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri na usafirishaji, Serikali inajitahidi sana kuwekeza katika sekta hii muhimu kwa uchumi wetu. Bado kuna haja ya kuongeza uwekezaji katika sekta hii hususan kwa kuwekeza katika bandari zetu, reli na barabara zetu zote zinazounganisha nchi yetu na nchi za jirani. Nchi yetu itafaidika sana kwa kuwekeza katika sekta hii, nchi za jirani zinategemea sana bandari zetu, reli na barabara zetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Jeshi la polisi, askari wetu wanafanya kazi nzuri sana, tuwakumbuke kwa kuwapatia nyumba bora zinazokidhi mahitaji na haki za binadamu. Mgawanyo wa maghorofa 30 yatakayotumia fedha kutoka *NSSF* hauzingatii haja ya kuwapatia nyumba nzuri askari wanaoishi nje ya Dar es Salaam. Naomba Ofisi ya Waziri Mkuu iingilie mgawanyo huu ili sehemu kubwa ya askari wetu nchi nzima wafaidike na mradi huu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kukuza mauzo ya nje, mauzo yetu ya nchi za nje ni madogo sana kulingana na kiasi cha bidhaa zinazoagizwa kutoka nje. Hali hii inachangia kwa kiasi kikubwa kushuka kwa thamani ya shilingi yetu ikilinganishwa na fedha zingine za kigeni kama dola, pauni na kadhalika. Tunahitaji mikakati mahsusi ya kukuza mauzo ya bidhaa na huduma zetu nje. Tuanze kwa kutia mkazo katika huduma za usafiri na usafirishaji pamoja na utalii. Aidha, tuongeze uzalishanji wa mazao yetu ya asilia pamoja na ya viwandani. Kwa kufanya hivyo, tutaongeza sana nafasi za ajira kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kasi ya ukuaji wa uchumi wetu, mpaka sasa kasi ya ukuaji wa uchumi wetu (7.0% - 7.9%) kwa miaka mitano ijayo ni ndogo sana ikilinganishwa na kasi ya ongezeko la watu (2.9%).

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameliona tatizo hili na katika hotuba yake amesisitiza haja ya kuiongeza kasi hii mpaka kati ya 8% - 10%. Tutekeleze mikakati itakayotuwezesha kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maji safi na salama, naomba Ofisi ya Waziri Mkuu ifuatilie kwa karibu sana utekelezaji wa mradi wa Benki ya Dunia wa miradi kumi katika kila Wilaya. Mradi huu ni muhimu sana, lakini utekelezaji wake unasuasua sana. Aidha, mradi wa maji safi na maji taka wa mjini Tabora unaofadhiliwa na Serikali za Uswiss na Tanzania nao unasuasua pia. Naomba Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ifuatilie utekelezaji wa mradi huu kwa karibu sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa shule za sekondari, naipongeza Serikali chini ya usimamizi na uratibu wa karibu wa Waziri Mkuu kwa utekelezaji mzuri wa mradi huu nchi nzima. Aidha, napenda nisisitize haja ya kuwa na mipango mizuri ya kufundisha walimu wa kutosha na kama hatuwezi kuwapata walimu wa kutosha toka hapa nchini, si vibaya kama Serikali inaweza kuangalia uwezekano wa kupata walimu toka nchi za nje kama vile *peace corps.* Utaratibu huu ulifanyika miaka ya nyuma mara tu baada ya Uhuru.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ujenzi wa shule za sekondari, vile vile Serikali yetu inatilia mkazo ujenzi wa vyuo vya *VETA* katika Wilaya zote nchini. Huu ni uamuzi mzuri na hasa kama utatekelezwa ka umakini wa hali ya juu. Aidha, tutafanikiwa vizuri katika eneo la elimu ikiwa tutaongeza katika orodha ya vyuo tutakavyojenga hapa nchini iwe ni vile vinavyojulikana kama *Polytechnics* katika kila Mkoa. Vyuo vya aina hii vitakuwa ni chimbuko la stadi *(skills)* mbalimbali katika ngazi za juu zaidi ya zile zipatikanazo katika vyuo vya *VETA.* Kwa hiyo, naishauri Ofisi ya Waziri Mkuu isimamie vyema uanzishaji wa vyuo vya *Polytechnics* hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, leo kama nilivyotangaza siku ya Ijumaa ni kupokea majibu toka upande wa Serikali; nilikuwa nimetangaza muda ukawa mfupi kidogo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Sasa tabu ya Kanuni zetu kwa sasa zinaita Ofisi ya Waziri Mkuu nayo ni kama Wizara ambapo siyo sahihi. Ni jambo ambalo tumelisahihisha katika Marekebisho ya Kanuni. Kwa hiyo, mpangilio utakuwa kama ifuatavyo na ninatumia mamlaka yangu chini ya Kanuni 126 “kurekebisha mambo pale ambapo hakuna utaratibu rasmi.”

Kwa hiyo, tutatumia robo saa kwa Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Luka Siyame, kama mchangiaji lakini akijibu hoja na Mheshimiwa Celina Kombani. Halafu nusu saa kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Masuala ya Bunge na Uratibu. Halafu saa moja kwa Waziri wa TAMISEMI kwa sababu hilo ni eneo ambalo limechangiwa sana. Muda usiozidi saa moja kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambapo tutaenda hadi saa 7.00 au saa saba kasorobo hivi. Kwa hiyo, basi tutaingia kwenye Kamati ya Matumizi mnamo saa 11.00 jioni, nayo tutajaribu tufanye kwa muda wa saa moja, naambiwa vifungu viko vingi ni 83. Lakini tutajaribu tuone tutakavyokwenda. Baada ya hapo, ninatazamia saa 12.00 kamili kumwita Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Kwa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Dr. Luka Siyame, Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. LUKA J. SIYAME):** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami nishiriki katika kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge kuhusu hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa mwaka 2007/2008.

Kabla sijafanya hivyo, naomba nami kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Mbozi hususan wale wa Jimbo la Mbozi Magharibi niungane na wenzangu kutoa pole kwa ndugu na jamaa za wahanga wa ajali za barabarani zilizotokea sehemu mbalimbali hivi karibuni nchini ikiwa ni pamoja na Singida, Monduli na Mbeya.

Pia kwa majonzi makubwa kabisa natoa pole kwa familia ya marehemu Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia aliyetutoka wiki iliyopita. Naomba Mwenyezi Mungu awape moyo wa ustahimilivu wakati wa kipindi hiki kigumu.

Aidha, kwa niaba ya wale wote tuliokuwa wanafunzi wa Kitivo cha Tiba, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pamoja na Wahadhiri wetu ambao wengine tuko nao hapa Bungeni leo, napenda kutoa pole kwa familia ya aliyekuwa Mhadhiri wetu mahiri, Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Akina mama na Uzazi Dr. David Risasi ambaye alifariki siku ile ile aliyofariki Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia. Naomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina!

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea zaidi naomba kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kumpongeza yeye binafsi, Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu, Mwenyekiti Mtendaji, Kamishna wa Tume, Wakurugenzi, Watendaji na wafanyakazi wote wa Ofisi yake na Taasisi zake kwa hotuba nzuri iliyotayarishwa kwa umahiri mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa ruhusa yako naomba nijibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kwa mtiririko ufuatao. Ninazo hoja tatu, kuhusu kukabiliana na maafa na hoja saba kuhusu Udhibiti wa UKIMWI.

Kuhusu hoja za kukabiliana na Maafa: Mheshimiwa George Malima Lubeleje Mbunge wa Mpwapwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, na Mheshimiwa Masoud Abdallah Salum, Mbunge wa Mtambile, waliitaka Serikali ifanye maandalizi madhubuti ya kupambana na Maafa na Majanga.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali imeendelea kutekeleza sera, sheria na mwongozo wa kitaifa juu ya kukabiliana na Maafa na kwa sasa inaifanyia marekebisho sheria iliyopo ya mwaka 1990 ili iweze kuendana na sera iliyopo sasa kuhusu suala hili.

Serikali imefanya tathmini na kuainisha kitaalamu majanga mbalimbali yaliyotokea nchini kuanzia mwaka 1872.

Ili kufanikisha Sera ya Taifa kuhusu kukabiliana na Maafa, mbali na ngazi ya Taifa, Serikali imeunda Kamati za Maafa za Mkoa na Wilaya na kwa kuanzia imetoa mafunzo kwa mikoa minane.

Aidha, Serikali imeanzisha programu endelevu kuhusu namna ya kukabiliana na maafa kitaifa.

Serikali pia inaendelea kushiriki na kutekeleza mipango mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa inayohusu kukabiliana na maafa. Mifano michache ikiwa ni pamoja na kuandaa na kushiriki katika operesheni ya kuigiza maafa ya mafuriko katika Mikoa ya Lindi, na Mtwara iliyopewa jina "*Operation Blue* Ruvuma" iliyofanyika mwaka jana katika Mkoa hiyo miwili ikihusisha majeshi ya anga ya nchi zote za *SADC.*

Mheshimiwa Spika, vilevile kushiriki kwenye mikutano mbalimbali kama Mkutano wa Kundi la Kukabiliana na Majanga lijulikanalo kama *Golden Spear* uliofanyika nchini Misri mwishoni mwa mwaka jana ukihusisha nchi za Pembe ya Afrika, Misri, Afrika ya Mashariki na Kati, na pia Mkutano wa Kwanza wa Dunia kuhusu namna ya kupunguza Maafa na athari zake uliopewa jina la *Global Platform for Disaster Risk Reduction* uliofanyika Geneva Uswisi mwezi uliopita kwa hisani ya Shirika la Umoja wa Mataifa lijulikanalo kama *International Strategy for Disaster Reduction*.

Mheshimiwa Ali Said Salum Mbunge wa Ziwani alitoa hoja kuwa kuna upendeleo katika utoaji wa misaada ya maafa, hivyo akaitaka Serikalli irekebishe hali hii.

Mheshimiwa Shoka Khamis Juma Mbunge wa Micheweni alitoa hoja kwamba Serikali itoe huduma kwa uwiano ulio sawa kwa Tanzania Bara na Visiwani pindi maafa yanapotokea.

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu hoja hizo mbili kwa pamoja kama ifuatavyo:- Mosi, napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa Serikali inashughulikia maafa bila kujali eneo yalipotokea wala itikadi za waathirika wa maafa hayo. Hata hivyo, utaratibu wa kushughulikia maafa kwa upande wa Tanzania huratibiwa na Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu; na kwa Upande wa Zanzibar huratibiwa na Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Kiongozi. Kwa hakika ofisi hizi hufanya kazi kwa ushirikiano wa karibu sana.

Pili, Mheshimiwa Spika, misaada itolewayo pindi maafa yatokeapo, hutolewa kulingana na tathmini zinazofanywa na wataalamu kwa kushirikiana na Mikoa na Wilaya husika na kwa kulingana na uwezo uliopo. Hivyo basi, tunawaomba Waheshimiwa Wabunge washirikiane na viongozi wa Serikali wa maeneo yao na kwa kutumia Kamati husika za maafa kutoa tathmini sahihi za maafa mara yanapotokea ili Serikali iweze kuyashughulikia ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, naamini kuwa huu ni wakati muafaka wa kutoa pongezi za dhati kwa viongozi wa Mikoa ya Tabora, Shinyanga na Mwanza kwa jinsi walivyojipanga vizuri kushughulikia wananchi wao wakati wa mafuriko kutokana na mvua za msimu uliopita.

Pia napenda kuwapongeza viongozi wa Mikoa ya Dodoma, Arusha, Manyara na Morogoro kwa kazi kubwa iliyofanywa wakati wa mlipuko wa ungojwa wa Homa ya Bonde la Ufa.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na hoja kuhusu Udhibiti wa UKIMWI, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na Mheshimiwa George Simbachawene Mbunge wa Kibakwe, waliitaka Serikali iweke sheria kuwabana na kuwaadhibu vikali wale wote wanaobainika kusambaza virusi vya UKIMWI kwa makusudi.
Hivi sasa Serikali inaandaa Muswada wa Sheria ambao utaletwa Bungeni kwa ajili ya uamuzi wa Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mbunge wa Hai, Mheshimiwa Meryce Emmanuel, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salum, Mbunge wa Mtambwe na Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mbunge wa Njombe Magharibi, waliitaka Serikali ifuatilie na kudhibiti matumizi ya fedha za udhibiti wa UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina utaratibu wa kufuatilia matumizi ya fedha za UKIMWI zinazopitishwa katika mikondo miwili. Moja, zinazopitia kwa wakala wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI. Mikoani zinadhibitiwa na Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Pili, zinazokwenda kwenye Halmashauri zinafuata masharti ya matumizi ya fedha za Serikali na kukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Hata hivyo, kuna fedha zinazokwenda moja kwa moja kwenye Asasi na Mashirika yasiyo ya Kiserikali (*NGOs*) kutoka kwa wahisani kwa ushauri wa Halmashauri husika na Tume ya Kudhibiti UKIMWI. Tunawaomba Waheshimiwa Wabunge, washirikiane na viongozi katika maeneo yao kusimamia matumizi ya fedha zinazopita katika mikondo hiyo na endapo kuna taarifa kuwa baadhi ya asasi hizi zinatumia fedha hizo visivyo, basi taarifa hizo ziwasilishwe Ofisi ya Waziri Mkuu haraka kwa hatua zaidi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mbunge wa Mbarali, alitaka kufahamu ni vigezo gani vinatumika kutoa fedha za UKIMWI kwa Wizara, Taasisi za Serikali, Idara zinazojitegemea na Halmashauri za Wilaya na Miji. Serikali hutoa miongozo ya utengenezaji wa mpango wa kupambana na UKIMWI kwa Wizara, Idara na Mamlaka za Serikali za Mitaa kila mwaka. Vigezo vinavyotumika kwa Wizara na Idara za Serikali hutokana na uchambuzi ambao umefanyika kuonyesha ukubwa wa tatizo kwenye Wizara au Idara. Baada ya hapo Wizara hutengeneza Mpango Mkakati wa miaka mitano na Mpango wa kila mwaka wa kudhibiti UKIMWI.

Mamlaka za Serikali za Mitaa hupewa fedha kwa kuzingatia kiwango cha maambukizi kimkoa, idadi ya watu na kiwango cha umaskini.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Benilith Mahenge, Mbunge wa Makete, aliitaka Serikali iweke utaratibu ili Taasisi na Mashirika yasiyo ya Kiserikali yanayotoa huduma za UKIMWI yawe yanatoa taarifa kwa Halmashauri husika. Huu ndio utaratibu ambao Serikali imeelekeza. Taasisi na Mashirika binafsi yana uwakilishi kwenye Kamati za UKIMWI za Wilaya, Kata na Vijiji. Hivyo basi taarifa zao zinapaswa kutolewa kwenye ngazi hizo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Phares Kashemeza Kabuye, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, alitaka Serikali iweke utaratibu wa kuwapa wagonjwa wa UKIMWI vyakula vyenye virutubisho. Hivi sasa Tanzania ina watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI wapatao milioni 2. Serikali hivi sasa imebeba mzigo wa kutoa dawa za kurefusha maisha kwa wagonjwa wa UKIMWI wapatao laki mbili, hivyo basi, kutaka kuitwisha mzigo mwingine wa kutoa lishe bora kwa wanaoishi na Virusi vya UKIMWI itakuwa sawa na kumkamua ng'ombe mpaka tone la mwisho la damu. Jamii ya Watanzania, hususan familia za waathirika ina jukumu la kuhakikisha wanaoishi na Virusi vya UKIMWI wanapata lishe bora. Serikali inaendelea kuuelimisha umma juu ya umuhimu wa lishe bora ikiwa ni pamoja na watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI. Mheshimiwa Ali Said Salim, Mbunge wa Ziwani na Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mbunge wa Chonga, waliitaka Serikali itenge fedha za kutosha kutoka kwenye bajeti ya ndani badala ya kutegemea wahisani kupambana na UKIMWI na dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, kiasi kikubwa cha fedha kinachotumika kudhibiti dawa za kulevya hapa nchini ni fedha za ndani. Aidha, kwa kuelewa umuhimu wa kupambana na UKIMWI, Serikali imekuwa ikiongeza kiasi cha fedha katika bajeti yake kila mwaka. Hata hivyo, kutokana na uwezo mdogo wa Serikali kifedha, mchango wa wahisani utaendelea kuhitajika ili kuziba pengo.

Mwisho, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka; aliwataka Wabunge wote wapime UKIMWI ili kuonyesha mfano.Suala la kupima UKIMWI ni la hiari. Hata hivyo, Waheshimiwa Wabunge, viongozi mbalimbali na wananchi wote wanahamasishwa kujitokeza kupima UKIMWI ili kuitikia wito uliotolewa na Mheshimiwa Rais wetu wa kupima UKIMWI kuanzia tarehe 14 Julai, 2007. Hatua hii itawawezesha wananchi wote kujua afya zao na kuchukua hatua zinazostahili kufuatia matokeo ya upimaji huo. Napenda kuwahakikishia wananchi kuwa Serikali imejiandaa kikamilifu na vifaa kwa ajili ya shughuli hiyo vipo vya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru tena na naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutoa shukrani

zangu za dhati kwa ndugu, jamaa na marafiki na majirani walionifariji kwa njia moja au nyingine wakati wa msiba wa marehemu mama yangu uliotokea tarehe 1 Mei, 2007. Shukrani za pekee zifike kwako Mheshimiwa Spika, ambaye ulifika katika sehemu ya tukio pamoja na Waheshimiwa Wabunge watatu akiwemo Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Janeth Massaburi na Mheshimiwa Vita Kawawa. Shukrani za pekee ziende kwa Mama Regina Lowassa ambaye alikuwa karibu nami wakati wowote wa msiba huo. Nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge, hasa kwa kipekee nimshukuru Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda kwa shukrani za pekee ambapo alijaribu kuokoa maisha ya marehemu mama yangu, lakini haikuwezekana. Bila kuwasahau Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi, Mameya na wananchi wa Wilaya ya Ulanga wakiongozwa na Dr. Juma Ngasongwa. Nawashukuru na Mungu awabariki. Nirudi kwenye hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli tunaziheshimu hoja zao zote na kuzithamini, tunajua wametoa mchango mkubwa ili kuleta maendeleo kwa wananchi, tunazipokea na tunaahidi kwamba tutazifanyia kazi. Hoja ya kwanza ni kujaza nafasi wazi kwa Wakuu wa Idara katika Halmashauri kama vile Waweka Hazina. Serikali inatambua tatizo la uhaba wa watumishi katika Idara mbalimbali za Utumishi wa Umma. Mpaka mwaka 2005 mwishoni idadi ya Wakuu wa Idara wa Halmashauri walikuwa 1,146. Nafasi wazi kwa wakati huo zilikuwa 306 na hadi sasa nafasi 83 zimejazwa, nafasi wazi mpaka sasa hivi ni 223 zikiwemo za Waweka Hazina wanne tu. Serikali imeamua kulegeza masharti badala ya kutangaza nafasi hizo; na sasa kwa wale watumishi ambao wana sifa katika Idara mbalimbali wanathibitishwa badala ya Kukaimu. Aidha, Halmashauri zote zimeelekezwa kwa wale ambao wana sifa wathibitishwe mara moja na zoezi hili linaendelea.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, ni watumishi wanaokaa muda mrefu katika kituo kimoja cha kazi. Serikali imelitambulia hilo na kwa kuanzia ofisi yangu imefanya sensa kwa Halmashauri 66 ambapo watumishi 2,966 wamekaa kwa muda mrefu katika vituo hivyo. Uhamisho huo umeanza kufanyika ukiwahusisha Maafisa Kilimo, Maafisa Ushirika, Wahasibu, Watumishi wa Ardhi pamoja na Ujenzi. Katika kutekeleza zoezi hili kuna gharama kubwa Waheshimiwa Wabunge. Kwa mfano, kwa Wilaya ya Mwanga tu watumishi 68 wanatakiwa kuhamishwa. Kwa kuwa zoezi hili ni la gharama tunafanya pole pole kulingana na uwezo wa fedha, lakini linatekelezwa kwa ufanisi kabisa. Natoa agizo kwa Halmashauri za Wilaya ambazo zina watumishi wale ambao ni wabovu, watumishi ambao hawana nidhamu wasingoje mpaka wahamishwe, ni jukumu la Halmashauri husika kuwachukulia sheria za kinidhamu badala ya kuomba wahamishiwe katika Wilaya nyingine. Kwa sababu unahamisha mzigo kutoka Halmashauri moja na kupeleka Halmashauri nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la tatu, ni Maafisa Kilimo, Afya na Ushirika kupelekwa katika Kata ambako fedha za maendeleo zipo. Serikali inatambua umuhimu wa kupeleka watumishi wa kutosha katika mamlaka za Serikali za Mitaa hapa nchini ili kuleta Maendeleo.

Kwa mwaka 2007/2008 wataalamu wa kilimo 2500 wataajiriwa na wataalamu wa afya 3,000 wataajiriwa na Serikali na kupangwa katika Halmashauri mbalimbali. Aidha,

Serikali inatambua tatizo la upungufu wa maafisa ushirika katika Halmashauri. Hii ni changamoto kwetu na tunalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni Serikali itoe elimu juu ya faida, maana na umuhimu wa mikopo inayotolewa. Serikali kwa kupitia Benki Kuu imetoa mafunzo kwa watumishi 9 kwa kila Halmashauri wakiwemo Maafisa Mipango, Afisa Ushirika, Afisa Maendeleo ya Jamii, Afisa Biashara ili nao watoe mafunzo katika ngazi ya Vijiji, Kata na Halmashauri kwa ujumla kuhusu faida ya mikopo inayotolewa na Serikali. Pia Serikali inatumia mitambo, vyombo vya habari na vipeperushi kutoa elimu kuhusu umuhimu wa mikopo hiyo. Faida ya mikopo hii yenye riba nafuu ni kuongeza kipato kwa wananchi ili kupunguza umaskini miongoni mwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni la barabara ya Miangarua hadi Kibeta kutengewa fedha katika mwaka huu wa fedha 2007/2008. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba katika mwaka wa fedha 2007/2008 barabara hii imetengewa jumla ya shilingi milioni 290 chini ya programmu ya Mfuko wa Barabara za Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni fidia kwa upotevu na vifo vya upotevu wa mifugo wakati wa kuhamisha mifugo toka Ihefu. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Mheshimiwa Rais aliunda Tume ya Kuchunguza utekelezaji wa zoezi la kuwahamisha wafugaji kutoka bonde la Ihefu. Tume ilitembelea maeneo hayo wafugaji wamekuwa wakihamishwa na maeneo ambayo walikuwa wamehamia. Taarifa ya Tume imeshawasilishwa na Mheshimiwa Rais tarehe 6 Juni, 2007 matokeo yatatangazwa baada ya Mheshimiwa Rais kupitia na kufanya naamuzi.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni Serikali irejeshe huduma za majosho na kuboresha malambo kwa ajili ya mifugo. Ili kumpunguzia mfugaji gharama za uzalishaji Serikali imeandaa utaratibu wa kutoa madawa ya mifugo kwa wafugaji kwa kutumia njia ya ruzuku kwa kushirikisha sekta binafsi. Katika utaratibu huu upatikanaji wa madawa ya kuogesha mifugo utakuwa wa gharama nafuu. Taratibu za kuyapata Makampuni yatakayoingia Mkataba na Serikali zimeanza. Aidha, Halmashauri kupitia Mpango wa Maendeleo wa Kilimo wa Wilaya (*DADPs*) zimeelekezwa kuonyesha shughuli za ujenzi wa majosho na malambo zilizoibuliwa na wananchi katika mipango yao kupata ruzuku ya uwezeshaji.

Mheshimiwa Spika, swali lingine ni kuhusu Wilaya ya Mbinga kutokuwa na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inayo taarifa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Mbinga anayo Ofisi ndani ya majengo ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga. Ofisi yangu itafuatilia kufahamu upungufu uliopo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni upatikanaji wa magari ya kubeba wagonjwa *(ambulance).* Serikali inao mpango wa kupeleka magari katika vituo vyote vya afya nchini. Kwa mwaka 2005/2006 magari 30 yalinunuliwa na yamegawanywa; kwa mwaka 2006/2007 magari 33 yamenunuliwa na yamegawanywa katika Halmashauri mbalimbali. Mwaka huu Serikali haikutenga fedha kutokana na ufinyu wa bajeti, lakini hata hivyo Serikali inalitambua tatizo hili na inafanya kila njia ili kuweza kununua magari hayo.

Lakini niwashauri na Wakurugenzi katika Halmashauri mbalimbali nao watafute vyanzo mbalimbali ili kukidhi haja ya magari hayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Shule za sekondari za kutwa ambazo ziko mbali na makazi zijengewe hosteli, Serikali inakubaliana na hoja ya Waheshimiwa Wabunge. Kwa kuzingatia hilo imetoa michoro kwa ajili ya ujenzi wa majengo mbalimbali yakiwemo majengo ya hosteli. Ufafanuzi zaidi utatolewa na Mheshimiwa Waziri wa Elimu atakapotoa hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni mchango wa Serikali katika ujenzi wa Shule za Msingi uongezwe kufikia shilingi milioni 6 kwa darasa na shilingi milioni 8 kwa nyumba ya mwalimu. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa kuzingatia hali halisi ya gharama za vifaa vya ujenzi na thamani ya fedha ya Tanzania, Serikali imebadili viwango hivyo katika mwaka huu wa fedha na kutenga shilingi milioni 5.5 kwa darasa na shilingi milioni 7.5 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya mwalimu.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni miji midogo kupewa hadhi ya Halmashauri ya Miji. Mamlaka ya Miji Midogo kuwa Halmashauri ya Miji inatakiwa iwe na vigezo vifuatavyo: Uwezo wa kifedha yaani vyanzo vyao, idadi ya watu wasiozidi 30,000, kuwekwa kwa huduma za afya, hospitali na kadhalika. Kwa Halmashauri ya Mji Mdogo wa Muheza imeanza rasmi tarehe 1 Julai, 2007. Ni vyema Mji Mdogo huo ukafanya kazi kwanza ili uzoefu utakaopatikana utumike katika kuomba kuupandisha hadhi kuwa Halmashauri ya Mji.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni ukarabati wa vituo vya afya na zahanati ya Wilayani Kwimba. Tunasema kwamba mwaka 2006/2007 Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba ilipelekewa shilingi milioni 324 kwa ajili ya shughuli za ukarabati wa zahanati na vituo vya afya. Jukumu la kituo cha afya gani kikarabatiwe ni la Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara na madaraja katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea kwa mwaka 2007/2008. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa mwaka 2007/2008 Halmashauri ya Wilaya ya Songea imetengewa jumla ya shilingi milioni 95 kwa ajili ya madaraja na shilingi milioni 348 kwa ajili ya ujenzi wa barabara. Kama nilivyosema hapo juu barabara zipi zitengenezwe ni suala la Halmashauri husika kulingana na vipaumbele vya Wilaya yao.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni Serikali iwarejeshe Mameneja wa Vijiji. Ni kweli Serikali iliwahi kuajiri Mameneja wa Vijiji ambao walikuwa wasomi kielimu. Utaratibu huo ulishindikana kwa sababu mbalimbali. Ili kuimarisha shughuli za vijiji Maafisa Watendaji wa Vijiji lazima wawe na uwezo wa kutosha wa kielimu. Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma inaelekeza kwamba Maafisa Watendaji wa Vijiji huwa na sifa ya elimu isiyopungua Kidato cha Nne na mafunzo ya kitaaluma. Kazi zilizokuwa zinafanywa na Mameneja wa Vijiji ndizo hizo hizo sasa hivi zinafanywa na Watendaji wa Vijiji na Mitaa. Watendaji hao wanafanya kazi nzuri kwa baadhi ya maeneo. Serikali haina mpango wa kuwarejesha Mameneja wa Vijiji.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni mikopo kwa ajili ya wanawake na vijana isitolewe kisiasa au kiitikadi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali ilianzisha mikopo kwa ajili ya wanawake na vijana ili kuinua kipato chao. Utaratibu uliopo haujaonesha kuwa unayo matatizo makubwa. Utaratibu wa kutoa mikopo hiyo unahusisha Kamati zilizoundwa na Halmashauri zenyewe, Ofisi yangu haijapokea malalamiko yoyote ya kutolewa mikopo kiitikadi. Serikali inasisitiza utaratibu uliopo ufuatwe bila ya upendeleo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni ujenzi wa barabara za lami katika Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga. Tunasema kwamba kwa mwaka huu 2006/2007 Serikali imetenga shilingi milioni 430 kwa ajili ya ujenzi wa barabara za lami katika Manispaa ya Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni taa za barabarani za Jiji la Dar es Salaam kwamba nyingi ni za zamani na nyingine hazipo kabisa. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba upo mpango kabambe wa kufufua na kuweka taa mpya katika barabara zilizoko Jiji la Dar es Salaam. Mpango huu unahusisha Halmashauri nne na *TANROAD*. Halmashauri ya Kinondoni imekwishaingia mkataba na mkandarasi wa kuweka taa katika barabara zake 16. Taa zilizopo kwenye barabara ya Morogoro na Ali Hassan Mwinyi zimefanyiwa matengenezo. Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi kwamba kuanzia mwezi uliopita kuna mafundi ambao wanatengeneza taa hizo katika Jiji letu la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni Serikali kuweka utaratibu wa kuwa na Naibu Mkurugenzi. Tunasema kwamba suala hili tunalipokea na bado linafanyiwa kazi na Serikali. Suala lingine ni Wilaya ya Rorya ipewe magari matatu ya wagonjwa. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kutokana na ufinyu wa bajeti magari hayo hayapo kwa sasa hivi. Mheshimiwa angevuta subira hatuwezi kumwahidi kutoa magari hayo kwa sababu kwa mwaka huu wa 2007/2008 hazikutengwa fedha zote kwa ajili ya ununuzi wa magari, tunazihimiza Halmashauri ziweze kupanga katika bajeti zao. Suala lingine ni Madiwani na Watendaji wa Vijiji wakopeshwe vyombo vya usafiri.

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Halmashauri ziwajibike kuwawezesha Watendaji na Madiwani ili watekeleze majukumu yao. Kwa hiyo, ni jukumu la Halmashauri kwa kushirikiana na asasi mbalimbali kutoa vyombo vya usafiri. Kwa mfano, ningependa kuwapongeza Halmashauri ya Mbinga na Chunya ambao wanatoa huduma hizo kwa watendaji wao.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu madai ya uuzwaji wa msitu wa Soledo Wilayani Kiteto. Taarifa hii imepokelewa na uchunguzi utafanywa kuhusu tuhuma hizo.

Suala lingine ni mafunzo ya mgambo yaimarishwe katika vijiji vya mpakani hasa Wilayani Ngorongoro. Serikali imepokea ushauri wa Mbunge na kwa mwaka 2007/2008 Mkoa wa Arusha umepangiwa shilingi milioni 12 kwa ajili ya kuimarisha Ofisi ya Mshauri wa Mgambo wa Mkoa na shilingi milioni 2.4 kwa kila Wilaya ili kusaidia kuendesha shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. BATILDA S. BURIAN):** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kutujalia sisi sote kuwa salama siku hii ya leo. Aidha, napenda kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hoja ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu iliyopo mbele.

Mheshimiwa Spika, naomba kutamka wazi, tena mapema kabisa, kuwa naunga mkono hoja hii kwa kwa asilimia 100. Naunga mkono hoja hii kwa namna ilivyoweza kuzingatia kwa uzito wa pekee utekelezaji wa kazi za Serikali kwa mwaka uliopita na kutoa mwelekeo wake kwa mwaka ujao wa 2007/08. Aidha, naiunga mkono hoja kwa kuonyesha malengo na vipaumbele vinavyolenga kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 kupitia Makadirio ya Matumizi ya fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2007/08. Lakini mwisho, naunga mkono hoja hii kwani nina mchango wangu mdogo katika kumsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii pia kwa masikitiko makubwa kutoa pole kwa familia na ndugu wa Marehemu waliopoteza maisha hivi karibuni kufuatia ajali mbalimbali za magari hususan wale wa Singida, Arusha na wale viongozi wa Ushirika wa Nyanza (akiwemo Mheshimiwa Stephen Kazi aliyekuwa Mbunge wa Mwanza Mjini). Mwenyezi Mungu awape moyo wa subira Ndugu na Jamaa wa Marehemu na aziweke roho zao wote mahala pema peponi. *Amin*!

Mheshimiwa Spika, kwa namna pekee kabisa natoa pole kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwako wewe Mheshimiwa Spika, Wabunge wote, Wazazi, Ndugu na Jamaa wote, kwa kumpoteza Mbunge mwenzetu, Marehemu Amina Chifupa Mpakanjia. Naomba Mwenyezi Mungu ampokee mwenzetu aliyetangulia na kumlaza mahali pema peponi. *Amin*!

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa pole zangu, sasa naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniteua kushika wadhifa huu wa kuwa Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu, kushughulikia masuala ya Bunge na Uratibu. Aidha, nawashukuru Mhe. Dkt. Ally Mohamed Shein, Makamu wa Rais na Mhe. Edward Lowassa (Mb), Waziri Mkuu, kwa imani kubwa waliyonayo kwangu mimi. Napenda kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa ushirikiano mnaonipatia katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu yangu. Vilevile napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Naibu Mawaziri, KM, OWM, TAMISEMI, Wakuu wa Taasisi zetu zote, Wakurugenzi na watumishi wote katika ngazi zote kwa ushirikiano wao ambao ndio umefanikisha kazi hii ambayo tunahitimisha leo.

Aidha, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa uongozi wake na ushauri anaonipatia kuniwezesha kutimiza malengo na majukumu yanayoambatana na kazi zangu. Kadhalika, nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa busara zako na mwongozo ambao daima umekuwa ukinipatia.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda sasa kuchukua nafasi hii kuchangia baadhi ya hoja zilizojitokeza wakati wa kujadili hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa 2007/08. Kwanza, nitachangia kwa kifupi sana kuhusu hoja chache zinazotokana na majukumu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kama mratibu wa shughuli zote za Serikali na baadaye nitachangia hoja mbalimbali zinazotokana na shughuli zinazoratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu mwenyewe. Kwanza kabisa hatuna budi tukakumbuka kwamba hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imetoa maelezo kwa muhtasari tu kuhusu mipango ya sekta mbalimbali. Waswahili wanaweza kusema hiyo ilikuwa bashrafu, miziki yenyewe itatoka katika sekta zenyewe husika wakati wa kuwasilisha bajeti zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzungumzia kwa uchache, suala la huduma za afya ni miongoni mwa maeneo yaliyochangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi. Masuala yaliyoguswa, tena kwa uzito wa pekee, yanahusu ubora wa huduma zenyewe, upungufu wa watumishi, upungufu wa vifaa na vitendea kazi, idadi ya vifo vya watoto na akina mama wajawazito na masuala yanayohusiana na UKIMWI ambayo Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Luka Siyame ameyafafanua kwa ufasaha mkubwa.

Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kuwa Serikali kupitia bajeti hii inakusudia kuboresha huduma za afya ili zipatikane kwa urahisi na kuwafikia wananchi wengi zaidi hususan walioko vijijini. Aidha, Serikali tayari imekwishapitisha Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Afya utakaotekelezwa kwa kipindi cha miaka 10 kuanzia mwaka huu, kwa awamu mbili za miaka 5. Kwa mwaka huu utahusisha utoaji wa mafunzo zaidi kwa wataalamu ili kuongeza idadi ya kutosheleza mahitaji kwenye zahanati na Vituo vya Afya vilivyopo nchini. Serikali itaongeza vifaa na ajira ya wataalamu wakiwemo waliostaafu ambao wana nguvu na uwezo wa kuwatumikia wananchi ikiwa ni sehemu ya mkakati wa kutekeleza Malengo ya Maendeleo ya Milenia ya kupunguza vifo vya watoto wa umri hadi miaka 5 na kupunguza vifo vya akina mama waja wazito.

Waheshimiwa Wabunge wengi walizungumzia suala hili ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Dr. Mahenge, Mheshimiwa Zungu na wengine wengi ambao Mheshimiwa Waziri Mkuu atawatambua wakati wa majumuisho yake. Aidha, niseme tu katika kipindi hiki Serikali iko katika hatua za kurekebisha Sera ya Afya ya mwaka 1990 kuwezesha kukabili changamoto mbalimbali zilizopo hivi sasa na za baadaye ili kuhakikisha huduma zinatolewa kwa ufanisi na zinalenga makundi maalumu, ikiwa ni pamoja na kuimarisha huduma vijijini. Sekta ya Afya ni pana sana na inagusa maeneo mengi, hivyo maelekezo ya kina yatakayogusa nyanja mbalimbali yatatolewa na Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii wakati atakapowasilisha hoja ya bajeti yake kwa mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi walihoji kama kweli Serikali ina mpango wa mkakati wa muda mrefu kwa sekta hii. Baadhi ya Wabunge ambao walizungumzia hili ni pamoja na Mheshimiwa Degera, Mheshimiwa Dr. Sigonda, Mheshimiwa Chilolo, Mheshimiwa Rizik, Mheshimiwa Prof. Mtulia, Mheshimiwa Joyce

Masunga, Mheshimiwa Suzan Lyimo na Mheshimiwa Mhagama. Sote tunafahamu kuwa Sekta ya Elimu ni muhimu sana kwa maendeleo ya jamii zetu na Taifa kwa ujumla na kwamba ndiyo nyenzo ya kuondoa umaskini na kuleta maendeleo kwa haraka zaidi. Serikali kwa kutambua hilo, inaendelea kuhakikisha Sekta ya Elimu inaimarishwa na kuboreshwa. Aidha, kutokana na umuhimu wake, Serikali imeongeza rasilimali zaidi na kuifanya kuwa na kipaumble cha kwanza katika bajeti ya mwaka huu kwa kupatiwa kiwango cha asilimia 18.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa nafasi yake kama mratibu inakamilisha Ripoti ya Mpango wa kimkakati wa miaka 10 kwa Sekta ya Elimu ambayo inaonyesha wazi utekelezaji wa sekta hii kuanzia Elimu ya Awali hadi Chuo Kikuu. Hivyo basi maelezo ya kina yatatolewa na Mawaziri wanaoshughulikia sekta hii ambao ni pamoja na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi lakini pia Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, vile vile Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia suala la miundombinu na hasa barabara. Ni kweli kuwa barabara nyingi zimeharibika kutokana na mvua nyingi zilizoendelea kunyesha kwa kipindi kirefu kuliko ilivyo kawaida na hivyo kusababisha uharibifu mkubwa. Serikali inaelewa umuhimu wa miundombinu ya barabara na reli katika kuinua uchumi wetu na pia katika kuboresha huduma za usafirishaji na uchukuzi. Hii ndiyo imeifanya Serikali kuiwekea sekta ya miundombinu kipaumbele cha pili katika bajeti ya mwaka huu.

Mikakati ya Serikali inalenga kuhakikisha kuwa barabara zilizoanza zinakamilishwa pamoja na kuendelea kujenga nyingine. Aidha, Serikali itahakikisha kuwa usafiri wa reli uliopo unaboreshwa na ujenzi wa reli mpya kwa kanda maalumu (*strategic zones*) za kibiashara na kiuchumi kama vile reli ya Tanga – Arusha inaunganishwa na Musoma na kuweza kutumia fursa za biashara zilizoko kule. Lakini vile vile Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba kunakuwa na mipango madhubuti wa kuunganisha miundombinu ya reli katika maeneo ya Mtwara ili kuweza kutoa fursa kwa uvunaji wa madini katika maeneo ya Mchuchuma. Serikali itaendelea na mazungumzo hayo ambayo yanawashirikisha marafiki zetu mbalimbali wa Maendeleo (*Development Partners*) ili waweze kuchangia katika kufanikisha mipango hii. Ufafanuzi zaidi kuhusu sekta ya miundombinu kwa ujumla wake utatolewa na Waziri anayehusika wakati atakapowasilisha hotuba ya bajeti yake katika Mkutano huu hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, eneo jingine ambalo Waheshimiwa Wabunge wengi wamelichangia linahusu sekta ya kilimo. Sekta hii ni pana sana kwani kwa maana ya sekta inajumuisha pia masuala ya ufugaji. Waheshimiwa Wabunge wameizungumzia sekta hii wakiitaka Serikali kuiboresha kwa kuwa na mikakati mizuri na endelevu inayohusu upanuzi wa kilimo cha umwagiliaji, usambazaji mzuri na kwa wakati, pembejeo ikiwemo mbolea, kilimo cha kisasa na cha kibiashara, n.k.

Mheshimiwa Spika, napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imedhamiria kuleta mapinduzi katika sekta ya kilimo kwa kuweka mikakati itakayowawezesha wakulima wetu kushiriki na kunufaika kutokana na pato na rasilimali

nyingine wanazowekeza huko. Mkakati mmojawapo ni ule uliowekwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu ambao ameitisha mkutano maalumu utakaofanyika kesho tukijaliwa ambapo Wakuu wa Mikoa pamoja na Mawaziri wote katika sekta ya kilimo, maji na miundombinu na nishati ili kuhakikisha kwamba masuala ya kilimo yanaendelea kupewa kipaumbele cha umuhimu wa kipekee. Chini ya mkakati huu, utaratibu maalumu umewekwa ambapo Wakuu wa Mikoa wamejipanga vizuri kuhakikisha kuwa kilimo kinakuwa na tija kwa wananchi wengi zaidi ikiwa ni pamoja na kuweka mapendekezo ya kurahisisha upatikanaji wa pembejeo.

Naomba nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuanzisha mkakati huu ambao nina matumaini kama ilivyokuwa kwa Sekta ya Elimu basi utaleta matunda yaliyokusudiwa katika muda mfupi ujao. Mikakati zaidi ya Serikali kuhusu uendelezaji na upanuzi wa kilimo cha umwagiliaji ni kuhakikisha kwamba pembejeo inayojumuisha mbegu bora, upatikanaji wa zana bora za kilimo, mbolea, madawa ya kuua wadudu waharibifu wa mazao, huduma za ugani, n.k. itaelezewa kwa kina na Waziri mwenye dhamana kwenye hoja ya bajeti yake itakayowasilishwa hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, suala jingine ambalo limezungumzwa kwa uzito wa pekee na Waheshimiwa Wabunge linahusu mikopo ya wajasiriamali. Wengi wa waliolizungumzia, wameonyesha kukerwa sana na utekelezaji ulivyokuwa na hasa kwa upande wa Taasisi za fedha ambazo zimepewa jukumu la kukopesha wananchi waliohitaji mikopo zimeendesha shughuli zao kwa urasimu na kwa kasi ndogo kuliko ilivyotegemewa.

Mheshimiwa Spika, kwa hili, mimi binafsi napenda kwanza kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa namna alivyoweza kuamua kutoa fursa hii ya mikopo ya masharti nafuu inayodhaminiwa na Serikali kwa wananchi wake. Aidha, naomba tumpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuingilia kati na kutatua matatizo mbalimbali yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji huu wa mikopo kwa kuwaita watekelezaji wakuu wa Taasisi zile za fedha. Matatizo yaliyojitokeza yamekuwa changamoto kwa Serikali na hivyo yatasaidia sana kuboresha utekelezaji wa mpango huu katika miaka inayokuja.

Serikali itaendelea kwa kushirikisha taasisi hizo za fedha ili kuboresha huduma hiyo. Aidha, katika awamu ya pili ya utoaji wa mikopo ambapo zitaelekezwa kwenye taasisi ndogo ndogo kama vile *SIDO*, Benki za Wananchi, *SCULT* n.k. zitalenga kuchukua uzoefu uliopatikana ili kuboresha utoaji mikopo hii ya wajasiriamali ili kufikia wananchi wengi zaidi hasa vijiji kwa kasi inayokubalika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda sasa kuchangia katika baadhi ya hoja zinazotokana na shughuli zinazoratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wametaka kuwepo kwa utaratibu wa kupata vitambulisho vya Kitaifa ili kuhifadhi vizuri kumbukumbu kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Aidha, wapo baadhi ya Wabunge walioitaka Serikali izingatie na kuhakikisha kuwa kila anayepata sifa ya kuwa mpiga kura anaandikishwa na anayepoteza sifa anafutwa. Hoja hizi zimechangiwa na Mhe. George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile na Mhe. Dkt. Wilbrod Peter Slaa, Mbunge wa Karatu na Naibu Msemaji wa Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Serikali tayari imeanza mchakato wa kuandaa vitambulisho vya uraia ambavyo hatimaye vikishatolewa vitatumika pia katika kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, halikadhalika uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura utaanza mwaka huu wa fedha.

Lengo kuu ni kufanya uboreshaji mara mbili kabla ya Uchaguzi Mkuu ujao. Katika zoezi hilo, Serikali inakusudia kuhakikisha kuwa wale wote wenye sifa za kupiga kura wanaandikishwa na wale waliopoteza sifa wanafutwa. Zoezi hili litafanywa kikanda kama ilivyokuwa kabla ya Uchaguzi Mkuu uliopita na Serikali imetenga fedha kwa madhumuni ya zoezi hili katika mwaka wa fedha wa 2007/08.

Mheshimiwa Spika,wakati wa kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuna Waheshimiwa Wabunge waliochangia kuikumbusha Serikali kuboresha utaratibu ili kuhakikisha amani na utulivu unadumishwa wakati wa uchaguzi na kuitaka Serikali kuyafanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza katika Uchaguzi Mkuu uliopita. Wapo walioitaka Serikali iweke utaratibu kwa wananchi walioko nje ya nchi kupewa fursa ya kupiga kura wakati wa Uchaguzi Mkuu na wengine wameomba utaratibu wa majimbo na mipaka uangaliwe upya.

Aidha, kuna Waheshimiwa Wabunge walioishauri Serikali kuongeza nafasi za upendeleo za uwakilishi kwenye Bunge. Baadhi ya Wabunge waliozungumzia masuala hayo ni pamoja na Mhe. Dkt. Wilbrod Peter Slaa, Mhe. Ania Said Chaurembo, Mhe. Fatma Abdallah Mikidadi na Mhe. Zuleikha Yunus Haji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, matukio ya uvunjaji wa amani yaliyojitokeza ni katika sehemu chache tu wakati wa chaguzi mbalimbali. Hata hivyo, Serikali imekuwa ikihakikisha kuwa siku zote matukio hayo yanadhibitiwa na kunakuwepo na amani, usalama, mshikamano na wananchi wanashiriki zoezi la uchaguzi bila wasiwasi wowote. Serikali itaendelea kushirikiana na wadau wote ili chaguzi ziwe za amani na utulivu. Aidha, Serikali inayafanyia kazi mapendekezo mbalimbali kwa lengo la kuboresha sheria ili kuondoa upungufu ambao ulijitokeza kwenye uchaguzi uliopita.

Kuhusu wananchi walioko nje ya nchi kuruhusiwa kupiga kura, Sheria iliyopo kwa sasa haiwaruhusu kupiga kura huko waliko. Hata hivyo, Serikali imeanza kuangalia maeneo yanayohitaji kuboreshwa kwenye sheria ikiwa ni pamoja na hili. Kuhusu majimbo na mipaka, hili ni suala linalozingatiwa kwa mujibu wa Katiba ya Nchi na hivyo napenda kulihakikishia Bunge hili kuwa utaratibu wa kuangalia upya mipaka ya majimbo unatarajiwa kufanyika kabla ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010.

Kwa nafasi za upendeleo za uwakilishi, ningeomba kuchangia kuwa kama inavyofahamika, uwakilishi wa ubunge wa viti maalum umezingatia matakwa ya Kikatiba na Kisheria. Vilevile uwakilishi wa makundi maalumu unategemea Katiba za Vyama husika, kwa mfano, suala hili ni la kisera na liko wazi ndani ya Katiba ya Chama cha Mapinduzi na linatekelezwa kikamilifu.

Naomba kuwahusia wenzangu wa Vyama vingine kuweza kuiga mfano huu wa Chama cha Mapinduzi ili kuongeza uwakilishi wa makundi maalumu katika Bunge hili Tukufu. Tanzania imefikisha asilimia 30 ya uwakilishi wa wanawake kwenye Bunge kama ambavyo malengo ya *SADC* yanavyotaka. Aidha, mchakato wa kufikia asilimia 50 kwa mujibu wa malengo ya *AU* unaendelea chini ya usimamizi wa Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge Kabuye aliyehoji kuhusu Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuwa katika Ofisi ya Waziri Mkuu upo uwezekano wa kupata maagizo kutoka ofisi hiyo na kuifanya isiwe huru. Aidha, kuna mwingine aliyetaka Rais asiwe na Mamlaka ya kumteua Mwenyekiti na Tume hiyo.

Naomba niwaelimishe Waheshimiwa waliochangia hoja hizo kuwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa uhakika ni huru na inafanya kazi zake kwa mujibu wa Katiba na Sheria. Ofisi ya Waziri Mkuu ni kiungo tu kati ya Tume na Serikali. Kwa suala la uteuzi wa Mwenyekiti wa Tume, napenda kuchangia kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiyo inayoelezea kuwa atateuliwa na Rais katika kazi yake ya Urais na siyo kama Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. Kwa sasa Serikali haioni sababu ya kubadili utaratibu huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imetakiwa kuangalia upya uhusiano wa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu (*CDA*) na Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma. Hoja hii ni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ambayo iliwasilishwa na Mheshimiwa George Malima Lubeleje. Ni kwa kweli kuwa mji wa Dodoma ni eneo maalumu ambalo linatambulika na ni tofauti na maeneo mengine. Tangu lilipotamkwa kisheria na kuundwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu hapa Dodoma, hatua mbalimbali zilichukuliwa na Serikali ili kutenganisha majukumu ya Mamlaka zilizopo kadri ilivyoonekana inafaa. Mwaka 1988 kupitia Waraka wa Baraza la Mawaziri Na. 7, majukumu ya *CDA* na Manispaa ya Dodoma yaliweza kuainishwa. Kwa mujibu wa Waraka huo *CDA* jukumu lake ni kujenga miundombinu mikubwa na kuikabidhi Manispaa na mamlaka nyingine. Kazi ya Manispaa ni kuendesha shughuli za huduma za kijamii. Serikali imeanza kuangalia upya uhusiano na majukumu ya Mamlaka hizi mbili kwa lengo la kuongeza ufanisi na kuondoa dhana ambayo ipo. Aidha, Tume ya Ushauri ya *CDA* na Bodi yake ya Wadhamini zinajumuisha wajumbe kutoka Manispaa ili kuimarisha uhusiano.

Mheshimiwa Spika, pia ilijitokeza hoja ya kuitaka Serikali isukume Vyama vya CCM na *CUF* viongeze kasi ya mazungumzo ya Muafaka unaojadiliwa hivi sasa. Waliochangia hoja hiyo ni Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa na Mheshimiwa Juma Said Omar. Naomba niwafahamishe Waheshimiwa Wabunge kuwa mazungumzo ya Muafaka

yanayoendelea kati ya vyama hivyo yana mwelekeo mzuri. Utaratibu wa mazungumzo hayo ni kwa Vyama vya CCM na *CUF*, Serikali kwa upande wake itaendelea kujenga mazingira mazuri ya kisiasa tu kuhakikisha muafaka unafikiwa na amani hapa nchini inadumishwa.

Mheshimiwa Spika, ilikuwepo hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuweka utaratibu wa kukutana na Viongozi Wakuu wa Vyama vya Siasa kwa lengo la kujenga ushirikiano. Ushauri huu ulitolewa na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, nami napenda kumhakikishia kuwa ushauri wake umezingatiwa. Zilijitokeza hoja kadhaa kuhusu zoezi la kuwahamisha wafugaji kutoka Bonde la Ihefu, kuandaa mikutano na wadau kabla ya utekelezaji wa mazoezi ya aina hii kwenye maeneo mengine na kutoa fidia mapema kwa wananchi wa vijiji 7 vinavyotakiwa kuhama. Hoja hizo zilichangiwa na Waheshimiwa wafuatao:- Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Mpanda na Mheshimiwa Ali Saidi Salum

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa sikivu sana katika zoezi hili. Ni mara tu baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi na viongozi mbalimbali, Mheshimiwa Rais aliunda Tume iliyoongozwa na Jaji Chande Othuman ili kuangalia matatizo yaliyojitokeza katika zoezi la kuhamisha wafugaji wa Bonde la Ihefu. Baada ya uchunguzi kufanyika, Tume hiyo imewasilisha taarifa yake kwa Mheshimiwa Rais. Naomba niwashauri Waheshimiwa Wabunge kwamba tusubiri maelekezo ya Mheshimiwa Rais ambayo yatafanyiwa kazi kwa vyovyote vile.

Mheshimiwa Spika, ilikuwepo hoja ya kusikitisha sana kuhusu kuongezeka kwa ajali za barabarani na ambayo iliitaka Serikali kuweka mikakati ya kudhibiti hali hiyo. Kwa umuhimu wake, hoja hiyo ilichangiwa na Wabunge wapatao sita wakiwemo hawa wafuatao:- Mheshimiwa Halima Kimbau, Mheshimiwa Bgd. Gen. Mstaafu Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Mariamu Mfaki, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Capt. Mstaafu George Mkuchika na Mheshimiwa Damas Nakei.

Serikali imepokea kwa masikitiko makubwa taarifa za ajali zinazotokea katika maeneo mbalimbali nchini. Ajali hizi kwa sehemu kubwa, pamoja na mambo mengine, zimesababishwa na uzembe wa madereva, ubovu wa magari na nyingine kutozingatiwa kwa Sheria za Usalama barabarani. Serikali itaendelea kushirikisha wadau mbalimbali ili kupunguza tatizo hili. Aidha, Jeshi la Polisi limeelekezwa kujipanga vizuri zaidi katika kusimamia Sheria za Usalama barabarani ikiwa ni pamoja na kukagua leseni za madereva na kuendelea kutoa elimu ya matumizi bora ya barabara. Vilevile kushauri kuhusu aina ya magari yanayotumiwa kwa ajili ya biashara ya uchukuzi na hasa kusafirisha wanadamu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Omar Kwaangw' alidai kwamba katika mojawapo ya hoja zake kuwa kitabu chenye Ahadi za Serikali zilizotolewa Bungeni hakijatolewa na aliitaka Serikali itoe maelezo. Kitabu chenye Ahadi za Serikali zilizotolewa Bungeni huwa kinatolewa mapema sana mara tu baada ya Mkutano wa Bunge la Bajeti. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2006/07, kufuatia Ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kitabu cha taarifa ya Utekelezaji wa Ahadi za Serikali Bungeni kwa nusu

mwaka kiliwasilishwa Ofisi ya Bunge baada ya Mkutano wa Saba wa Bunge. Kitabu chenye Utekelezaji wa Ahadi za Serikali kwa mwaka mzima 2006/07 kitatolewa kabla ya Mkutano huu wa Nane wa Bunge kuahirishwa.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walichangia kupongeza utaratibu wa stakabadhi za mazao. Mpango wa stakabadhi za mazao ghalani ni mpango wa majaribio ambao umeonekana unafaa. Mpango huu unatekelezwa chini ya Programu ya Uendelezaji Mifumo ya Masoko ya Mazao ya Kilimo. Programu hii inatekelezwa katika mikoa minane ya Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Iringa, Ruvuma, Mbeya na Rukwa. Lengo la Mpango huo ni kuwawezesha wakulima kuhifadhi mazao yao wakisubiri bei iwe nzuri. Lakini pia kutumia stakabadhi hizo kupata mikopo. Ninachoweza kushauri ni kutumia fursa zilizopo katika programu mbalimbali kama *TASAF, ASDP*, *PADEP* kuweza kuingiza mpango huu wa stakabadhi za mazao.

Mheshimiwa Spika, ilikuwepo hoja ya Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed ya kutaka ufafanuzi utolewe kuhusu kasma ya "*Employment Allowance*" iliyoko katika mafungu ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Hizi ni posho za aina mbalimbali zinazotolewa kwa watumishi wenye stahili ya posho hizo Serikalini. Posho hizo ni pamoja na:-

- Gharama za likizo;
- Kulipia mavazi rasmi;
- Kulipia hoteli kabla ya mtumishi kupatiwa nyumba;
- Posho ya nyumba;
- Posho ya Vikao;
- Posho ya Kazi za ziada; na
- Posho ya Kujikimu ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Ilitolewa hoja na Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa ambaye alimtaka Mheshimiwa Waziri Mkuu awe na Ofisi ndogo Zanzibar. Tunapenda kumwarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba suala la uratibu katika masuala ya Muungano lipo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais na tayari eneo la kujenga Ofisi yake Zanzibar imepatikana na ujenzi utaanza rasmi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Manju Msambya aliishauri Ofisi ya Bunge kuhakikisha kuwa inakuwa makini katika kutoa vibali vya wafanyabiashara ndani na nje ya eneo la Bunge kwa usalama na kwa kuepuka kukaribisha matapeli. Aidha, Mheshimiwa Mbunge alishauri kuangalia vizuri utaratibu wa fomu za mikopo ya wanafunzi kuweka kipengele cha kiongozi wa dini kuidhinisha. Ushauri wa Mheshimiwa Mbunge tutazishughulikia ili kuweza kuhakikisha mambo yote yanarekebishwa.Suala jingine ambalo lilizungumziwa ni suala la chaguzi katika Kata mbalimbali. Hili lilizungumzwa na Mheshimiwa Stephen Galinoma. Napenda kukuhakikishia kwamba chaguzi katika Kata zote zitafanywa kwani zimepangiwa fedha katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, udhibiti wa madawa ya kulevya ulizungumzwa na Waheshimiwa Wabunge kwa kutoa ushauri kwamba Serikali iangalie zaidi kuboresha Sheria. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge hasa kufuatia Hotuba ya

Mheshimiwa Rais aliyoitoa wakati wa maadhimisho ya siku ya kupiga vita dawa za kulevya kwamba Watanzania tuwe karibu na vijana wetu lakini pia tuhakikishe kwamba maeneo ya shule hayageuzwi kuwa vituo vya kuuzia dawa za kulevya. Mapambano yanaendelea, utaratibu wa kuhakikisha kwamba sheria inaboreshwa iweze kuwa kali zaidi inafanyika na taratibu zote za kuwa na vituo kwa ajili ya kuweza kuwasaidia vijana wetu zinaendelea na tayari kuna kituo hapa Dodoma. Napenda kukiri kwa dhati ya moyoni mwangu kwamba ushirikiano na maelekezo niliyopata kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika yameniwezesha kuifanya kazi yangu iwe nyepesi kuliko nilivyotarajia. Vile vile nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri, Wajumbe wa Kamati ya Uongozi na Tume ya Huduma za Bunge na Wabunge wenzangu wote kwa ushirikiano mkubwa ambao mmenipatia katika kipindi chote. Aidha, naishukuru familia yangu na hususan mume wangu kwa kwa kuniunga mkono, kunivumilia na kunipa *support* kubwa katika kipindi chote hiki cha kazi.Baada ya kusema maneno haya naomba tena kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana, natumaini kabla ya Mkutano huu wa Nane kwisha utamtambulisha mumeo hapa katika Bunge hili.(*Kicheko*)

Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa muda wa saa moja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na mimi niweze kuchangia hoja ambayo ipo mbele yetu na kama walivyosema wenzangu pengine nitangulie kusema kwa kweli naiunga mkono moja kwa moja. Hotuba imeweka mambo mengi vizuri ya kueleweka lakini kubwa imeonyesha jitihada za Serikali hii ya Awamu ya Nne katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapunduzi. Kwa hiyo, nadhani ni jambo zuri wengi tukaiunga mkono ili tuweze kwenda vizuri. Lakini pili nataka nitumie nafasi ya awali kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa maelekezo yake kwangu ya mara kwa mara kuhususiana na eneo hili kubwa lenye mambo mengi na kwa kweli linahitaji maelekezo ya aina hiyo ili kuweza kuisaidia Serikali kusimamia eneo hili vuzuri zaidi.

Naomba niwashukuru sana wenzangu mawaziri na Naibu Mawaziri kwa msaada wao mkubwa sana ambao muda wote wamekuwa wakinipa kama mtekelezaji katika ngazi ya Halmashauri kuhusiana na masuala mbalimbali ya kisekta. Ushirikiano wa karibu kati ya ofisi yetu na Waheshimiwa Mawaziri wa kisekta kwa kweli umeniwezesha kufanya kazi kuwa nyepesi kidogo. Naomba sana niwashukuru wananchi wa Mkoa wa Rukwa kwa ujumla wao wote na hasa Jimbo langu la Mpanda Mashariki kwa kuendelea kuniunga mkono lakini vilevile kuendelea kutuona Wabunge wa Mkoa mzima wa Rukwa kama chachu katika maendeleo ya Mkoa wa Rukwa. Tunaomba ushirikiano huo waendelee kuutoa ili nasi tuweze kuendelea kuwahudumia vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya machache naomba basi niende moja kwa moja katika hoja iliyo mbele yetu kwa kujaribu kutoa ufafanuzi katika baadhi ya maeneo. Najua sitaweza kuyamaliza yote, lakini tumepata michango kwa Waheshimiwa

Wabunge 73 ya moja kwa moja hapa Bungeni. Vilevile nimepata kwa njia ya maandishi kutoka kwa Wabunge 87 na kila mmoja alikuwa na hoja kadhaa katika maelezo yake. Kwa hiyo, si rahisi lakini tutajitahidi kuhakikisha kwamba maelezo haya tunayachapisha kama kawaida baadaye tutayagawa ili muweze kupata fursa ya kuona majibu tuliyowapa. Nianze na hoja alizozieleza Mheshimiwa George Malima Lubeleje. Kwanza, ilikuwa ni Kurekebisha dosari zilizopo na kuweka utaratibu wa kisheria wa uhusiano miongoni mwa mamlaka za Jiji la Dar es Salaam. Bahati nzuri Serikali imekwishabaini migogoro na matatizo yanayoendelea katika Jiji kwa maana ya mfumo ulivyo hivi sasa. Pande moja ni uhusiano lakini tunaamini vilevile pengine kuna mambo ya msingi zaidi, hivyo tumeunda timu ambayo sasa inalifanyia uchambuzi suala hili kwa mujibu wa Sheria, Sura ya 288 ili tuweze kuona ni namna gani tunaweza tukaboresha muundo wa Dar es Salaam. Lakini kama Wabunge mlivyoshauri si vizuri tukaiga muundo huu katika maeneo mengine kabla hatujajiridhisha na ufanisi wa muundo wa sasa. Kwa hiyo, tutajitahisi kukamilisha jambo hili katika mwaka huu wa fedha unaoanza 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lubeleje vilevile alitaka kujua kuhuhu kujaza nafasi wazi katika Shirika la Masoko Kariakoo na kushauri kuwa ikiwezekana jiji lichukue hisa zote zilizoko katika soko hilo badala ya Serikali. Tumekubaliana na ushauri wake ni mzuri tutaliangalia suala hilo lakini vilevile tutaangalia kama kuna umuhimu wa Serikali kuendelea kushikilia hisa asilimia 100.

Mheshimiwa Lubeleje, Mheshimiwa Mwinchumu, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Mussa Hassan Zungu, Mheshimiwa Salim Abdallah Khalifan, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Peter Slaa na Mheshimiwa Stella Manyanya, walitaka kujua jambo moja ambalo nafikiri ni la msingi sana kuhusiana na Ujenzi wa miundo mbinu ya Usafiri katika kukidhi mahitaji ya wakazi wa Jiji la Dar es Salaam. Jambo hili Mheshimiwa Waziri Mkuu amelieleza vizuri sana katika Hotuba yake na naomba mwende moja kwa moja kwenye aya ya 32, huo ndio mtazamo wa Serikali na tutajitahidi kuhakikisha kwamba tunatekeleza hayo ambayo tumedhamiria kuyafanya katika juhudu za kuboresha hali ya usafiri katika jiji letu la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Masilingi alitaka kujua ni lini Serikali itatoa kiasi cha shilingi milioni 50 kwa ajili ya kusaidia kujenga Kituo cha Afya kilichopo pale Kaigara kule Muleba, naomba niseme tu kwamba Halmashauri yake imetenga shilingi milioni 30 kwa ajili ya Kituo hicho. Lakini vilevile pamoja na kuwapongeza sana Halmashauri yake ambayo wameweza kupata fedha ile ya ruzuku ya maendeleo kwa kiasi cha shilingi milioni 824,060,000 ambazo kwa kweli wanaweza vile vile wakazitumia katika kuhakikisha wanakamilisha kituo hicho, namwomba Mheshimiwa Masilingi atumie fursa hiyo kuweza kupata bakaa wakati Serikali inaendelea kutazama kwa siku zijazo kama kutahitajika msaada zaidi.

Mheshimiwa Spika, watumishi wanaoharibu kituo kimoja kuhamishiwa kituo kingine, ilikuwa ni hoja ya Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Pandu, Mheshimiwa Ali Juma Haji na Mheshimiwa Bujiku Sakila. Tumekuwa tunalisema hili mara nyingi kwamba huwa hatufanyi hayo ambayo mnahisi tunayafanya lakini ni vizuri

tukaendelea vilevile kulieleza na hapa nataka niseme mambo makubwa mawili. Mwenye mamlaka ya nidhamu juu ya watumishi katika Halmashauri ukimwondoa Mkurugenzi Mtendaji ni Halmashauri zenyewe.

Kwa hiyo, rai yangu kwenu Waheshimiwa Wabunge kwa kuwa ninyi ni chachu kubwa sana katika Halmashauri zetu, haya mambo ya uharibifu, ubadhirifu uzembe ni mambo ambayo mnapaswa moja kwa moja kuyasimamia pale kwa kuwafungulia mashtaka kulingana na taratibu za sheria. Hiyo itawasaidia sana kuweza kudhibiti hali potofu ambayo haiendeni na matarajio ya wananchi katika Halmashauri zetu.

Mtumishi pekee ambaye yupo chini ya Ofisi yangu ni Mkurugenzi Mtendaji na yeye vilevile bado tuhuma huwa zinaanzia kwenye Halmashauri kisha zinaletwa kwetu kwa ajili ya hatua zaidi. Kwa hiyo, bado Halmashauri zina mamlaka makubwa sana kuhusiana na watumishi hawa. Hata hivyo naomba niseme kwa ufupi tu kwamba kwa mwaka 2006/2007 tulikuwa na jumla ya mashauri kama 152 katika Halmashauri 27 ambayo yapo katika hatua mbalimbali za hatua za nidhamu na katika kipindi hicho waliofukuzwa kazi ni 24 waliorejeshwa kazini 45 baada ya kuonekana hawana hatia, waliotiwa hatiani na mahakama kwa maana ya kesi za jinai 2, kesi zinazoendelea ni 79 na bahati mbaya waliokufa bila kesi kumalizika ni 2 na hii inafanya jumla ya watumishi 152.

Mheshimiwa Spika, vilevile kulikuwa na hoja ya uwezo wa wananchi kuendelea kuchangia katika mpango wa ujenzi wa zahanati na jambo hili limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi akiwemo Mheshimiwa Mwijage, Mheshimiwa Aziza Ali, Mheshimiwa Ahmed Salam, Mheshimiwa Ramadhani Maneno, Mheshimiwa Phares Kabuye, Mheshimiwa Tedy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Messy Emmanuel, Mheshimiwa Stella Manyanya na Mheshimiwa Elizabeth Batenga.

Mheshimiwa Spika, hapa nafikiri hatuna ujanja inabidi kwa kweli tujitahidi kwenda na hali halisi tuliyonayo sasa. Na kwa kweli mfano mzuri ni kwenye elimu ya Sekondari. Kama kweli kiwango ambacho tulikuwa tunaweza kupeleka watoto shule kingebaki asilimia 23, ningefanya nini? Ambao wamejitahidi wakafaulu tumejitahidi lakini hatujawamaliza wote ndiyo wametufikisha karibu asilimia 84. Hili kundi kama si juhudi za Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali ya Awamu ya Nne mlitaka watoto hawa wabaki mitaani? Kwa hiyo, ni dhahiri kabisa kama Serikali ilibidi kuchukua hatua za makusudi kuhakikisha tunatumia chachu na nguvu kubwa ambayo wananchi wanayo hasa katika maeneo yanayowagusa na matokeo yake wote mmeyaona. Sasa eneo hili la sekta ya afya mimi, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali kwa ujumla hatuoni kama linamtatiza mwananchi kwa sababu ni kero.

Mheshimiwa Spika nilifikiri tukitaka kupunguza vizazi ambavyo mnaviona sasa hivi kwa watoto wachanga chini ya miaka mitano, akina mama wajawazito na magonjwa mengine tunadhani suluhu ni kwenda na sera hii ambayo Rais ameamua kuiweka bayana mbele yenu na kwa kweli tukitumia fursa tulizonazo za kuhamasisha wananchi kiwango kitakachochangiwa hakitakuwa cha kutisha kiasi cha kuwafanya wasichangie juhudi hizi nzuri na ni kwa manufaa yao wenyewe. Kwa hiyo, mimi rai yangu kwenye eneo hili ni

kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wote tujaribu kukubaliana na rai hii, tutajitahidi kutokutumia mabavu kama ambavyo tumefanya kwenye Elimu ya Sekondari na tunaamini wananchi wengi wanaunga mkono jambo hili kwa kuwa ni kwa manufaa yao.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mudhihir alituletea hoja moja kuhusiana na ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Kitomanga. Tumeipokea kwa mikono miwili lakini lazima tukiri vilevile kwamba kwa bahati mbaya haikuwa imewekwa katika utaratibu wa kupata fedha kupita Mkoani kama Bajeti nyingine za kawaida. Tunaomba tumwahidi kwamba kwa kuwa inawezekana isiwe rahisi kupata fedha katika muda huu tulionao kuweza kutimiza azma aliyokuwa nayo basi tumwombe Mheshimiwa Mudhihir tumwahidi kwamba katika Bajeti ijayo tutahakikisha jambo hili tunalipa kipaumbele. Tumesita kidogo kuondoa zile shilingi milioni 155 katika mradi wa ujenzi wa ofisi ya Mkoa. Kwa kweli ni kwa sababu nzuri tu pamoja na matakwa haya mengine mazuri ya Hospitali lakini vilevile pale Lindi panahitajika Ofisi ya Mkoa yenye uwezo wa kutunza watumishi ambao ndiyo wanatusaidia kusimamia shughuli za maendeleo.

Kwa hiyo, ndiyo wanatusaidia sana kusimamia shughuli za maendeleo, hivyo pale kuna mradi pale wa ukarabati wa jengo la zamani, lakini vile vile tunao mradi wa kujenga jengo jipya ili tuweze kutoa nafasi nzuri zaidi kwa watendaji tulionao pale. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mudhihir chonde chonde, tunakusihi sana kwenye hili najua nia yako ni nzuri tutajitahidi. Lakini na sisi tutaendelea kulitafakari tuone kama kuna jambo lolote katikati hapo ambalo tungeweza tukafanya kwa sababu Serikali ni pana na inawezekana pengine tukapata ufumbuzi kabla ya kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Stephen Galinoma na Mheshimiwa Benedict Losurutia pamoja na Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba waliomba sana kuondoa upendeleo katika ujenzi wa ofisi 40 kwa mwaka 2007/2008. Naomba niseme tu kwamba tumelifanyia kazi kwa kadiri tulivyoweza, tunajua fedha zilizotengwa ni kidogo kwa awamu ya kwanza na ndiyo maana unaona inaleta kidogo haja na umuhimu wa kuwa na uhakika ni namna gani tutaweza kugawa hizo ofisi 40.

Tumeshaanza kulifanyia kazi kwa maana ya kupata takwimu juu ya maeneo yote, lakini baadae kupitia kwa Waziri Mkuu tutamshirikisha Mheshimiwa Spika ili aweze kujua ni maeneo yapi tunafikiria kwa kuanzia yangeweza. Lakini misingi tuliyonayo tuitumie, moja, ni kuhakikisha kwamba unakuwepo uwiano kati ya Wabunge wanaotoka Visiwa vya Zanzibar na Wabunge wanaotoka upande wa Tanzania Bara katika mgao tutakaokuwa tumeutengeneza, kila upande upate lakini kulinga vilevile na idadi ya Wabunge kama tunavyojua idadi yake ilivyo. Kwa upande wa Visiwani tutahakikisha kwamba tunatambua ipo Unguja na Pemba, kwa hiyo, kiwango chochote kitakachotengwa cha ujenzi wa ofisi tutatumia vilevile uwiano kati ya maeneo hayo mawili ili angalau kila eneo lipate kidogo kidogo kulinga na uwezo tulionao hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, lipo swala la vigezo vya kupatiwa ruzuku ya maendeleo ya Halmashauri kwamba vilegezwe, na hili Mheshimiwa Grace Kiwelu alilisema sana, Mheshimiwa Harrison Mwakyembe naye amelizungumza sana lakini vilevile

Mheshimiwa Ali Juma Haji naye vilevile aliligusia jambo hili. Niseme tu kwa ujumla kwamba fedha hii ya maendeleo imeanzishwa na Serikali katika kuleta chachu, tunataka tu kuleta hamasa kwa Halmashauri zetu. Yanayohitajika hakuna jipya hata moja ni yale yale ambayo ni Sheria ya Fedha na Sheria nyingine zinazohusiana na Serikali za Mitaa.

Kwa hiyo, kimsingi ni kutaka Halmashauri zizingatie utawala bora, hilo moja. Lakini upande wa pili ni lazima Waheshimiwa Wabunge tukubali vilevile kuwa tusipong'ang'ania jambo hili la kuhakikisha fedha za wananchi katika Halmashauri zetu zinatumika vizuri haitakuwa busara kusema tu peleka pesa hata pale ambapo mnajua kuna upungufu mkubwa. Hiki ni kichocheo na mimi rai yangu kwa wananchi tutaendelea kuwaambia nani kakukosesha fedha zako za maendeleo ili wawe wakali zaidi kuzibana Halmashauri kuhakikisha wanatekeleza sheria kama inavyotakiwa. Sasa basi pamoja na hili nililolisema lazima niseme kwamba jambo hili msidhani kwamba halina *improvement* ndani yake hapana! Tangu tumeanza mpango huu ni miaka kama mitatu iliyopita, sasa kwa mwaka 2004/2005 ni Halmashauri 25 tu kati ya 47 ziliweza kupata fedha hizo.

Lakini mwaka 2005/2006, Halmashauri 66 zikapata fedha hii ya maendeleo kati ya 121 na mwaka 2006/2007 Halmashauri 84 kati ya 121 nazo zikakidhi vigezo, walionekana kweli wametimiza wajibu wao wa kusimamia utawala bora. Lakini faraja zaidi ni kwa mwaka 2007/2008 ambapo Halmashauri 109 kati ya 121, zimefuzu kuweza kuwapatia wananchi fedha ya maendeleo. Kwa hiyo, ni vizuri tukaendelea kukaza uzi kwenye eneo hili kwa upande mmoja kuwadhibiti kikamilifu wale ambao tunadhani hawasimamii fedha vizuri. Lakini wakati ule ule kuzidi kutoa elimu kwa madiwani ili vile vigezo vinavyohitajika basi muda wote iwe ni ajenda ya kudumu katika Halmashauri. Na tunaamini kabisa kama si mwaka wa kesho basi mwaka kesho kutwa tunaamini huenda Halmashauri zote zikawa zimetimiza. Hapo tukifika nina hakika Waheshimiwa Wabunge wote tutafarijika kwamba angalau fedha ya umma imepata mweleko wa matumizi bora.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Chacha Wangwe kidogo alihoji juu ya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ambao anasema ni makada wa CCM kuwa ni wenyeviti wa Kamati za ulinzi na usalama. Kwa mujibu wa Sheria ya Tawala za Mikoa Namba 19 ya mwaka 1997, moja ya majukumu ya Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya ni ulinzi na usalama katika maeneo yake. Sasa kulitekeleza jambo hili inabidi ujiundie utaratibu utakaokuwezesha kusimamia eneo hili vizuri.

Kwa hiyo, suala la Kamati zile za Ulinzi na Usalama ni kumsaidia Mkuu wa Mkoa muda wote kujua kinachoendelea, kujua hali ya ulinzi na usalama katika Mkoa wake na kuchukua hatua zinazostahili pale inapohitajika tena haraka inavyowezekana. Sasa suala la ukada au kutokuwa kada mimi nadhani si muhimu sana katika eneo hili la ulinzi na usalama, kikubwa ni kuhakikisha ulinzi na usalama upo.

Mheshimiwa Gedion Cheyo, alitaka vilevile kujua muundo wa Sekretarieti za Mkoa na uhusiano wake na Halmashauri. Muundo huu kwa sababu limekuwa jambo la muda mrefu ambalo Serikali imekwishaufanyia marekebisho, sasa hatuna tena ile *clusters* badala yake tumekwenda kwenye utaratibu unaofanana sana na ilivyokuwa siku za

nyuma isipokuwa tumeshindwa kuziita Idara kwa kuwa kimuundo Mkoa ni sehemu ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na ni Idara. Kwa hiyo, pale tumeanzisha sehemu badala ya kuwa na Idara.

Kwa kuondoa haya na kuanzisha hizi sehemu mpya karibu saba, tunaamini kabisa kuwa tutaweza kutimiza jukumu hili vizuri zaidi na itasaidia vilevile kutoa mwelekeo mzuri sana namna ya kuzisaidia Halmashauri zetu. Kwa hiyo, baada ya kukamilisha hili zoezi kama kawaida tutatoa waraka unaoonyesha sasa muundo mpya ukoje Mkoani.

Mheshimiwa George Simbachawene alikuwa kidogo na matatizo na utaratibu wa utoaji wa zabuni. Tumepokea rai yake lakini nilitaka niseme tu kwa kweli utaratibu ule unazingatia Sheria na lengo lake ni kujaribu kuweka vitu ambavyo vinaweka uwazi katika upatikanaji wa zabuni mbalimbali. Lakini kwa kuwa ameonyesha kidogo wasiwasi kuhusiana na gharama tutalifanyia kazi tuone kama kweli fedha nyingi zinapotea kwa sababu ya vikao basi tutalisimamia vizuri na kufanya marekebisho yanayotakiwa.

Mheshimiwa Spika, barabara za Wilaya na ujazio zipatiwe fedha za kutosha, ni hoja iliyosemwa na Mheshimiwa Sarungi, Mheshimiwa Mbarouk Mwandoro, Mheshimiwa Suleiman Kumchaya na Mheshimiwa Lucy Owenya, wote wamejaribu kulieleza jambo hili na mimi nilieleze tu Bunge lako Tukufu kwamba jambo hili limezingatiwa katika Bajeti ya mwaka 2007/2008.

Lakini naomba vilevile niseme kwamba pamoja na kwamba fedha zimeongezwa kutoka shilingi bilioni 35.7 mpaka shilingi bilioni 65.5, bado fedha hizi mipango yake ya barabara gani zitumiwe zitatoka kwenye Halmashauri zenyewe. Kwa hiyo, ni vizuri Waheshimiwa Wabunge mkawa karibu na hizo Halmashauri ili muweze kuona zile programu wanazowasilisha kwetu zimezingatia barabara hizo za ujazio kwa kiasi gani lakini vilevile barabara nyingine za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, pia ilikuwepo hoja kwamba Serikali iweke utaratibu wa kuziwezesha Halmashauri kujitegemea zenyewe katika rasilimali watu na fedha. Sera hii inaendelea kutekelezwa kama ilivyoelezwa katika aya ya 59 – 62 ya hotuba ya bajeti ya Waziri Mkuu. Huo ndio mwelekeo na ndiyo azma ya Serikali na tuna hakika baada ya mazoezi tuliyoyapanga kuyafanya, tutaweza kufanikisha jambo hilo kwa kiasi cha kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, kwamba Serikali iweke chombo kidogo cha kuangalia uwezo wa kila Halmashauri na vyanzo vyake vya mapato kama alivyokuwa amehoji Mheshimiwa Vedastus M. Manyinyi, tunakubaliana na hofu yake, lakini nataka nimhakikishie tu kwamba jambo hili linazingatiwa na Serikali katika mfumo wake ulivyo, inafanya hayo hayo ambayo alikuwa anafikiria hayafanyiki. Kwa hiyo, pengine tutakachofanya ni kuimarisha tu jambo hilo ili liweze kuonekana wazi wazi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Omari Kwaangw' alitaka kujua fedha zilizotengwa kwa ajili ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Manyara Manyara ni kiasi gani.

Kwa mwaka 2007/08 Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Manyara imetengewa jumla ya Sh. 885,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Manyara.

Lakini nataka nimwarifu vilevile kwamba kwa bajeti hii iliyomalizika hivi karibuni, Mwaka 2006/2007, Mkoa ulipata jumla ya Sh. 1.6 bilioni kwa njia ya uhamisho kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa. Hii inafanya jumla ya fedha zote kwa kukamilisha majengo yale kuwa Sh. 2.5 bilioni na tunaamini kabisa sasa Makao Makuu ya Mkoa wa Manyara yatakuwa yamekamilika na tunaamini watumishi watakuwa na sehemu nzuri ya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Omari Kwaangw' vilevile alitaka kujua Ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Manyara unaendeleaje na kwamba mbona haukuwekewa fedha, itawezekanaje! Atatuwia radhi kwa jambo hili. Lakini najua na yeye anafahamu kwamba uamuzi wa Serikali ulifanyika baada ya kuona kwamba hatuwezi kuwa na mtawanyo wa *resources* ndogo kama hizi kwa miradi mingi ambayo mnataka iende kwa wakati mmoja.

Kwa hiyo, tuliona pengine ni vizuri tukamilishe kwanza huu ujenzi wa Makao Makuu, halafu tuanze pole pole sasa kufanya hiyo kazi nyingine. Lakini yeye anajua kwamba tulitoa fedha za awali ambazo zimesaidia sana katika kuchora lakini vile vile kufanya tathmini ya hali ya udongo pale ambapo Hospitali hiyo tunategemea ijengwe. Kwa hiyo, tutajitahidi kadri sasa tunavyokwenda tukishamaliza huu mradi mkubwa, basi turejee katika miradi mingine ambayo tunafikiri ni muhimu sana kwa ajili ya kuendeleza Mkoa wa Manyara.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ahmed Salum alitaka Halmashauri ziwadhamini wananchi kukopa matrekta na pembejeo. Ni jambo zuri, ni wazo zuri. Lakini nataka tu niseme kwamba kwa vyovyote vile itakavyokuwa, Halmashauri ikiamua kudhamini jambo lolote maana yake ni Serikali Kuu tunaingia jukumu la kudhamini kwa sababu mwisho wa safari ni lazima zile fedha katika udhamini huo zilipwe. Kwa hiyo, tutajitahidi kwanza, kuboresha tu uhusiano wetu na Sekta Binafsi ambayo kwa kweli ina mchango mkuwa sana katika eneo hili ili tuweze kuwasaida vizuri zaidi wakulima wetu katika maeneo yetu. Lakini vilevile tutajaribu kushirikiana na vyombo vingine ambavyo vina uwezo wa kutoa udhamini kabla hata Serikali hatujajiingiza katika kazi hiyo ili iweze kufanyika kwa ufanisi zaidi.

Lakini niseme tu kwamba, kwa sababu Serikali ilishafanya uamuzi wa msingi kwenye eneo la vifaa hivi kama matrekta, kuondoa ushuru, kuondoa kodi mbalimbali, kwa kweli ni fursa nzuri kwetu sisi Wabunge kujaribu kutoa hamasa kwa vyombo mbalimbali ili viweze kusaidia katika eno hili kwa kuwa gharama zake ni nafuu kuliko kama tusingeondoa huo ushuru. *(Makofi)*

Mheshimwa Spika, lipo suala la Wabunge wa Viti Maalum katika Kamati za Halmashauri za Jiji la Dar es salaam. Muundo wa Halmashauri za Jiji la Dar es salam kidogo ni tofauti na Majiji mengine kwa sababu lina wajumbe wengi wa Viti Maalum.

Lakini ni dhahiri kwamba wajumbe wote wanapaswa kuwa wajumbe katika Mabaraza ya Madiwani katika Manispaa zetu za Dar es salaam. Marekebisho mliyoyapitisha hapa ya Sheria Na. 7 na Na. 8 ya mwaka 1982, yalikuwa na lengo ambalo tunafikiri ni zuri. Tutalichukua sisi wenyewe jambo hili kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu amepewa mamlaka pale inapoonekana kwamba Viti Maalum ni zaidi ya watatu katika Halmashauri moja. Idadi inayozidi sheria imetuwezesha kumshauri Waziri Mkuu hao wanaozidi tuwatawanye katika Halmashauri zinazozunguka Halmashauri hiyo iliyopo. Kwa hiyo, tutafanya utafiti kidogo tuone nani anaweza kwenda kusaidia katika eneo jingine kwa sababu hawa ni Wabunge wa Mkoa mzima, hivyo, ni halali kwao kuweza kutoa mchango mahali popote ndani ya Jiji la Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Telele alifikiri kuna mkanganyiko wa Sheria za Vijiji ile ya mwaka 1975 na Sheria ya Serikali za Mitaa pamoja zile za Ardhi kwamba zinagongana pengine na Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro. Ninachoweza kusema hapa ni kwamba kila sheria imetengenezwa kwa madhumuni mahususi. Tumejaribu kuzipitia sheria zile; tumejaribu kulitafakari sana kwa kina, lakini hatukuona hasa kwamba kuna migongano ambayo tunaweza tukasema inafanya mambo yasiweze kutekelezeka. Kwa hiyo, tuko radhi kwa Mheshimiwa Telele, kama kuna jambo *specific* ambalo pengine alikuwa amelilenga basi tuko tayari kushauriana naye ili tuone kama tunaweza tukaondoa hiyo kasoro kwa kadri tutakavyoona inawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Joyce Masunga, Mheshimiwa Mgeni J. Kadika pamoja na Mheshimiwa Chrisant M. Mzindakaya, walitaka vilevile kujua kwamba fedha zilizotengwa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji maji kwa nini hazitoshi. Mimi si mtaalamu sana wa eno hili, lakini nina hakika Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika atapata nafasi ya kulieleza vizuri sana jambo hili kwa sababu uko mpango ule wa kuendeleza kilimo, lakini vile vile uko mpango wa umwagiliaji. Kwa hiyo, nafikiri pengine itakuwa *fair* kwake kuweza kujua afanye nini kwenye eneo hili. Lakini mimi niseme tu kwamba bado ziko fedha ambazo nazo tumezihusisha moja kwa moja na mpango ule wa kutoa fedha ya ruzuku ambao ukikidhi vigezo fulani fulani unaweza kabisa ukafanikiwa kufanya kazi hii ya sekta ya kilimo katika umwagiliaji kuwa nyepesi. Kwa hiyo, nitaomba wakati anawasilisha Mheshimiwa Waziri, basi tuone ni maeneo gani ambayo mlikuwa bado hamjaridhika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Joyce Masunga vilevile alitaka Maafisa Kilimo wakopeshwe vyombo vya usafiri. Nalo hili pengine kwa vile linatugusa tu, labda niseme kwamba kwa bajeti hii ambayo kama itapita kwa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, ni dhahiri mle ndani tuna watumishi 2500 ambao kwa muundo ulivyo, wote wanategemea kuwa na vyombo vya usafiri katika ngazi ya Tarafa, Kata mpaka ngazi ya Vijiji na hivyo itaendelea kwa bajeti itakayofuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, alihoji kama kweli kuna matunda hasa yaliyopatikana kutokana na maboresho yanayoendelea katika Serikali za Mitaa. Mheshimiwa Dr. Slaa ni mwelewa sana, mimi kidogo alipohoji hili, nikajiuliza rafiki yangu anasema kweli! Ni kweli maboresho haya hayajaonyesha matunda yoyote? Bado anatikisa kichwa! Kwa hiyo, na mimi nataka niseme kwamba si kweli! Mimi siamini kwamba maboresho haya eti hayajafanya kitu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya Mpango huu yalikuwa Kuboresha Mfumo wa Serikali za Mitaa kupitia dhana ya upelekaji madaraka kwa wananchi ili kuziimarisha Serikali za Mitaa ziweze kutoa huduma bora. Sasa mafanikio yake kwa kutaja machache ni kama ifuatavyo:-

Eneo ambalo wote mnalijua, Ushirikishwaji wa wananchi katika kupanga na kutekeleza miradi yao kwa njia ya kuibua miradi na hatimaye kupata fedha kwa ajili ya kuitekeleza ni jambo ambalo limetokana na mpango huo.

Kumekuwa na ongezeko kubwa sana la rasilimali fedha zinazopelekwa sasa katika Halmashauri zetu na nataka niseme kwamba ongezeko ni kubwa. Tulipoanza maboresho mwaka 2000, fedha zilizopelekwa kwenye Halmashauri zilikuwa ni shilingi bilioni 217. Leo tunazungumza ni trilioni moja kwenye bajeti ya mwaka huu. Hiyo yote ni msukumo wa azma ya Serikali kupeleka madaraka kwa wananchi, lakini chachu yake na mchanganuo wake umetokana na maboresho.

Lakini vile vile tumeboresha miundo ya Halmashauri kwa kuzingatia matakwa ya kila Halmashauri. Sasa, hili limetusaida sana sehemu nyingine kupunguza, lakini vilevile kuongezeka kwa uelewa wa wananchi kuhusu uwezo na madaraka waliyonayo kwa umma. Hili nalo limetokana na juhudi hizi ambazo ni muhimu sana katika kusimamia eneo hili.

Lakini Sambamba na mpango huu wa maboresho ulioanza mwaka 2000 tunaweza kuona mabadiliko katika utunzaji wa mahesabu ya Serikali za Mitaa, hati chafu sambamba na hayo maboresho zimepungua kutoka 75 mwaka 2000/2001, hadi hati 4 mwaka 2005/2006. Hii yote ni msukumo hata kama Mheshimiwa Dr. Slaa atasema si kweli. Lakini ukweli ni kwamba maboresho yameleta msukumo mkubwa sana katika kuwapa elimu wataalamu wetu na Mkurugenzi na kumwezesha kusimamia vizuri jambo hili. Ni sawa tunakiri kuwa bado tunahitaji kufanya kazi kubwa zaidi na ndiyo azma ya Serikali kuzidi kufanya jambo hili liwe bora zaidi ili wananchi waweze kufaidika zaidi. Sasa ni kweli hakuna jambo ambalo halina gharama, kwa hiyo, mradi huu nao una gharama na ni kubwa. Lakini ukilinganisha na matokeo kwa maana ya mtazamo wa muda mrefu, ni dhahiri kabisa kwamba ni vizuri mpango huu ukaendelea hadi utakapokamilika ili matunda yake yaweze kuwa makubwa zaidi. Kwa hiyo, mpaka sasa tumeishatumia kiasi cha shilingi bilioni 90.5, na Wahisani wamechangia jumla ya Shilingi bilioni 67.7 kwenye Mfumo wa kuzipatia Serikali za Mitaa ruzuku ya maendeleo. Hivyo siyo vyema kubeza mafanikio ambayo yanatokana na Mpango huu. Mimi nadhani pale pazuri, tukiri na pale ambapo mnataka tuzidi kufanya kazi vizuri, mseme hivyo na sisi tutakuwa radhi kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini, nataka nimwambie Mheshimiwa Dr. Slaa kwamba kwa maboresho haya tunayoyafanya, Uganda, Kenya, Malawi, Ghana, Nigeria na Nepal wote wamekuja Tanzania kuona ni nini tunafanya ambacho kimesaidia kuleta mabadiliko makubwa kiasi hiki. Sasa mimi nafikiri haya yote ni jambo jema na ni vizuri tukaliona

kwamba ni *positive* na pengine tunakokwenda litatusaidia kuimarisha sana Serikali zetu za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kutumia *Njia Tatu*, Jijini Dar es saalam: Hoja ilikuwa ni kwamba nyinyi wakubwa mmetoa wapi utaratibu huo? Nani wengine wanafanya jambo hili? Lakini mimi niseme kwamba Wabunge wote niliowasikiliza hapa kwa sehemu kubwa wamepongeza sana utaratibu huo, umepunguza sana kadhia iliyokuwepo. Hili ni jambo jema, sasa wapi tumeiga jambo hili: tumeona *China-Beijing* wanafanya, tulikwenda *Brazil* tulikuta wanafanya, ndiyo maana tukapata nguvu na sisi kusema tujaribu. Inawezekana mwanzoni lina matatizo kidogo, lakini baada ya kuzoea, utaona jambo hili litatusaidia pamoja na ile mikakati mingine ya kupunguza kiasi kikubwa sana cha matatizo ya msongamano pale Dar es salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Jenista Mhagama, alitaka kujua wale wakandarasi wanaochimba kokoto kwa ajili ya ujenzi wa barabara, kwa nini wasilipe ushuru! Niseme tu kwamba Sheria Na.19 ya Nishati na Madini inazitaka Wizara husika ambazo zinakuwa na Mikataba na hao wakandarasi wanapotaka kuchimba kokoto mahali popote waombe kwenye Wizara hiyo ili waweze kupata msamaha kwa ajili ya huyo mkandarasi kuweza kupata kokoto hizo bila kulazimika kutozwa ushuru. Vinginevyo bila msamaha ni lazima mkandarasi huyo alipe ushuru. Kwa hiyo, kuepuka hilo, ni kufuata tu utaratibu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya, aliuliza hoja ya kwamba Serikali ishindanishe Halmashauri za Wilaya na kuzipanga katika madaraja, na mimi nafikiri ni jambo jema. Lakini nataka kumwambia tu kwamba tunachojaribu kufanya sasa hasa katika mpango wa fedha za maendeleo ni kuzishindanisha hizo Halmashauri ili tuone yupi anaendelea kutimiza wajibu wake inavyotakiwa. Lakini rai yake bado ni nzuri, tutapanua wigo, tutajaribu kuweka na maeneo mengine ambayo yanaweza kusaidia kuzidi kutoa chachu na kuimarisha Serikali zetu za mitaa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Capt. George Mkuchika na Mheshimiwa Suleiman Kumchaya walilisemea kwa nguvu sana suala la kurudisha *Export Levy* kwa Halmashauri. Tumelipokea, na mimi nasema na wao waendelee kulisukuma kupitia *RCC*. Nina hakika tukiunganisha mawazo haya mawili, tutapata ufumbuzi kwa sababu Serikali hii ni sikivu, sidhani kama ni jambo ambalo liko mbali sana na uwezo wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbarouk Mwandoro, alitaka kujua kwamba ni kwa nini Halmashauri mpya hazirithi rasilimali toka Halmashauri mama kama *case* ya kwake ambapo Muheza ni Halmashauri na sasa Nkinga nayo itakuwa Halmashauri. Anasema kwa nini zisirithi baadhi ya mali? Ninaomba nitoe maelezo haya vizuri kwa sababu ni tofauti kidogo na swali la Mheshimiwa Mntangi. Mheshimiwa Mntangi aliulizia Wilaya, ndiyo maana tukamwambia, Wilaya hakuna cha kurithi kwa sababu Wilaya ni sehemu ya Serikali. Tunachofanya ni kujenga Makao Makuu ya Wilaya, mwisho tunamsaidia magari na vitendea kazi kama lilivyo jukumu la Serikali. Halmashauri ni tofauti. Halmashauri ni vyombo vya kutekeleza shughuli za maendelo.

Kwa hiyo, ilimradi sasa Nkinga itakuwa ni Halmashauri, lazima kuwepo mgawanyo wa mali kati ya Muheza na Nkinga na kwa kawaida zoezi hilo linasimamiwa na Halmashauri yenyewe na mkiona kuna mvutano, tuambieni tutaleta wataalamu waweze kusaidia kuleta hali ya haki miongoni mwa Halmashauri hizo mbili.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Philip Marmo, alitaka kujua maombi ya usajili wa uandikishaji wa vijiji vipya yanashughulikiwaje. Sasa hili bahati nzuri limeelezwa na limekuwa likielezwa sana. Lakini naomba nimhakikishie Mheshimiwa Marmo kwamba tumeshapokea maombi ya vijiji vingi sana, sikumbuki vizuri kama na lile la kwake lipo. Lakini, tutajaribu ku-*check* tuone kama yaliwasilishwa, lakini bado mimi nasema hata kama hayajawasilishwa, bado kwa maeneo haya tunasema tutayapokea tu, kazi yetu ni kuyachambua na kuona kama yanakidhi vigezo na hatimaye kuwasilisha kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa mapendekezo tutakayokuwa tumeona yanafaa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Galinoma, alitoa hoja moja nzuri kwamba sheria ya Serikali za Mitaa kifungu cha 74(2) ipitiwe upya ili Wenyeviti wa Kamati zote za Halmashauri zote waruhusiwe kuingia katika Kamati ya Fedha/Mipango/Utawala. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Galinoma, labda kama ana jambo lingine ambalo alikuwa nalo wakati anahoji jambo hili, wenyeviti wote wa Kamati za kudumu pale ni wajumbe na Manaibu Meya na Makamu wenyeviti nao ni wajumbe. Mbunge anayewakilisha Jimbo hilo naye vilevile ni mjumbe katika Kamati hiyo. Lakini kama iko Kamati ambayo pengine anahisi tumeiacha, mimi nitashukuru sana akiniambia ili tuweze kutoa ufafanuzi kwa Mkurugenzi mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Marmo vile vile aliuliza kama zile shilingi milioni 10 wanazodaiwa na Bodi ya Mikopo kama kweli ni halali au hapana! Nadhani alihisi kama vile tunaionea Halamashauri yake. Naomba nimhakikishie kwamba ni kweli wanadaiwa. Mkopo huo ni wa mwaka 1999 na ulikuwa wa shilingi milioni 21,640,000/=. Mkopo huo ulitokana na lile lile nililokuwa nalisema, mgawanyo wa Halmashauri mbili. Kwa hiyo, unarithi mali, lakini unarithi na madeni vile vile, hivyo, nao walirithi hilo deni, wakaja wakalipunguza kidogo. Nimwombe tu Mheshimiwa Marmo, chonde chonde tujitahidi tumalize hilo deni ili lisije tena baadaye likakosesha uwezekano wa kupata.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Marmo vilevile alisema tumefanya uhamisho wa watumishi pale kwenye Halmashauri yake, lakini inaonekana tumekuwa *slow* kujaza nafasi. Tunakiri, tuliondoa watumishi wane, lakini walipata uhamisho. Kwanza, niipongeze Halmashauri wote walipata uhamisho kwa sababu walipandishwa vyeo. Kwa hiyo, Halmashauri yake iliweza kutoa watumishi ambao walionekana ni bora, wanaweza kuchangia huko mbele ya safari. Tumekwishampelekea Afisa Maendeleo ya Jamii na Afisa Kilimo Mwandamizi lakini tutajitahidi kuharakisha kujaza nafasi hizo ambazo bado.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Aloyce Kimaro, alisema jambo moja ambalo ni zuri, kwamba Serikali za Vijiji zitoe taarifa za mapato na matumizi ya fedha zitolewazo na Serikali. Alilosema Mheshimiwa Kimaro ndilo tunalolifanya na mimi naomba nirudie

kwa nguvu sana, Waheshimiwa Wabunge tusaidieni. Ni jukumu la Serikali za Vijiji kutoa taarifa zote zinazohusiana na mapato na matumizi ya fedha katika maeneo yao. Tumekuwa tukilisema sana wekeni taarifa hizo kwenye mbao za umma ambapo panaonekana wazi ili kila mwananchi aone nini kinaendelea.

Lakini wakati mwingine ni kweli kuna kuficha ficha na hasa Mtendaji anapokuwa kidogo anajua akilisema litamletea tatizo. Lakini wajibu wetu ni kuwaumbua hawa wote ambao hawatimizi wajibu wao vizuri.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia, alihoji juu ya uwajibikaji wa viongozi wakuu katika Wilaya na kwamba Viongozi wakuu katika Wilaya wasikae katika kituo cha kazi kwa muda mrefu. Nina hakika kwamba Mheshimiwa Prof. Mtulia analijua hili. Tumejitahidi sana, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Rais, kila inapowezekana *DC* akikaa muda ambao nafikiri amezoeleka mno, basi tumekuwa tunajitahidi kuwabadilisha ili akaonyeshe uwezo wake tena katika sehemu nyingine. Kwa hiyo, kwa viongozi hawa ni dhahiri kabisa kwamba tunalifanya hilo kwa nia nzuri. Lakini nataka niseme wako vilevile Wabunge wanaotuambia msimwondoe huyu, mzuri sana, *DC* huyu asitoke na Mkurugenzi asitoke, wakati upande mwingine mnasema wanakaa mno. Kwa kweli tunajaribu ku-*balance*, pale tunapoona uko umuhimu, tunafanya. Sehemu nyingine tunafumba macho, mnabaki na viongozi hao, wakati huo huo tukiona wamechoka, ni vizuri ukalisema. Lakini nataka niwambie Mheshimiwa Prof. Mtulia kwamba kila kiongozi ndani ya Halmashauri, ndani ya Wilaya, anajua hawezi kukaa nje ya kituo siku zinazozidi kiwango kinachotakiwa, vinginevyo inabidi apate kibali maalumu kwa sababu huduma kwa wananchi ni muhimu zaidi kuliko hayo mambo yake mengine yanayomtoa hasa kama ni mambo ya binafsi linakuwa si jambo la busara sana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lekule Laizer, alisema kuwa Serikali iongeze fedha za bajeti ya Wilaya ya Longido. Kwa Mwaka wa Fedha 2007/08 Serikali imetenga kiasi cha Shs. 300,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya Halmashauri na Sh.502,614,000/= kwa ajili ya Matumizi ya kawaida kwa kuanzia. Vilevile Ofisi ya Mkuu wa Wilaya kwa Mwaka wa Fedha 2007/08 imetengewa kiasi Sh. 114,000,000/= kwa ajili ya Matumizi mengineyo ambayo ni ongezeko la zaidi ya asilimia 100 ya bajeti ya mwaka 2006/07. Jumla ya Sh. 195 milioni zimetengwa chini ya Bajeti ya Maendeleo kwa ajili ya ujenzi wa ofisi na nyumba ya Mkuu wa Wilaya. Kwa hiyo, tutaendelea kuisaidia Wilaya hiyo kwa kadri ya uwezo utakavyokuwa unapatikana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro amehoji vilevile kwamba Serikali ifanye mpango wa kuipatia Wilaya mpya ya Mkinga watumishi wenye uwezo, hasa Mkurugenzi, pamoja na watumishi wengine mbalimbali. Tutalizingatia. Tunatambua ni Wilaya mpya na tunajua vilevile tunampa Halmashauri mpya. Tutajitahidi kutimiza azma hiyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri alizungumzia suala la Serikali izipe kipaumbele Halmashauri mpya. Tunakubaliana naye na tutajitahidi sana. Lakini nataka niseme vilevile kwamba Serikali imetenga kwenye Halmashauri yake shilingi 200,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya Halmashauri mpya ya Siha, shilingi. 429,000,000/= Matumizi Mengineyo na Shilingi 2,579,220,000 kwa ajili ya

Mishahara. Vilevile Serikali itaendelea kutenga fedha kwa kadri ya uwezo utakavyoturuhusu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Meryce Emmanuel naye alirudia suala la Zahanati na Vituo vya Afya lianze kwa mwaka 2010. Nimelieleza hili hapo awali, naomba kurudia tu kwamba ni azma ya Serikali na Mheshimiwa Waziri Mkuu aliliweka vizuri kwamba kwa mwaka huu wa fedha, hatujengi Vituo vya Afya na Zahanati, tutaboresha kwanza vilivyopo na itatupa nafasi vilevile ya kujiandaa sasa kwa bajeti itakayofuta ambayo ndiyo tunadhamiria kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Peter Serukamba pamoja na Mheshimiwa Stephen Galinoma, walitamani suala la ugatuaji madaraka, kwa maana ya Elimu na Afya, libaki kwa sekta husika. Naomba tu nirejee nilichosema juzi kwamba TAMISEMI kwa maana tuna Halmashauri zenye watu, hawa ni watekelezaji wa yote yanayotoka Serikali Kuu ambayo yanatokana na Chama cha Mapinduzi. Sisi hatutungi sera, sisi hatu-*train* watu kwa maana ya kuandaa watu wenye taaluma kwa sababu taaluma hizo hatuna. Fedha zinatengwa kutoka Serikali Kuu, kwa hiyo, jukumu langu mimi kama kiongozi wa TAMISEMI ni kusimamia zile Halmashauri kutekeleza yanayofanyika. Ujenzi wa madarasa ni jukumu letu, ujenzi wa Zahanati ni jukumu letu, na kadhalika. Bado Wizara ya Elimu, Wizara ya Afya na Wizara nyingine zote, zina kauli kubwa tu juu ya mambo yanayoendelea kwenye Halmashauri kwa sababu ndio wanaotoa fedha na lazima waridhike kwamba fedha hizo zinatumika. *Collectively,* sisi wote kama Serikali, wajibu wetu wote umeziandama Halmashauri. Kwa hiyo, sioni kama kuna mahali tunasigana sana kiasi cha kufikiri kwamba pengine ingekuwa hivi, kwa sababu hata nikisema zirudi huko bado yatakayoamuliwa huko lazima nije nitekeleze mimi kwenye ngazi ya Wilaya. Kwa hiyo, ni kitendawili, lakini tunadhani tulivyokuwa tukiamua pengine si vibaya sana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, anasema Watumishi waliosimamishwa na Halmashauri ya Kigoma na baadaye walirejeshwa na TAMISEMI na wakahamishiwa vituo vingine. Yako mambo yaliyojitokeza kwenye Halmashauri hiyo:- Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma ni kweli liliwasimamisha kazi Mkurugenzi Mtendaji, Afisa Elimu, Mganga Mkuu, Mhandisi wa Maji na Afisa Kilimo (W), katika kikao chake cha kawaida cha tarehe 25/04/2006. Zilikuwepo tuhuma mbali mbali za ubadhirifu, ufujaji wa fedha n.k. Tatizo lilipoibuka, kwanza, walikiuka utaratibu kwa maana kwamba mnapoamua sasa kuwachukulia hawa hatua kwa utaratibu waliofanya, ni lazima Baraza lile kwanza liketi kama Kamati, lisiendelee kuketi kama Baraza, mkae kwanza kama Kamati ili muweze kufanya kazi ya kusimamia masuala ya nidhamu, hili kwa bahati mbaya halikufanyika. Pili, Halmashauri hiyo, tulilazimika kuingilia kati kwa sababu kazi yangu pamoja na wataalam wangu vile vile ni kutenda haki kwa watumishi ambao wako kule. Kwa sababu hiyo, ililazimika tuingilie kati ili utaratibu ufuatwe.Kwa hiyo, tumefanya hilo jambo na wale wote waliotakiwa kuchukuliwa hatua tumekwishaamua kuzichukua na wala si kwamba baada ya pale tukawahamisha tu kienyeji, hapana! Wote walishughulikiwa kwa mujibu wa taratibu, tumewachukulia hatua zinazostahili. Nataka kumhakikishia kwamba juhudi hizo zimefanywa na kama ambavyo tumekuwa tukisema, kamwe hatuwezi kukubali mbovu basi akaachwa hivi hivi bila kuchukuliwa hatua.

Kwa hiyo, kati ya Watumishi 8 waliotuhumiwa na kufunguliwa mashtaka, wawili iliamuliwa wafukuzwe kazi, wengine 5 walionywa baada ya kupima uzito wa matatizo waliyokuwa nayo. Mmoja suala lake ilibidi lipelekwe Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa sababu uko utaratibu ambao kwa upande wa walimu inabidi ushughulikiwe chini ya utaratibu huo. Lakini vilevile kwa sababu Halmashauri ilikuwa imeazimia Mkurugenzi afukuzwe kazi na kwa sababu nilizozieleza, ilibidi baada ya kulifanyia uchambuzi tuliamua kumvua madaraka. Kwa hiyo, tukamwondoa kwenye Ukurugenzi na tukamtoa pale kumweka kwenye kazi za kawaida kwa kuwa uwajibikaji ndio ulikuwa tatizo kubwa katika eneo lile.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Brig. Gen. Ngwilizi, alileta rai nzuri sana juu ya upigaji muziki ovyo na makele makubwa Jijini Dar es salaam. Naomba niseme tu kwamba jambo hili si dogo, ni kubwa. Kubwa kwa sababu burudani nayo ni sehemu ya maisha, watu lazima tupate muda kidogo wa kupata burudani kwa upande mmoja, na pengine hasa kwa vijana itakuwa kwa kweli mtu ukisema upige marufuku miziki yote leo, nadhani utaleta kizaazaa kikubwa sana. Kwa hiyo, ni lazima twende vile vile kujaribu ku-*balance* jambo hili. Kwa kweli baada ya kupata taarifa hii, tulichofanya, tulikutana na Wakuu wa Mikoa pamoja na Mheshimiwa Khatib ambaye ndiye Waziri wa Sekta inayohusika.

Tumelizungumza jambo hili kwa kirefu lakini tumegundua kwamba ziko sheria zinazoingiliana sana katika eneo hili. Vilevile tumegundua kwamba baadhi ya kumbi ambazo zinalalamikiwa sasa, wananchi ndio wamezifuta kwa sababu zilipojengwa ilikuwa ni pembeni halafu tukaruhusu majengo, sasa imegeuka tena kuwa kero. Lakini, wako vile vile ambao wameamua kugeuza nyumba za makazi kuwa ni kumbi za starehe. Kuna mkanganyiko wa mambo mengi ambayo tumeona ni vizuri basi tuunde a *joint team* kati ya Wizara hizi mbili, tulifanyie uchunguzi wa kina na kisha tutatoa ushauri kwa Serikali kwa kadri itakavyowezekana. Lakini tuliona vile vile kama nilivyotangulia kusema, pengine kwa sasa jambo ambalo nafikiri linawiana na jambo hili, tukubaliane tu kwamba kwa wale wote ambao wanapiga muziki hasa katika *open bars*, ni vizuri wakafanya hiyo shughuli kwa sauti ambayo ni *manageable*. Sasa tutaziomba Halmashauri zijaribu kusimamia hilo wakati tunatafuta ufumbuzi wa kudumu. Lakini baadae tulimwomba Mheshimiwa Khatib alitolee kauli rasmi jambo hili ili tuweze kupata maelezo ambayo yatatusaidia zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Paul Kimiti, alihoji juu ya watumishi wa Halmashauri yake ya Manispaa ya Sumbawanga ambao anasema kwa kweli ndio chanzo cha kukosa fedha za ruzuku ya maendeleo. Tunataka tumwambie kwamba watumishi 6 wamekwishachukuliwa hatua za kinidhamu kwa sababu walikiuka taratibu mbalimbali za usimamizi wa fedha na tutahakikisha jambo hilo linakwenda kwa kasi zaidi ili tuweze kuharakisha kulimaliza. Mheshimiwa Kimiti vilevile alitaka kujua kama tumetimiza ahadi yetu ya kutoa fedha kidogo kwa ajili ya kutoa gari la Zimamoto. Manispaa wanalo gari la zimamoto, lakini nadhani hoja yake anaona gari lile dogo. Nakuomba Mheshimiwa Kimiti, chonde chonde ndugu yangu, ni bora hicho kidogo ulichonacho, kwa kuwa wengine hata hicho kidogo hawana. Uwezo tulioupata wakati huo, ndio

ukatuwezesha kutoa gari hiyo pamoja na kwamba tunajua si kubwa kama yale magari makubwa. Lakini kadri uwezo utakavyoongezeka, tutafanya hiyo kazi kwa uhakika zaidi. Vilevile Mheshimiwa Kimiti aliomba juu ya suala la ujenzi wa lami katika Halmashauri yake. Kwa hiyo, kwa mwaka wa fedha 2007/2008 tumetenga shilingi milioni 300, tunadhani zitasaidia kidogo kuondoa baadhi ya vumbi katika Manispaa yake ya pale Sumbwanga.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Nuru Bafadhili, alikuwa amehoji Bunge lako hili kuhusiana na Mgombea aliyeshinda Kiti cha Udiwani *Old* Korogwe na kwamba hajaapishwa. Aliniambia kwanza kabla, tukalifanyia kazi. Lakini bahati nzuri ameshaniletea ki-*note*, amekwishapata maelezo.

Ni kweli tuliona kulikuwa na upungufu katika jambo hilo kwa sababu lilikuwa Mahakamani, bahati nzuri Mahakama imekwishaamua na amenihakikishia yeye mwenyewe kwamba Jumatano, Diwani huyu atakuwa anarejea tena katika nafasi yake. Ataingia katika nafasi yake ya Udiwani na ataapishwa kulingana na utaratibu ulivyo.

Mheshimiwa Spika, na pengine niongezee kusema kwamba naomba sana Halmashauri hizi tujitahidi sana kuzingatia sheria, tusiwe tunazua kesi nyingine ambazo unakuta hazina msingi. Imetokea hivyo Tanga, imetokea hivyo Kigoma na sehemu zote tumebaini kwamba ni kwa sababu tu ya kutoshauriwa *properly* sheria inasema nini, na kwa hiyo mamlaka ya Halmashauri iweje. Hoja si Diwani wa Upinzani kutoka, hapana! Hoja ni kwamba kama anatoka atoke kwa utaratibu wa kisheria, hilo ndilo jukumu nililopewa na lazima muda wote tulizingatie.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tuhuma dhidi ya Afisa Mipango Miji wa Jiji la Tanga, tunalipokea hili suala, tunalijua, tumekuwa tunalifanyia kazi, baadae tutampa maelezo ya kina juu ya hatua mbalimbali zilizochukuliwa kwa huyu Afisa Mipango Miji. Kwa hiyo, tunaomba tu afanye subira wakati tunakamilisha hilo zoezi.

Mheshimiwa Dr. Slaa amesema kwamba Serikali iangalie utaratibu wa *trams* na *underground railway sytem*. Tunapokea ushauri wake na ni sehemu ya mpango mzima wa juhudi za Serikali katika eneo la Dar es salaam. Vilevile alisema tuwe na mpango maalumu wa kuongeza maghorofa ya kuegesha magari. Bahati nzuri jambo hili tumekwishalianza. *NSSF* wanayo, *PPF* jengo wanalo, *DICC* vilevile tumeweka hiyo huduma. Lakini rai yake ni ya msingi sana na tutaendelea kushirikiana na sekta zinazohusika, kwa uwekezaji wa majengo basi nalo lizingatiwe.

Mheshimiwa Dr. Slaa vile vile alisema Mikakati ya kukabili changamoto ya msongamano wa magari lisiwe suala la Dar es Salaam tu bali tuzingatie kwa maeneo mengine tunalipokea na tutatoa maelekezo kwa majiji mengine yote ambayo tumekuwa tukifanyakazi nao kwa karibu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Raymond, amesema Miji yote iendelezwe hatua kwa hatua ili kuepuka matatizo tunayopata hivi sasa. Tunakubaliana na rai yake na kwa kweli sababu mojawapo ya kutangaza zile mamlaka za Miji midogo ilikuwa ni kwanza

kuruhusu sana Mamlaka hizo kuanza kuingia katika utaratibu wa Mipango Miji tusingoje mpaka mambo yameharibika. Kwa hiyo, tunadhani kama alivyosema Naibu Waziri asubuhi hii, Halmashauri zote zikitekeleza vizuri uamuzi ule tutakuwepo na mabadiliko mazuri kuhusiana na ujenzi sasa unaofuata sheria.

Kodi za majengo hazikusanywi ipasavyo *TRA* ikusanye ushuru wa majengo *(property tax).* Tumelikubali ni wazo zuri sisi wenyewe tulikuwa tumeanza kulifikiria hivyo kwa hiyo tutashirikiana na Manispaa pamoja na *TRA* tuweze kuboresha kiwango cha makusanyo katika eneo hili la *property tax*. Uendeshaji wa Kamati za Ushauri wa Wilaya na stahili zake aliliulizia sana Mheshimiwa Msambya. Tumemuelewa. Lakini asiwe na mashaka kwamba tutaendeshaje kamati zile, zitaendeshwa kwa utaratibu wa kawaida kupitia Bajeti ya Mkoa ambao ndiyo watasimamia katika ngazi ya chini.

Ujenzi wa Ofisi za Mitaa, nataka tu niseme mama Wambura kwamba kwa bahati nzuri Halmashauri nyingi nilizotembelea tayari wameshaanza kujenga Ofisi za Kata. Mfano mzuri ni Dar es Salaam. Lakini hata ukija Mpanda utakuta tumejitahidi sana. Mbinga nimeona vile vile wamejitahidi sana. Kwa hiyo, kwa kweli jukumu la kujenga ofisi za kata kwa ajili watendaji wao ni jukumu la Halmashauri na wakitumia *resources* zilizopo ni jambo linawezekana kabisa bila matatizo yoyote. Kwa hiyo, mimi nidhani tuhimize Serikali hizo ziweze kutimiza wajibu wao.

Mheshimiwa Spika, Uwekaji wa taa za Barabarani katika Manispaa ya Mtwara tumelipokea. Lakini nataka niseme Mtwara nao wanao wajibu wa kufanya hiyo kazi, kama tutaibua miradi nikwa ajili ya kusaidia lakini kwanza kabisa wenye kilio ni wao wenyewe. Ujenzi wa Barabara za lami katika Manispaa, ya Dodoma kama Makao Makuu, aliuliza Mheshimiwa Mfaki. Serikali kwa kuzingatia umuhimu wa Mji wa Dodoma mwaka 2006/07 ilijenga Km. 1 ya lami kwa Tshs. 200.0 milioni. Sasa najua nikisema kilomita 1 mtasema nayo unajivunia nasema si haba. Hata hiyo Kilomita moja haikuwepo. Mwaka wa fedha 2007/08 tumetenga Sh. 332 milioni, kwa ajili ya matengenezo sasa ya kawaida. Lakini vile vile Serikali imetenga Sh. 450.0 milioni kwa kujenga Km. 3.3 za lami. Vile vile imetenga Sh. 273.0 milioni kwa ajili ya matengenezo ya muda maalum kwa barabara za changarawe km. 18. Serikali itaendelea kuona umuhimu wa kuendeleza Manispaa yetu ya Dodoma hasa katika sekta ya miundombinu jambo ambalo ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Makato ya mishahara kwa watumishi wa Halmashauri Mheshimiwa Kigwalilo alitaka kujua kuna mkono Serikali hivi pengine kwamba sisi ndiyo tunatoa maagizo hayo nasema la hasha, hakuna mkono wa Serikali na naomba niseme hapa hakuna mtumishi anayeweza kukatwa mshahara wake kama hakutoa ridhaa yeye mwenyewe maana hilo ni *fundamental aspect* ambayo lazima izingatiwe. La sivyo yatakuwa ni mambo ambayo Serikali kwa ujumla wake pengine imetoa maelekezo ambayo yanaeleweka na yako bayana kabisa, vinginevyo haturuhusu jambo jingine nje ya utaratibu huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kigwalilo vile vile alihoji Makamu Mwenyekiti kwamba kwa nini asigombee kwa mara ya pili kama anaona inafaa. Naomba niliseme hili na kwa Waheshimiwa Wabunge wote ni vizuri mkalijua Makamu Mwenyekiti, Naibu

Meya, ruksa kugombea nafasi hiyo kwa mara ya pili kama anataka. Sheria haimkatazi hata kidogo na ni vizuri Halmashauri zikajua hilo kwa sababu wakati mwingine mnataka kuwanyima watu mnawawekea tu mikwala pengine kwa sababu za binafsi lakini kwa mujibu wa Sheria zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lyamba mgogoro kati ya Mamlaka ya Maji Mikumi tunaufahamu naomba utupe muda tulifanyie kazi kidogo baadaye tutakujibu vizuri sana kwa maandishi juu ya matokeo uliopo pale ambao kidogo ni wa muda mrefu kati ya mamlaka na uongozi.

Barabara ya Mlalo – Mbaramo ni mbaya. Sh. 66 milioni zilitolewa lakini hazikutengenezwa kutokana na kukosa kibali cha kupitishia barabara hiyo katika msitu wa Shaguyu. Mheshimiwa Ngwilizi naomba niseme kwamba barabara ya Mlalo yenye urefu wa 15 ni kweli ilitengewa kiasi hicho cha fedha, fedha hizo zimetengeneza barabara yaani kwa maana ya *new contraction* yenye urefu wa kilomita 3.3. Kwa hiyo, tutaendelea kuzidi kuisaidia Halmashauri hiyo kwa kadri itakavyowezekana. Kwa mwaka huu Wilaya ya Lushoto imetengewa shilingi 335,000 milioni kwa ajili ya matengenezo ya barabara kwa ujumla. Kwa hiyo, jaribu kutumia fursa hiyo vile vile kuona kama unaweza ukachukua hela kidogo pale ukapeleka kwenye hiyo barabara.

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Felix Kijiko katika maelekezo yake ametuambia juu ya jambo moja linaloendelea katika eneo lake. Mifugo iliyoondolewa ndani ya hifadhi ya Moyowosi Kigosi Wilaya ya Kibondo hisia ni kana kwamba pengine anaona kama kuna tatizo hivi lakini nataka niseme tu dhahiri kwa ni kosa kwa mifugo kuingia kwenye eneo lolote ambalo ni hifadhi. Kwa hiyo, wajibu wa Serikali ilikuwa ni kuwakamata vatu wale wote waliohusika na kuingia au kukaidi sheria hiyo na wako 7 pamoja na mifugo yao na wote hao wamepelekwa mahakamani. Kwa hiyo, mimi nafikiri Mheshimiwa Kijiko, fanya subira tu tuone mahakama itakavyoamua. Wakitiwa hatiani ndiyo basi tena wanayo ruksa ya kuweza kukata rufaa.

Pia Mheshimiwa Lucy Owenya, ameulizia juu ya taa za barabarani na ambazo nyingi anasema hazifanyi kazi, bahati nzuri Naibu Waziri, amejaribu kulieleza hili. Lakini nataka nimhakikishe kwamba kwa Jiji la Dar es Salaam tumedhamilia kufanyakazi kwa kiasi kikubwa sana chini ya mradi ule wa jumla lakini vile vile kutokana na juhudi za makusudi katika baadhi ya maeneo.

Serikali iweke utaratibu wa kuwa na Naibu Mkurugenzi, hili limeshazungumzwa tayari. Serikali iandae utaratibu mzuri wa kuwapatia usafiri wanafunzi katika Jiji la Dar es Salaam. Hili litakwenda sambamba na mradi mzima ambao tunakwenda nao wa kuboresha suala zima la miundombinu Dar es Salaam. Kwa hiyo, naomba tu nimwombe Mheshimiwa Riziki Juma, pamoja na Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al – Oassmy, kama alivyosema Waziri Mkuu katika ukurasa wa 20/23 hili litakabiliwa vizuri zaidi chini ya utaratibu huo.

Hospitali ya Wilaya ya Misungwi Mheshimiwa Shibiliti chonde naelewa tatizo lako na bahati nzuri nilifika pale. Lakini bado uwezekano wa Serikali si mkubwa sana kuweza kukupa ahadi ya uhakika. Lakini wewe na mimi tumekuwa karibu sana katika

matatizo mbalimbali. Nafikiri tuendelee kulizungumza hili kwa sababu halikutengewa Bajeti, tunaweza pengine tukafika mahali tukaona kama kuna ufumbuzi. Upungufu wa wahandisi wenye sifa katika Halmashauri. Kwa sasa Mheshimiwa Kimbita hali iko hivi, Halmashauri 112 kati ya 122 zina wahandisi wenye yaani shahada na stashaha ya juu. Kwa hiyo, Halmashauri 10 ndiyo bado tunadaiwa kuweza kuboresha na kuwapa watu wenye sifa na juhudi zinaendelea nina hakika tutafanikiwa. Lakini nataka nirudie kusema kuwa na sifa hizo siyo hoja kubwa bado ni uadilifu na usimamizi wa karibu wa watumishi wetu katika Halmashauri zetu.

Pia Mheshimiwa Benson Mpesya barabara ya *Airport* Iyela km 1 unataka ijengwe kwa kiwango cha lami sawa, mwaka 2007/2008 tumekutengea milioni 300 kwa ajili ya barabara hiyo. Naamini itasaidia kidogo. Halafu Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya alitaka upelekaji wa madaraka uende sambamba na uwezeshaji. Tunaipokea rai yake tumekuwa tukijaribu kulifanya hilo tutaendeleza juhudi hizo na ndio maana unaona fedha nyingi sasa zinakwenda huko kwa kuwa ndiyo uwezeshaji wenyewe tunaouzungumza. Lakini vile vile tunaimarisha mafunzo kwa ngazi mbalimbali.

Halmashauri ya Kasulu kupewa hadhi ya Mamlaka Mheshimiwa Nsanzugwanko. Naomba nikuambie tu kwamba Kasulu tayari ni Mamlaka ya Mji mdogo tangu mwaka 2004. sasa nadhani alichokuwa anatafuta ni kwamba anataka iwe Halmashauri ya Wilaya, basi tutimize kwanza hii awamu ya kwanza tuona mtakavyojitahidi tutaona sasa kama hizo sifa nyingine mtaweza kuzipata. Halafu Mheshimiwa Kimbau, ulitaka watendaji wanaotoa taarifa zisizo sahihi wachukuliwe hatua, tumepokea rai yake kuhusiana na Korogwe tutalifanyia kazi. Mheshimiwa Kimbau vile vile alitaka Madiwani watembelee miradi mbalimbali. Tumelipokea tumekuwa tukitoa maelekezo tutaendelea kulisukuma kwa kadri itakavyowezekana.

Pia Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, anataka Serikali itoe fedha nyingi kwa Wilaya ya Mkinga, nimelisema kidogo lakini nataka nikuahidi tutaongeza kasi kwa sababu tunajua unahitaji sana fedha kwenye eneo hilo. Serikali ifanye ufuatiliaji fedha za UKIMWI zinazopelekwa kwenye Halmashauri, tumekuwa tukifanya lakini tutaendelea kulitazama kwa karibu zaidi kwa kuwa ni jambo la msingi sana na si fedha hizo tu lakini fedha zote kwa ujumla wake. Pia Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim amesema minada iimarishwe juhudi zipo tutaendelea kuimarisha na nafikiri Waziri wa Mifugo, atalieleza vizuri zaidi. Serikali ikarabati mabwawa kwa ajili ya kuimarisha kilimo cha umwagiliaji ameuliza Mheshimiwa Teddy Kasella – Bantu liko chini ya *ASDP* na mimi nina hakika Waziri wa Kilimo atapata nafasi pengine ya kulieleza vizuri zaidi.

Mheshimiwa Samson Mpanda maandalizi mazuri kwenye maeneo inakohamia mifugo tulishajitahidi na kama mtakavyokumbuka tulikuwa tumetenga milioni 150 kwa ajili ya kuanza kutengeneza miundombinu nina hakika Waziri wa Maendeleo ya Mifugo atajitahidi kulieleza.

Uimarishaji wa hifadhi ya mazingira katika maeneo ya ufukwe ni *agenda* ya kudumu na tutaendelea kuifanyia kazi muda wote. Kwa upande wa hospitali ya Songea Mama Manyanya kwa mwaka wa fedha 2007/2008 tumetenga milioni 600 kwa hiyo nina hakika zitakusaidia sana. Mhandisi vile vile alitaka juhudi ziendelee kuhimiza wananchi

kuendelea kutekeleza miradi ya kujitolea, kama nilivyosema ni pamoja elimu na ujenzi wa afya tumepokea ushauri wake tutaendelea kuimarisha.Uondoaji wa taka katika jiji ni *agenda* ya kudumu na tutaendelea kuliendeleza kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema basi naomba kwa mara nyingine niunge mkono hoja hii kwa asilimia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mizengo Pinda, sasa nitamwita mtoa hoja Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, anazo dakika 50 kama hazitatosha basi tutaona utaratibu mwingine tutakaoweza tutatumia. Karibu sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniangalia kwa jicho la huruma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kupata nafasi kuhitimisha hoja iliyojadiliwa takriban kwa siku tano na kwa umakini na umahiri wa juu sana. Napongeza wote walijadili hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na mimi kwa masikitiko makubwa, napenda kutoa salaam za pole kwa ndugu, jamaa na marafiki kwa kifo cha Marehemu Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia. Naamini tutakubaliana kuwa Taifa limempoteza kijana mchapakazi na kiongozi mahiri aliyejitolea kwa hali na mali kulitumikia Taifa lake. Nawaomba wote tushirikiane kwa kila mmoja kwa imani yake tumwombee Marehemu Amina ambaye ametangulia mbele ya haki ili Mwenyezi Mungu aiweke Roho yake Mahali Pema Peponi. Aidha, tuwaombee ndugu, jamaa na marafiki hasa wazazi wake ili Mwenyezi Mungu awape nguvu ya kustahimili msiba huu mzito.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa pongezi zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, wakati wa kuchangia hoja hii. Pongezi hizo zinatupa nguvu ya kufanyakazi zetu kwa nguvu zaidi. Ahsante sana kwa pongezi zenu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja hii imechangiwa na jumla ya Waheshimiwa Wabunge 166. Kati ya hao wabunge 80 wamechangia kwa kuzungumza na 86 wamechangia kwa maandishi. Waliochangia kwa kuzungumza na kwa maandishi ni kama ifuatavyo:

Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Grace S. Kiwelu, Mheshimiwa Christopher Ole - Sendeka, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe, Mheshimiwa Estherina J. Kilasi, Mheshimiwa Emmanuel J. Luhahula, Mheshimiwa Vedastusi M. Manyinyi, Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', Mheshimiwa James D. Lembeli, Mheshimiwa Eustace O. Katagira, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, Mheshimiwa Joyce M. Masunga, Mheshimiwa Kaika S. Telele, Mheshimiwa Ania S. Chaurembo na Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Aziza S. Ali.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Capt. John D. Komba, Mheshimiwa Salum Ally Salum, Mheshimiwa Benedict K. Losurutia, Mheshimiwa Luhaga J. Mpina, Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Ramadhani A. Maneno, Mheshimiwa Said Amour Arfi na Mheshimiwa George Mkuchika, Mheshimiwa Halima O. Kimbau, Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Mheshimiwa Mbaruk K. Mwandoro, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Suleiman O. Kumchaya, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge, Mheshimiwa Meryce M. Emmanuel, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Phares K. Kabuye, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Dunstan D. Mkapa, Mheshimiwa Kassim Issa, Mheshimiwa Teddy L. Kasella – Bantu, Mheshimiwa Haroud S. Masoud, Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nkayamba, Mheshimiwa Brig. Hassan Ngwilizi na Mheshimiwa Idd Mohamed Azzan,

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mheshimiwa Mariam R. Kasembe, Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye, Mheshimiwa Shally J. Raymond, Mheshimiwa Manju S. O. Msambya, Mheshimiwa Abdul Jabiri Marombwa, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mheshimiwa John Shibuda, Mheshimiwa Florence E. Kyendesya, Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu, Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Dr. Luka J. Siyame, Mheshimiwa Celina C. Kombani, Mheshimiwa Dr. Batilda S. Burian na Mheshimiwa Mizengo K. Peter Pinda. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa Sevelina Mwijage, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa Wilson M. Masilingi, Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya, Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Fred M. Tungu, Mheshimiwa Mustafa H. Mkulo, Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Charles O. Mlingwa, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Felix N. Kijiko, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mheshimiwa Dr. Guido G. Sigonda, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi, Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Juma S. Omar, Mheshimiwa Emmanuel J. Luhahula, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Mgeni J. Kadika, Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mheshimiwa Philip S. Marmo, Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mheshimiwa Benedict Losurutia, Mheshimiwa Janet Massaburi, Mheshimiwa Lekule M. Laizer, Mheshimiwa

Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mheshimiwa Paul P. Kimiti na Mheshimiwa Mwaka A. Ramadhan.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Charles M. Kajege, Mheshimiwa Dr. Samson F. Mpanda, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Hadija Saleh Ngozi, Mheshimiwa Mwanahamis Kassim Said, Mheshimiwa Masolwa C. Masolwa, Mheshimiwa Faustine K. Rwilomba, Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, Mheshimiwa Devota M. Likokola, Mheshimiwa Mohamed Ali Said, Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili, Mheshimiwa Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfan, Mheshimiwa Haji, Mheshimiwa Martha J. Umbulla, Mheshimiwa Damas P. Nakei, Mheshimiwa Laus O. Mhina, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassmy Mheshimiwa Ali S. Salim, Mheshimiwa Mohamed R. Abdallah, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Manju O. Msambya, Mheshimiwa Anastazia J. Wambura, Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki, Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga, Mheshimiwa Hassan C. Kigwalilo na Mheshimiwa Clemence B. Lyamba.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge hawa kwa michango yao na narudia tena kwa pongezi zao walizozitoa kuhusu hoja niliyoiwasilisha.Kutokana na muda niliopangiwa haitawezekana kutoa majibu kwa hoja zote zilizotolewa. Nawahakikishia kwamba hoja hizo na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge umezingatiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri wa Nchi, Mheshimiwa Mizengo Pinda, (Mb) Mheshimiwa Dr. Batilda S. Burian, (Mb) na Naibu Mawaziri Mheshimiwa Celina Kombani, (Mb) na Mheshimiwa Dr. Luke Siyame, (Mb) waliochangia na kutoa maelezo na ufafanuzi wa kina na hivyo kujibu baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge, kuwa hoja zote zinazohusu sekta mbalimbali zimewasilishwa rasmi kwa Waheshimiwa Mawaziri wanaohusika na watazijibu wakati watakapokuwa wanahitimisha hoja za Wizara zao. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo naomba sasa nianze kupitia baadhi ya hoja ambazo zilijitokeza wakati wa mjadala. Ningependa kuanza na ugawaji wa rasilimali za taifa mikoani. Hoja ilikuwa ni kwamba Mikoa ambayo ipo nyuma kimaendeleo izidi kupewa kipaumbele katika Bajeti ya Taifa. *(Makofi)*

Wabunge waliochangia hoja hii ni Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa Halima Mdee Mheshimiwa Said Nkumba na Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, hao watano.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kugawa rasilimali kwa Mikoa yote Tanzania kwa kuzingatia vipaumbele vya kitaifa, usawa na pia kuzingatia maeneo yaliyo

na mahitaji maalum. Kutokana na hitoria ya nchi yetu kwamba ipo baadhi ya Mikoa ambayo inaonekana iko nyuma kimaendeleo hasa kutokana na miundombinu duni kama vile barabara, umeme na mawasiliano. Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuongeza viwango vya fedha vinavyotolewa kwa Mikoa hiyo ili kuongeza kasi ya maendeleo. Mikoa ninayoizungumzia ni Kigoma, Rukwa, Tabora, Lindi, Mtwara na Ruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, katika Bajeti ya maendeleo ya Mkoa wa Kigoma, kwa mwaka 2006/2007 ilikuwa ni shilingi bilioni 3.44 ikilinganishwa na shilingi bilioni 12.30 tulizotenga mwaka 2007/2008. Hili ni ongezeko la shilingi bilioni 8.84 ambalo ni sawa na asilimia 257. Kwa Mkoa wa Lindi, Bajeti ya maendeleo kwa mwaka 2006/2007 ilikuwa shilingi bilioni 1.83 ikilinganishwa na shilingi bilioni 15.30 zilizotengwa katika mwaka 2007/2008. Hili ni ongezeko la shilingi bilioni 13.45 sawa na asilimia 735. *(Makofi)*

Hii ni mifano michache tu inayoonyesha jinsi Serikali inavyojali Mikoa inayoko nyuma kimaendeleo. Kwa ujumla kumekuwepo na ongezeko la fedha zinazotengwa katika Bajeti kila mwaka kwa ajili ya Mikoa hiyo yote. Nitatoa takwimu. Kama nilivyosema Kigoma kutoka bilioni 3 mwaka 2006 mpaka mwaka huu bilioni 12,274, Mkoa wa Lindi kutoka bilioni 1.8 kwenda bilioni 15.2, Mtwara bilioni 2 kwenda bilioni 15, Rukwa bilioni 1 kwenda bilioni 11, Ruvuma kutoka bilioni 1.6 kwenda bilioni 19 na Tabora kutoka bilioni 1 kwenda 12 nina uhakika na Urambo zitafika. *(Makofi/Kicheko)*

Pamoja na hatua hizo, katika mwaka wa fedha 2006/2007, kwa makusudi kabisa mikoa hiyo pia iliongezewa jumla ya Shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya uboreshaji miundombinu katika maeneo yao ambapo kila Mkoa ulipata shilingi milioni 200. Aidha, katika Bajeti ya mwaka 2008/2009. Serikali imetenga fedha kwa mikoa 11 kwa ajili ya kukarabati Hospitali za Mikoa. Kati ya Mikoa hiyo, Mikoa mitano ya Ruvuma, Rukwa, Tabora, Lindi na Kigoma imetengewa shilingi milioni 600 kwa mwaka. Hii ni hatua ya kwanza. Awamu ya pili, itakayohusisha mikoa iliyobaki itatekelezwa mwaka ujao wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali inaendelea kuboresha miundombinu muhimu katika mikoa hiyo hasa barabara, umeme na mawasiliano. Serikali itaendelea kutoa kipaumbele kwa Mikoa hiyo, kulingana na ukuaji wa uchumi na uwezo wa fedha wa Serikali. Itoshe kusema tumetekeleza ahadi tuliyoisema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili ambalo limezungumzwa na Wabunge wengi sana, mnisamehe nisiwataje sasa kwa sababu ya muda usimamizi wa fedha katika Halmashauri wamezungumza Wabunge 23. Nakubaliana na hoja zao *concerns* zao walizotoa kuhusu fedha katika Halmashauri kimsingi tunakubaliana nao. Lakini kama alivyoeleza Mheshimiwa Pinda, kuna mabadiliko yanayotokea katika Halmashauri si kwamba wamekaa vile vile hapana, baada ya kukumbushwa wamebadilika katika baadhi ya maeneo. Kwa mfano; takwimu zinaonyesha kuwa kuna mafanikio ya utunzaji wa vitabu vya Hesabu za Halmashauri nchini toka mwaka 2000. Kwa mfano, katika mwaka 2000/2001, kulikuwa na Halmashauri tatu (3) zilizopata hati safi, Halmashauri 75 zilizopata Hati chafu na Halmashauri 37 zilizopata Hati zenye masharti za Ukaguzi

kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Mwaka 2004/2005 Halmashauri 62 zilipata Hati safi, Halmashauri 4 zilipata Hati chafu na Halmashauri 51 zilipata Hati zenye masharti. Lengo la Serikali ni kuimarisha utunzaji wa vitabu vya hesabu za Halmashauri zote nchini ili kuhakikisha kuwa hakuna Halmashauri hata moja itakayopata hati chafu. Lengo hili tumekusudia kulisimamia ili litekelezeke kwa kufanya yafuatayo:-

Kuzingatia taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, ambapo kwanza Halmashauri zilizopata hati chafu, zitapatiwa wataalam ili kuweka mkakati wa kuondoa upungufu na kujiimarisha.

Pili, katika muda wa ufungaji wa Hesabu za Halmashauri yaani Julai – Septemba 2007, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI itazifuatilia Halmashauri ili kuona ufungaji wa hesabu unafanywa kwa ukamilifu. Tutaifanya kutoka *centre* kufuatilia.

Tutaimarisha Ukaguzi wa Ndani, kwa madhumuni ya kubainisha na kuyashughulikia kabla ya kukaguliwa na Mkaguzi wa Nje na kuhakikisha kuwa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kina Wakaguzi wasiopungua watatu (3). Katika hilo tutahakikisha kuwa kila Halmashauri ina Kamati ya Ukaguzi inayofanya kazi, kuimarisha ukaguzi na ufuatiliaji katika ngazi ya Mkoa.

Tatu, tutaimarisha ukaguzi wa ndani katika Halmashauri kwa kukifanya kitengo cha ukaguzi wa ndani kuwa kitengo kinachojitegemea na kuwajibika moja kwa moja kwa Mkurugenzi wa Halmashauri. Nne, Kutakuwa na mpango wa kazi wa masuala ya ukaguzi *(Audit Programme).*

Tano, tutahakikisha taarifa za ukaguzi za kila robo mwaka zinajadiliwa katika Kamati ya Ukaguzi na kufuatilia utekelezaji wa Kamati.

Sita, Taarifa pamoja na majibu ya Kamati yatawasilishwa kwenye Kamati ya Fedha ili kuwezesha Madiwani kujadili na kutoa maamuzi. Saba, kuimarisha Mfumo wa utoaji taarifa ya Mkaguzi wa Nje katika Wizara, Mkoa na Halmashauri. Nane, kuhakikisha kuwa taarifa ya Mkaguzi wa Nje inawasilishwa mbele ya Baraza la Madiwani ikishuhudiwa na Mkuu wa Mkoa ule. *(Makofi)*

Tisa, Mikoa na Halmashauri kufuatilia na kushughulikia taarifa ya awali ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali na kuhakikisha kwamba majibu yanatolewa kwa haraka na kwa usahihi ili kupunguza hoja za ukaguzi mwisho wa mwaka. Wasiwe hodari wa kujenga majibu, wawe hodari kuzuia hoja za ukaguzi, majibu hayasaidii. *(Makofi)*

Kumi, kuhakikisha Sekretariati zote za Mikoa zina Mkaguzi wa ndani kwa ajili ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ambaye atahusika na taarifa za Mamlaka za Serikali za Mitaa za kila robo mwaka na kuhakikisha Wataalam wa fedha wa Kanda wa Programu ya Uboreshaji wa Serikali za Mitaa na kwenye Sekretariati za Mikoa wanatekeleza wajibu wao inavyotakiwa.

Usimamizi wa fedha, kwanza, kuwa na watumishi wenye sifa na wa kutosha wa fani za Uhasibu, Ukaguzi na Manunuzi; Kuimarisha matumizi ya komputa kwa kuunganisha idara zote za fedha za Halmashauri na Hazina; Kuendelea kutoa mafunzo kwa Watumishi wa Idara ya Fedha, Ukaguzi na Manunuzi: Kuwa na vikao vya tathmini na watumishi wa Halmashauri; Kuhakikisha kuwa taarifa za utekelezaji kila robo mwaka zinatolewa na kujadiliwa na Kamati ya Madiwani na kuoanisha mifumo ya Ukaguzi na ufuatiliaji iliyopo katika Halmashauri ili kubaki na mfumo wenye tija.Tumeanza kufanya nini, Mheshimiwa Mbunge mmoja alisema ninasema tu hamjachukua hatua, si kweli kama namna moja ya kuhakikisha kuwa usimamizi wa fedha ni mzuri katika Halmashauri, Mamlaka za nidhamu zimekuwa zikichukua hatua pale kasoro zinapobainika. Katika kipindi cha Julai, 2006 – Juni, 2007 Jumla ya Watumishi 179 walichukuliwa hatua za nidhamu au kufikishwa katika vyombo vya Sheria. Watumishi waliochukuliwa hatua wamegawanyika katika makundi yafuatayo:-

Wakurugenzi walioteremshwa vyeo ni 23 katika kipindi cha mwaka mmoja, waliohukumiwa kifungo 1, Walioachiwa huru na mahakama 3, kesi za zinazoendelea 2.Watumishi wengine, waliofukuzwa kazi ni 24, walioachiwa huru na mahakama 45, waliofungwa 2, ambao kesi zinazoendelea ni 79. Kwa hiyo, nasisitiza kwamba tunachukua hatua kwa kufuata sheria za nchi. Hao kama nilivyowataja wamechukuliwa hatua kwa kufuata sheria za nchi, lakini kutokana ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali. Zoezi hili litaendelea ili kuhakikisha kunakuwa na usimamizi mzuri wa Fedha na Mali za Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, katika kikao alichoitisha rasmi kwa Viongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa tarehe 29 Aprili, 2007 kujadili taarifa hiyo, aliagiza Mabaraza ya Madiwani kukutana na kujadili taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Mikutano hiyo ifanyike wakiwemo Wakuu wa Mkoa na Wakaguzi Wakazi.

Pia, Mheshimiwa Rais aliyaagiza Mabaraza ya Madiwani kutokuwaonea haya watakaobainika kufuja fedha za Halmashauri. Maagizo haya yameanza kutekelezwa na Mikoa. Tumeanza kupata taarifa za waliobainika na kasoro na hivyo hatua zimeanza kuchukuliwa. Kwa mfano, Halmashauri ya Wilaya ya Kahama. Kazi inaendelea kule.

Natoa wito kwa Mikoa ambayo pengine bado haijatekeleza agizo hilo kufanya hivyo mara moja. Aidha, Waheshimiwa Wabunge ni viongozi muhimu sana katika Halmashauri. Mnao wajibu wa kuhudhuria vikao vya Halmashauri na hasa hivi ambavyo vinajadili mambo ya bajeti na fedha za Halmashauri. Mkiwepo mambo mengine mtagundua.

Lakini kama hamhudhurii vikao hivyo mkaja kuhoji huku mambo yataharibika kwa sababu hakuna mtu anayeangalia. Nawasihi Waheshimiwa Wabunge, mhakikishe angalau hivyo vikao vinavyojadili fedha mnapata ratiba mapema muweze kuhudhuria na kushiriki ili tusaidiane kubadilisha hali.

Mheshimiwa Spika, Viongozi na Watendaji wote wanatakiwa kuwa makini zaidi katika taratibu za matumizi, ukusanyaji wa mapato na utunzaji wa hesabu kwa kuzingatia Sheria tulizojiwekea. Hoja nyingine ni uanzishaji wa Maeneo Mapya ya

Utawala, hii hoja nisipowasoma Waheshimiwa Wabunge, waliochangia wataleta hoja na imejengwa kweli kweli juu ya eneo hili. Nitawataja ili wasikike kwamba kwa kweli wameomba jambo hili. Mheshimiwa Mgana Msindai , Mheshimiwa Pascal Degera, Mheshimiwa Gaudensi Kayombo na Mheshimiwa, Gideon Cheyo.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Benedict K. Losurutia, Mheshimiwa Ramadhan Maneno, Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Samson Mpanda, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Mussa Zungu, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mheshimiwa Alhaj Prof. Juma A. Kapuya, Mheshimiwa Manju Msambya, Mheshimiwa Philip S. Marmo, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa Dr. Guido G. Sigonda, Mheshimiwa Prof. Idris A. Mtulia, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Khadija Al-Qassmy, Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa na Mheshimiwa Gideon A. Cheyo.

Wote hawa wamejenga hoja vizuri kweli. Nilipokwenda Singida, ilikuwa kali zaidi. Wote wanaomba ama Mkoa ama Wilaya ama Tarafa ama Kijiji na wengi wao waliochangia hii wanaomba majimbo yagawanywe, Wilaya zigawanywe na Mikoa igawanywe. Naomba nitoe maelezo kidogo:-

(a) Madhumuni ya Kuanzisha maeneo mapya ya utawala ni kusogeza huduma karibu na wananchi, kurahisisha utawala na kuboresha utawala bora hasa ukizingatia kuwa yapo maeneo ambayo ni makubwa sana na yana miundombinu mibovu na hivyo kusababisha maeneo hayo kutofikika kiurahisi.

(b) Vigezo vinavyozingatiwa ni: Ukubwa wa eneo, Idadi ya watu, Sababu za Kijiografia, Hali ya uchumi na Hali ya huduma za jamii

(c) Taratibu za kufuatwa. Utaratibu unaotakiwa kuzingatiwa unatofautiana kulingana na aina ya eneo la utawala linalotaka kuanzishwa. Taratibu zaujumla zinazotakiwa kufuatwa ni:-

Kuwepo kwa hitaji la ngazi hiyo ya Utawala, Kuwepo kwa idhini kutoka vikao vinavyohusika, Utayari wa Wananchi kuchangia ujenzi wa miundombinu kama vile Ofisi na majengo mengine, Idhini ya mamlaka husika ya kuanzisha eneo la utawala yaani Rais kwa upande wa Mikoa na Wilaya na Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa kwa Tarafa, Kata na Vijiji.

(d) Gharama za Kuanzishwa maeneo mapya ya utawala. Naomba mnisikilize sana eneo hili la gharama. Gharama za kuanzisha maeneo ya utawala zinatofautiana kulingana na aina ya eneo la utawala na majukumu ya eneo hilo kama ifuatavyo:-

(i) Mikoa, kuanzisha Mkoa mmoja ni Shilingi bilioni 10;
(ii) Kuanzisha Wilaya moja ni Shilingi bilioni 4.5;

(iii) Kuanzisha Halmashauri ni Shilingi bilioni 5.5; na
(iv) Kuanzisha Tarafa ni Shilingi milioni 15.

Kata ni Shilingi milioni 50* Ndiyo milioni 50 sawa sawa. Tarafa ni milioni 15, kwa hiyo hii ni kubwa. Ni kubwa kwa sababu ya Extesion Officers, ambao wanahitaji Ofisi, nyumba za kuishi na vitendea kazi katika Kata. *(Makofi)*

(e) Maombi yaliyopokelewa. Hadi kufikia mwezi huu, mwezi Juni mwaka huu jumla ya maombi 485 ya kuanzisha maeneo mapya ya utawala yamepokelewa kama ifuatavyo:-

Wanaotaka Mikoa ilikuwa ni mikoa mitatu kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| Wilaya | - | 35; |
| Tarafa | - | 13; |
| Kata | - | 207; na |
| Vijiji | - | 227. |

Kwa kuzingatia idadi kubwa ya maombi yaliyopokelewa na kutokana na gharama kubwa ya kuanzisha maeneo hayo ya utawala ni dhahiri kuwa uanzishaji wa maeneo hayo ni gharama kubwa sana. Hivyo, Serikali itakuwa inaanzisha maeneo hayo kwa kuzingatia umuhimu wa pekee pamoja na uwezo wa Serikali kugharamia uanzishaji wa maeneo hayo.

Pale itakapoonekana upo umuhimu wa kuanzisha maeneo mapya ya utawala, katika ngazi za wilaya Serikali inaona ni vema basi tuanze na Halmashauri. Ipatikane Halmashauri kabla hamjagawa ile Wilaya, mpate Halmashauri tofauti katika Wilaya ile, jambo hili ni kubwa tunaendelea kulitakari pamoja na maombi ya Mkoa wa Mwanza, Jiji la Mwanza kuwa Jiji kama Jiji la Dar es Salaam. Michakato yote hii tunaitafakari.

Lakini tunataka ieleweke jamani ni mapesa mengi sana na ninyi hapa ndiyo mnapanga vipaumbele itabidi tuchague kipaumbele cha kupunguza ili tupeleke kwenye uendeshaji na utawala.

Posho kwa Madiwani. Hoja ni kuwa posho ya shilingi 60,000 ni kidogo na zitolewe na Serikali Kuu. Aidha, Madiwani wapewe posho za kujikimu na za vikao. Serikali itoe idhini kwa Halmashauri zidhamini Madiwani kukopa vyombo vya usafiri, ili kuwawezesha kufika katika maeneo yao ya kazi kuhudumia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawa pia ni wengi. Lakini pia niwaseme, nisiposema Madiwani hawatakuwa wamewasikia:-

Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Suzan A.J. Lyimo, Mheshimiwa Sijapata J. Nkayamba, Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, Mheshimiwa Anastazia J. Wambura, Mheshimiwa Vedastus M. Manyinyi, Mheshimiwa Ramadhani A. Maneno, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa

Mercy Emmanuel, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Hassan C. Kigwalilo, Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga, Mheshimiwa Halima O. Kimbau, Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu, Mheshimiwa Mariam R.Kasembe, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Manju S.O. Msambya, Mheshimiwa Suleiman O. Kumchaya, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Jenister J. Mhagama, Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi, Mheshimiwa Gideon A. Cheyo, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, Mheshimiwa Eustace O. Katagira Mheshimiwa Said A. Arfi, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba na Mheshimiwa Foya G. Kimbita. *(Makofi)*

Kimsingi, Serikali hivi karibuni imekubali kuboresha maslahi ya madiwani kwa kuweka viwango vipya vya posho kama ifuatavyo:-

Posho ya mwezi Shilingi 60,000 ndiyo mnasema haitoshi.
Posho ya Kikao Shilingi 40,000;
Posho ya madaraka kwa Wenyeviti wa Kamati Shilingi 40,000 kwa mwezi na Posho ya madaraka kwa Mwenyekiti/Meya wa Halmashauri kati ya Shilingi 100,000 - 350,000 kwa mwezi kulingana na uwezo wa Halmashauri.

Ili kuhakikisha kuwa Waheshimiwa Madiwani wanawajibika kwa Wananchi na Halmashauri zao na kuimarisha dhana ya kupeleka madaraka kwa Wananchi, Serikali inasisitiza kuwa posho hizo zitokane na mapato yanayotokana na vyanzo vinavyokusanywa na Halmashauri zenyewe. Haitakuwa sawa sawa Serikali Kuu kuwatolea fedha zile. Tukishaanza kuwatolea maana yake vile vile tutawanyima uhuru wao. Serikali inaangalia na kuchambua vyanzo vya mapato vya Serikali Kuu kwa madhumuni ya kuziongezea Halmashauri vyanzo zaidi ili ziweze kutoa huduma bora na kumudu gharama za uendeshaji. *(Makofi)*

Ni mchakato unaoendelea tuangalie ni kodi zipi tuanze kuzirejesha kwa Halmashauri wazikusanye ili waweze kulipana mafao hayo wanayohitaji. Lakini Serikali vile vile inaangalia uwezekano wa kulipa kiinua mgongo kwa kiwango cha asilima 25 ya posho ya mwezi ya diwani kwa kipindi alichotumikia. *(Makofi)*

Pili, Serikali inafanyia Kazi suala la stahili za Madiwani kama vile matibabu, huduma za mazishi na unafuu wa Kodi pale ambapo madiwani watanunua vyombo vya usafiri kwa mfano pikipiki. Maelekezo yatatolewa kwa Halmashauri pale taratibu zitakapokuwa zimekamilika. Haya matatu kimsingi yana uamuzi; ya Baraza la Mawaziri, yanafanyiwa kazi. Haya ndiyo tunaweza kusema yatawafikia Madiwani. *(Makofi)*

Lakini changamoto ameieleza vizuri sana Mheshimiwa Pinda, changamoto kwa Halmashauri ni kuongeza jitihada za kukusanya mapato kutokana na vyanzo vilivyopo kwenye maeneo yao.

Muniwie radhi sana kwa mfano, *property tax* pale Dar es Salaam kumejaa majengo mengi sana lakini hayachajiwi *property tax* hawalipi kodi. Sasa tumekubaliana kuwaomba *TRA* angalau kwa mwaka huu wa fedha hebu wawasaidie kukusanya halafu wawarejeshee. Lakini eneo ambalo wanaweza kupata pesa nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuhamia Dodoma: Wabunge waliochangia hoja hii ni Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Manju A. S. Msambya, Mheshimiwa Maria S. Mfaki, Mheshimiwa Dr. Wilbroad P. Slaa, Mheshimiwa George M.Lubeleje, Mheshimiwa Mwinchum A. Msomi, na Mheshimiwa Grace S. Kiwelu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa rafiki yangu Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, rafiki yangu wa siku nyingi sana. Tumekuwa naye Bungeni siku nyingi sana. Hodari sana, siku ile akachukua Ilani ya Uchaguzi ya CCM akainukuu. Lakini kwa makusudi akanukuu eneo moja tu. Ilani inasemaje. Nitanukuu maeneo mawili ya msingi. Kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Iringa-Dodoma-Arusha na kukamilisha ujenzi wa barabara ya Dar es Salaam-Dodoma-Mwanza kama mkakati wa kuendeleza mji wa Dodoma ili uweze kuvivutia vitega uchumi. *(Makofi)*

Pili kuweka vivutio kwa sekta binafsi ili ishiriki katika uwekezaji kwenye ujenzi wa miundombinu inayohitajika katika ukuaji wa mji. Na katika uwekaji wa huduma mbalimbali zinazokidhi mahitaji ya watumishi wa Serikali na wananchi kwa jumla. Haya mawili tumeyazingatia. Liko la kwanza lile nilisema tutengeneze sheria ya *CDA*. Tunategemea mwakani tutaleta sheria ya Kuanzisha Makao Makuu. Lakini haya mengine mawili tumeyazingatia kweli kweli. Nitapitia maeneo maeneo machache:-

(a) Serikali kwa wakati huu imeelekeza nguvu zake katika kuboresha mazingira mazuri ya Mji wa Dodoma na kuimarisha miundombinu ya barabara zinazounganisha mkoa wa Dodoma na mikoa mingine ikiwemo barabara ya Iringa-Dodoma-Singida-Babati-Arusha. Kwa mfano:-

Ujenzi wa Barabara ya Dodoma-Iringa yenye kilomita 267. Mkataba wa Mhandisi Mshauri na kazi ya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na maandalizi ya nyaraka za zabuni za ujenzi utatiwa saini Julai 2007. Kazi hizi zitakamilika katika mwaka 2007/2008. Kazi hii inagharamiwa na *Nordic Development Fund (NDF).* Utafutaji wa fedha za ujenzi sambamba na kazi ya usanifu unafanywa na wafadhili mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB).*

Pili, ujenzi wa barabara ya Dodoma-Babati yenye kilomita 261, kazi ya upembuzi yakinifu imekamilika. Mhandisi Mshauri anaendelea na usanifu wa kina. Kazi hiyo inagharamiwa na *Nordic Development Fund.* Na inatarajiwa kukamilika mwaka 2007/2008. Ujenzi wa Barabara ya Babati-Minjingu yenye kilomita 61. Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina pamoja na maandalizi ya nyaraka za zabuni zimekamilika chini ya ufadhili wa *Nordic Development Fund.* Fedha za ujenzi

zimepatikana kutoka *African Development Bank,* ikiwa ni sehemu ya Mradi wa Singida-Babati-Minjingu ambao unatarajiwa kuanza mwaka 2008. *(Makofi)*

(b) Pili, miundombinu ya elimu, tayari Serikali imeanzisha Chuo Kikuu cha Dodoma ambacho kitakuwa na uwezo wa kudahili wanafunzi 40,000 kitakapokamilika na kitaanza kuchukua wanafunzi 1,000 Septemba mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, utakapokuja Bunge la mwezi wa kumi, vile vilima pale Chimwaga, vitatu vitakuwa vimeanza kazi. Wanajenga *NSSF*, wanajenga *PPF* wanajenga *PSPF*. *Hostel* na sehemu za wanafunzi. Kwa hiyo, Dodoma itakuwa imebadilika. *(Makofi)*

Lakini vile vile kuna vyuo vingine vikuu vingine vya binafsi vinavyotarajiwa kujenga mjini Dodoma. Kwa mfano *St. Jones* ambacho kitaanza Septemba mwaka huu kwa kudahili wanafunzi 700.

Shirika la Kanisa la Katoliki la Wajesuiti limepewa eneo la hekta 200 huko Ihumwa kwa ajili ya kuanzisha ujenzi wa chuo cha mafunzo ya elimu na kilimo.

(c) Serikali kwa msaada wa Benki ya Dunia na nchi ya China imeweza kupata chanzo cha maji mengi katika eneo la Mnzakwe kwa ajili ya matumizi ya wakazi wa Manispaa ya Dodoma. Zamani Dodoma kulikuwa na shida ya maji. Sasa ni historia. Mji wa Dodoma ndio mji pekee wenye mitambo ya maji yenye kuzalisha maji maradufu ya mahitaji halisi ya maji. Kwa mfano uzalishaji wa maji ni meta za ujazo ($M^3$) 6,657,721, wakati mitambo ina uwezo wa kuzalisha meta za ujanzo ($M^3$) 14,600,000. Mahitaji halisi ya maji Dodoma ni meta za ujazo ($M^3$) 7,560,000. Hivyo uzalishaji wa maji unatoa nafasi kubwa kwa wakazi wote watakaohamia Dodoma kwa ajili ya Makao Makuu kuwa na uhakika wa kupata maji safi na salama. *(Makofi)*

(d) Hospitali - Mfuko wa Bima wa Afya umetenga fedha za kujenga majengo yatakayotumika kutoa huduma ya hadhi ya daraja la kwanza kwa wagonjwa katika hospitali ya Mkoa wa Dodoma kuanzia mwaka huu wa fedha. *(Makofi)*

(e) Fedha - Mamlaka ya Uendelezaji Makao Makuu *CDA* kwa mara ya kwanza wamepewa bilioni 1.4 kwa mwaka wa fedha 2007/2008 kwa ajili ya kuboresha mandhari na miundombinu ya Manispaa ya Dodoma ukilinganisha na shilingi milioni 428 mwaka 2006/2007 lakini vile vile Bajeti hii mtakapoipitisha kuna makazi mapya ya Waziri Mkuu yatakayojengwa Dodoma, kuna makazi mapya ya Mheshimiwa Spika yatakayojengwa Dodoma. *(Makofi)*

Ilani imetumia maneno kwa uangalifu sana, tutahamia Dodoma awamu kwa awamu.Mimi nina hakika tukikamilisha miundombinu hii hata kasi ya kuhamia Dodoma itakuwa kubwa na ya haraka zaidi. *(*Makofi*)*

Kusimamia na kuratibu mapato ya matumizi ya Serikali. Wabunge waliochangia hoja hii ni:-

Mheshimiwa Suzan A.J. Lyimo, Mheshimiwa Dr. Harysson G. Mwakyembe, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Dr. Wilbroad P. Slaa, Mheshimiwa Aziza S.Ally, Mheshimiwa Luhanga J. Mpina, Mheshimiwa Ramadhan A. Maneno, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe na Mheshimiwa Mercy Emmanuel, Mheshimia Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim.

Wengine ni Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mheshimiwa Sijapata F. Nkayamba, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salum, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga, Mheshimiwa George B. Simbachawene, Mheshimiwa Grace S. Kiwelu, Mheshimiwa Mheshimiwa Omari S. Kwaangw' na Mheshimiwa Juma Said Omar. *(Makofi)*

(a) Kuwekwa kwa Kamati, tarehe 12 Aprili mwaka huu, Baraza la Mawaziri lilikutana mjini Dodoma kupokea na kujadili Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu hesabu za mwaka 2005/2006. Taarifa hiyo ilidhihirisha kuwepo kwa udhaifu katika Serikali Kuu na Serikali za Mitaa katika usimamizi, udhibiti na uratibu wa mapato na matumizi ya Serikali.

Kutokana na hali hiyo, Baraza la Mawaziri liliamua pamoja na mambo mengine, kwamba zianzishwe Kamati za Kusimamia, Kudhibiti na Kuratibu Mapato na Matumizi katika Taasisi za Serikali zikiwemo Wizara, Mikoa na Halmashauri.

Hivyo, kuanzia mwaka wa fedha 2007/2008, kila Taasisi na Halmashauri inaagizwa kuunda Kamati husika.

(b) Majukumu ya Kamati, Kusimamia, kudhibiti na kuratibu mapato na matumizi katika taasisi inayohusika.

(c) Ratiba ya Vikao vya Kamati, zitakutana kila robo mwaka ambapo zitajadili Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti. Wajumbe wa Kamati ni viongozi waliopo katika Wizara na walioko katika Mikoa. Kwa upande wa Serikali za Mitaa mfumo uliopo wa usimamizi, udhibiti na uratibu wa mapato wa matumizi wa Halmashauri husika utaendelea.

Hata hivyo, taarifa za kila robo mwaka kwa kila Halmashauri zitawasilishwa Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI kuzingatia ratiba itakayotolewa na Wizara hiyo. Ili kurekebisha udhaifu uliojitokeza katika usimamizi na udhibiti wa fedha za Serikali imeagizwa kwamba Kamati husika ziwe zimeundwa na kuanza kazi katika mwaka wa fedha 2007/2008.

Napenda kusisitiza kwamba hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali si lazima uwe wizi au ubadhirifu wa fedha za umma. Hoja ya ukaguzi ni dai la Mkaguzi la kupewa taarifa zaidi kuhusu matumizi yaliyofanywa. Kwa hiyo, ikisemekana

ametoa hoja ya ukaguzi trilioni moja hazionekani, haina maana kwamba zimeshaliwa zote hizo. *(Makofi)*

Hoja hizo hutolewa baada maelezo baada ya taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kutolewa, akiuliza trilioni moja maelezo yanapelekwa na unakuta sehemu nyingi fedha zile zinakuwa zimepungua au hoja imekwisha kabisa.

Kwa mfano, kuanzia Julai 2005 hadi Juni 2006, hoja zinazohusu malipo yasiyokuwa na nyaraka yalikuwa shilingi bilioni 1.3 lakini hadi sasa nyaraka zote zinazohusika na kiasi hicho zimewasilishwa kwa wakaguzi na zinaendelea kuhakikiwa. *(Makofi)*

Katika kipindi hicho, malipo yenye nyaraka pungufu yalikuwa shilingi bilioni 56.5 kiasi ambacho kinahusisha bakaa ya hoja za miaka ya nyuma ya Shilingi bilioni 1.6. Lakini hadi sasa nyaraka zenye jumla ya shilingi bilioni 33.7 zimehakikiwa na hoja zimefungwa. Asilimia 91 ya nyaraka zilizobaki zinaendelea kuhakikiwa na Wakaguzi. *(Makofi)*

Maelezo ya ufafanuzi kuhusu maana halisi ya hoja za ukaguzi yalitolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwenye vyombo vya habari na pia yalitolewa na Waziri wa Fedha wakati akijibu swali ndani ya Bunge lako Tukufu. Suala muhimu kwa watendaji wote ni kuhakikisha kuwa hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu zinajibiwa ipasavyo na kwamba lengo liwe kutokuwa na hoja za Wakaguzi badala ya kujibu Hoja za Wakaguzi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu samahani. Waheshimiwa Wabunge si vizuri tukafika pahala ambapo nikalazimika kutumia Kanuni ya 21(iii) hasa kwa kumkatiza Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ili aendelee na kwa raha tu ili afike mwisho nzuri, ningeomba sasa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Masuala ya Bunge atoe hoja ya kutengua Kanuni ya 21(iii) ili tuweze kuendelea hadi hapo Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapomaliza majibu yake. *(Makofi)*

**Hoja ya Kutengua Kanuni ya 21(3)**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (BUNGE):** Mheshimiwa Spika, kama ulivyosema kwa kuwa shughuli ya leo hii asubuhi hatutaweza kukamilisha kwa muda uliopo, naomba basi kwa ruksa yako kuomba Bunge hili kutoa hoja kwamba tutumie Kanuni ya 21 fasili ya (iii) ili tuweze kumalizia shughuli iliyopo mbele yetu na kumwezesha Mheshimiwa Waziri Mkuu akamaliza hitimisho ya Bajeti yake.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja ilitolewa na Kuafikiwa)*

*(Bunge lilipitisha Hoja ya Kutengua Kanuni ya 21(3*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja iliyo mbele yetu ni kutengua Kanuni ya 21(iii) ili kumwezesha Mheshimiwa Waziri Mkuu aendelee kutoa majibu ya hoja iliyopo hadi muda ambao utakaotosheleza. Sasa hoja hiyo imekwishatolewa na imeungwa mkono. *(Makofi)*

Kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimeona kitu kimoja ambacho pengine Waheshimiwa Wabunge watapenda kukitazama kwa tafsiri yake. Mheshimiwa Tatu Ntimizi ameketi Kiti cha Mheshimiwa John Malecela leo. *(Makofi)*

*Serjeant-At-Arms* angalia na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, ameenda hapo hapo. *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nilipomwona Mheshimiwa Anne Kilango Malecela anasogelea pale nikafikiria zitapigwa ngumi sasa hivi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa tuhuma za ubadhiribu wa fedha dhidi ya Benki Kuu. Waliochangia hoja hii ni. Mheshimiwa Dr. Wilbroad P. Slaa, Mheshimiwa Amad Mohamed, Mheshimiwa Suzan A.J. Lyimo, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe na Mheshimiwa Lucy Owenya.

Mheshimiwa Spika, ujenzi katika hifadhi ya Serengeti, Mbunge aliyechangia hoja hii ni Mheshimiwa Lucy Owenya.

Mheshimiwa Spika, suala la uharibifu wa mazingira katika Hifadhi ya Serengeti limeshabikiwa sana ndani na nje ya nchi na watu ambao ama hawana takwimu sahihi au hawana nia njema na nchi yetu.

(a) Ujenzi wa Hoteli, Mbuga ya Serengeti imeungana na Mbuga ya Masai Mara ya Kenya, ina ukubwa wa kilometa za mraba 3,000. Eneo hili ni asilimia 18.7 tu ya Mbuga ya Serengeti yenye ukubwa wa kilometa za mraba 16,000. Zilizoko Kenya ni 3,000 tu, hizi 14,000 ziko ndani ya Tanzania. *(Makofi)*

Pia mkumbuke mzunguko wa wanyama katika Mbuga za Serengeti, umetangazwa kama moja ya maajabu mapya ya dunia. *(Makofi)*

Yanatangazwa halafu tunaambiwa tusijenge. Lakini mzunguko wa nyumbu unakuwa Masai Mara kule Kenya kwa kipindi cha miezi miwili tu miezi 10 iliyobaki wako Tanzania. *(Makofi)*

Wenzetu kule Kenya wamejenga hoteli 340 zenye vyumba 4,700. Eneo lao dogo zaidi, wanyama wanakaa muda mfupi zaidi, lakini angalia wana vyumba 4700. Tanzania,

hoteli zetu zote zilizopo pale zina vyumba 940 tu. Kumbuka ukubwa wa eneo, kumbuka muda wanyama wanakokaa huku. Sisi ndiyo kiasi hicho. Halafu tunaambiwa tusijenge hoteli. Sisi eneo letu ni zaidi ya mara sita ya eneo la Masai Mara. Tunaambiwa tusijenge hoteli. *(Makofi)*

Hoja hizi waliosikiliza *BBC* wiki iliyopita, *Lake Natron,* liko mpakani vile vile upande wa pili Kenya wana kiwanda cha Soda Ash sisi Tanzania tunazungumza habari ya kuanza kiwanda upande wa Tanzania na Kampuni ya *Total* na tunaambiwa tutaharibu mazingira. *(Makofi)*

Narudi Masai Mara. Wenzetu Kenya mwaka jana peke yake walikusanya milioni 750 dollars Tanzania tulikusanya dola 30 milioni tu basi, wao wana 750 sisi tuna 30 million only. Tunaambiwa tusijenge hoteli. Napenda kuwaambia hao wanaotulalamikia na kumwambia Mheshimiwa Lucy Owenya. Tutajenga. *(Makofi)*

Tanzania ni mojawapo ya nchi ambayo haihitaji kufundishwa juu ya kutunza mazingira au kuhifadhi wanyamapori. Wakatafute watu wa kuwafundisha, Tanzania tunafahamu na tunafanya. *(Makofi)*

Serikali itatumia matokeo ya utafiti wa kisayansi kuelekeza uwekezaji na kuhakikisha unazingatia sera yetu ya Taifa ya Wanyamapori. Sera yetu. *(Makofi)*

Kwa kuzingatia hayo, Serikali imeangalia upya *General Management Plan (GMP)* ya Serengeti na kuamua kuongeza hoteli za nyota tano (5) au zaidi ili zifikishe jumla ya vitanda tena sisi tunakuwa very modest ili na sisi tufikie vitanda 4,500 ifikapo mwaka 2012. Maeneo ambapo hoteli hizo zitajengwa zitazingatia matakwa yote ya hifadhi ya Wanyamapori. Sisi kama kawaida yetu, maeneo ambazo hoteli hizi zitajengwa, yatazingatia matakwa yote ya hifadhi ya wanyamapori na suala la mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uko vile vile ujenzi unaoendelea ambao umetukana sana na akachorwa Mheshimiwa Basil Mramba kwamba ndiye anayeleta barabara na vitu gani. Wanaotulalamikia ni hao hao majirani na watu wasiotupenda. Tumeamua kujenga barabara. Katika hifadhi ya Serengeti barabara hii, barabara kutoka Musoma mpaka Arusha yenye urefu wa kilomita 214 sasa hivi yanapita ma-bus naomba mnisikilize kidogo.

(b) Ujenzi wa Barabara, katika Hifadhi ya Serengeti, inapita barabara kuu kutoka Musoma mpaka Arusha. Katika barabara hii yenye urefu wa kilometa 214 yanapita mabasi makubwa, malori makubwa ya mizigo.

Aidha, ndani ya mbuga hii kila siku zinatua ndege 15 kwa siku zinatua katika kiwanja cha Seronera, 15 kwa siku katika kiwanja cha *Fort Ikoma* na 15 zingine katika viwanja vya Lobo na Kirawira kila siku. Serikali imefanya utafiti wa kina juu ya madhara

kwenye mazingira ya hifadhi na wanyama, na kuangalia njia za kupunguza usumbufu huo.

Hivyo, Serikali imeamua, badala ya kuweka lami barabara ya Kilometa 214 inayopita katikati ya hifadhi ya Serengeti, ijenge barabara ya lami ya kilometa 45 kuanzia eneo la Tabora B, Wilaya ya Serengeti, kupitia Kaskazini kwa Hifadhi ya Serengeti mpaka Mto wa Mbu, kupitia Loliondo, *Lake Natron* na Engaruka. *(Makofi)*

Serikali pia imeamua ujenzi wa kiwanja cha ndege katika mji wa Mugumu ambao uko kilometa 16 kutoka ukingo wa magharibi wa Hifadhi ya Serengeti ili kupunguza idadi ya ndege zinazotua ndani ya hifadhi ya Serengeti. *(Makofi)*

Miradi hii itapunguza idadi ya ndege na magari ndani ya hifadhi kwa watalii wanaotoka Arusha kutumia usafiri wa ndege wanapofika Mugumu badala ya kurudi Arusha wakipitia ndani ya hifadhi.

Wasiotutakia nchi yetu mema wanasema barabara iliyopangwa kujengwa itaathiri hifadhi, wakisahau kuwa hivi sasa tunayo barabara ya kilometa 214 inayopita ndani ya hifadhi hiyo hiyo.

Aidha, wanasema eti kiwanja cha Mugumu kitakuwa na madhara kwa wanyama, lakini wanasahau kwamba *Kruger National Park,* ya Afrika Kusini ina kiwanja kinaitwa Skuza, pale Nairobi wanasahau kwamba Jomo Kenyatta Airport kipo kilometa tano tu kutoka *Nairobi National Park.* Chetu kilomita 16 vyao vipo ndani kabisa. Isipokuwa Tanzania ni nongwa ikifanyika, hatuwezi kukubali. *(Makofi)*

Kama viwanja hivi havina madhara yaliyobainika kisayansi; iweje kiwanja kinachojengwa Mugumu kilometa 16 kutoka kwenye mbuga kiwe na madhara hayo.

Katika kuamua kuhusu jambo hili, ni vyema tuwe makini na tutetee maslahi ya nchi yetu. Sisi ni nchi huru, tunaamua mambo yetu. Tanzania yetu itajengwa na Watanzania wenyewe na wala sio mtu mwingine yeyote kutoka nje ya nchi yetu. *(Makofi)*

Tupo kwenye ushindani wa kutangaza maliasili zetu na kuvutia watalii ili kupata rasilimali kwa maendeleo ya nchi yetu. Tujihadhari kutetea sana kutetea na kushabikia hoja zenye athari kwa maslahi ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Benki Kuu. Imechangiwa na Mheshimiwa Dr. Wilbroad P. Slaa, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Suzan A.J. Lyimo, Mheshimiwa Christopher Olonyokie-Ole-Sendeka, Mheshimiwa, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe, Mheshimiwa Lucy Owenya. Jambo hili limepata mjadala mkali sana ndani ya Bunge hili, magazeti yameandika sana ndani ya magazeti na vyombo vingine. Nadhani tumefikia mahali na sisi tungependa kueleza maoni yetu. Kwanza Serikali imechukizwa na jambo hili na imechukua hatua mara moja. *(Makofi)*

Tumechukizwa na kustushwa na Taarifa kwamba kuna fedha zimepotea ndani ya Benki. Kwa hiyo, baada ya kuchukizwa na jambo lenyewe, tumemwagiza *Controller and Auditor General* tunamwamini ni mtu shupavu, ashirikiane na audit za kimataifa wakague benki wajue imekuwaje jambo hili kama ni kweli. Je, ni kweli? Nani anahusika? Ni akina nani na tuchukue hatua gani na tuchukue hatua gani ili jambo hili lisije likatokea tena kama kweli limetokea. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Serikali tumechukua hatua kabla ya kuja hapa Serikali imechukua hatua. Kwa hiyo, nilikuwa nawasihi wenzangu wa upinzani Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Mheshimiwa Slaa kwamba jamani jambo hili halihitaji Kamati Teule ya Bunge. *(Makofi)*

Jambo hili halihitaji Kamati Teule ya Bunge kwa sababu linashughulikiwa na vyombo hivyo. Lakini la pili, sio hivyo tu, tumeshirikiana na kushauriana na Wafadhili wetu wanaotusaidia katika miradi, pamoja na *IMF* juu ya utaratibu wa kufanya juu ya jambo hili. Na utaratibu tuliokubaliana ni huu wa kumteua *Controller and Auditor General* na kutafuta an *International Audit Firm* ya kufanya kazi hii. Tunadhani huu ni utaratibu muafaka. *(Makofi)*

Baada ya taarifa hiyo kupatikana tutachukua hatua zinazopasa na Bunge hili litaarifiwa. Kwa hiyo, hatuhitaji Kamati Teule ya Bunge. Lakini la pili, Benki Kuu ni roho ya nchi ya uchumi wa nchi. Si chombo hivi hivi, hata kama kuwa inawezekana, mambo yenyewe labda yametokea kweli, sijui sina hakika mimi. Lakini tujue kwamba Benki Kuu hii ni moja ya Benki Kuu zinazokubalika hapa Afrika kwa kazi nzuri. Tujue Benki Kuu hii imechangia sana katika mabadiliko ya uchumi yanayoendelea ndani ya nchi yetu. Tujue ndani ya Benki Kuu ile wapo vijana Watanzania wanaume kwa wanawake wanaofanya kazi yao kwa makini na kwa vizuri sana. Kwa hiyo, tusiwahukumu wote kwa pamoja lakini tunasema jambo hili tumeliona, tunalichukulia hatua. Hatuna haja ya Kamati tutasaidiana kutoa taarifa wakati huo nini tumefanya baada ya kupata taarifa kamili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika mwisho, tumekaa hapa, tumesikiliza hotuba ya Waziri wa Mipango, hotuba ya Waziri wa Fedha na nimesikiliza mjadala wa Ofisi ya Waziri Mkuu. Napenda kuwaambia wanachama wa Chama Cha Mapinduzi, Wabunge wa CCM na Watanzania waliotuchagua kwamba Ilani ya Uchaguzi ya CCM inatekelezeka. *(Makofi)*

Ilani ya CCM inatekelezeka na tumeanza kuitekeleza. Nataka nitumie mfano ule alioutumia Rais Mkapa hii ilikuwa ni ndege ilikuwa ni kwenye run way. Sasa tumeanza kupaa. *We are track, we are on time.* Tuko timamu na tuko kwa wakati. Nawaomba tusikubali kuyumbishwa. Tunayo malengo yetu kwenye Ilani tuliyokubaliana ya maisha bora kwa kila Mtanzania, tung'ang'anie hayo hayo bila kuyumbishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaweza nasema wewe unakumbuka ile kauli mbiu yetu, kasi mpya, ari mpya na nguvu mpya, haikutoka hivi hivi. Tumefikiri kwa makini na

kusema tukifanya kwa kasi mpya, kwa ari mpya na nguvu mpya Tanzania yenye neema inawezekana. *(Makofi)*

Nawaombeni tuongeze kasi, tuongeze nguvu, tuongeze ari katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi. Tufanye kazi kwa bidii zaidi, tuache mapokeo*, business as usual* tuachane nayo. Nimeisema sana, tuachane nayo. Kazi ni kwa akili na maarifa ndiyo. Lakini unajua kwa mfano, kila nikisema nikipita katika baadhi ya maeneo ni *business as usual.* Au unamkuta mtu anakuambia pole kwa kazi. Pole kwa kazi, kwani tulipata msiba? Yaani unapeana pole kwa kazi ni kana kwamba ulikuwa kwenye msiba. Hapana bwana, tupeane hongera kwa kazi. *(Makofi)*

Tupeane hongera kwa kazi. Tuchape kazi tupeane hongera kwa kazi na siyo pole. Uchumi huu unaweza kukua kwa asilimia, alikuwa anaisema Mheshimiwa Kaboyonga, kati ya 8, 9 mpaka 10 tunaweza kuukuza uchumi huu, tunaweza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wa CCM tuliwaahidi Watanzania maisha mema kupitia Ilani yetu, tung'ang'anie Ilani yetu. Tusimamie Ilani yetu. Tunaweza. Ndege imeanza kupaa na mimi nawahakikishieni 2010 tutakuwa very comfortable. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana Waheshimiwa Wabunge. Hapo tulipofika kwa asubuhi hii nadhani ilikuwa ni vizuri tuliongeza muda kidogo kumwezesha Mheshimiwa Waziri Mkuu kumaliza vizuri.

Sasa ninalo tangazo tu kwamba Wabunge wote wanawake wabaki ndani ya Ukumbi kuna Mkutano mfupi. Napenda pia nitambue uwepo wa Mheshimiwa Mama Regina Lowassa, tafadhali mama usimame. *(Makofi)*

Na yule rafiki yangu wa kawaida Richard Lowassa. Bahati njema yeye ni Spika wa mwaka 2030. Kwa hiyo, siyo tishio sana kwangu, ila aendelee hivyo. Ule Mkutano kumbe ni kwenye Ukumbi wa Msekwa aah! Basi wanawake *TWPG* Ukumbi wa Pius Msekwa. Sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 11 tutakapoingia katika Kamati ya Matumizi.

*(Saa 07.07 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge samahani kidogo tunaingia hatua ya Kamati ya Bunge baada ya kuwa hoja ilitolewa na kuungwa mkono, lakini ili kuiamua ndio maana tumeingia katika hatua hii. Natoa tahadhari kwa Waheshimiwa Wabunge ambao hawapendi sana kutumia vifungu leo itakuwa shida kidogo, kwa sababu nailiona kama ni jambo la uvivu tu la Mbunge kusimama anasema mshahara wa Waziri hajui mahali popote pengine kwa hiyo mimi sitaruhusu mshahara wa Waziri ila kwa jambo la sera kama kuna kifungu kinahusika na lazima kinahusika usisimame Mshahara wa Waziri

halafu ukasema kituo cha afya cha Kisarawe, haikusaidii lolote nitakataa tu. Nimeona niseme mapema wale ambao hawakusoma chochote wanasubiri tu mshahara leo kwa kweli watasikitika, baada ya hapo katibu labda utamke tena sasa.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 25 - Ofisi ya Waziri Mkuu**

Kif. 1001 – *Administration and General... ...* 3,372,489,000/=

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vote ya 25 programu Na. 10 Sub Vote 1001 kifungu 250100 basic salary ya Waziri Mkuu *Policy Issue.* Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati anafanya majumuisho hapa kuna mambo mawili ambayo mimi niliya-rise moja amelijibu moja ameliacha na haya ndio aliyojibu ndio nataka kupata maelezo zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja katika mambo ya sera aliyoyazungumza Mheshimiwa Waziri Mkuu ni suala la benki kuu na...

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Hamad kifungu hakihusiki kabisa lakini mishahara ya Wasaidizi wa Waziri Mkuu, wapishi, dobi na kadhalika. Nasema Waheshimiwa tutaokoa muda kama mtazingatia vifungu vyenyewe, anachozungumzia ni badala ya 37 yeye kaenda 25.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie programu ya 10 sub vote ya 1001 *other goods and services not clarified.* Ninatumia kifungu hivi kwa sababu bahati mbaya sana vifungu vyetu havitaji *specific item.* Sasa nilipokuwa na-*rise* hoja nilizungumzia suala kuhamishia makao makuu, nashukuru kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu ameeleza, sina nia ya kwenda kushika shilingi lakini napenda nipate ufafanuzi kwenye huduma hii ya makao mkuu, kwa sababu kimsingi tukitazama sana Bajeti ilivyopangwa amezungumza kwamba milioni 1.4 ndio zimetolewa..

**MWENYEKITI**: Samahani sana Dr. Slaa, bado hii ni *domestic house hold* ya Waziri Mkuu, subiri mfike mahali ambapo inahusika.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tungependa kupata maana yake tuna vitabu ishirini, kuna hiki cha blue na kuna kingine sasa labda ungetuelekeza kuwa kwamba ni vote gani basi inayohusu Waziri ili tuweze tukaelekeza hoja zetu kule.

**MWENYEKITIl**: Sasa sijui mimi sidhani kama wakati huu kwa mzoefu kama wewe nifanye tutorial hapa, lakini kwa faida yenu basi kama ndiyo hiyo mnatafuta

mshahara wa Waziri Mkuu ni 37 jamani someni vitu hivi hakuna aina vitabu kitabu ni hiki tupo kwenye kitabu cha pinki.

**MHE. MWANAWETU SAID ZARAFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasubiri.

**MHE. TATU M. NTIMIZI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, *Sub Vote* 101 kifungu cha 250100 mshahara wa Waziri, *desk salary…*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa narudia kwa mara nyingine tena kwa kweli kama hamkusoma vitabu hivi mtaniona mbaya tu kwa sababu tutapita tu kama ndio namna hii. Wengi mnatoa hotuba kali halafu basi, baada ya hapo, mara ya kwanza ndio mnaviona vitabu sasa, tayari mmekuwa navyo.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii vote 25 imeandikwa *Estimate of the Amount required in the year, ending 30th June, 2008 the salary and expenses of the Prime Minister,* ndio imeandikwa hapa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa John Cheyo, mimi nakueleza uhakika wa jambo hili, hii *Prime Minister* kwenye hii *Traditionally* tunaanza na sehemu ambayo inahusu matumizi ya *House Hold,* na watumishi wote pale. Ukija thelathini na 37 utakayakuta maneno hayo ambayo ndiyo *Prime Minister Office*, sasa kama unahoji juu ya quzini ni chakula kinapelekwa Ikulu Ndogo na hivi naweza kukuruhusu lakini haya hayasiki hapa.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Tunasubiri mshahara wa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 27 – Msajili wa Vyama vya Siasa**

Kif. 1001 – *Administration and General*… …17,993,139,000/=

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu**

Kif. 1001- *Administration General*… … … 5,329,953,500/=

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana programu Na. 10 *Vote* 1001 kifungu 250100 *Basic Salaries-Pensionable Posts* za Waziri Mkuu pamoja na kifungu 250300 *Employment Allowances* kwa hiyo vifungu viwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kwanza *policy*, Waziri Mkuu wakati tunachangia kwenye hoja nilichangia *issue* mbili kubwa za benki kuu pamoja na suala la mafuta, la

benki kuu Waziri Mkuu amesema kwamba Serikali imekubali kuajiri auditor kutoka nje ili aweze kufanya uchunguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yetu ni kwamba hivi sasa Benki Kuu tayari imeshatumia kama bilioni 500 kwa ajili ya majengo peke yake na data tunazo zote, sasa najua kuna Wizara ya Fedha baadaye mbele lakini kwa sababu ni suala la *policy* na amelitoa maamuzi nataka kuweka msingi tu kwamba, sisi kwanza hatujaridhika na ule uamuzi na kwamba tutawasilisha hoja yetu rasmi ya kwamba haturidhiki na kuundwa kwa *Auditor General* badala yake tunapendekeza bado *select committee* ya Bunge kwa sababu bado maeneo ambayo ni makubwa sana na matumizi makubwa sana tuliyoyagundua yanahitaji Bunge kwa mujibu wa Sheria na Katiba ya nchi. Katiba ya Nchi inalitaka Bunge kifungu 63 kusimamia Serikali, tunafikiria kwamba Bunge lina-*lowly* yake na Serikali ina *lowly* yake mbali. Serikali inaweza kuendelea na uchunguzi wake, lakini *lowly* ya Bunge kama Bunge bado inasimama pale pale na inahaja ya Bunge kufanya kazi yake. Sisi tunafikiri huu ni msingi na tutaulinda msingi huo kwa hiyo tungependa hili tu kuweka *position* yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili ni kwamba nilielezea suala la mafuta Pemba, nilitegemea Waziri Mkuu atatoa statement, hakusema chochote katika majibu yake yote, suala la mazungumzo ya uchimbaji wa mafuta Pemba, ambayo mazungumzo mlikuwa mnayafanya na Waziri Kiongozi kwa muda mrefu lakini hukulitolea maelezo yoyote, tulitaka kupata maelezo ya hayo mawili.

**MWENYEKITI**: Hilo la *BOT* tutasubiri wakati muafaka ambao mnadhani unafaa, na natumaini hakuna mwingine tena anasimama kurudia hayo hayo labda hili la mafuta sasa.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kwa kuuliza suala la mafuta, kama nilivyosema katika hotuba yangu mazungumzo ya kero za muungano ni mazungumzo ya endelevu, hatuwezi kuyaanza leo na kumaliza kesho. Tufahamu kwamba hizi ni nchi mbili zilizoungana zikiwa na haki sawa, kila mmoja kila upande wake kuwa na haki sawa. Ni kweli tumezungumza suala la mafuta, tumekubaliana kutafuta *consultant* atakayetushauri kama tukipata mafuta mgao uweje, *consultant* ametafutwa amekwishapewa *term of reference* atakapokamilisha kazi yake tutaiweka *Public*, kwa sasa tunaendelea na mazungumzo. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na kama ulivyosema la BOT sitarudia, lakini kwa kuwa nilileta ile hoja basi huko mbele tutakapofika hoja itawasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie sasa kifungu cha 261100 kama nilivyoseama wakati wa mchango niliomba maelezo ya kina kuhusu suala la kuhamia makao makuu. Kama nilivyoeleza kuna Wizara zilizohamia Dodoma na kwa bahati nzuri Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa Waziri wa Maji ni mmoja wapo waliohamia na tulimpongeza kwa kazi hiyo lakini kwa bahati mbaya hata zile Wizara zilizohamia Dodoma, sasa zimerudi Dar es Salaam, naambiwa Wizara ya Maji iko Ubungo, Wizara

ya Ushirika iko njiani kuhama na Wizara sina hakika kama Ofisi ya Waziri na yenyewe inahamia au vipi, lakini tulitaka kujua na kama nilivyosema kuna maneno mengi tu mtaani na wananchi wakisema sisi tukiyapokea ni lazima tuyaulize hapa. Tuna maneno kwamba tunaigarimu taifa kwa kuwa na ofisi Dodoma na tuna ofisi Dar es Salaam, hasa kwa zile Wizara ambazo zinazaniwa zimehamia lakini ziko pia Dar es Salaam na kwa kuwa shughuli nyingi ziko Dar es Salaam. Hata wale walioko Dodoma lazima warudi Dar es Salaam muda mrefu. Sasa tulitaka kujua, kama tunatumia bilioni 3 sasa Dar es Salaam sasa kujenga makazi ofisi mpya ya Waziri Mkuu ni kwanini au ni kitu gani kinazuia bilioni tatu hizo zikajenga ofisi ya Waziri Mkuu Dodoma ili adhima yetu ya kuhamia Dodoma kweli iwe hadhima iliyothibitika kimatendo, nashukuru.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo ya Mheshimiwa Dr. Slaa, nilitoa maelezo asubuhi ya jinsi tunavyohamia Dodoma. Kuhamia Dodoma ni mkakati na Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Dr. Slaa hahitaji kutufundisha mkakati bora wa kuhamia Dodoma. Kwa shilingi milioni tatu anazozizungumza si kujenga ofisi mpya, ni zile ofisi zilizoko pale ambazo zimepasuka na majengo ya zamani ambayo yanafanyiwa ukarabati sio ofisi mpya inajengwa Dar es Salaam. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutumia kifungu cha 81(2)(b) sijaridhika na maneno ya Mheshimiwa Waziri Mkuu tunapohoja hapa, tunahoji kama Wabunge bila kujali tumetoka chama gani, wananchi wangu wa Karatu ambao sio wa CCM pia wanalipia kodi. Kwa kauli ya Waziri Mkuu si kauli ambayo inatusaidia kwa sababu katika hoja tumesema Watanzania wote, wa vyama vyote tunalipia, sasa kama ilani ya chama kimoja kinafanya wananchi waendelee kugharamia na tusihoji mimi nafikiri si sahihi, mimi ningependa kupata maelezo. Nilikuwa nimesema kwamba napenda maelezo si siasa, maelezo nayoomba ni kama tunaendelea kujenga Dar es Salaam je, Waziri Mkuu anatuambiaje kwamba huu mkakati ambao unaendelea miaka nenda rudi na tunaendelea kujenga Dar es Salaam kwa nguvu zote, ni lini mkakati huu basi tunataka kuona programu ambayo Waziri Mkuu atatuambia polepole au hii awamu kwa awamu tungetaka kujua ratiba ya awamu kwa awamu ili tuweze hata kuwaambia wananchi wetu kwamba hela mnazolipa ni kweli zinatumika vizuri lakini akitujibu hivi kisiasa mimi nafikiri si sahihi kwa sababu wananchi wote wa Tanzania wanalipa na hata wale ambao tumepiga kura lakini si CCM tumepigia kura CCM na wote tunalipwa kodi zinazofanana.

**MWENYEKITI:** Nikukumbushe mambo mawili tu, Mheshimwa Dr. Slaa kwamba wewe pia unaulizia kisiasa na anayekuruhusu kuhoji ni Mwenyekiti ambaye ni Spika sio Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Nakushukuru kwa ufafanuzi huo Mheshimiwa Spika, mimi namshangaa rafiki yangu Dr. Slaa, tutahukumiwa sisi kwa Ilani yetu baada ya miaka mitano hapo ndio watanzania mlisema mtahamia Dodoma kwa utaratibu huu umefikia wapi, mmedanganya au mmetekeleza watatuhukumu baada ya miaka mitano sio sasa. Lakini asubuhi nilieleza mkakati wetu wa kuhamia Dodoma, tatizo hapa ni uelewa, sisi

tumesema na miundombinu ndio, Mheshimiwa Slaa, anafikiria ukihamishia Wizara zote hapa kesho basi ndio umehamia makao makuu. Katika Ilani yetu tumesema tunaanza na miundombinu na nimeeleza asubuhi hapa, miundombinu ya barabara, miundombinu ya elimu, miundombinu ya maji hayo ndio sisi mkakati wetu wa kuhamia Dodoma na tutahukumiwa na wapiga kura baada ya miaka mitano tumetekeleza vipi Ilani yetu ya Uchaguzi. Kwa sasa ningependa kumhakikisha Mheshimiwa Dr. Slaa, hii ni awamu ambayo imehamia Dodoma kwa kasi kubwa kuliko awamu nyingine zote na ni vizuri ukatambua hivyo. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana programu ya 10 sub vote 1001 na basic Salary ya Mheshimiwa Prime Minister ni sub vote 250100. Wakati nachangia nilizungumza kwamba hakuna mtu amaye anakataa wananchi kuchangia ujenzi wa *Secondary School*. Lakini niliweka angalizo kwamba kwa uzoefu ambao tumeona msukumo ambao unaotoka kwa *Regional Commissioners* ambao wako chini ya *Prime Minister* umefikisha mahali ambapo watu wanachanga kwa lazima na wanadhalilishwa kiasi cha kuchukuliwa vitu kama hivi ambako kuna kuku, kuna chungu cha kupikia, kuna baiskeli…

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa John Cheyo picha peke yake za vyungu na nini hatujui umezitoa wapi, zinathibitisha vipi kwamba vyungu vya watu vinaweza kuwa umepiga picha Dodoma hapa hapa? Tutajuaje ni vya Bariadi hivyo?

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unataka ninaweza nikakuridhisha kuwa kwamba vimetoka Ibunju ambayo ni Bariadi, lakini nimetoa tu kueleza point yangu ni kuwa kwamba wakati nachangia nimesema labda basi ni vizuri ili kuweza kuwasaidia hawa wananchi kwanza Waziri Mkuu akatamka bayana kwamba michango si lazima na hili nasema ni jambo la maana sana hata kwa nilivyomsikia kwa hotuba yake leo asubuhi kuwa kwamba mnapaa ili mfike kule mnakopalia ni wananchi wasidanganywe kuwa wataletewa maisha bora kwa kila Mtanzania lakini ile ilani haijasema kwa gharama ya nani wala haijasema ni kwa michango. Sasa lakini sisi hatubishi juu ya michango ninachotaka tu kusikia kutoka kwa Waziri Mkuu basi kama vile mlivyo na uwezo wa kuweza kuhamasisha watu watu wahamasihwe kuchanga na wachange kwa kiwango kisichozidi uwezo wao, na katika hotuba yangu katika mchango wangu nilisema angalau 5000 lakini isiwe 50,000, 100,000 kwa lazima, nyinyi mnaweza kusema MMh, lakini huo ndio ukweli. Kwa hiyo mimi kwa niaba wananchi wa Bariadi nataka tamko la Waziri Mkuu kwanza si lazima, pili kiwango kile kisizidi uwezo wa wananchi.

**MWENYEKITI**: Mimi ningependa Mheshimiwa Waziri Mkuu nimuite Mheshimiwa Chenge, kwa sababu *Bariadi District* ina majimbo mawili, je, inakuwaje iwe upande wa Mheshimiwa Cheyo, isiwe upande wa Mheshimiwa Chenge, hebu Mheshimiwa Chenge tusaidie kidogo.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti,nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi kwa niaba ya Serikali niweze kusema kidogo kuhusiana na haya

madai ya Mheshimiwa Momose Cheyo, kama tunavyofahamu wote Wilaya ya Bariadi ina majimbo mawili ya uchaguzi, na ametaja kijiji ambacho anadai ndio picha alizozichuku Ibulyu iko katika Jimbo la Bariadi Magharibi, ambako Mbunge wake ni mimi mwenyewe, kama ni aina ya uchokozi unaweza kuona sasa.Lakini Wilaya ya Bariadi imeitikia vizuri san asana suala zima la ujenzi wa sekondari. Kwa nguvu za wananchi, kwa hiari yao wenyewe kwa utaratibu ambao wamejiwekea wameweza kujenga zaidi ya shule za sekondari 40. Na siku hiyo alipopita Mheshimwa Mbunge katika kata ya jimbo la Bariadi Magharibi ambapo wananchi walikuwa katika hamasa ya ujenzi wa sekondari na nyumba za walimu. Alileta kebei na kuwachochea wananchi waache ujenzi wa shule na nyumba za walimu.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Hiyo siyo sawa.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Lakini wananchi wenyewe waliona umuhimu wa shule yao, waliendelea bila hata kumsikiliza Mheshimiwa John Cheyo.

Nimalizie kwa taarifa tulizonazo, mimi mwenyewe kama Mbunge wa Bariadi Magharibi, Jimbo la Mheshimiwa John Cheyo la Bariadi Mashariki hata bati moja au mfuko mmoja wa cement hajachangia. Lakini watoto wanaosoma katika shule hizi ni watoto wetu wote, ni watoto wa Bariadi na watoto wa ndugu zake na ndugu zangu na wajomba zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona niyaseme hayo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Kwa kutumia kanuni 81(b) kwanza pamoja na kuheshimu Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu nililotegemea ni kutoka kwa Waziri Mkuu, sio Serikali, lakini hilo la kwanza nitaliacha.

La pili, sikutaka tuwe na marumbano hapa ya Bariadi mbili, kwa sababu mambo ambayo ameyasema Mheshimiwa Chenge si kweli. Leo unaweza ukapiga simu Bariadi, mtu wa kwanza kuchangia mshahara mdogo unaonipa Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mimi, shilingi milioni 2.5 kwa *cheque* na *cash.*

Kwa hiyo, anayoyasema ni uwongo mtupu na wanaomsikia sasa hivi kwamba hakuna wanaokamatiwa kuku wao kama wanajua anajidhalilisha yeye mwenyewe kwa sababu ni ukweli mtupu. Tuache hayo mambo ya Bariadi. Ninachosema, hakuna anayekataa kuchangisha, ninachotaka ni mwongozo hata kwenye Serikali, unaambiwa hata kama mtu ana deni, kuna asilimia ambayo huwezi ukaikata, leo unasema huyu mtu anapata chini ya dola moja kwa siku, huwezi ukachukua shilingi laki moja kwa nguvu. Hayo ndiyo ninayoyasema kule Bariadi, wananchi nimeshawaambia wachange kama ninavyochanga mimi na ninasema awamu kwa awamu na ndio maana tumezijenga zile shule kwa kushirikiana. *Very simple* tu, nataka *statement* kutoka kwa Serikali kwamba, tunapowaomba wananchi mchango ni mchango wa hiari, tuwahamasishe. Pili, *equation* kutoka kwa Waziri Mkuu kwamba, jamani msiwachangishe watu kwa sababu unataka tu Waziri Mkuu atakapopita akute shule zimeshajengwa.

Hilo tu ndilo ninaloomba na wala mimi siwatakii mabaya watu wa CCM mimi nina hakika Mheshimiwa Rais anataka awamu ya pili lakini sidhani kwamba wanaochangisha kwa nguvu wanamtakia mema Rais kwa sababu michango ya nguvu haiwezi ikatoa kura ambayo Mheshimiwa Rais aliwaambia wananchi nitawaletea maisha bora kwa watanzania wote na hakusema kwa kuwachangisha kwa nguvu mpaka kuchukua sufuria zenu za chakula. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sababu na mimi natoka kwenye utamaduni huohuo, unaweza kusimama hapa Mheshimiwa John M. Cheyo ukasema kwamba, utaratibu wetu wa *Masumle* katika makabila ya Wanyamwezi na Wasukuma ni kulazimisha?

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Masumle* ambayo ninayasema ni kwamba, kwa mfano, sisi tunasema kwamba anapigwa *mchenya, mchenya* haukuwa unakwenda unachukua mabaki ya mtu sisi tumefika mahali Bariadi mtu anasimama anasema ...

**MWENYEKITI:** *Mchenya* unachukua nini? Tujibu.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kidogo.

**MWENYEKITI:** Kama nini?

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Unachukua kitu kidogo kama vile unaweza kuchua chumvi, lakini huchukui baiskeli na kuku ya mtu. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Kwa karne ya 21 hiyo unayoiita chumvi sasa hivi hata sufuria ni sehemu ya *mchenya* tu. Kwa hiyo, tunaendelea Mheshimiwa Haroub Said Masoud .

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Nataka jibu, naomba jibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tusimuache hivihivi, tatizo hapa ni lile nililosema asubuhi tumeanza kupaaa, yaani ndege imeanza kupaa ndiyo inayompa mataizo Mheshimiwa John Cheyo. *(Makofi)*

Wilaya ya Bariadi na Mkoa mzima wa Shinyanga ni moja ya Mikoa ambayo ilikuwa nyuma sana kielimu na ndiyo maana kulikuwa na matatizo ya kuua akina mama wenye macho mekundu wanasingiziwa lakini kumbe ni degedege, kulikuwa na tatizo kubwa sana la elimu.

Baada ya Mkuu wa Mkoa mpya kwenda kule Brig. Gen. Balele, amefanya kazi nzuri sana. Nataka kuchukua nafasi hii kuupongeza uongozi wa Serikali katika Mkoa wa Shinyanga na hususan Bariadi, wamefanya kazi nzuri sana. Wamefanya kazi nzuri kiasi ambacho wameongoza katika Mikoa, yaani katika Mikoa iliyoongoza kwa kupeleka wanafunzi Sekondari, Mkoa uliokuwa nyuma kabisa ni Shinyanga, sasa hivi umefanya vizuri sana, umepeleka wanafunzi wote Sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, huyu Mheshimiwa kinachomsumbua ni kwamba, mafanikio haya ni makubwa sana, yanampa tabu rohoni. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa John Cheyo, bado unataka kusema tu? Sasa haya yatakuwa ni marumbano.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo marumbano, naomba basi mtumie njia ambayo basi nitashika mshahara. Maana yake mimi ninachoomba ni kitu kidogo tu, yaani naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aseme michango ni hiari, *that is all*.

La pili, aseme pawe na kiwango ambacho kinatekelezeka siyo kwa nguvu, *that is all*.

**MWENYEKITI:** Sasa Mheshimiwa John Cheyo kwanza, nikusaidie tu. Ukienda nchi ya jirani kama Kenya, usije ukasema unaomba kitu kidogo, utakamatwa kwa rushwa. *(Kicheko)*

Basi sijui sasa kama kweli nahitaji majibu, maana yake tunaelewa jinsi inavyotekelezwa ni hiari lakini unapigwa faini za kawaida za jadi kwa kutokutekeleza. Sasa wapo wakorofi, hata ufanye nini wapo wakorofi wanakataa, hao ndiyo wanaweza kuwa wanalalamika. Tunaendelea Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

*Vote 37 - Program 10, Sub Vote 1001***,** *item 250100,* Mwaka juzi nilipokuwa nikichangia nilieleza ubadhirifu au uzembe wa matumizi mabaya ya Serikali na Mheshimiwa Waziri Mkuu, leo asubuhi alipokuwa akijibu kwenye majumuisho yake, alieleza hatua zilizochukuliwa zaidi kwenye Halmashauri ikiwemo baadhi ya waliohusika kufukuzwa kazi au kushushwa vyeo. Lakini sikusikia hatua zilizochukuliwa kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, ambapo nilieleza bayana kwamba, nako kuna matatizo kama haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kulikuwa kuna hoja hiyo lakini katika jibu letu, ubadhirifu ambao ulikuwa unazungumziwa kwa upande wa ofisi yetu katika Fungu hili la 37, ilihusika stakabadhi ambazo zilikuwa hazikupatikana wakati wa kufanya uhakiki na *Auditor* tayari alishapewa akahakiki na suala hilo likafungwa. Kwa hiyo, hakukuwa na hoja yoyote kwa pale. *(Makofi)*

**MHE. MWANAWETU SAID ZARAFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Vote 37, Kifungu kidogo cha …

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, nadhani huna hoja.

**MHE. MWANAWETU SAID ZARAFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana, ni kifungu kidogo namba *261100 - other goods and service not classified above*. Kifungu hiki nilikuwa nimeuliza kuhusu *By-laws* za Halmashauri ambazo hazijapitishwa. Kwa hiyo, naomba leo hii Mheshimiwa Waziri Mkuu, anifafanulie ni lini Halmashauri yetu ya Kilwa hizo *By-laws* zetu tutaweza kupitishiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Kwanza *By-laws* zinapitishwa na Halmashauri, labda hazijawekwa saini na Waziri?

**MHE. MWANAWETU SAID ZARAFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu kumjibu Mheshimiwa Mbunge, kwa maana ya kutoa ufafanuzi juu ya hizo kama ifuatavyo:-

Ni kweli Kilwa wameleta hizo Sheria Ndogo, tumezihakiki pale ingawa zilikuwa na makosamakosa kidogo lakini mengine tuliyarekebisha na tunafikiri baada ya muda si mrefu, tutakuwa tumepata idhini kwa sababu ndiyo tumempelekea Mheshimiwa Waziri Mkuu na baadaye tutazirejesha. Lakini tunakiri tumeshazipata tunafikiria kuziondoa wakati wowote.

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Langu lilikuwa juu ya kuhamia Dodoma, lakini kwa sababu limeshaulizwa naondoa hoja yangu.

**MWENYEKITI:** Kwa sababu limekwisha jibiwa, sawa. Mheshimiwa Tatu M. Ntimizi.

**MHE. TATU M. NTIMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Sub-Vote 1001,* Kifungu 250100 - Mshahara wa Waziri Mkuu. Katika majumuisho yake mchana huu, alizungumzia kuhusu gharama za uanzishaji wa maeneo ya utawala kama Mikoa, Wilaya, Tarafa, Kata na Vijiji. Ni kweli nafahamu kwamba zina gharama zake, lakini kuna tamko ambalo Rais Mstaafu alitamka, Kata ya Igalula kwenye Jimbo langu la uchaguzi na Tarafa ya Kizengi na Kata ya Kigwa. Sasa pamoja na gharama zilizopo, tamko hili la Rais Mstaafu ina maana haitaenziwa kutokana na gharama alizozungumza Mheshimiwa Waziri Mkuu au tuwaambie vipi wananchi kwamba tusubiri katika orodha ya kawaida licha ya kuenzi tamko alilolitamka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Kabla Serikali haijajibu, tamko linasema nini? Ni lazima tuelewe tamko linasema kitu gani.

**MHE. TATU MUSA NTIMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2004 alipokuja Rais Mstaafu katika jimbo langu la uchaguzi, pamoja na Halmashauri kuandika kuomba Tarafa katika jimbo hilo, bado wananchi wanaendelea kusubiri kama watapata enzi hiyo. Basi katika kusubiri sana alipofika Rais ikabidi wamweleze kwamba, wamesubiri sana hali ya Tarafa ilivyo, hali ya Kata ya Igalula ilivyo, basi akakubaliana na maelezo waliyokuwa wamemweleza viongozi kuanzia mkoa mpaka Tarafa yenyewe.

Mheshimiwa Rais Mstaafu akasema basi natamka kwamba, Serikali igawe Tarafa hiyo na iwepo Tarafa ya Kizengi na akatamka kwamba, Kata ya Kigwa itakuwepo. Sasa bado utekelezaji unasuasua na leo baada ya kuelezwa hayo bado wananchi wanauliza, kwa hiyo, tamko lake halikuenziwa, tusubiri utaratibu wa kawaida kutokana na fedha.

Sasa wananchi hawatanielewa, naomba ufafanuzi kwamba matamko hayo aliyoyatamka Rais Mstaafu, yatafuata mlolongo mwingine tena upya au yatatekelezwa kama alivyokuwa ametamka Rais?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maelezo ya ufafanuzi kuhusiana na suala ambalo amelielezea Mheshimiwa Tatu Musa Ntimizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, analolisema ni kweli na Rais Mstaafu wakati ule aliona jambo hili lije lishughulikiwe katika awamu inayofuata na tuliarifiwa na ofisi yangu imekuwa ikiyafanyia kazi, si hilo tu na kama mlimsikiliza vizuri Mheshimiwa Waziri Mkuu, amejaribu kuonesha maombi tuliyokwisha kuyapata mpaka sasa ni mengi, kilichofanya tukachelewa kwenda na mojamoja ni kwa kwa sababu tuliona ni vizuri tulifanye zoezi hili kwa upana zaidi.

Kwa hiyo, kufuatia jambo lile tuliamua kuomba Halmshauri na Wilaya zote tupate maombi yao ambayo tuliyapata na kwa sasa kwa kweli kilichobaki walikuwa wanakamilisha uchambuzi na baada ya hapo tutawasilisha kwa maana ya vipaumbele maana hatuwezi kwa yote. Kwa hiyo, tutazingatia yale yaliyotokana na ahadi lakini vilevile tutatazama vigezo vingine ikiwa ni pamoja na ukubwa wa maeneo katika kumaliza hilo ambalo analiomba. Lakini tunalijua na tunafikiri asiwe na mashaka juu ya jambo hilo.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi nitauliza katika *Vote 37 Program 10, Sub Vote 1001*, Kifungu cha 260200, pamoja na Kifungu cha 26100, yaani hicho cha kwanza cha *Education Materials, Supply and Services* halafu na cha *Utilities*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata maelezo ya Kikatiba kwa sababu hatuwezi kuendesha Serikali kwa njia ambayo ni ya kutumia mila na desturi za kibabila na makabila mbalimbali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe, nenda kwenye kifungu tupo kwenye Kamati ya Matumizi.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo. Ninapenda kujua ya kwamba katika *Education Materials and Supplies,* Ofisi ya Waziri Mkuu na Waziri Mkuu mwenyewe amezungumza ya kwamba, zimejengwa shule 1,084 na wananchi. Sasa hizo fedha ambazo zimetumika kujenga na hayo *materials* ndiyo ambayo sioni *categorisation* yake hapa kwamba zimeingia katika *vote* ipi kwa sababu hizo ni fedha ambazo zimetoka kwenye mifuko ya watu na siyo fedha za Serikali na ni fedha ambazo zilikuwa tayari zimeshalipiwa kodi ziko kwenye mifuko ya watu. Kwa sababu alituambia kwamba watu wanachangia harusi lakini hizi fedha za harusi ndizo ambazo tayari zimeshalipa kodi; sasa hizi ambazo zimejenga hizo shule zote zimewekwa katika *vote* gani? Kwa sababu sisi hatuwezi kupitisha vitu ambavyo havipo katika bajeti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chacha Wangwe, hapa tunazungumzia bajeti ya Serikali, yaani mchango wa Serikali katika shughuli mbalimbali, Bunge hili haliwezi kukaa hapa kutazama michango yote iliyochangwa na iwekwe humu, hiyo ni michango ya wananchi unaweza kuiulizaHalmashauri yako ya Tarime. *(Makofi)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna michango ambayo inatolewa na wafadhili ambayo tumeambiwa ni 42% ya bajeti yetu na hawa ni wafadhili wa ndani. Sasa yenyewe iko wapi, maana hatujui ni *percentage* ngapi, ndivyo ninavyouliza kwa sababu ni kitu ambacho kimezungumzwa hapa na Waziri Mkuu.

Wale waliochanga vilevile wanatakiwa wajue *for the record* kwamba, wamechangia shilingi bilioni ngapi na kwa sababu wamesema kwamba hilo zoezi litakuwa ni endelevu, litaendelea mpaka kwa Zahanati na Vituo vya Afya, basi wajiandae ili wajue ni kiasi gani ambacho wanatarajiwa tena kuendelea kufadhili pamoja na kwamba ni michango kama ilikuwa ni ya nguvu au ya hiari lakini ziko wapi? Hazionekani hapa, hiyo ni moja.

La pili, katika 26100 - *Utilities,* Waziri Mkuu amezungumzia kuhusu Mbuga ya Serengeti, ambayo inapakana na Jimbo langu la Tarime na ameeleza *utilities* ambazo Serikali inataka kuzijenga ndani ya mbuga hiyo na akaeleza hata wingi wa ndege unaotua kwa upande wake wa Umasaini …

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chacha Wangwe, hivi vyote viwili nakuvumilia tu, cha kwanza *Education Materials and Supplies* ni kwa maana ya Ofisi ya Waziri Mkuu ndani ya Ofisi wala siyo Mikoa au hayo unayosema ni pale kwenye Idara ya Utawala kuelimisha watumishi wa Ofisi wa Waziri Mkuu.

La pili, *utilities* ndiyo dogo kabisa wala hicho unachosema hakihusu ujenzi wa viwanja vya ndege na vitu vya namna hiyo.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana lakini nafikiri *message sent*. *(Kicheko)*

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika mchakato unaoendelea kati ya Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Kiongozi wa kutatua kero za Muungano, kuna suala zima la mgawanyo wa ...

**MWENYEKITI:** Fungu gani Mheshimiwa?

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani. Ni *Vote 37, Program 10, Sub-Vote 1001, item 250100* - Mshahara wa Waziri Mkuu.

Kuna suala zima hili la mgawanyo wa pesa za wahisani, tuna mradi huu mkubwa wa *SDP,* ambao ni wa miaka saba, utagharimu shilingi trilioni 2.5 na mwaka huu peke yake, imetengewa kutumia shilingi bilioni 53. Nataka kuuliza katika hili, nafasi ya Zanzibar iko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, mchakato huu wa kuhimiza ujenzi wa shule kama walivyoeleza wenzangu sitaki niingie katika malumbano, shule nyingi zimejengwa lakini ni kweli kwamba, malalamiko yapo na hata Waziri Mizengo Kayanza Peter Pinda kakiri asubuhi hapa.

Sasa asubuhi kwa bahati nzuri Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, amesema kwamba, kutakuwa na mkutano na Wakuu wa Mikoa wote kuhimiza kilimo. Sasa wasiwasi wangu au masuala yangu yako hapa kwamba, je, uhimizaji huu wa kilimo utakuwa sawasawa na ule wa elimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Jaribu kufafanua hilo la pili utakuwa sawasawa namna gani sasa.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa sababu huu wa elimu kama tulivyosikia Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Phares K. Kabuye na sasa hivi Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe kwamba, umekuwa na matatizo ya manung'uniko ya watu namna ulivyofanywa ulikuwa unaleta kero kubwa kwa watu.

Sasa huu wa elimu ambao utakuwa pengine ni mradi au mchakato mkubwa zaidi, je, *methodology* yake itakuwa ni ileile au kuna mpango maalumu umeandaliwa? Labda tungepata maelezo hapa. Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Kwa kweli Waheshimiwa Wabunge leo sijui vipi, lakini Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, ufafanuzi tafadhali.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kutoa ufafanuzi kidogo tu kwamba, Mpango wa *ASDP* ulipangwa kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali mbalimbali ambazo zinachangia katika *Agricultural Basket Fund*.

Suala la sehemu ya pili ya Muungano, tumelizungumza baina yetu na wenzetu wa Zanzibar na tumekubaliana ya kwamba, kupitia Hazina mpango mahususi wa aina hiyo, utatengenezwa kwa ajili ya Zanzibar. Kwa hiyo, hivyo ndivyo makubaliano yalivyo na hakuna tatizo lolote baina ya sehemu hizi mbili za Muungano.

Kuhusu utaratibu gani unatumika kwa ajili ya kutekeleza *ASDP* kwamba, itakuwa ni kama elimu, sijui kinachozungumzwa juu ya elimu ni kitu gani, kwa sababu hata maelezo ambayo alikuwa anayatoa Mheshimiwa John M. Cheyo, kwa kawaida hiari inaanzia kwenye makubaliano, mkisha kukubaliana hiari inakwisha, utekelezaji unaanza na sasa kama ni hiari tu, inaweza ikawa hiari ya kuacha vilevile kutekeleza ambayo nadhani hata katika *Democracy* hiyo si sahihi.

Lakini kwa upande wa *approach* yetu kuhusu kilimo vilevile kuna hiari kwa sababu miradi yote inayotekelezwa chini ya *ASDP* inatokana na maamuzi ya wananchi wenyewe, wanaibua mradi kwa hiari halafu utekelezaji unafuata. Sasa hiari ikija wakasema tunamwagilia halafu wewe ukachukua maji ukayapeleka mtoni badala ya shambani, hiari ile vuruga maamuzi ya utekelezaji. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hiyo, hiari inaendelea inaanzia kwenye kuamua halafu utekelezaji unakwenda na Kanuni zinazoweka jamii pamoja katika kutekeleza.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts*………... Sh. 564,403,500
Kif. 1003 - *Policy and Planning* ............. Sh. 2,100,001,700
Kif. 1004 - *Information, Education and Communication* ......................................... Sh. 117,656,200
Kif. 2001 - *Civil Affairs Contingencies* … Sh. 720,110,100
Kif. 2002 - *National Festivals* …………… Sh. 433,620,300
Kif. 3001 - *Parliamentary and Political Affairs* ......................................... Sh. 268,228,200
Kif. 5001 - *Coordination of Government Business*…................................................ Sh. 500,327,400
Kif. 7001 - *Government Printer*……… Sh. 2,205,221,100

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

**Fungu 42 – Ofisi ya Spika**

Kif. 1001 - *Administration and General* … Shilingi 5,511,204,200

Kif. 2001 - *National Assembly*…………. Shilingi 36,895,218,800

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 56 – TAMISEMI**

Kif. 1001 - *Administration and General* ...... Shilingi 2,188,670,700

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Vote 56, *Sub Vote 1001*, Kifungu kidogo 250100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Pangani, inaidai Kampuni ya *Amboni Limited* shilingi milioni 79, tumepata barua kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu baada ya kuipeleka Mahakamani kwamba tuondoe shauri hili Mahakamani na kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu italishughulikia na kulipatia ufumbuzi wa kudumu.

Suala hili lina *audit query* kwa miaka mingi bado halijafutika na wanahimiza kwa nini hili deni halilipwi. Sasa vikao mbalimbali vimekaa ndani ya Halmashauri hata katika vikao vya Mkoa vya *RCC* na kwamba hili deni kisheria Halmashauri ni lazima ilipwe. Lakini toka Ofisi ya Waziri Mkuu kusema kwamba, italipatia ufumbuzi wa kudumu toka mwaka 1999 hadi hii leo hatujalipwa fedha hizo.

Mimi naomba nipate ufafanuzi kwani hizi fedha tunazihitaji na tuna madeni tunataka kulipa na tunategemea mapato kutoka maeneo mbalimbali ili tulipe madeni hayo. Sijui tutapata maelezo gani kutoka Serikalini? Ahsante sana.

**WAZIRI WA NCHI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Mohamed R. Abdallah kwa kuleta jambo hili mbele yako.

Tumesema tutalishughulikia jambo hili kwa sababu tumegundua kwamba, tuna matatizo yanayofanana na yale ya Pangani katika maeneo mengi kidogo, tuna mgogoro huo Karagwe kwa upande wa kahawa lakini tumegundua vilevile kwamba tuna migogoro mingine kwenye mazao mengine ambayo ni ya biashara. Kwa hiyo, tumeona kwamba badala ya kuhangaika na jambo moja, kama Serikali tumeona tukusanye maeneo haya yote tukae chini na Mheshimiwa Waziri Mkuu tumshauri, kwa sababu wenye uwezo wa kuishauri Serikali kufuta madeni ni Ofisi hii. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah kwamba, hatukufanya hivi kwa sababu tunataka kulipuuza hapana, lakini kwa sababu tumeona mambo haya kumbe yako katika maeneo

mengi kidogo. Kwa hiyo, yote tuyachanganue kwa pamoja halafu tutoe uamuzi ambao tunadhani utasaidia Halmashauri zote, ambazo wanadai vyombo hivi vya kibiashara katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* ......... ...... Sh. 352,417,800
Kif. 1003 - *Policy and Planning Division* ...... Sh. 496,119,600
Kif.1004 - *Management Information Systems Division* .................................................... Sh. 396,577,500
Kif. 1005 - *Legal Services Limited* ............. Sh. 327,022,600
Kif. 1006 - *Internal Audit Unit* ......................... Sh. 227,771,100
Kif. 2001 - *Regional ADMN Coordination Division* ..................................................... Sh. 721,521,900

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 - *Management Services* ................ Sh. 12,492,968,200

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kifungu kidogo cha 261100 - *Other Goods and Services.*

Asubuhi Mheshimiwa Waziri alijibu ...

**MWENYEKITI:** Lakini una habari kwamba, kifungu hicho kinahusu *Honorarium,* Gharama za Mazishi na *Supplies Debts* ndiyo *Other Goods and Services.*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hakuna kinachoonesha hicho, kwa bahati mbaya na Mbunge anapopata *Other Goods and Services* hatujui hapa Bungeni hiki kifungu kimeandikwa tu *Other Goods ...*

**MWENYEKITI:** Ulikuwa na muda wa kuiuliza Serikali, ni wajibu wako, sasa hilo unalotaka kulisema liweke kwenye kifungu kinachohusika ama sivyo tutakuwa tunavunja Kanuni tunaenda ovyo tu. Umekwama? Tunaendelea.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2003 - *Sector Coordination Division* ........... Sh. 66,167,273,000
Kif. 3001 - *Organizational Development Division* ... Sh. 5,992,088,600

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya*

*Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 61 - Tume ya Uchaguuzi**

Kif. 1001- *Administration and General* ...... Sh. 10,416,712,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 91 – Tume ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya**

Kif. 1001 - *Administration and General* .......... Sh. 1,148,416,000

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu – 92 Tume ya Kudhibiti UKIMWI**

Kif. 1001 - *Administration and General* ............. Sh. 295,660,000
Kif. 1002 - *Finance ADMN and Resource Mobilization* .......................................................... Sh. 2,333,880,500
Kif. 1003 - *Monitoring, Evaluation, Research and MIS* ................................. .............. Sh. 219,325,000
Kif. 1004 - *Advocacy Information Education and COMM* ................................................... Sh. 397,362,500
Kif. 1005 - *District and Community Response* Sh. 391,590,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. PHOEBE MMBAGA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Kanuni ya 81(2)(a) tunasoma mafungu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, yaani fungu zima la Mkoa, hatuendi kwenye mshahara na vitu vya namna hiyo.

Fungu 70 - Mkoa wa Arusha .................. Sh. 39,048,122,000
Fungu 71 - Mkoa wa Pwani ................ Sh. 32,754,701,000
Fungu 72 - Mkoa wa Dodoma ............... Sh. 43,339,072,000
Fungu 73 - Mkoa wa Iringa ................. Sh. 47,673,776,000
Fungu 74 - Mkoa wa Kigoma .................Sh. 33,848,932,000
Fungu 75 - Mkoa wa Kilimanjaro ......... Sh. 54,299,656,000

*(Mafungu yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 76 -Mkoa wa Lindi ...................... Sh. 25,245,862,000
Fungu 77- Mkoa wa Mara ....................... Sh. 40,617,038,000
Fungu 78 - Mkoa wa Mbeya .................... Sh. 58,165,872,000
Fungu 79 - Mkoa wa Morogoro …............ Sh. 48,184,683,000
Fungu 80 - Mkoa wa Mtwara …............ Sh. 30,947,397,000
Fungu 81 - Mkoa wa Mwanza .............. Sh. 66,961,503,000
Fungu 82 - Mkoa wa Ruvuma …........... Sh. 35,204,742,000
Fungu 83 - Mkoa wa Shinyanga …........... Sh. 59,591,131,000
Fungu 84 - Mkoa wa Singida ...........… Sh. 28,907,590,000

*(Mafungu yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 85 – Mkoa wa Tabora …....... .... Sh. 39,096,416,000

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia *Vote* hii, *Progromme 10, Sub-vote* 1001, kifungu kidogo 281300 - *Road Transfers.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikifanya *cross reference* kwamba fedha hizi zitakwenda wapi katika orodha ya barabara zitakazofaidika ni pamoja na Tabora - Kigwa na Tabora - *Singida Border.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu hapa ambayo napenda nipate ufafanuzi wa Serikali ni kwamba, barabara hii kwa kila dalili namna inavyoonekana ni *tracker road*, siyo *regional road.* Kutokana na hali hii, ndiyo maana kwenye fedha zilizotengwa kwenye kifungu hiki ni shilingi milioni 150 tu. Sasa barabara hiyo ni mbaya sana, kuitengeneza kwa shilingi milioni 150 ni kujidanganya. Serikali bora ingelielewa hilo na ikatenga fungu linalostahili hadhi ya barabara hiyo na uharibifu uliokuwepo. Barabara husika ni Tabora-Kigwa-Tabora mpaka Singida *Border*. Matatizo yangu ni mawili; kwanza, iko *classified as regional road* na si kwa sababu inaunganisha Singida - Tabora - Kigoma na kwa kweli inakwenda mpaka nchi za nje. *It should be under track road*. Hiyo ni hoja yangu ya kwanza.

Hoja yangu ya pili, kwa sababu ya kunyimwa *track road* imetengewa shilingi milioni 150, ni fedha ndogo sana kwa umuhimu wa barabara hiyo na kama tunataka kufufua uchumi kwa Mkoa wetu wa Tabora. Nahitaji maelezo ya ziada.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu nitoe maelezo yafuatavyo kwa taarifa anayoitaka Mheshimiwa Kaboyonga. Suala kama barabara hiyo ni *track road* au *regional road,* upande mmoja wa sarafu hiyo hiyo, kwa sababu kama itaangukia upande wa *track road* itasimamiwa na *TANROADS* na kama iko

kwenye *regional road* itasimamiwa na *regional roads*. Kwa hiyo, wasiwasi kwa maana hiyo haupo. Lakini tutaangalia sisi Wizarani ipo katika *classification* ipi tujiridhishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la pili kwa kiwango ambacho wote tunafahamu barabara nyingi nchini sasa hivi haziko katika hali nzuri ikiwemo barabara muhimu ambayo ameitaja Mheshimiwa Mbunge. Kiasi ambacho kimetengwa ni kidogo ndiyo, kwa uharibifu ambao upo katika barabara hiyo, lakini iwapo tutakisimamia vizuri na kuhakikisha kwamba maeneo ambayo ni korofi kabisa yanatengenezwa, nadhani itatuvusha wakati tunakusanya nguvu ya kuweza kuitengeneza vizuri zaidi barabara hiyo katika urefu wote huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia vizuri fedha hiyo si kwa barabara yote, itakuwa ni kwa kilometa chache tu ambazo wamegundua kwamba zimeharibika sana na zinahitaji *intervention* ya haraka sana. Lakini kilio hicho tunakielewa.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa maelezo mazuri. Lakini kama alivyoeleza kiasi kilichotengwa ni kwa maeneo ambayo anasema ni korofi na kwa kweli ni korofi. Napenda nimsaidie kiasi hicho kilichotengwa ni kwa ajili ya kutengeneza kilomita 15 tu katika barabara yote kutoka kwenye *Singida Border* mpaka kufika Tabora Mjini, yaani kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri ni kwamba, katika barabara ile sehemu korofi ni kilomita 15 tu, jambo ambalo si sahihi. Kuna eneo moja la Kizengi katika Mbuga ya Nyaua, ambako bila kuweka madaraja mazuri barabara ile haitapitika kwa sababu haijawa barabara na kujenga daraja moja zuri. Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu ni mtaalam katika hili, anaelewa. Hoja niliyojaribu kuijenga ni kwamba shilingi milioni 150 kwa kilomita zaidi ya mia mbili na kitu, ingawa tunachukua sehemu korofi tu, lakini si kilomita 15. Naomba Mheshimiwa Waziri akubali turudi kwenye *drawing board,* tuone namna tutakaavyoweza kurekebisha hali hii, ili barabara hiyo ipitike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hiyo ndiyo fupi zaidi kuliko hata ile inayotengenezwa sasa hivi kufika Tabora kwa kupitia Manyoni - Singida - Nzega - Tabora. Ukishakuwa Itigi kwenda Tabora unapunguza umbali kwa kilomita takribani 200; sasa kwa nini Serikali hailioni hilo na kujaribu kuitengeneza barabara hiyo ipitike?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hoja yangu ni kwamba, baada ya maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, shilingi milioni 150 kwa barabara hiyo na kwa umuhimu wake ni kama tunacheza tu. Hatujafanya kazi nzuri kwa ajili ya kuifungua barabara hiyo kwa matumizi mazuri na kwa maendeleo ya uchumi wa Tabora, pamoja na Urambo,Kigoma, Kaliua na kadhalika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri unataka kusema. Nadhani inaeleweka tunavyofahamu ni kwamba kuna mipango ya kuijenga kwa lami. Kwa hiyo, hizo ni fedha za kuwezesha kama dharura paweze kupitika.

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 86 – Mkoa wa Tanga ......................... Sh. 51,509,552,000
Fungu 87 – Mkoa wa Kagera .......................... Sh.46,709,072,000
Fungu 88 – Mkoa wa Dar es Salaam ................. Sh.53,818,589,000
Fungu 89 – Mkoa wa Rukwa ............................ Sh.28,642,437,000
Fungu 95 – Mkoa wa Manyara ........................ Sh.28,543,411,000

*(Mafungu yaliyoyatajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu**

Kif. 1001 – *Administration and General* ... Sh.1,783,999,000
Kif. 1003 – *Policy and Planning* ..…  … Sh. 1,412,694,500
Kif. 5001 – *Coordination of Government* Business ... Sh.19,516,168,000
Kif. 7001 – *Government Printer* ......................... Sh. 1,120,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 42 – Mfuko wa Bunge**

Kif. 2001- *National Assembly* …........................... Sh. 312,000,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu – 56 Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**

Kif. 1001 - *Administration and General* …............... Sh. 125,000,000
Kif. 2002 - *Local Government Coordination Division* ...Sh.20,313135,000
Kif. 2003 - *Sector Coordination Division* ................ Sh.7,215,204,000
Kif.3001 - *Organization Development* .................. Sh.23,368,339,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 91 – Tume ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya**

Kif. 1001 - *Administration General* ................… Sh. 400,000,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 92 - Tume ya Kudhibiti UKIMWI**

Kif. 1001- *Policy, Planning and National Response* … Sh. 13,418,395,000
Kif. 1002 - *Finance ADMN and Resource Mobilization* …....................................................... Sh. 1,248,789,000
Kif. 1003 - *Monitoring,Evaluation,Research and MIS* ..Sh. 2,236,400,000
Kif. 1004 - *Advocacy Information Education and Comm.* ........................................................... ..Sh. 9,482,700,000
Kif. 1005 - *District and Community Response* …... Sh. 23,245,925,00

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 70 - Mkoa wa Arusha ................... Sh. 15,987,727,000
Fungu 71 - Mkoa wa Pwani .................... Sh. 16,484,566,500
Fungu 72 - Mkoa wa Dodoma.................... Sh. 16,239,079,000
Fungu 73 - Mkoa wa Iringa ....................... Sh. 18,514,444,000
Fungu 74 - Mkoa wa Kigoma ..................Sh. 12,279,414,000
Fungu 75 - Mkoa wa Kilimanjaro …..........Sh. 7,775,407,000

*(Mafungu yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Fungu 76 – Mkoa wa Lindi …....................... Sh. 15,299,367,000

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikichangia hapa nilizungumza juu ya habari ya hospitali ya Wilaya na ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, kwa kutuahidi kwamba, jambo hili litashughulikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini aliyekoswa na nyoka akikanyaga nyasi humustua. Ni nani atakayeiarifu Halmashauri ya Wilaya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge kifungu gani?

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 76, *Sub-vote* 1001, vifungu vidogo vya 6338 na 6340. Ni nani atawaarifu wananchi wa Wilaya ya Lindi, yaani sisi Madiwani kwamba jambo hilo liliondoka kwa bahati mbaya lakini sasa litarudi, nani atawaarifu.; Waziri wa TAMISEMI au *RAS* ambaye aliamua?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mudhihiri, vifungu hivyo ni vya ujenzi wa *Regional Block*.

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo fedha hizo zimehamishwa zimepelekwa *Regional Block.* Fedha ambazo zilikuwa zijenge Hospitali ya Wilaya zilihamishwa zikapelekwa *Regional Block*. Ndiyo maana hapo

unaona kuna *rehabilitation* jengo hilo hilo na kuna *construction* jengo hilo hilo, mafungu mawili kwa mpigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina ugomvi wa hilo maana Waziri ametuhakikishia. Nataka tu kujua ni nani atakuja kutuambia sisi wananchi wa Lindi. Huyo huyo aliyeondosha hii hapa au ni Serikali, maana mimi siamini kama *RAS* anaweza kuja kulifanya hili. Mtaniwia radhi kwa sababu hamuelewi, sisi watu wa Lindi tunamfahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAMISEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati najibu hoja hapa nilijaribu kulieleza jambo hili na nikajua Mheshimiwa Mudhihir tutasaidiana vizuri tu. Nataka tu kusema kwamba kwanza, kwa kuieleza hapa Bungeni kwa namna alivyolieleza, wapiga kura wake wamemsikia na mimi katika kutoa ufafanuzi wamenisikia vilevile. Lakini pengine kujibu hasa rai yake nimwahidi tu kwamba, sisi tutachukua jukumu la kumwarifu Mkuu wa Mkoa juu ya jambo hili na yeye tutampa kazi ya kwenda kuieleza Halmashauri yake, sasa kama ana tatizo na *RAS,* lakini *Boss* wake ni Mkuu wa Mkoa, kwa hiyo, sisi tutam-*address* Mkuu wa Mkoa.

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 77 - Mkoa wa Mara ............................. Sh.12,794,273,000
Fungu 78 - Mkoa wa Mbeya ................................ Sh.16,351,948,000
Fungu 79 - Mkoa wa Morogoro ....................... Sh. 17,641,273,000
Fungu 80 - Mkoa wa Mtwara ........................... Sh.15,074,279,000
Fungu 81 - Mkoa wa Mwanza …......................... Sh.23,281,837,000

*(Mafungu yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Fungu 82 - Mkoa wa Ruvuma ........................... Sh. 19,070,637,000
Fungu 83 - Mkoa wa Shinyanga ......................... Sh. 19,971,558,000
Fungu 84 - Mkoa wa Singida ............................. Sh. 10,921,044,000
Fungu 85 - Mkoa wa Tabora ............................ Sh. 12,767,180,000

*(Mafungu yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 86 - Mkoa wa Tanga … ......................... Sh. 18,920,762,000

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 86, *Sub-vote 2002 - Economic and Development Support,* kuna miradi mingi ambayo imeorodheshwa hapa kwa ajili ya maendeleo katika Mkoa wa Tanga ikiwemo Wilaya ya Pangani. Naomba tupate kauli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohammed R. Abdallah kifungu kipi?

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema *Sub-vote 2002,* sasa katika hiki kifungu kuna hizi *programmes* zote ambazo zinatakiwa zitekelezwe katika Mkoa wetu. Kwa hiyo, ninazungumza *in general*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, wakati huu ni wa kupitisha makadirio, huwezi ukawa unazungumzia *in general,* huu siyo wakati wa mjadala wa hotuba.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi niende kwenye *Sub-Vote 4202 - Local Government Road Network Programme*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napenda nipate kauli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kama Mkuu wa Serikali, *programme* hii tunahitaji hizi *network* zifanye kazi. Tuna tatizo la Kivuko cha Pangani utekelezaji wake utakuwa ni mgumu. Sasa tunafahamu kwamba, Kivuko cha Pangani *tender* yake ilifutwa na inaweza ikachukua mwaka mzima hatujapata kivuko kingine. Hivi Serikali ina ufumbuzi gani kwa sababu nikija nikahoji tena katika Wizara husika majibu yatakuwa ni yale yale. Angalau basi tupate matumaini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, anatuambia nini katika suala hili. Ahsante sana.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda nitoe tamko la Serikali kuhusiana na Kivuko cha Pangani. Napenda kusema kwamba, tatizo lililokuwepo la kusubiri *no objection* kutoka kwa Benki ya Dunia sasa limekwisha. Juzi wametoa kibali hicho kwa maana ya kwamba, tuweze sasa kutangaza upya zabuni kama ilivyokuwa imekusudiwa na tunakusudia kufanya kwa haraka.

Tumepeleka *message* pia ili tukubaliane, kwa kutambua kipindi kirefu ambacho kimepita tangu tupeleke maombi yetu ya *no objection* na hali ilivyo katika kivuko hicho, tuone kama tungeweza tukaharakisha mchakato huu wa kupata mzabuni atakayetujengea kivuko kipya pale Pangani. Kwa hiyo, kivuko kipya kinakuja, kimechelewa lakini angalau kifike kwa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Hongera sana Mheshimiwa Rished.

*(Fungu lililotajwa hapojuu lilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Fungu 87 - Mkoa wa Kagera .............................. Sh. 18,643,407,000
Fungu 88 - Mkoa wa Dar es Salaam ................... Sh. 23,290,192,000
Fungu 89 - Mkoa wa Manyara ............................ Sh. 11,269,764,000

*(Mafungu yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya*

*Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Fungu 95 - Mkoa wa Manyara ........................... Sh. 9,904,108,000

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ninachangia *Vote 95, Sub-vote* 1101, kifungu kidogo 6385 - *Construction of Council Headquater,* nilisema kwamba, katika mwaka 2006/2007 tumepewa shilingi milioni 120. Lakini nikahoji kwamba, kwa mwaka huu wa 2007/2008 tumepewa sifuri. Nikauliza sababu ni nini? Pili, nikasema basi pamoja na sababu zitakazokuwepo, tunaomba tupate fungu hili kwa sababu *council* nyingine zimepewa. Nataka kujua kwa sababu hoja hii haikujibiwa wakati Waziri akihitimisha, sasa naomba maelezo.

La pili, kwenye fungu hilo la 95 lakini *Sub-vote* 3001, kifungu kidogo 5402 - *Construction of Regional Hospital,* nilihoji vile vile kwamba, ujenzi wa Hospitali ya Mkoa mwaka uliopita ulipewa shilingi milioni 100, lakini mwaka huu tumepewa sifuri. Maelezo nimepewa lakini wakati nilipokuwa naeleza tatizo la Mkoa wa Manyara na Babati kuzidiwa na watu kutokana na kuwa Makao Makuu ya Mkoa, nilisema Hospitali ya Wilaya ya Babati, inahitaji kuimarishwa na nikaomba nikasema basi kwa kutumia mafungu mengine, najua Serikali ina mafungu mengine kama vile *Health Sector Programme Support* au mengine walau Hospitali ya Wilaya ifanyiwe ukarabati iweze kubeba huo mzigo mzito ambao sasa hivi unabebwa na hiyo Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata maelezo kwenye maeneo hayo mawili. Ahsante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la kwanza juu ya ujenzi wa Makao Makuu ya Halmashauri, nilichukua fursa ya kumwandikia barua leo hii mchana na nikamkabidhi baada ya kuona kwamba ni kweli katika maelezo hatukuwa tumelitolea maelezo.

Lakini naomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Kwaangw' kwamba, jambo hili tunalifahamu na yeye nina hakika analifahamu vizuri sana. Serikali imesema iko tayari kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi hiyo, isipokuwa wanataka kwanza wapate maelezo juu ya matumizi ya fedha za awali zilizotolewa mwaka uliopita.

Sasa tulimwita Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri husika, tukamwuliza juu ya jambo hili akasema ni kweli walitumia utaratibu wa kawaida wa kutangaza zabuni na wakapata wakandarasi na yeye huyu mshindi ndio alionekana ametoa fedha iliyo chini ambayo ilikuwa shilingi milioni 60 kwa ajili ya kuchora ramani na gharama nyingine zinazoendana na jengo hilo.

Sasa Serikali kwa maana hiyo bado, kwa maana ya Hazina wanataka maelezo sasa yawasilishwe kwao rasmi. Kwa hiyo, ndiyo jukumu tutakalolifanya na baada ya pale tukipata *clearance* kutoka Hazina baada ya kupeleka maelezo, tunaamini jambo hilo linaweza likashughulikiwa bila matatizo yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Hospitali ya Mkoa, ni kweli safari hii haikutengewa fedha lakini sababu ipo. Kujenga Hospitali ya Mkoa ni mradi mkubwa sana na mara ya mwisho tulikuwa tumetenga fedha kidogo kwa ajili ya uchoraji ramani, pamoja na kufanya utafiti juu ya udongo wa eneo lile, jambo ambalo limekamilika.

Sasa tulitaka katika kuingia katika ngwe ya kwanza kujenga lakini imeonekana kubeba mradi wa kuanza kujenga Hospitali ya Mkoa wakati Ofisi ya Mkoa haijakamilika, inaweza isiwe busara sana. Kwa hiyo, tukaona bora tumalize kwanza jengo hili la Mkoa ili tuweze kutoa nafasi sasa kwa mwaka unaofuata tujikite katika kuanza kujenga mradi mwingine mkubwa wa hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupanga ni kuchagua na tulifikiri pengine tukichagua hivyo tutakuwa tumepanga vizuri zaidi. Lakini nakubaliana naye kwamba, hali ya hospitali kwa kweli mimi ile siiiti Hospitali ya Wilaya kwa sababu mazingira yake ni mabaya, yapo duni sana na inaeleweka kwa sababu ilikuwa ni kituo cha afya lakini katika uamuzi wa Serikali wa kujenga Mkoa ule kama Mkoa Mpya, tumelazimika pole pole kuanza kuinua hadhi yake kwa kujaribu kukarabati hapa na pale. Lakini kwa kweli kinachohitajika pale ni uamuzi wa msingi wa kujenga hospitali kamili mpya na wala si kuendelea tena kufanya ukarabati katika kile kituo.

Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Kwaangw' na wananchi wa jimbo lake lote kwamba, Serikali tumedhamiria kutekeleza hilo kwa dhati kabisa, lakini tunamwomba afanye uvumilivu kwa sababu kujenga mkoa kuna mambo mengi, tunaomba tuanze jambo hili katika bajeti inayokuja ili tuweze kujipanga vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwa furaha kubwa, napenda kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi baada ya kujadili Taarifa ya Mapato, Mapitio na Mwelekeo wa Kazi za Serikali, imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Asasi zilizo chini yake na yale ya Ofisi ya Bunge kwa mwaka wa fedha 2007/2008, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila ya mabadiliko. Hivyo basi, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako liyakubali Makadirio hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA**: Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka 2007/2008 yalipitishwa na Bunge)*

**Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa Mwaka 2007/2008**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala iliyochambua bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu (Fungu 20 na 30), Menejimenti ya Utumishi wa Umma (Fungu 32), Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Fungu 33) na Tume ya Utumishi wa Umma (Fungu 94), Bunge lako sasa lipokee na kujadili mapitio ya utekelezaji wa kazi kwa mwaka wa fedha 2006/2007, pamoja na mpango wa kazi wa mwaka 2007/2008.

Aidha, naomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Fedha ya Ofisi ya Rais - Ikulu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuishukuru Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Tatu Musa Ntimizi, Mbunge wa Igalula, kwa ushirikiano na ushauri mzuri uliotolewa wakati wa kujadili Makadirio ya Matumizi kwa mwaka 2007/2008, hatua ambayo imetuwezesha kuandaa na kuwasilisha Bungeni hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nikushukuru wewe mwenyewe, pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuliongoza Bunge hili Tukufu kwa ujasiri na umahiri mkubwa. Chini ya uongozi wenu shupavu, Bunge hili limeweza kufanya mambo mengi na yenye manufaa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu, naomba kumshukuru na kumtakia afya njema Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, ambaye kwa ushahidi wa wazi kabisa, ameweza kusimamia na kutekeleza shughuli za Chama, Serikali na Taifa kwa ujumla. Aidha, kwa namna ya pekee, naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais, kwa msukumo na ubunifu wake mkubwa, hasa katika mikakati yake inayolenga kuwajenga na kuwaimarisha wajasiriamali, ili waweze kujikomboa na umaskini. Hii inaonesha dhamira ya dhati aliyonayo

Mheshimiwa Rais katika kuharakisha maendeleo ya nchi na watu wake. Tunaomba Mwenyezi Mungu, aendelee kumjalia afya njema ili nchi izidi kunufaika na busara zake.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kumpongeza Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa juhudi zake za dhati katika kuimarisha Muungano, pamoja na kusimamia shughuli za maendeleo kote nchini. Aidha, nampongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, Mbunge wa Monduli, kwa hotuba yake yenye upeo mpana ambayo imetoa dira ya utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa mwaka 2007/2008.

Pia, nawapongeza Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Dkt. Juma Alifa Ngasongwa, Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, kwa hotuba zao ambazo zimebainisha misingi, sera, malengo na mwelekeo wa bajeti na uchumi wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, napenda kwa namna ya pekee kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Batilda S. Burian, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu – Bunge, Mheshimiwa Bernard K. Membe, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na MheshimiwaWilliam Ngeleja, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini.

Vile vile ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge waliojiunga na Bunge hili kwa kuteuliwa au kuchaguliwa katika mwaka wa fedha wa 2006/2007, nikianza na Mheshimiwa Yusuf Rajab Makamba, Mbunge wa Kuteuliwa, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mbunge wa Tunduru na Mheshimiwa Florence Essa Kyendesya, Mbunge wa Viti Maalum.

Aidha, natumia fursa hii pia kuwapongeza waliochaguliwa kuwakilisha nchi yetu ya Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki, ambao ni Mheshimiwa Dkt. Didas John Massaburi, Mheshimiwa Dkt. Amani Walid Kabourou, Mheshimiwa Dr. George Francis Nangale, Mheshimiwa Sylvia Kate Kamba Mheshimiwa Septuu Nasoro, Mheshimiwa Abdallah Ally Hassan Mwinyi, Mheshimiwa Dkt. Said Gharib Bilal, Mheshimiwa Janeth Deo Mmari na Mheshimiwa Dkt. Fortunatus Lwanyatika Masha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006/2007 kumekuwa na tukio la kihistoria katika Taifa letu, kwani kwa mara ya kwanza tumepata mwanamke Mtanzania, ambaye ameteuliwa kushika nafasi ya juu katika Umoja wa Mataifa. Hivyo, napenda kwa dhati kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Asha-Rose Migiro, kwa kuteuliwa kwake kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Uteuzi wake ni ishara inayoonesha heshima kubwa tuliyonayo Watanzania katika Jumuiya za Kimataifa.

Mheshimiwa Spika„ katika mwaka wa fedha 2006/2007, Bunge lako Tukufu na Taifa limewapoteza Wabunge wake wawili, ambao ni aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Bunge), Marehemu Juma Jamaldin Akukweti, aliyefariki tarehe 4

Januari, 2007 kwa ajali ya ndege iliyotokea katika Uwanja wa Ndege wa Mbeya na Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia aliyefariki 26 Juni, 2007.

Tunawakumbuka pia watumishi watatu wa Serikali, ambao walifariki dunia kutokana na ajali ya ndege iliyowatokea pamoja na Mheshimiwa Akukweti. Tunamwomba Mwenyezi Mungu, azilaze roho zao mahali pema peponi. Pia tunamwomba Mwenyezi Mungu, atupe moyo wa subira sisi sote, pamoja na ndugu wa marehemu. *(Amin)*

Mheshimiwa Spika, hotuba hii inahusu Ofisi ya Rais ambayo inajumuisha Ikulu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, naomba kidogo kuna jambo limetokea ambalo Waheshimiwa Wabunge, nimegundua makosa. Nilikuwa natumia Kanuni ya 49 na hivyo kuwapa Mawaziri saa moja, lakini kumbe ilitakiwa nitumie Kanuni ya 81 ambayo inawapa kuwasilisha hoja za matumizi kwa nusu saa. Sasa tumegundua kabisa na haya ndiyo baadhi ya mapungufu ya kanuni zetu.

Nakuombeni na nitamwomba Waziri wa Nchi, kwa sababu sasa ni hoja, atoe hoja kwamba tutengue hii kanuni ya 81 ili wanaowasilisha nakusudia vitu kama kilimo, nishati, kuwaambia wawasilishe kwa nusu saa inasababisha mjadala kuzidi kuwa mrefu bure. Kwa hiyo, tutengue kanuni hiyo kwa hotuba za bajeti ili Mawaziri waweze kuwasilisha hoja zao kwa kipindi kisichozidi dakika 60. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. BATILDA S. BURIAN):** Mheshimiwa Spika, kufuatilia maelekezo yako, naomba basi Bunge lako Tukufu, likubali kutengua Kanuni hii ya 81(1) ili kuruhusu Waheshimiwa Mawaziri wanapotoa hoja zao za bajeti waweze kutumia muda usiozidi saa moja.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA**: Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniongeza muda ingawa nilijiandaa chini ya huo muda.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, ambayo inajumuisha Ikulu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma. Ofisi ya Rais ni elekezi katika utendaji na uendeshaji wa shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ofisi ya Rais, Ikulu inayo Mafungu

mawili; Fungu 20 kwa ajili ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Fungu 30 kwa ajili ya Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Ofisi ya Rais, Ikulu, iliendelea kutekeleza majukumu ya kuongoza, kufuatilia, kuratibu uendeshaji bora wa Serikali na kusimamia utekelezaji wa maamuzi ya Rais na Baraza la Mawaziri. Maelezo ya kina ya shughuli nilizozitaja hapo juu, yameainishwa katika kitabu cha hotuba katika ukurasa wa sita hadi wa kumi. Kazi nyingine zilizotekelezwa katika kipindi hiki ni pamoja na:-

(a) Kuendelea kutoa huduma za ushauri kwa Rais katika masuala ya siasa, jamii, uchumi, sheria, diplomasia na ushauri mwingine wenye lengo la kumsaidia Rais na Baraza la Mawaziri kufanya maamuzi.

(b) Baraza la Mawaziri lilifanya vikao 67 ambapo nyaraka 261 zilijadiliwa na kutolewa maamuzi. Aidha, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ilitoa ushauri wa nyaraka 149 katika vikao vya Makatibu Wakuu *(IMTC),* pamoja na kujadili nyaraka zingine 136. Pia, Waratibu 30 wa Shughuli za Baraza la Mawaziri walipatiwa mafunzo juu ya kuandaa sera, miswada, kutayarisha na kusambaza nyaraka za Baraza la Mawaziri.

(c) Kushughulikia masuala ya mawasiliano kwa umma juu ya utendaji kazi wa Serikali kwa upande mmoja na kutoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali kutoka kwa wananchi kwa upande mwingine.

(d) Rufaa 110 za watumishi wa umma zilizowasilishwa kwa Rais na Katibu Mkuu Kiongozi zilichambuliwa na kutolewa uamuzi. Aidha, malalamiko 333 ya watumishi wa umma yalichambuliwa na kutolewa uamuzi kwa maelekezo ya Rais na Katibu Mkuu Kiongozi.

(e) Mkakati wa Awamu ya Pili wa Kupambana na Rushwa uliandaliwa na kuzinduliwa na Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, tarehe 10 Desemba, 2006. Aidha, wafanyakazi 460 kutoka Wizara na Taasisi za Umma walipatiwa mafunzo kuhusu mkakati wa kuzuia rushwa na utawala bora.

(f) Programu ya kuimarisha Uwajibikaji, Uwazi na Uadilifu katika Utendaji wa Umma *(Accountability, Transparency and Integrity Programme – ATIP)* wenye lengo la kuziimarisha taasisi zote zinazosimamia masuala ya maadili na utawala bora, imeanza kutekelezwa. Madhumuni ya programu hii ni kuziwezesha taasisi zinazohusika, ambazo ni Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Taasisi ya Kuzuia Rushwa, Kitengo cha Uratibu wa Utawala Bora na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

(g) Maafisa Mawasiliano Serikalini 89 kutoka Wizara na Taasisi za Serikali walipatiwa mafunzo juu ya kuandaa mikakati ya kuwasiliana na umma kwa kutumia vyombo vya habari mbalimbali. Aidha, utaratibu wa kujenga uhusiano mzuri na vyombo vya habari umeandaliwa na umeanza kutekelezwa. Utaratibu huu unalenga kutambua mambo yaliyojiri kwenye vyombo vya habari na kutoa maelezo pale inapobidi.

(h) Jumla ya watumishi 3,155 wa vyombo vya Ulinzi na Usalama walitunukiwa Nishani za Kitaifa. Aidha, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ameanzisha Nishani mpya tatu ambazo ni Nishani ya Utumishi wa Muda Mrefu na Maadili Mema, Nishani ya Utunzaji wa Mazingira na Nishani ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

(i) Mkutano na vyama vya siasa na mashirika ya kiraia ulifanyika kwa lengo la kukuza mahusiano baina ya vyama vyenyewe na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Majukumu makubwa ya TAKURU ni kuzuia, kupambana na kuelimisha umma kuhusu athari mbalimbali zinazotokana na kujihusisha na vitendo vya rushwa. Aidha, TAKURU inalo pia jukumu la kuishauri Serikali kuhusu namna ya kuziba mianya ya rushwa. Katika mwaka wa fedha 2006/2007, TAKURU ilitekeleza kazi zifuatazo:-

(a) Kuratibu marekebisho ya Sheria Mpya ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ambayo ilipitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Aprili, 2007. Sheria hii mpya imeainisha makosa ya rushwa 24 kutoka makosa manne katika Sheria ya awali Na. 16 ya mwaka 1971, ambayo sasa imefutwa.

(b) Upelelezi wa majalada 2,304 pamoja na majalada 1,272 yaliyofunguliwa na kupokelewa kuhusu tuhuma za vitendo vya rushwa kipindi hicho uliendelea katika maeneo mbalimbali nchini, ambapo jumla ya majalada 1,188 yalishugulikiwa na kukamilika na hivyo hatua mbalimbali kuchukuliwa ikiwemo kufikisha kesi 89 mahakamani na kutoa mapendekezo ya hatua za kinidhamu dhidi ya watuhumiwa katika majalada 182. Majalada 320 yalihamishiwa polisi baada ya kubainika kuwa tuhuma hizo hazihusu makosa ya rushwa. Aidha, uchunguzi wa majalada 597 haukuweza kubaini kuwepo kwa makosa yoyote na hivyo kufungwa.

(c) Jumla ya kesi za rushwa 268 ziliendeshwa mahakamani zikiwemo kesi mpya zilizofikishwa mahakamani kipindi cha 2006/2007. Kesi 50 zilitolewa uamuzi baada ya kukamilika kusikilizwa mahakamani ambapo kati ya hizo kesi 25 watuhumiwa wake walihukumiwa vifungo, kesi 9 ziliondolewa mahakamani kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo kutokutokea mashahidi baada ya kesi kukaa muda mrefu mahakamani bila kusikilizwa na kesi 16 watuhumiwa waliachiwa huru.

(d) Kununua majengo mawili ili kupunguza tatizo la uhaba wa ofisi, jengo moja kwa ajili ya ofisi ya Mkoa wa Shinyanga na jingine kwa ajili ya ofisi ya Wilaya ya Kongwa. Aidha, ofisi mpya 16 za Wilaya zimefunguliwa na hivyo kuwa na jumla ya ofisi za Wilaya 113. Pia, ofisi tatu za Mikoa maalum ya Ilala, Kinondoni na Temeke zimefunguliwa na hivyo kuwa na jumla ya ofisi za Mikoa 24.

(e) Tafiti 14 zimefanyika ili kubaini mianya ya rushwa na hatimaye kutoa mapendekezo ya namna ya kuziba mianya hiyo. Aidha, Machapisho 1,600 yaliyotokana na utafiti yametolewa kwa wadau mbalimbali kwa lengo la kuelimisha njia bora za

kudhibiti rushwa. Kazi nyingine ni kama zilivyoainishwa katika ukurasa wa 10 wa kitabu cha hotuba yaani ukurasa wa 13.

Mheshimiwa Spika**,** Awamu ya Pili ya *TASAF* ina jukumu la kuisaidia jamii katika kuainisha kero zao, kuweka vipaumbele, kutekeleza, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi ili kuboresha hali zao za maisha. Utekelezaji wa *TASAF* ni sehemu ya jitihada za Serikali za kupambana na umaskini kupitia dhana ya ushiriki wa jamii.

Miradi inayoibuliwa na wananchi na kusaidiwa na *TASAF* imeelekezwa kuboresha huduma za jamii, kutoa ajira kwa kaya zenye upungufu wa chakula na kuongeza kipato kwa watu wa makundi maalum wakiwemo watoto yatima, wajane, wazee, watu wenye ulemavu na waishio na virusi vya UKIMWI. Ili kufanikisha hayo yote, *TASAF* ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Kushirikiana na jamii, kupitia Halmashauri za Wilaya Tanzania Bara, na Ofisi ya Waziri Kiongozi kwa upande wa Visiwa vya Unguja na Pemba, katika kuainisha vipaumbele vyao, kupanga pamoja na kutekeleza miradi inayotatua kero zao. Pia miradi ambayo haikukamilika katika Awamu ya Kwanza ya *TASAF* ilijumuishwa katika mchakato huo ili ikamilishwe.

(b) Mafunzo yenye lengo la kuimarisha uwezo wa usimamizi na kuboresha uwajibikaji yametolewa kwa watendaji katika Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa, Jiji na Vijiji/Shehia ili kuhakikisha kwamba miradi inatekelezwa kwa kufuata taratibu zilizowekwa na katika viwango vinavyokubalika. Jumla ya washiriki 8,690 wa Kamati za Usimamizi wa Miradi, viongozi 379 wa Halmashauri za Vijiji, Kamati za Mitaa na Kamati za Ushauri za Shehia na watendaji 1,008 wa Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji wamepata mafunzo hayo.

(c) Kusaidia utekelezaji wa miradi iliyoibuliwa na wananchi katika Halmashauri zote za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji kwa upande wa Tanzania Bara na Visiwa vya Pemba na Unguja kwa upande wa Tanzania Visiwani. Hadi sasa wananchi wameomba ufadhili na kuidhinishiwa miradi 2,561 yenye thamani ya Sh. 36,591,798,931. Kati ya miradi hiyo, 1,974 ni ya maendeleo ya jamii, 162 ni ya kaya zenye uhaba wa chakula na 425 ni ya watu wa makundi maalumu.

(d) Kusimamia taratibu zinazowezesha taasisi mbalimbali kupitisha fedha *TASAF* kwa malengo maalum *(Ring-fenced Facility)*. Hadi sasa, utaratibu huu unatumiwa kwa miradi ya *Marine and Coastal Environmental Management Program (MACEMP)* na *Participatory Forest Management (PFM).* Fedha kutoka miradi hiyo inafanya kazi katika maeneo husika. Aidha, Kamisheni ya UKIMWI Zanzibar *(ZAC),* inapitisha fedha *TASAF* kwa ajili ya miradi ya UKIMWI inayotekelezwa katika visiwa vya Unguja na Pemba. Pia, *Organization of Petrolium Exporting Countries (OPEC)* inapitisha fedha zake *TASAF* kwa ajili ya utekelezaji wa miradi inayoibuliwa na wananchi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, MKURABITA imepangwa kutekelezwa katika awamu nne ambazo ni kufanya tathmini ya ukubwa wa sekta isiyo rasmi; Maandalizi ya

Maboresho; Utekelezaji pamoja na Kukua kwa Mitaji na Utawala Bora. Kwa sasa MKURABITA iko katika Awamu ya Pili, yaani Maandalizi ya Maboresho. Katika mwaka 2006/2007 MKURABITA ilitekeleza shughuli zifuatazo: -

(a) Utafiti wa msingi wa sekta isiyo rasmi unaolenga katika kuweka vigezo vya kuratibu ukuaji wa sekta hiyo, umefanyika katika Jiji la Dar es Salaam na Manispaa ya Zanzibar. Taarifa muhimu zilizopatikana zitatumika katika kuandaa mabadiliko yanayokusudiwa.

(b) Kuwawezesha walengwa ambao kwa sasa wameshaanza mchakato wa kurasimisha rasilimali na biashara zao kukamilisha urasimishaji na kuanza kutumia rasilimali na biashara hizo kupata mikopo na fursa nyingine katika soko rasmi. Mawasiliano na Benki ya Akiba, *CRDB, NBC* na *Eurafrican Bank* yanaendelea ili kuona uwezekano wa benki hizo kurekebisha masharti ya mikopo.

Mheshimiwa Spika, Utumishi wa Umma ni nguzo ya taifa lolote duniani. Watumishi wa umma hutoa mchango mkubwa katika kulinda na kujenga heshima ya nchi, kudumisha usalama, amani na utulivu na kuiwezesha Serikali kutekeleza shughuli zake ipasavyo. Hivyo, daima utumishi wa umma lazima uwe hatua moja mbele ili kujenga mazingira yanayowezesha kuwepo utawala bora, ufanisi na uwajibikaji.

Katika kufanikisha majukumu haya, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma inatekeleza Mpango wa Kuboresha Utumishi wa Umma unaolenga kuinua kiwango cha utoaji huduma katika Utumishi wa Umma. Chini ya mpango huu, maeneo yanayopewa kipaumbele ni pamoja na:-

(a) Kuwawezesha watumishi wa umma kufanya kazi kwa uaminifu na uadilifu na kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizopo.

(b) Kuweka mifumo inayowezesha utendaji kazi wa watumishi kupimwa na kutunzwa kulingana na viwango vya utendaji kazi vilivyopo na kuhakikisha kwamba kuna mazingira mazuri ya kazi ambapo sheria na kanuni zinatumiwa kwa haki na usawa.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana tulilieleza Bunge lako Tukufu kuhusu shughuli mbalimbali ambazo Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ilipanga kutekeleza katika mpango wa mwaka 2006/2007. Naomba sasa nitumie fursa hii kutoa taarifa ya mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa mpango huo kama ifuatavyo:-

(a) Wizara nane, Idara tano zinazojitegemea, Wakala wa Serikali saba na Ofisi nne za Mikoa, zimewezeshwa kuboresha mazingira ya kazi kwa kuzipatia vitendea kazi kama vile kompyuta na samani za ofisi.

(b) Wakala moja ya Serikali ya Mabasi yaendayo kwa Kasi Dar-es-Salaam imeanzishwa na Idara nyingine tano za Serikali zipo katika hatua za mwisho za kubadilishwa kuwa Wakala.

(c) Mafunzo ya matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano yalitolewa kwa watumishi 150 kutoka Wizara na Idara mbalimbali za Serikali.

(d) Miundo na Majukumu ya Ofisi, Wizara na Idara nne zinazojitegemea imehuishwa na kuidhinishwa na Rais kwa utekelezaji. Aidha, Wizara tatu, Idara tisa na Wakala wa Serikali tatu zimekamilisha uandaaji wa Orodha za Kazi.

(e) Jumla ya wanawake 139 walipatiwa nafasi za mafunzo ya Uzamili pamoja na mafunzo ya muda mfupi ili kuwajengea uwezo na sifa kushika nyadhifa za juu. Aidha, idadi ya wanawake walio katika nafasi za uongozi wa juu.

(f) Ukaguzi wa watumishi walioajiriwa Serikalini umefanyika kwa kuanzia na Shule za Sekondari 2,357. Ukaguzi huo utakapokamilika taarifa zake zitasaidia kubainisha upungufu uliopo katika matumizi ya rasilimali watu, ubadhirifu katika mishahara na ukiukaji wa taratibu za kiutumishi ili kuwezesha hatua zinazostahili kuchukuliwa.

(g) Mashindano ya uandishi wa insha kuhusu maadili yaliendeshwa katika shule za sekondari ishirini kama njia mojawapo ya kuimarisha maadili mashuleni.

(h) Ujenzi wa jengo la kisasa litakalokuwa kituo cha Serikali-mtandao umeendelea kutekelezwa. Aidha, ujenzi wa mtandao wa Serikali elektroni utakaoziunganisha Idara, Wizara, Wakala na Serikali za Mitaa umeanza.

(i) Mfumo wa kompyuta wa taarifa za kiutumishi na mishahara umesambazwa katika Wizara kumi.

(j) Mikutano ya kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa mikataba ya huduma kwa mteja iliendeshwa katika mikoa mitatu ya Rukwa, Ruvuma na Mtwara. Aidha, elimu kuhusu masuala yanayotekelezwa katika juhudi za kuboresha Utumishi wa Umma ilitolewa kwa wadau mbalimbali wa Serikali kupitia vipindi vya radio, televisheni, magazeti na machapisho mbalimbali.

(k) Maonesho ya wiki ya Utumishi wa Umma yaliyoshirikisha taasisi zaidi ya 70 za Serikali yenye lengo la kukutanisha wananchi na watumishi wa umma kutoka taasisi mbalimbali yaliendeshwa ili kupata maoni ya wananchi juu ya utumishi wa umma na kupata fursa ya kueleza maboresho yanayoendelea katika utumishi wa umma.

(l) Viongozi wa Kitaifa Wastaafu waliendelea kupatiwa huduma kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, tangu kuanzishwa kwake kama Wakala wa Serikali mwaka 2000, Chuo cha Utumishi wa Umma kimeendelea kukua na kujiimarisha katika

utoaji wa huduma zake. Chuo kimepanua wigo wa mafunzo na kuhusisha nyanja za Utumishi, Utawala, Menejimenti na Uongozi kwa watumishi wa ngazi za juu na kati. Katika mwaka wa fedha 2006/2007 zaidi ya watumishi wa umma 1,500 wa ngazi za Uongozi walihudhuria mafunzo mbalimbali yaliyotolewa na Chuo.

Mheshimiwa Spika, Katika kuhakikisha kuwa mafunzo yanayotolewa na Chuo cha Utumishi wa Umma yanakidhi matarajio ya watumishi wa umma nchini. Chuo kimefanya jitihada kubwa katika kutafuta na kuendeleza wataalamu wake. Aidha, kwa lengo la kuboresha zaidi huduma zake, chuo kimejenga ushirikiano baina yake na vyuo mbalimbali vya kitaifa na kimataifa kama vile Chuo cha Watumishi wa Serikali, Singapore *(Singapore Civil Service College)*, Chuo cha Watumishi wa Umma cha Malaysia *(INTAN)* na *ESAMI*, Chuo Kikuu cha Mzumbe, Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo na Kituo cha Tanzania cha Mafunzo ya Maendeleo kwa Mtandao *(TGDLC).* Hivi sasa unaangaliwa uwezekano wa kushirikiana na vyuo vingine kama *RIPA* cha Uingereza, *UMI* cha Uganda na *GIMPA* cha Ghana.

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kama chombo kikuu kinachohusika na kukuza na kusimamia maadili ya viongozi wa umma, inatekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa kwenye Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Na. 13 ya 1995. Kwa kuhakikisha kuwa Viongozi wote waliotajwa katika Sheria hiyo wanatekeleza wajibu wao kwa uadilifu, uaminifu na uwazi. Moja ya wajibu wa msingi kwa viongozi wote wa umma ni kutoa Tamko la maandishi kuhusu mali au rasilimali na madeni kila mwisho wa mwaka au katika kipindi cha siku thelathini baada ya kupewa wadhifa au mwisho wa kutumikia wadhifa. Katika kipindi kinachoishia 31 Desemba 2006, jumla ya Viongozi wa Umma 6,415 walitumiwa Fomu za Tamko la Mali na Madeni. Hadi kufikia 30 Aprili, 2007 jumla ya Viongozi 3,317 walikuwa wametoa Tamko la Mali na Madeni.

Mheshimiwa Spika**,** Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, imeendelea na jitihada za kuimarisha ofisi zake sita za Kanda kwa kuajiri watumishi wapya 33 na kuwapatia mafunzo na vitendea kazi ili kuboresha utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Utumishi wa Umma inao wajibu wa kuhakikisha kwamba masuala yote ya Utumishi yanaendeshwa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa Ajira katika Utumishi wa Umma inazingatia Sifa, Uwezo na ushindani kwa madhumuni ya kufanikisha utendaji wenye malengo na matokeo yanayopimika. Katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Tume imetekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

(i) Kufanya ukaguzi wa rasilimali watu katika Wizara 23, Idara 6 zinazojitegemea, Ofisi 12 za Makatibu Tawala wa Mikoa na Mamlaka 31 za Serikali za Mitaa.

(ii) Walimu 5,055 walithibitishwa kazini, kati yao wanaume ni 2,371 na wanawake ni 2,684.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2007/2008, Ofisi ya Rais, Ikulu imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kuendelea kutoa huduma kwa Rais na kumpatia ushauri katika maeneo mbalimbali kama vile uchumi, siasa, jamii, sheria, mahusiano ya kisiasa, diplomasia, usalama wa nchi.

(ii) Kushughulikia rufaa za watumishi wa umma zinazowasilishwa kwa Rais na Katibu Mkuu Kiongozi.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Kuzuia Rushwa (TAKURU)katika mwaka 2007/2008, imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kuajiri watumishi 262 ili kufikia ikama ya watumishi 1,450 ambapo 250 ni nafasi mpya na 12 ni wa kujaza nafasi zilizo wazi.

(ii) Kufungua ofisi ndogo 9 katika vituo maalum na vya kibiashara kutokana na maeneo hayo kuwa na kero nyingi za rushwa. Maeneo hayo ni Chalinze, Ikwiriri, Makambako, Ilula, Isaka, Holili, Mtukula na Kyaka.

(iii) Kujenga ofisi moja ya mkoa na ofisi mbili za wilaya ili kuepuka gharama za kupanga. Aidha, ujenzi wa jengo la makao makuu utaanza katika kipindi hiki.

(iv) Kuendelea na uchunguzi wa tuhuma 2,037 zilizopo na nyingine zitakazowasilishwa. Kipaumbele kitawekwa katika tuhuma zinazohusu mikataba mikubwa, manunuzi Serikalini, matumizi ya fedha za Serikali katika miradi mikubwa pamoja na tuhuma nyingine zitakazoonekana kuisababishia Serikali hasara.

(v) Kuendelea kuendesha kesi 218 zilizopo mahakamani kwa sasa na zitakazoendelea kufikishwa mahakamani.

(vi) Kuendelea kuelimisha wananchi kuhusu vita dhidi ya rushwa kwa kutumia vyombo vya habari na machapisho mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF). TASAF* Awamu ya Pili itaendelea kushirikiana na jamii katika Halmashauri zote Tanzania Bara na visiwa vya Unguja na Pemba kwa upande wa Tanzania Visiwani, kutekeleza miradi yenye lengo la kutatua kero zao kwa kuzingatia vipaumbele vyao, ili kupunguza umaskini na kuboresha hali yao ya maisha. Katika mwaka 2007/2008, *TASAF* imepanga kutekeleza yafuatayo:-

Kuendelea kutoa mafunzo kwa wajumbe wa Kamati za Usimamizi wa Miradi 20,000 ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi. Mafunzo haya yanahusu utunzaji wa kumbukumbu sahihi za utekelezaji, kufanya manunuzi kwa kufuata taratibu zilizowekwa, kuandaa taarifa na kuziwasilisha kwa wadau.

Kuimarisha usimamizi wa miradi ili kuhakikisha miradi inatekelezwa kwa kuzingatia viwango vinavyokubalika na kuhakikisha kunakuwa na matumizi mazuri ya fedha za miradi. TASAF itashirikiana na wataalam wa Halmashauri zote za Tanzania Bara na Visiwa vya Pemba na Unguja kwa Tanzania Visiwani kusimamia kwa karibu utekelezaji wa miradi inayotekelezwa, ili kuongeza uwezo wa watekelezaji kufanya kazi kwa viwango na kuondoa matatizo ya kiufundi yanayoweza kujitokeza.

Kufanya tathmini ya miradi ili kubaini mafanikio na matatizo yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji. Tathmini hii inatarajiwa kufanyika kabla ya mwisho wa mwaka huu.

Kuendelea kuhamasisha jamii ili waunde vikundi vya kuweka akiba na kuwekeza katika shughuli za uzalishaji. Kazi hii itafanyika katika Halmashauri 75 zilizobaki kwa Tanzania Bara na katika Visiwa vya Unguja na Pemba kwa Tanzania Visiwani.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008 MKURABITA itaendelea kutekeleza jukumu lake la kuandaa mfumo wa kitaifa wa umiliki wa rasilimali na uendeshaji biashara kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya majaribio kulingana na mapendekezo ya maboresho yatakavyoendelea kutolewa.

(ii) Kuandaa utaratibu rahisi, wenye gharama nafuu, shirikishi na endelevu wa urasimishaji ardhi vijijini na mijini kwa mujibu wa sheria za Tanzania Bara na Zanzibar.

(iii) Kuandaa mfumo wa mawasiliano kati ya masijala mbalimbali hasa zinazohusu ardhi, watu na biashara ili kuweza kukusanya, kuhifadhi na kutoa taarifa kamilifu kuhusu umiliki mali na uendeshaji biashara kuanzia ngazi ya Kijiji/Shehia hadi Taifa. Aidha, mkakati wa mawasiliano utakaotumika kuwafikia walengwa utakamilishwa na kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma itaendelea na utekelezaji wa awamu ya pili ya Mpango wa Kuboresha Utumishi wa Umma ambao utaanza rasmi Januari 2008. Katika kipindi hicho kazi kubwa itakuwa ni kuwaelimisha wadau na umma kwa ujumla kuhusu utekelezaji wa mpango huu kwa kutumia njia mbalimbali, kama vile semina, warsha, vipeperushi, vipindi vya redio na televisheni na kwenye maonyesho mbalimbali kama vile wiki ya utumishi wa umma, sherehe za Sabasaba na Nanenane.

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili ya Mpango wa Kuboresha Utumishi wa Umma imelenga zaidi kuimarisha mifumo ya utendaji kazi, uwajibikaji wa taasisi na watumishi katika kutoa huduma kwa wananchi pamoja na uwekaji wa misingi ya ushirikishwaji wa wananchi katika mchakato wa utungaji wa sera mbalimbali zinazotekelezwa na Serikali. Aidha, mpango huu kwa sasa unaainishwa na mipango mingine ya kuboresha sekta

zingine za umma kama vile Fedha, Sheria na Serikali za Mitaa ili kuhakikisha kuwa mipango hii, kwa pamoja, inachangia katika juhudi za kuboresha utoaji huduma na kuwaletea wananchi maisha bora zaidi na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Utumishi wa Umma unaenda sambamba na jitihada za kuboresha maslahi ya watumishi wa umma. Serikali inatambua kuwa jitihada za kuboresha mifumo ya utoaji huduma kwa wananchi haziwezi kuleta matokeo mazuri bila kuwa na watumishi wenye ari na motisha ya kufanya kazi kwa bidii. Kutokana na ukweli huu, katika mwaka wa fedha uliopita Serikali iliunda Tume ya Kuchunguza na kushauri kuhusu namna ya kuboresha maslahi ya Watumishi wa Umma. Nafurahi kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa Tume hiyo iliwasilisha mapendekezo yake kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano tarehe 22 Januari, 2007. Mapendekezo ya Tume hii ndiyo yamekuwa msingi wa makadirio ya Bajeti ya Mishahara kwa Watumishi wa Umma katika Mwongozo wa Mpango na Bajeti wa mwaka 2007/2008 – 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, Upandishwaji wa Vyeo. Katika mwaka wa fedha 2007/2008 Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kupandisha vyeo jumla ya watumishi 85,267. Hii inajumuisha watumishi 25,597 kutoka Wizara na Idara Zinazojitegemea, watumishi 1,127 toka Sekretarieti za Mikoa na watumishi 58,544 toka Serikali za Mitaa. Aidha, katika watumishi watakaopandishwa vyeo toka Serikali za Mitaa wamo walimu 38,505 waliokuwa wamelundikana katika cheo kimoja kwa muda mrefu. Hii ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa azma ya Serikali ya Awamu ya Nne ya kutatua kero za walimu nchini.

Mheshimiwa Spika**,** Ajira Mpya na Mbadala. Katika jitihada za kutatua tatizo la uhaba wa watumishi kwenye sehemu mbalimbali za utoaji huduma, kwa mwaka 2007/2008 Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kugharamia ajira mpya 41,435. Sekta zilizopewa kipaumbele ni Elimu, nafasi 20,154 sawa na asilimia 49, Afya nafasi 4,187, sawa na asilimia 10, Usalama wa Raia nafasi 2,611 sawa na asilimia 6.3, Kilimo na Mifugo nafasi 2,500 sawa na asilimia 6.0 na nafasi zilizobaki 11,983 ni kwa ajili ya sekta nyingine. Aidha, Serikali pia imetenga fedha kwa ajili ya nafasi 5,321 za ajira mbadala ili kujaza mapengo ya watumishi ambao utumishi wao utakoma kwa sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Mishahara. Kwa mwaka 2007/2008 Serikali imepanga kutumia shilingi milioni 1,180,815 kwa ajili ya malipo ya mishahara. Kiasi hiki ni ongezeko la shilingi milioni 176,993 sawa na asilimia 17.62 ikilinganishwa na shilingi milioni 1,003,882 zilizotumika katika mwaka wa fedha 2006/2007. Kiasi hiki kitatumika kugharamia ajira mpya na kupandisha vyeo watumishi kama nilivyoeleza hapo juu. Kiasi hicho cha fedha pia kitatumika kutoa nyongeza za mishahara ikiwa ni mwanzo wa utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Rais.

Aidha, kama Waziri wa Fedha alivyosema Serikali imepunguza kiwango cha chini cha kukata kodi ya mapato ya ajira ili kupunguza mzigo wa kodi kwa wafanyakazi

wa kipato cha chini. Serikali itaendelea kufanyia kazi mapendekezo ya Tume kulingana na uwezo kifedha na kwa kadri uchumi wa nchi utakavyoendelea kukua.

Mheshimiwa Spika**,** Pia katika mpango wa mwaka 2007/2008, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma itaelekeza nguvu zake nyingi katika kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kubadilisha Idara 2 za Serikali kuwa wakala, pamoja na kuendelea kuimarisha Wakala 25 zilizopo.

(ii) Kuendelea kuhuisha miundo na majukumu ya Wizara, Idara Zinazojitegemea ili kuongeza ufanisi, kufuatilia utekelezaji wake na kuboresha taratibu za utendaji kazi. Aidha kazi nyingine itakuwa kuhuisha sheria, kanuni, sera na nyaraka mbalimbali zinazosimamia utumishi wa umma na ambazo zimepitwa na wakati.

(iii) Kuhuisha Mipango Mkakati ya Wizara, Idara Zinazojitegemea, Mikoa na Wakala za Serikali ili iendane na mwongozo mpya wa kuandaa Mipango Mkakati na Bajeti.

(iv) Kuendelea na ukaguzi wa orodha ya malipo ya mishahara kwa nia ya kudhibiti matumizi yasiyo sahihi.

(v) Kufanyia kazi na kutekeleza mapendekezo ya taarifa ya Tume ya Rais ya Kuboresha Maslahi ya Watumishi wa Umma.

(vi) Kuendelea kuwasiliana na wadau kupitia maonyesho ya wiki ya Utumishi wa Umma, maonyesho ya Saba Saba na Nane Nane pamoja na mikutano ya wadau katika Wilaya zote za Mikoa ya Singida, Tabora, Lindi na Pwani.

(vii) Kuandaa na kufanya mikutano kati ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na wawakilishi kutoka vyama visivyo vya kiserikali ili kushirikiana katika kuwahamasisha wananchi kujua haki yao ya kudai huduma bora kutoka kwenye ofisi za Serikali.

(viii) Kuendelea kuandaa makala na kurusha vipindi vya kuelimisha umma kupitia Radio, Televisheni, Magazeti, Majarida, Vipeperushi na Machapisho mengine kuhusu shughuli zinazofanywa na serikali kupitia Programu ya Kuboresha Utumishi wa Umma.

(ix) Kuendelea kuimarisha na kusambaza mfumo wa kompyuta wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara ili kukidhi mahitaji ya taarifa mbalimbali ya kiutumishi na mishahara, na pia mabadiliko yanayoendelea kutokea katika nyanja ya rasilimali watu na teknolojia ya habari.

(x) Kuendelea kutoa mafunzo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa viongozi na watumishi wa kada mbalimbali Serikalini.

(xi) Kufanya tathmini mbalimbali kuhusu uwezo na utayari wa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Ofisi za Mikoa na Wilaya katika matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano na kuandaa miongozo ya matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano katika kutoa huduma kwa wananchi.

(xii) Kuanza ujenzi wa kituo cha Kanda cha Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa Mwanza.

(xiii) Kuendelea kuweka mfumo mpya wa utunzaji na utumiaji bora wa Kumbukumbu katika ofisi sita za Wakuu wa Mikoa na Wizara mbili zenye Kumbukumbu maalumu.

(xiv) Kuanzisha kwa majaribio utekelezaji wa mfumo wa kushughulikia malalamiko katika Wizara saba.

Mheshimiwa Spika, pamoja na shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2007/2008 kama zilivyoorodheshwa hapo juu, suala la kudhibiti nafasi za ajira ili kuhakikisha kwamba hazivuki wigo kama ilivyoainishwa kwenye Ikama na katika bajeti litazingatiwa sana. Ili kuepuka matatizo yaliyotajwa hapo juu, hatua zifuatazo zimechukuliwa katika kukabiliana na ongezeko la mahitaji ya watumishi wa sekta mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Kuhakikisha kwamba mahitaji yote ya lazima yanazingatiwa katika Bajeti ya mwaka 2007/2008.

(ii) Kuwaagiza waajiri wote kuandaa mipango mikakati inayozingatia hali halisi ya mahitaji ya watumishi katika mwaka 2007/2008.

(iii) Kutoa mafunzo ya namna ya kuandaa makisio ya Ikama na bajeti ya mishahara ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Utumishi wa Umma. Katika mpango wa mwaka 2007/2008, Chuo cha Utumishi wa Umma kina mikakati ya kuendelea kupanua mafunzo na kutoa mafunzo ya kuendeleza viongozi wa Serikali katika ngazi zote kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kukamilisha uandaaji wa mwongozo wa kuendeleza stadi za uongozi.

(ii) Kuandaa mitaala ambayo itakidhi mafunzo ya kuendeleza Uongozi.

(iii)Kujenga uwezo wa Chuo ili kiweze kutoa mafunzo yatakayokidhi mahitaji ya maboresho Serikalini kwa ubora na gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika**,** katika mwaka ujao wa fedha, Serikali itaendelea kuhamasisha wananchi kutumia Kituo cha Mafunzo ya Maendeleo kwa njia ya Mtandao, na kuanzisha vituo vishiriki Mikoani ili kutoa nafasi kubwa zaidi kwa Watanzania kupata taaluma muhimu kwa kupitia kituo hiki.

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Katika mwaka 2007/2008, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kama chombo kimojawapo cha Serikali chenye jukumu la kukuza na kuimarisha maadili mema miongoni mwa viongozi wa umma katika kufanikisha dhana ya utawala bora nchini, imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuendelea na zoezi la kuhakiki mali za viongozi wapatao 400 walizotaja katika Tamko la Rasilimali na Madeni kwa madhumuni ya kuhakikisha kuwa mali zilizotajwa katika Tamko ndizo walizo nazo. Aidha, ulinganisho utafanywa kati ya mali zilizotajwa kwenye Tamko na maelezo ya kipato cha viongozi husika.

(ii) Kukamilisha uandaaji wa mfumo wa Benki ya Takwimu (Data Bank) ya Viongozi wa Umma na mali au rasilimali zao kwa ajili ya kurahisisha rejea na uwekaji kumbukumbu wa mali hizo na taarifa za viongozi kwa usahihi.

Kusimamia na kuendesha Mfuko wa *Facility for Ethics, Accountability and Transparency,* chini ya Mradi wa Benki ya Dunia katika kuboresha Sekta za Fedha na Sheria kwa lengo la kukuza Uwajibikaji, Uwazi na Uadilifu *(Accountability, Transparency and Integrity Program - ATIP).*

Lengo la Mfuko huu ni kuziwezesha taasisi za umma na binafsi zinazojihusisha na uwajibikaji, uwazi na uadilifu *(Oversight and Watchdog Institutions)* kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Aidha, Mfuko utavisaidia Vyama vya Kitaaluma *(Professional Associations)* ili viweze kuimarisha maadili ya taaluma miongoni mwa wanachama wake.

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma itashirikiana kwa karibu na taasisi nyingine za umma na za binafsi zenye majukumu sawia, ili kufikisha ujumbe wa maadili mema na utawala bora kwa viongozi na wananchi.

Aidha, wigo wa viongozi wa umma wanaowajibika na Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma umepanuka ili viongozi wengi zaidi wawajibike na Sheria hiyo. Hali hii inatoa changamoto kwa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kuimarisha na kuboresha utendaji kazi wake.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Utumishi wa Umma katika mwaka 2007/2008 Tume ya Utumishi wa Umma imepanga kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

(i) Kushughulikia rufaa za Watumishi dhidi ya maamuzi ya Waajiri na Mamlaka za Nidhamu na kuboresha miongozo iliyopo inayohusu masuala ya Utumishi wa Umma.

(ii) Kuandaa vipindi 52 vya radio na makala 52 za magazeti kwa lengo la kuelimisha umma kuhusu, kazi na majukumu ya Tume, taratibu za ajira, nidhamu na upandishwaji vyeo katika utumishi wa umma.

(iii) Kuendelea kushiriki katika mchakato wa uimarishaji wa ushirikiano baina ya Tume za Utumishi wa Umma za Afrika Mashariki na Tume ya Utumishi ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Majumuisho Ofisi ya Rais pamoja na Idara zilizo chini yake ambazo zimejumuishwa katika hotuba hii, kwa pamoja, inalo jukumu maalum la kujenga Utumishi wa Umma madhubuti, wenye uwezo wa kusimamia maendeleo ya Taifa hili kwa kuimarisha huduma kwa wananchi na kwa vyombo vingine vya uzalishaji, na kwa kusimamia utawala bora, wenye haki na usawa na unaojenga mazingira yenye utulivu na amani.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyolieleza Bunge lako Tukufu mwaka jana, Serikali madhubuti itatokana na utumishi wa umma unaoaminika; wenye kuchukua hatua sahihi pale unapotakiwa kufanya hivyo, unaotekeleza wajibu wake kitaalam na kwa moyo wa kujituma; na unaokumbuka kuwa upo kazini kutokana na dhamana uliyopewa na wananchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali madhubuti na inayoendeshwa kwa misingi ya kisheria, haki na usawa ni nguzo ya msingi katika kuleta demokrasia ya kweli na utawala bora, maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa wananchi. Kazi zote ambazo zimekuwa zikitekelezwa na Ofisi hii na Taasisi zake, zimelenga kwa njia moja au nyingine katika kujenga Serikali madhubuti yenye uwezo wa kusimamia maendeleo ya Taifa, kuimarisha demokrasia na utawala bora, mahusiano ya jamii, vyote vikilenga kukuza amani, utulivu na umoja wa kitaifa.

Mheshimiwa Spika, mafanikio katika Ofisi ya Rais, Ikulu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma kwa kiasi kikubwa yamechangiwa na misaada toka nchi rafiki na mashirika mbalimbali. Nachukua nafasi hii kuzishukuru nchi na mashirika yafuatayo: Uingereza, Uholanzi, Malaysia, India, Ujerumani, Australia, New Zealand, Singapore, Pakistan, Misri, Thailand, Uswisi, Italia, Korea ya Kusini na Benki ya Dunia, *NORAD, JICA, UNDP, UNIDO, DANIDA, CIDA, SIDA, USAID, ACBF, DFID,* Jumuiya ya Madola na Jumuiya ya Ulaya.

Kwa kumalizia hotuba yangu, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mawaziri wenzangu, Mheshimiwa Philip S. Marmo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais

(Utawala Bora) na Mheshimiwa Kingunge Ngombale Mwiru, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Siasa na Uhusiano wa Jamii), kwa ushirikiano wao mkubwa katika kusimamia majukumu tuliyopewa na katika matayarisho ya hotuba hii. Aidha, ninapenda kuwashukuru Bwana Phillemon Luhanjo, Katibu Mkuu Kiongozi, Bibi Rose Lugembe, Katibu Mkuu (Ikulu), Bwana George Yambesi, Katibu Mkuu (UTUMISHI), Wenyeviti na Makatibu wa Tume na Taasisi mbalimbali na Watumishi wote walioko katika Wizara, Mikoa, Wilaya na Idara zinazojitegemea, siyo tu kwa kazi nzuri na ushirikiano mkubwa wanaotoa katika kufanikisha malengo ya Serikali sehemu waliko, bali pia kwa mchango wao uliowezesha matayarisho ya hotuba hii ya bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika*,* baada ya uchambuzi nilioutoa hapo juu, ambao umeonyesha hali ya utekelezaji wa shughuli zilizofanywa na Ofisi ya Rais (Ikulu), Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma kwa mwaka 2006/2007, pamoja na mpango wa kazi kwa mwaka 2007/2008, naomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee maombi yetu ya fedha kwa mgawanyo ufuatao:-

Fungu 20: Ofisi ya Rais, Ikulu

§ Matumizi ya Kawaida Sh. 5,891,233,000

Fungu 30: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri

§ Matumizi ya Kawaida ...... Sh. 121,250,754,000

§ Mpango wa Maendeleo ....Sh. 69,590,206,000

§ Jumla ya Fungu 30. ni ......Sh. 190,840,960

Fungu 32: Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma:

§ Matumizi ya Kawaida .....Sh. 9,857,913,000

§ Mpango wa Maendeleo..... Sh. 27,624,847,300

§ Jumla ya Fungu 32 ni...... Sh. 37,482,760,300

Fungu 33: Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma**:**

§ Matumizi ya Kawaida ..... Sh. 1,500,009,000

Fungu 94: Tume ya Utumishi wa Umma:

§ Matumizi ya Kawaida ....... Sh. 7,818,121,000

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninapenda kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri nakushukuru sana kwanza umeokoa muda, kwa hiyo imekuwa vizuri tu. Sasa Waheshimiwa Wabunge, kwa Ofisi ya Rais sijapata mchangiaji hata mmoja. Wakati Waziri anasoma huwa wanaleta maombi, sasa sijayapata. Naona basi ipo nafasi asubuhi, baada ya ofisi hii tutaingia Ofisi ya Makamu wa Rais. Mimi ninavyoona ni vizuri hotuba hii ziwe zinasomwa asuhuhi. Tukienda na mtiririko huu zitakuwa zote zinasomwa jioni na zile nyingine zina mambo mengi marefu, hata watu wa vyomba wa habari tutakuwa tunawapa shida sana. Maana watakuwa wanazipata jioni.

Kwa hiyo, naomba Kamati ya Uongozi tukutane kesho saa saba na robo ili tuweze kupanga ratiba mpya ya mtitiriko wa jinsi Wizara zitakavyo jadiliwa. Lakini kesho asubuhi ni dhahiri tunaendelea na majadiliano kuhusu Ofisi ya Rais, kama ambavyo Mheshimiwa Waziri alivyowasilisha hotuba yake. Ninalo tangazo moja tu; kuna Mwenyekiti mmoja ameitisha Mkutano nadhani nitalisoma asubuhi kwa sababu sasa hivi silioni.

Baada ya kusema hayo na kwa kuwa hatuwezi kuendelea na shughuli yoyote hivi sasa, kwa sababu zote ni kama zimeisha na kwa sababu sina wachangiaji kwa sasa, hata hivyo muda hautoshi itakuwa ni dakika 25 ambazo ni chini ya nusu saa ambayo inatolewa. Kwa hiyo, katika hatua hii naomba nitamke kuahirisha shuhuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.19 mchana Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne*
*Tarehe 3 Julai, 2007 Saa Tatu Asubuhi)*